NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 13 Aprili, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 68

**Huduma ya Upasuaji – Kituo cha Afya Kala**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Serikali kupitia Mradi wa Mfuko wa Benjamin Mkapa ilidhamiria kujenga na kukamilisha huduma ya upasuaji kwenye Kituo cha Afya cha Kata ya Kala na baada ya mfuko huo kuacha shughuli zake hakuna juhudi inayoendelea.

(a) Je, kuna mpango wowote kuendeleza nia hiyo njema?

(b) Kwa kuwa kituo hicho kina upungufu mkubwa wa wataalam; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi wakiwepo wauguzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa za Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina vituo vya afya saba, kati ya hivyo vituo vinne vinamilikiwa na taasisi za kidini na vitu vitatu vinamilikiwa na Serikali. Vituo vya afya viwili vinavyomilikiwa na Serikali vinatoa huduma za upasuaji. Kituo cha Afya Kala kinamilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Sumbawanga. Taasisi ya Benjamin Mkapa ilijenga chumba cha upasuaji *(theatre)* pamoja na kutoa baadhi ya vifaa kwa ajili ya huduma za upasuaji katika Kituo cha Afya Kala mnamo mwaka 2016/2017.

Hata hivyo, huduma hizo zimekuwa hazitolewi kutokana na changamoto mbalimbali kubwa zikiwa ni upatikanaji wa wataalam kwa ajili ya kufanya huduma za upasuaji na kukosekana kwa huduma ya umeme na mfumo wa maji kwa ajili ya kuendeshea shughuli za upasuaji. Ili kukabiliana na hali hiyo Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 17.3 katika mwaka wa fedha 2017/2018, kwa ajili ya miundombinu ya maji na umeme ambapo fedha hiyo bado haijapokelewa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na upungufu wa watumishi katika Kituo cha Afya Kala, Halmashauri ilipeleka tabibu mmoja na wauguzi wawili ili kutoa huduma katika kituo hicho mwaka 2015. Aidha, Halmashauri ilipeleka gari moja la wagonjwa lenye namba za usajili SM 4467 mwaka 2017 kutoa huduma katika kituo hicho. Serikali itaendelea kupeleka wataalam wa afya katika kituo hicho kwa kadri watakavyopatikana. Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wamiliki wa Kituo cha Afya Kala ili kushirikiana katika kutatua changamoto ya

watumishi katika kituo hicho kwa kuwa watumishi watatu waliopo sasa katika kituo hicho wote wameajiriwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi pamoja na majibu ya Serikali, naomba nieleze kwamba gari lililopo Kituo cha Afya Kala ni bovu sana na halifanyi kazi na Kala ipo umbali wa kilometa 150; hakuna mawasiliano yoyote ya simu wala barabara haifai. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwenye huduma za afya zinazotolewa kwenye vituo vyenye udau wa Serikali na wadau wengine, wananchi wa Kala wameamua kujenga kituo cha afya kwenye Kijiji cha King'ombe wao wenyewe, lakini vilevile wako wananchi wengine wameamua kujenga kutoka kwenye kata zao, Kata ya Ninde, Kata Kate na Kata ya Nkandasi. Je, Serikali iko tayari kuunga mkono juhudi hizi za wananchi?

Swali la pili Waziri wa Afya alipotembelea kwetu alituahidi kutupata shilingi milioni 400 kwenye Kituo cha Afya cha Wampembe na mpaka sasa sijaona fedha hiyo zimeonekana katika vitabu mbalimbali, lakini pia hatujazipokea; je, Serikali bado ina mpango huo wa kutupatia pesa katika Kituo hicho cha Wampembe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi kwa dhati kwa moyo wao wa kujitoa kuhakikisha kwamba vinajengwa vituo vya afya baada ya kuona kwamba changamoto ya kuwa katika hivi vya ubia inawakabili. Katika Serikali kuunga jitihada za wananchi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika pesa

ambayo inatarajiwa kupatikana muda si mrefu Kituo cha Afya Kasu nacho ni miongozi mwa vituo vya afya ambavyo vinaenda kupatiwa fedha ili viweze kujengwa na kuweza kutoa huduma ambazo wananchi wanatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili ameniambia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Afya alivyoenda baada ya kuona changamoto kwa wananchi wa Wampembe aliahidi kituo hicho kingeweza kupatiwa jumla ya shilingi milioni 400 ili kiweze kupanuliwa. Naomba nimhakikishie kwamba ahadi hiyo bado ni thabiti ni suala la tu la muda, pesa ikipatikana hatutasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa ujumla wake naomba uniruhusu, unajua unapokuwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wako kwenye Halmashauri moja na majimbo yako mawili ni sawa na ambavyo unapokuwa na watoto mapacha. Ni wajibu wako kuhakikisha kwamba unakuwa na *balancing* ambalo kama Serikali tunaenda kulifanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa waraka wa kusitisha taratibu wa upandishwaji wa baadhi ya zahanati kwenda vituo vituo vya afya ikitaka vituo vya afya vijengwe kwenye kila kata, lakini kwamba Halmashauri zetu hazina fedha za uhakika za kujenga lakini hata wananchi wenyewe hali ya uchumi ni ngumu kuweza kujenga vituo hivyo vya afya.

Je, Serikali kwa nini msifikirie kwa upya kubatilisha uamuzi huo na kuangalia zile zahanati ambazo kwa kweli zinakidhi haja ziweze kupandishwa kuwa vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya suala zima la kupandisha zahanati kuwa vituo vya afya, kwanza naomba tukubaliane, zahanati zina ramani zake na vituo vya afya vina ramani zake. Hoja ya msingi ni kwamba tungependa wananchi wapate huduma ya afya jirani sana, naomba kwa sababu mpaka sasa hivi tulikuwa tunaongelea tuna asilimia 12 tu ya vituo vya afya na bado na uhitaji wa zahanati bado uhitaji ni mkubwa.

Naomba azma hiyo ya Serikali yakuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na zahanati na kila Kata kunakuwa na kituo cha afya bado ndio msimamo wa Serikali na wananchi waendelee kushiriki ili tuhakikishe kwamba huduma hii ina inawasogelea wananchi kwa karibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

Na. 69

**Uhaba wa Vitanda katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Katika Hospitali ya Rufaa ya Rukwa kumekuwepo na tatizo la wanawake wajawazito na waliojifungua kulazwa katika kitanda kimoja.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo hilo katika hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto, naomba kujibu

swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na changamoto ya akina mama wajawazito na waliojifungua kulala katika kitanda kimoja inayochangiwa na ufinyu wa nafasi katika jengo la wazazi lililopo kutokana na ongezeko la idadi ya watumiaji wa huduma hizi hasa kwa kuwa hospitali hii ilianza kama kituo cha afya mwaka 1974. Vilevile tatizo hili linachangiwa na ukosefu wa Hospitali za Wilaya katika Halmashauri za Kalambo na Sumbawanga hali inayosababisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kuhudumia wateja wote wanaotoka kwenye halmashauri zote mbili.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, Wizara imeweka mikakati ya ufumbuzi wa changamoto hii kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia Mpango Kabambe wa Hospitali wa mwaka 2017/2018 yaani *Comprehensive Hospital Operation Plan*, Wizara imekamilisha ukarabati wa wodi mbili na hivyo kuongeza nafasi ya vitanda kwa ziada 20 ambavyo tayari vinatumika na hivyo, kupunguza msongamano uliokuwepo.

(ii) Serikali inafanya ujenzi na upanuzi wa miundombinu katika vituo vya afya sita ambavyo ni Mazwi, Nkomolo, Kirando, Mwimbi, Legezamwendo na Milepa ndani ya Mikoa hii. Kupanua wigo wa kujifungua kwa njia ya upasuaji. Hatua hii itapunguza tatizo la akina mama wajawazito wengi kupewa rufaa kujifungua katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

(iii) Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetenga jumla ya shilingi bilioni 100.5 katika mwaka 2018/2019 kwa ajili ya upanuzi wa Hospitali za Halmashauri 67 ambapo kila moja imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1.5. Halmashauri za Mkoa wa Rukwa zinatarajiwa kunufaika na fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu kwamba Serikali kupitia mikakati hii itatoa tatizo la msongamano wa

akina mama wajawazito waliojifungua katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri umekiri kwamba katika Mkoa wa Rukwa hakuna Hospitali ya Wilaya hata moja na nia ya sisi wawakilishi na Serikali kwa ujumla ni kuhakikisha sio kuepusha au kupunguza vifo vya wanawake na watoto ila ni kuhakikisha suala hilo linapotea kabisa linakwisha kwa ya kuwasaidia wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la kuepusha vifo hivyo sio kuandaa tu vitanda ila ni kuhakikisha tunatengeneza mazingira rafiki ya mama anayejifungua pamoja na mkunga. Kwa maana hiyo kunahitajika vitanda ambavyo vitakuwa na *instrument* kwa ajili ya kuepusha masuala hayo. Ni lini sasa Serikali itapeleka vitanda ambavyo vitakuwa rafiki kwa wauguzi pamoja na wanawake wanaweza kujifungua?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri wa Afya alipokuja Sumbawanga Mjini katika maadhimisho ya siku ya wanawake aliahidi kuleta magari mawili ambayo yataendana na mazingira yaliyopo katika Mkoa wa Rukwa ambayo yataweza kuwasaidia wanawake kutoka kwenye mazingira walionayo kuna umbali mrefu kufika kwenye Hospitali ya Rufaa. Ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza kuhusiana na suala la vitanda, Serikali hii ya Awamu ya Tano katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi

bilioni 269 na bajeti hii imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hatuna uhaba wa fedha, tatizo lililopo ni kwamba Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa, Vituo vyetu vya Afya pamoja na Hospitali za Wilaya hazijaagiza vitanda hivyo. Kwa hiyo, niendelee kumwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na hospitali yake ambapo ina upungufu wa viwanda ili hospitali hiyo husika kwa kutumia fedha ambazo Serikali inazitoa waweze kuagiza vitanda hivyo. Vitanda vipo katika Bohari yetu ya Madawa ya *MSD*.

Swali lake la pili, ameuliza ni lini magari ambayo Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ya kuweza kuyapata. Sasa hivi Serikali kupitia Wizara ya Afya imeagiza magari na yatakapopatikana ahadi hiyo itatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari, ajiandae Mheshimiwa Kabati.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, tatizo hili la wanawake wajawazito waliojifungua ku-*share* vitanda lipo pia kwenye Hospitali ya Wilaya ya Arumeru na mimi nikishirikiana na *DMO* aliyekuwepokwa sababu ya *PR* tulipata wafadhili ambao walikuwa tayari kutujengea *maternity ward* kubwa na nzuri na kisasa kabisa kwa kushirikiana na mimi na Dkt. Okiyoo ambaye alikuwa *DMO* wa kwetu. *Unfortunately* kwa sababu binafsi ambazo siko tayari kuzitaja hapa tumeshazijadili pia na Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Mkurugenzi aliyekuwepo akafanya yake wakamhamisha *DMO* kumpeleka Lindi.

Baada ya kupitia na kwenda kupitia zile *parameters* hapo Wizarani TAMISEMI tukagundua kwamba aliondolewa kwa sababu binafsi na bahati ambaya wale wafadhili ambao walikuwa watujengee ile *maternity ward* ilitokana na mahusiano binafsi ambayo tulikuwepo sisi na wao na yule daktari. Kwa hiyo, baada ya yeye kuondoka ni kama wameingia mitini vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuuliza tu Serikali iko tayari kumrudisha yule bwana ili ule mradi ukamilike halafu baada ya hapo wamhamishe? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri swali tofauti lakini kama ninyi wazoefu mna uwezo jibuni. Mheshimiwa Waziri TAMISEMI:

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali si mtu, kama alikuwa *DMO* pale ame-*coordinate* pale kwamba *maternity* ijengwe pale suala la yeye kuhama haiwezi ikawa kigezo cha kwamba mchakato huo usiendelee ni vizuri akarithisha hiyo kazi nzuri ambayo aliyokuwa ameishainza ili *DMO* aliyepo sasa afanye kuhakikisha kwamba hilo linakamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anakwenda Mbeya alipitia katika hospitali yetu ya Iringa na akajionea changamoto kubwa kabisa ambazo ziko katika mkoa wetu. Kwanza kabisa ni udogo wa eneo la hospitali ambayo iko katika mkoa wetu ambayo kwa kweli pia kuna muingiliano wa Magereza. Tatizo kubwa Madaktari Bingwa hawana kabisa maeneo ya kuishi kwenye lile eneo na wagonjwa wanapata shida sana wanapokuja kutibiwa usiku na vilevile alielezwa kuhusiana na eneo ambalo mkoa umeutafuta ili kuwepo na *alternative* mbili aidha magereza itoke au walipie lile eneo ili madaktari wetu waweze kuwasaidia wagonjwa usiku.

Je, sasa Serikali inatuambiaje maana yake hili ni tatizo la muda mrefu ili wananchi wa Mkoa wa Iringa waweze kutatua hiyo changamoto? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa sababu jambo hili amekuwa akilifuatilia sana na hii inaonyesha ni jinsi gani anavyojali masuala ya ustawi wa wananchi wa Iringa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani imelitafakari sana jambo hili na kuona kwamba kilicho rahisi kuhama ni Magereza kwa sababu kwanza eneo lipo na lipo ndani ya Manispaa na kiusalama liko vizuri zaidi kuliko pale ambapo wagonjwa au ndugu wanaoenda kuwaona wagonjwa hulazimika kupita mbele ya geti kubwa la gereza ambacho kiulinzi inaleta matatizo. Kwa maana hiyo sisi kama Wizara tunaendelea tu kuangalia *logistic* za kibajeti ili tuweze kuanza utaratibu huo wa kuhamisha gereza ili kutoa fursa nzuri ya wananchi kuweza kupata matibabu na *expansion* ya Hospitali ya Mkoa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

Na. 70

**Umuhimu wa Elimu ya Unasihi**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Kutokana na ugumu wa maisha na mabadiliko ya mtindo wa kuishi, baadhi ya wananchi wamekata tamaa ya kuishi.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutoa elimu ya unasihi kwa wale wanaohitaji?

(b) Je, ni vyuo vingapi hapa nchini vinatoa wataalam wa elimu ya unasihi?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto mbalimbali za maisha zinazowakabili watu na kuwasababishia msongo wa mawazo. Changamoto hizo ni pamoja na hali ya umasikini, magonjwa, migogoro ya kifamilia, kujihusisha na matumizi mabaya ya dawa za kulevya na ulevi, ukatili na unyanyasaji wa kimwili, kijinsia na kisaikolojia. Aidha, Wizara inatambua umuhimu wa huduma za unasihi na msaada wa kisaikolojia na jamii katika kusaidia kuondokana na msongo wa mawazo. Kwa kuzingatia umuhimu wa huu wa huduma hiyo, Serikali huwatumia Maafisa Ustawi wa Jamii waliopo ili kutoa huduma hii.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanya ugatuaji wa huduma za ustawi wa jamii kwenda katika Halmashauri ili kufikisha huduma za ustawi wa jamii ikiwemo unasihi karibu zaidi na wahitaji walio wengi. Katika ugatuaji huo jumla ya Maafisa Ustawi wa Jamii 731 tayari wameajiriwa katika halmashauri 185. Wizara itaendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kadri bajeti itakavyoruhusu ili kuwa na wataalam wa kutosha katika eneo la huduma za unasihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyuo 18 vinavyotoa elimu ya unasihi kati ya hivyo viwili ni vya umma na 16 ni vya binafsi. Taasisi ya Ustawi wa Jamii inatoa mafunzo ya fani ya ustawi wa jamii katika ngazi ya cheti, stashahada, shahada na shahada ya uzamili kwa lengo la kupata Maafisa Ustawi wa Jamii wenye utaalam wa kutoa huduma za unasihi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya wanafunzi 265 walidahiliwa katika ngazi zifuatazo; cheti 192, stashahada 216, shahada 189 na shahada ya uzamili 28. Katika mwaka wa masomo 2017/2018 jumla ya wanafunzi 607 walidahiliwa

katika ngazi zifuatazo; cheti 186, stashahada 210, shahada 190 na shahada ya uzamili 21. Aidha, Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara kimeanza kutoa mafunzo ya wasaidizi wa ustawi wa jamii katika mwaka 2017/2018 ambapo jumla ya wanafunzi 225 wamedahiliwa katika ngazi za cheti 192, stashahada 216, shahada 189 na stashahada ya uzamili 28. Wanafunzi hawa baada ya kuhitimu watakuwa na jukumu la kutoa huduma za unasihi katika ngazi ya kata, vijiji na mitaa na katika vituo vya afya na zahanati.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa mnaona ukitaka jambo lako unatakiwa u-*lobby* namuona Mheshimiwa Nassari ana- *lobby issue* yake pale kwa Waziri. Mheshimiwa Toufiq. *(Makofi)*

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi hawafahamu waende wapi pale matatizo wanapohitaji unasihi na hii imejidhihirisha hivi karibuni baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kutangaza wanawake waliotelekezwa waende kwake, wamejitokeza wengi sana, sambamba na hilo na wanaume pia walijitokeza. Sasa nilitaka kufahamu je, Serikali haioni imefikia wakati wa kuhabarisha jamii kwamba huduma hizi zinatolewa ili waweze kupata huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Maafisa Ustawi wa Jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii wako katika ngazi mbalimbali, je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga siku maalum walau siku mbili kwa wiki na kutenga maeneo maalum ili wananchi waweze kwenda kupata ushauri wa unasihi badala ya kusubiri kwenda kipindi cha muda wa kazi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni kuhusiana na suala la uelewa wa wananchi, tunapokea ushauri wake na tutaufanyia kazi kwa lengo la kujengea uelewa na nitoe rai tu kwa wananchi kwamba huduma za ustawi wa jamii zipo katika Halmashauri zote na katika baadhi ya maeneo hadi katika ngazi ya kata. Wanapokuwa na changamoto zinahusiana na masuala ya migogoro ya familia masuala ya ustawi, watoto yatima, waende katika ofisi za Halmashauri ama za ngazi ya kata kuweza kupata huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili katika swali lake la nyongeza ameulizia kwamba kwa nini Serikali isitenge siku maalum na maeneo maalum ili huduma hii iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Maafisa Ustawi wa Jamii ni waajiriwa wa Serikali na wapo muda wote kuweza kutoa huduma hizi kwa hiyo, huduma hizi zinatolewa siku zote za kazi katika muda wa masaa ya kazi katika maeneo husika ngazi ya Halmashauri, kata na mitaa ambapo Maafisa Ustawi wa Jamii wapo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

Na. 71

**Upungufu wa Madaktari Bingwa – Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga inakabiliwa na upungufu wa Madaktari Bingwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Azza Hillal Hamad kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya kuwatetea wananchi wa Shinyanga hususani katika sekta ya afya nataka kumpongeza sana kwa jitihada zake hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha kutoa huduma za kibingwa Hospitali za Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga inahitaji kuwa na Madaktari Bingwa wa fani sita muhimu ambazo ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akinamama na Wajawazito, Daktari Bingwa wa Afya ya Kinywa na Meno, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Daktari Bingwa wa Mionzi, Daktari Bingwa wa Upasuaji na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto. Aidha, Serikali inatambua kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga kwa sasa ina Madaktari Bingwa watatu tu ambao ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akinamama na Wajawazito, Daktari Bingwa wa Upasuaji na Daktari Bingwa wa Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuzihamisha Hospitali za Rufaa za Mikoa kuwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara inaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya kina kujua hali halisi ya mahitaji ya Madaktari Bingwa na fani zao katika Hospitali zote za Mikoa, Kanda Maalum na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Baada ya kukamilisha tathmini hii Wizara itawapanga upya madaktari bingwa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya kila hospitali ya mkoa, kanda, hospitali maalum na zile za Taifa, lengo ni kuwa kila Hospitali ya Mkoa iwe na Madaktari Bingwa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza.

**MHE. AZZ H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini niseme tu suala la tathmini linachukua muda mrefu na tathmini hii haijulikani itakwisha lini. Narudi palepale kuuliza swali langu la nyongeza, ni lini Serikali italeta Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tatizo la upungufu wa watumishi katika sekta ya afya limekuwa ni tatizo kubwa hata katika vituo vyetu vya afya na zahanati. Je, Serikali inajipanga vipi kuhakikisha upungufu tulionao katika vituo vya afya na zahanati unakwenda kumalizika kabisa ama kupungua kwa kiasi kikubwa? Nakushuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Ninyi Afya na TAMISEMI mko vizuri, jibu tu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba bado tuna changamoto kubwa sana ya watumishi katika sekta ya afya, watumishi tuliokuwa nao ni takribani asilimia 52 tu ya idadi ya watumishi ambao hatunao. Katika mkakati wetu wa kwanza ameuliza ni lini tutapeleka Madaktari Bingwa, Serikali inaendelea kufanya jitihada kama nilivyosema tumeshakamilisha zoezi la tathmini tunajaribu sasa kuhakikisha kwamba wale wachache tuliokuwa nao baada ya kupata taratibu za kiutumishi tutawahamisha, lakini sambamba na hilo tunatarajia kupata kibali kipya cha ajira ambao wale watumishi watasambazwa katika maeneo mbalimbali ya kwenye uhitaji ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga, Hospitali za Wilaya, Vituo vya afya na Zahanati kulingana na mahitaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Aisharose na Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi hii na nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuweza kuniwezesha kunipa fedha

za Kituo cha Afya cha Mwese na fedha za Kituo cha Afya cha Mishamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo la nyongeza ambalo nilitaka kujua, Mkoa wa Katavi kwa ujumla na Wilaya ya Tanganyika ambako kuna Kituo cha Afya cha Mwese, Kituo cha Afya cha Kalema, Kituo cha Afya cha Mishamo, sambamba na zahanati zilizomo kwenye Wilaya ya Tanganyika na Mkoa kwa ujumla wa Katavi kuna uhaba mkubwa sana wa madaktari kwenye sekta hiyo ya afya. Ni lini Serikali ina dhamira ya dhati kutoa tatizo la uhaba wa watumishi wa sekta ya afya katika Mkoa wa Katavi hasa Wilaya ya Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya swali la msingi nimeelezea kwamba bado ni kweli tuna changamoto kubwa sana ya rasilimali watu katika sekta ya afya. Katika mwaka huu wa fedha Serikali ilitoa kibali cha ajira cha watumishi 3,152 ambao walisambazwa katika mikoa mbalimbali, lakini vilevile nimesema katika jibu langu la msingi tunatarajia kupata kibali kipya cha kuajiri watumishi katika Serikali ikiwa ni pamoja na sekta ya afya. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Mbunge pindi kibali hicho kitakapotoka Mkoa wa Katavi utakuwa ni mmoja wa mikoa ambayo tutazingatia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aisharose.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga linafanana kabisa na tatizo lililopo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida inatakiwa kupokea wagonjwa 50 kwa siku, lakini inapokea wagonjwa zaidi ya

200; na hospitali hii ina uhaba mkubwa sana wa Madaktari Bingwa, vifaatiba kama kama *CT-SCAN*, *MRI,* pamoja na gari la kubebea wagonjwa. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka vifaa tiba vya kutosha lakini na Madaktari Bingwa pamoja na gari la kubebea wagonjwa ili wananchi wake waweze kupata huduma bora za afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inakiri kwamba kuna uhaba wa Madaktari katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida na kama nilivyowaeleza katika majibu yangu ya msingi changamoto hiyo tunaitambua, tumeweza kupeleka madaktari wachache, lakini tunatambua kwamba bado hawatoshi. Katika kibali kipya ambacho tutakachokipata mahitaji ya Mkoa wa Singida yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hili ni ameulizia suala la vifaa, niendelee kumuomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Singida kama nilivyosema sasa hivi fedha kwa ajili ya bajeti ya dawa, vitendanishi na vifaatiba tunavyo vya kutosha, hospitali zinatakiwa ziainishe vifaa ambavyo wanavyovihitaji ili kuweza kuvipata. Tahadhari yangu ni kwamba teknolojia nyingine ambayo wanaiulizia ya kwamba kuwa na *CT-SCAN* na *MRI* katika ngazi hizi kwa sasa bado hatuna uwezo na wataalam wa kuweza kuzisimamia na kuvihudumu. *CT-SCAN* na *MRI* tumeanza katika miongozo yetu zinaanza kutumika katika ngazi za Hospitali za Kanda. Kadri tutakavyokuwa tunajenga uwezo basi tutazishusha chini katika ngazi ya rufaa Hospitali za Rufaa za Mikoa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla sijauliza swali la nyongeza kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mawaziri wote wanaohusika

kuona wahudumu kwenye wizara hii kwa kunipunguzia tatizo la wafanyakazi, baada ya kunipatia wafanyakazi sita kwenye kada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya shida iliyopo wale wafanyakazi sita imekuwa kama tone la damu kwenye bahari. Kwa hiyo, shida iliyopo katika hospitali yetu ya Wilaya ya Liwale ni kubwa sana kiasi kwamba wauguzi wawili wanahudumia wodi tano kwa wakati mmoja, jambo hili ni baya sana vilevile linapunguza ufanisi wa kazi.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuniongezea wafanyakazi kwenye kada hii ya wauguzi ili kuongeza ufanisi kwenye hospitali ile ya wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tunajua na tunatambua mahitaji ya watumishi wa afya ikiwa ni pamoja na Manesi katika hospitali za Liwale. Pindi tutakapopata watumishi basi Wilaya ya Liwale ni moja ya wilaya ambayo na sisi tutaizingatia.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Nishati Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

Na. 72

**Kusuasua kwa Mradi wa *REA* Buhigwe**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-
Utekelezaji wa mradi wa umeme wa *REA* Wilayani Buhigwe unasuasua sana.

Je, ni lini vijiji vyote na vitongoji vyake pamoja na taasisi za umma zitapata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Buhigwe ina kata 20, vijiji 44 na vitongoji 190. Kupitia Miradi ya *REA* Awamu ya Pili vijiji 14 vilipatiwa umeme, vijiji hivyo ni Kasumo, Kalege, Nyanga, Biharu, Kigege, Bulimanyi, Nyamugali, Songambele, Kavomo, Buhigwe, Mulera, Munanila, Manyovu na Mwayaya. Aidha, katika awamu hiyo taasisi mbalimbali za umma zilipatiwa umeme ikiwamo Shule ya Msingi ya Kalege, Kituo cha Afya cha Muyama, Zahanati ya Buhigwe, Kituo cha Polisi cha Buhigwe, pamoja na Ofisi ya Uhamiaji ya Munanila nayo ilipatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vipatavyo 22 vya Wilaya ya Buhigwe vimejumuishwa katika Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza unaotarajiwa kuanza kutekelezwa Mwezi Mei, 2018 katika Wilaya za Buhigwe, Kasulu, Kigoma na Uvinza. Utekelezaji wa mradi huu umechelewa kuanza katika Wilaya hizo kutokana na mmoja wa wakandarasi walioomba kazi hiyo kuilalamikia kampuni iliyokusudiwa kupewa kazi hiyo mahakamani. Vijiji vitakavyopelekewa umeme ni pamoja na Nyakimwe, Mkatanga, Rusaba, Nyaruboza, Muhinda, Kibande, Kajana, Bweranka, Kigogwe, Kibwigwa, Kinazi, Kitambuka, Munzese, Bukuba, Nyankoronko, Migongo, Mubanga, Mugera, Kirungu, Katundu, Munyegera na Nsagara. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilometa 103.64 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 na kilometa 142 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa transfoma 71 na uunganishwaji wa wateja wa awali 3,011. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 8.53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote na vitongoji vyake pamoja na taasisi za umma zitapelekewa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu baada ya taratibu zote zinazoendelea kukamilika. Vijiji nane vilivyobaki vitapatiwa umeme kupitia awamu ya tatu mzunguko wa pili ambao

unatarajiwa kuanza Novemba, 2019 na kukamilika Juni, 2021, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Obama.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwanza napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza kabisa Wizara hii inafanya kazi kubwa na ya kutukuka, lakini ni ukweli unaojulikana kwamba sisi katika Mkoa wa Kigoma na Katavi na hasa wananchi wangu wa Buhigwe umeme umechelewa kufika. Hivyo kwa *commitment* hii sasa ya Serikali kwamba ule mgogoro mtakuwa mmeumaliza kwamba Mei Mkandarasi atakuwa *site*. Kwanza kwa hatua hiyo kwa niaba ya wananchi wa Buhigwe na Mkoa wa Kigoma tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza; viko vijiji kama ulivyovitaja mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba vimeshapatiwa umeme lakini kwenye vitongoji umeme bado haujaenda. Nataka kufahamu mkandarasi huyu atakayeenda kupeleka umeme kwenye vijiji vilivyobaki je, atapeleka kwenye vitongoji, kwenye vijiji ambavyo tayari vimeshapewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nini *commitment* ya Serikali kwa sababu sisi mmetucheleweshea umeme kwa muda mrefu na wananchi wangu wanahitaji umeme kwenye vijiji vyao. Je, mkandarasi hamtaweza kumkwamisha kwamba hamna hela? Naomba *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwape pole wakazi wa Mikoa ya Kigoma na Katavi, lakini niwashukuru sana Wabunge wa maeneo hayo ya Mkoa wa Kigoma, Jimbo la Buhigwe, Kasulu, Uvinza pamoja na

Kigoma Vijijini pamoja na majimbo ya Mkoa wa Katavi kwa namna ambavyo wamekuwa wakifuatilia suala hili na kuwa na matumaini na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati pia nimepokea pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake yalikuwa mawili ambalo moja lilijielekeza vijiji ambavyo vimepatiwa umeme kama ambavyo jibu langu la msingi limesema, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maeneo ambayo Serikali inatambua yapo maeneo ya vijiji yalipata umeme lakini vipo vitongoji havikupata huduma hiyo na ndiyo maana Serikali imekuwa ikitekeleza mradi wa *densification* yaani ujazilizi na kwa sasa kwa mwaka unaokuja wa fedha 2018/2019 Serikali imeandaa mpango wa *densification* awamu ya pili ambayo itaenda kwenye mikoa mbalimbali ikiwemo Mkoa huu wa Kigoma. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao wote vitongoji ambavyo havina umeme kwenye vijiji vyenye umeme vitapatiwa huduma hiyo kupitia mradi wa *densification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi huyu atakapoanza kazi Mei, 2018 hatakwamishwa kwa sababu Serikali kupitia Wizara ya Fedha mpaka sasa imeshatoa pesa zaidi ya shilingi bilioni 221 ambavyo imetokana na chanzo hiki cha umeme *(REA)* ambao umetokana na tozo ya mafuta. Kwa hiyo, nimthibitishie Mbunge kwamba tatizo la pesa halipo, asante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hivi jibu hili zuri sahihi haliwi kwa Wabunge wote? Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mwilima na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, tarehe 13 Julai, 2017 aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambaye sasa ni Waziri wa Nishati alikuja kuzindua Mradi wa *REA III* katika Kijiji cha Nyamatala, Kata ya Ngula lakini hadi leo ni miezi saba hakuna hata eneo moja umeme umeshawaka. Nataka nipate majibu ya Serikali miezi

saba sio Kitongoji, Kijiji wala Kata na uzinduzi huo ulikuwa kimkoa. Nataka nipate majibu ya Serikali tatizo hasa ni nini na umeme huu utaanza kuwaka lini.

**MWENYEKITI:** Ahsante umeshaeleweka, Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ni kweli katika Mkoa wa Mwanza mkandarasi wa *Nippo Group Limited* yupo kazini na ninaomba nimfahamishe baada ya uzinduzi ule kazi ambazo ziliendelea ni pamoja na tathmini, uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niliarifu Bunge lako kipindi kile ambapo miradi inazinduliwa yapo mahitaji mbalimbali ambapo yalijitokeza kutoka kwa Wabunge kutokana na uhitaji wa nishati hii Vijijini. Kwa hiyo, tathmini ya ilivyokuwa inaendelea kufanyika na maeneo mbalimbali ambako wakandarasi walikuwepo, vipo Vijiji pia vya nyongeza pia vimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu kwamba kwa Mkoa wa Mwanza mpaka sasa mkandarasi yule ameshawasha Vijiji sita lakini naomba nimwelekeze Mkandarasi Nippo tulitoa maelekezo kwa wakandarasi wote wafanye kazi katika Wilaya zote, wawe na magenge ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pengine changamoto inayojitokeza mkandarasi huyu yupo katika Wilaya zingine hajafikiwa katika Jimbo lake. Lakini naomba nimthibitishie na wizara kwa awamu hii imepanga kufanya ziara katika Jimbo lake na kazi zitaendelea na kwa sababu mikataba hii inaonyesha na muda wa kazi ni kuanzia kipindi hiki mpaka Novemba, 2019 ndio zinakamilika, naomba nimtoe wasiwasi yeye Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo lake kwamba huduma hii ya umeme vijijini kama ilivyozinduliwa itapatikana kwasababu mkandarasi yupo ndani ya wakati, asante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa majibu mazuri, nitaomba ufupishe wapo wengi, wewe waambie tu tunakuja tulieni. Mheshimiwa Mwilima, Mheshimiwa Waziri muhusika. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali la Mheshimiwa Ndassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Ndassa kwa kweli wakati tunakwenda kuzindua alifanya kazi kubwa sana, lakini nimpe taarifa katika Jimbo lake tayari wakandarasi wapo katika Kijiji cha Nyamatara na Nyambiti; na Nyambiti na Nyamatara kesho wanawasha umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mheshimiwa Katibu wake na jana tuliwasiliana naye pale Nyamatara wameshasimika nguzo, transfoma wamepeleka juzi na kesho na keshokutwa wataendelea kuwasha kwenye vijiji viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Nguge pamoja na Nipo katika Mkoa wa Mwanza pia wameshawasha umeme lakini pamoja nahayo nitawasiliana na Mheshimiwa Ndassa tukae naye vizuri ili maeneo mengine vipaumbele tuweze kuwapelekea umeme haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. HASNA MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipa swali la nyongeza. Kwenye Vijiji vyangu vya Mwakizega, Kabeba na Lilagala tangu Awamu ya II ya *REA* nguzo zimeshawekwa na taratibu zote zimekamilika. Mradi ule ulitakiwa uzinduliwe mwezi wa pili mwaka jana 2017 lakini kwa masikitiko yangu makubwa Mheshimiwa Waziri umeshakuja Kigoma umepita umeenda Kibondo, wananchi wanauliza maswali, tumewekewa nguzo na transfoma tuizone? Ni lini umeme wa Kata hizi mbili za Mwakizega na Ilagala utawashwa rasmi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mwilima kweli nilitembea naye katika maeneo yake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge huyu kwa sababu kwanza tulienda eneo la Nguruka lililokuwa na shida kubwa tukawasha umeme Nguruka tukiwa pamoja, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hayo ambayo ameyataja eneo la Ilagala pamoja na Nguruka huyu mkandarasi wa *REA* Awamu ya Tatu anyekuja kufanya kazi ni kati ya maeneo ambayo ataanzia kuyafanyia kazi na kuyawashia umeme. Kwa hiyo, nimpe tu pongezi Mheshimiwa Mbunge kwamba avute subira wakati...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa utulivu.

**WAZIRI WA NISHATI:** ...mkandarasi tunampata katika mwezi huu kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza, tarehe 5 Mei ataanza kazi katika maeneo hayo na maeneo yatakayowashwa ni pamoja na Ilagala pamoja na Nguruka maeneo yaliyobaki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira tutafanya kazi pamoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zitto ajiandae Mheshimiwa Waitara.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme Kigoma ni wingi wa umeme na bahati mbaya sana Kigoma bado haijaunganishwa na Gridi ya Taifa na hata mpango ambao ulisainiwa kwa msaada wa Serikali ya Korea ambao Waziri wa Fedha alisaini takribani mwaka na nusu uliopita bado kabisa kuanza kutekelezwa. Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa mradi wa umeme wa maji wa Mto Malagarasi, Igamba III ambao ndio jawabu la kudumu la umeme katika Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi tu, wako wengi leo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe sahihisho kidogo sio Malagarasi Igamba III; ni Malagarasi Igamba II. Baada ya kusema hayo sasa ni kweli kabisa mradi wa Malagarasi ilikuwa kwanza utekelezwe wakati wa mradi wa *MCC* mwaka 2008, lakini ikaonekana kwamba kulikuwa kuna matatizo ya *REA species.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe taarifa katika Bunge lako tukufu ni kweli kabisa mradi huu sasa utaanza kutekelezwa kwenye mwaka huu wa fedha na tumeshatenga fedha na juzi Mheshimiwa Zitto nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge tulikuwa nao wakati tunakamilisha majadiliano ya Benki ya Maendeleo ya Dunia kwa ajili ya kufadhili mradi huo na zinahitaji dola milioni 149.5 kwa ajili ya kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Mbunge mradi huu unakwenda kutekelezwa kwenye mwaka huu wa fedha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Mwambalaswa. Waheshimiwa ulizeni kwa kifupi sana ili wote mpate majibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara katika Jimbo la Ukonga na tukafanya mikutano mpaka saa moja usiku, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu nijue kwamba Jimbo la Ukonga lina shida kubwa ya umeme ambayo Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wanafahamu. ningependa nijue katika hii mipango ya *REA* ambayo inaendelea Ukonga nao wategemee nini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Na mimi naomba nimpongeze Mbunge Mheshimiwa Waitara ni kweli tulifanya mikutano zaidi ya sita katika Jimbo lake na nimthibitishie baada ya mikutano ile kwa mwaka wa fedha unaokuja 2018/2019 Serikali inakuja na mpango wa *Peri-urban* kwa maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani na kisha itaendelea *Peri-Urban II.* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwambalaswa, ajiandae Mheshimiwa Flatei.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaishukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara sasa hivi mkandarasi yupo Wilayani Chunya kwa kupeleka umeme *REA III,* anafanya upimaji katika Vijiji vya Ifumbo, Soweto, Mawelo na vinginevyo. Kuna Kijiji kinaitwa Itumbi katika Kata ya Matundasi, kijiji hiki Serikali kupitia Wizara inajenga kituo cha mafunzo kwa wachimbaji wadogo *(center of excellence)* lakini Kijiji hiki hakimo kwenye Awamu namba tatu ya kupeleka umeme. Je, Serikali haiwezi kukiangalia Kijiji hiki kwa jicho la pekee na kupeleka umeme katika awamu hii ya tatu?

**MWENYEKITI:** Ahsante, ni lini tu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge katika swali lake. Kwa kweli kituo cha Matundasi pamoja na Itumbi ni kati ya maeneo ambayo yapo kwenye *center of excellence* kwa upande wa madini na baada ya kufanya *survey* Mheshimiwa Mbunge, kijiji kipo kwenye mpango sasa kwa sababu ni maeneo ya vipaumbele kwenye miradi ya maendeleo, kwa hiyo, kipo kwenye mpango wa fedha wa mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei ajiandae Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbulu Vijijini lina uhaba sana wa umeme na Mheshimiwa Waziri amefika. Sasa lini atakuja kuwasha umeme katika Jimbo la Mbulu Vijijini na anafahamu kwa sababu amefika na vijiji vingi havina umeme. Atutajie tu lini atafika Jimbo la Mbulu Vijijini kuwasha umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ni lini?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, vijiji vya Mheshimiwa Mbunge vya Mbulu Vijijini na Mbulu Mjini vyote vipo kwenye mpango wa *REA* mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wananchi wanahitaji umeme tena umeme wa uhakika lakini tumekuwa na tatizo la kukatika katika kwa umeme katika Mkoa mzima wa Dar es Salaam na hasa kule Temeke; na mwaka jana Mheshimiwa Naibu Waziri alituahidi hapa kwamba kufikia Disemba 2017 tatizo la kukatika kwa umeme litakuwa limekwisha, leo ni mwezi wa nne mvua zinanyesha na umeme unakatika sana Jijini Dar es Salaam. Serikali mnatuambia nini kuhusu tatizo la kukatika kwa umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Kwanza napenda nitoe taarifa katika Bunge lako hili, katika maeneo ya Mbagala na Gongolamboto kulikuwa na kero kubwa sana ya kukatika kwa umeme, wiki mbili zilizopita tumejenga *sub-*

*station* imekamilika na kwa hiyo Mbagala sasa nina amini wanapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, umeme huu wa Mbagala ambao ni wa gridi naishukuru sana Serikali yetu, tumeanza sasa kuunganisha umeme wa gridi kutoka Mbagala kwenda Ikwiriri kupitia Kibiti mpaka Somanga Fungu na umeme huu wa Mbagala ambao unatoka kwenye Gridi ya Taifa ndio tunaunganisha katika Mikoa yote ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuanzia mwezi uliopita nitoe taarifa katika Bunge lako kwamba hata Mikoa ya Mtwara na Lindi sasa itakuwa inapata umeme wa gridi badala ya umeme wa mashine inayotumia sasa. Hizo mashine zilizopo sasa zitatumika tu kama mashine za ziada. Kwa hiyo nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu inanisaidia sasa kutoa taarifa kwa wananchi wa Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kukatika kwa umeme kunatokana na sababu nyingi, sio sababu ya kuwepo kwa umeme au miundombinu, wakati mwingine ni kasoro ndogo ndogo, tunakiri kabisa zipo changamoto za maeneo machache kukatika kwa umeme katika baadhi ya nyakati za mida. Tutashirikiana na Waheshimiwa Wabunge kutatua matatizo hayo. Tunachoomba tupate taarifa inapotokea itilafu ya namna hiyo, lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa wananchi wa Mbagala kwa sasa wanaendelea kupata umeme wa uhakika zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali inafanya vizuri sana kwenye umeme vijijini lakini bado tuna tatizo kubwa kwenye umeme mjini ikiwemo Singida Mjini yapo maeneo ambayo hayana umeme. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kutuletea umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge Sima. Pamoja na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini tulifanya ziara katika Mkoa wa Singida na katika Wilaya ya Singida Mjini tuliona hilo tatizo. Kwa hiyo, nataka niseme ni kweli Serikali inatambua tatizo la uwepo wa ukuaji wa maeneo ya mijini na changamoto ya upatikanaji wa nishati kwa hiyo, inakuja na mpango wa *Peri-Urban* ambao utapeleka umeme katika miji inayokua kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata ni la *REA* vilevile kwa hiyo, tutoa fursa kwenye swali linalofuata. Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

Na. 73

**Hitaji la Umeme wa REA III Katika Baadhi ya Kata – Tabora Mjini**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Katika Jimbo la Tabora Mjini hasa vijiji na kata zilizopo nje ya Manispaa ikiwemo Kata ya Tumbi na vijiji vinavyoizunguka kata hiyo havijajumuishwa katika Mpango wa *REA* Awamu ya Tatu.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* katika kata na vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vijiji vilivyopo nje ya Manispaa ya Tabora ikiwemo Kata ya Tumbi havikujumuishwa katika utekelezaji wa mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza. Sehemu ya vijiji katika Kata ya Tumbi ilipatiwa umeme mwaka

2006 kupitia mradi wa umeme chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden. Kwa kuwa baadhi ya vijiji vya Jimbo la Tabora Mjini viko ndani ya Manispaa ya Tabora, Serikali kupitia mradi wa *Urban Electrification* itaendelea kuyapelekea umeme maeneo yaliyomo katika Mamlaka za Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali ni kuipatia umeme Kata ya Tumbi na Vijiji vilivyoizunguka Kata hiyo katika Manispaa ya Tabora kupitia mradi wa *Urban Electrification.* Aidha, mradi wa *Urban Electrification* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika utepeleka umeme katika vijiji na shule za Makunga, Mkinga, Mayeye, Shalua, Mtakuja, Chang'ombe, Itetemia, Itaga na Umanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine unaotarajiwa kutekelezwa ni *densification* kwa nia ya kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji ambavyo vimefikiwa na miundombinu ya umeme. Maandalizi ya awamu ya pili ya mradi huu yanaendelea na unatarajiwa kutekelezwa kwatika mwaka wa fedha 2018/2019. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Emanuel.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, nianze kwa kuishukuru hii Wizara ya Nishati chini ya Dkt. Kalemani pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Subira kwa kazi nzuri mnayofanya, hongereni sana. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Tabora kwa kuitamka inaonekana kama hata vile vijiji vinavyozunguka ni kama vipo karibu sana, lakini vijiji vingi vipo mbali na maeneo ya mjini. Huu mradi ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kusambaza umeme unaonekana unasuasua maeneo mengi ya vijiji hivi ambavyo vimetajwa. Kama kuna uwezekano naomba Serikali iangalie

uwezekano wa kuingiza vijiji hivyo kwenye mradi huu wa *REA III* ili viweze kupatiwa umeme haraka, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilipata taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri anaweza kufanya ziara Tabora wiki ijayo sehemu za Urambo, kwa kuwa Tumbi hii ninayoizungumzia ipo njiani, anapokuwa Mheshimiwa Waziri anaelekea Urambo lazima atapita Tumbi pale. Je, Waziri yupo tayari kusimama maeneo yale hata kwa dakika chache ili asikilize kero za wananchi pale zinazohusiana na hilo suala la usambazaji umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mwakasaka, kwanza hilo la pili nipo tayari kusimama, nitasimama na nitafanya kazi pale, Mheshimiwa Mbunge nakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vijiji kweli kabisa Jimbo la Tabora kwanza lina kata 29 na kata 15 zipo mjini na kata 14 kimsingi zipo vijijini ingawa ni za Manispaa. Nimpe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wake zile kata 14 ambazo kimsingi zipo vijijini tumezipelekea kwenye miradi ya *REA* kwenye mpango wa *Peri-Urban*. Kwa hiyo, wananchi wake wataendelea kupata umeme kama kawaida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri labda alikuwa analenga Naibu Waziri ndio asimame sasa wewe unataka kusimama wewe yeye alitaka Naibu Waziri, basi haina neno. Mheshimiwa Atupele.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuweza kupata nafasi ya kuja katika Jimbo langu la Busokelo, lakini nina swali moja tu kwamba ulivyokuja wana

Busokelo tulikuomba kwamba vijiji vyote ambavyo vipo kwenye *scope* ya *REA III* na kwa bahati mbaya sana hivi vijiji baadhi yao vina nyumba za nyasi lakini hii leo ninavyouliza swali kwako Mheshimiwa Waziri ni kwamba vile vijiji vimerukwa. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya Vijiji 8 ambavyo vimerukwa kwenye scope ambayo ipo sasa kwa *REA III? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Atupele, tulifanya ziara pamoja katika Jimbo lake na kwa kweli katika Jimbo la Busokelo vijiji takribani 50 vipo katika *REA* hii ya Awamu ya Tatu na mkandarasi *Stag International* tulimwelekeza afanye tathmini katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hyo, naomba nimthibitishie vile vijiji nane ambavyo vipo kati ya vijiji 50 ambavyo vitapatiwa umeme katika *REA* awamu hii mzunguko wa kwanza tunamwelekeza mkandarasi vyote avifanyie tathmini na kwa kuwa Serikali imeelekeza nyumba yoyote iwe ya tembe au kawaida zote zinapatiwa umeme na tumeshuhudia mara kadhaa tukizindua umeme na nyumba hizi ambazo zimewekewa umeme. Kwa hiyo, nataka niseme hakuna nyumba mbayo itabaguliwa na mkandarasi atavifikia vile vijiji vinane, asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Atupele yule mchezaji wa *Mbeya City* jana ni ndugu yako? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hawa Mchafu, ajiandae Mheshimiwa Haonga.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hangamoto ya umeme iliyopo manispaa ya Tabora inafanana kabisa na ile ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga katika Kata ya Tambani,

Mwandege na vijiji vyake. Je, ni lini sasa umeme utawaka kwenye Kata hizi ikizingatiwa mradi wa *REA I* na *REA II* tayari ulishapita? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nikiri kwa kweli kwa Mbunge wa Mkuranga, Mheshimiwa Ulega pamoja na Mheshimiwa Mchafu wamekuwa wakifuatilia sana masuala ya nishati ya umeme katika Wilaya ya Mkuranga. Na ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, mkandarasi wa Mkoa wa Pwani Sengerema tumezungumza naye na Jumapili hii atapeleka nguzo kwa ajili ya maeneo hayo ya Tambani, Mwandege ambapo pana ongezeko kubwa la wananchi na hususani Kijiji cha Mlamleni katika Wilaya ya Mkuranga. Nataka nimthibitishie kazi kuanzia Jumamosi hii nguzo zitafika na itaendelea katika Mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa haonga halafu Mheshimiwa Nagu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Jimbo la Mbozi lenye kata 11 kuna kata mbili ambazo karibu vijiji 14 havina umeme kabisa. Sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa hizi kata mbili za Magamba na Kata ya Bara zitapatiwa umeme wa *REA?* Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme mpango wa Serikali ni kupeleka umeme katika maeneo yote ambayo yamesalia, vijiji 7,873. Kwa hiyo, kwa kuwa swali lake limejielekeza kwenye kata mbili ambazo zina vijiji 14 na hakuna umeme kabisa, nataka nimuarifu kwa kipindi hiki cha 2018/2019 – 2019/2020 Serikali itakamilisha upelekaji wa umeme katika maeneo ya hizo kata mbili na vijiji vyake kwa mradi huu kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu

unaoendelea kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha na unaoendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nagu, Mheshimiwa Oran ajiandae na Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *REA* kwa kazi nzuri, lakini hata hivyo katika Wilaya yetu ya Hanang kuna changamoto nyingi ambazo tunaziona, kwa mfano kuna taasisi ambazo hazijapata umeme pale ambapo umeme umeletwa, kuna maeneo yanarukwa njiani wanakwenda kwingine, je, Waziri atakubali kuja kutembelea Hanang ili tuone changamoto hizo ili tuzisahihishe na kama anaweza kumtuma mkandarasi kuja kuona changamoto hizo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Nagu na tumekubali huo mwaliko wa kutembelea kwa kuwa sisi Wizara yetu pamoja na Mheshimiwa Waziri na viongozi mbalimbali tumekuwa tukifanya ziara kwa kuwa miradi hii inatekelezwa vijijini. Kwa hiyo, naomba nimuagize pia mkandarasi Angelic, tuliwapa maelekezo wakandarasi wote taasisi muhimu za umma zipatiwe huduma hii ya umeme na maelekezo ya Serikali kupitia Mheshimiwa Rais pia mwenyewe kwamba vijiji visirukwe. Kwa hiyo, naomba nisisitize maelekezo haya yako palepale na tutafanya ziara katika maeneo yote likiwemo Jimbo la Hanang.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran, ajiandae Mheshimiwa Mwamoto, tutamalizia na Mheshimiwa Frank. Waheshimiwa natoa fursa kwa sababu najua *REA* ina umuhimu wake.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa ziara walizozifanya kwenye Halmashauri

ya Mbeya. Naibu Waziri alitembelea kata ambazo hazina umeme kabisa lakini zinalizunguka Jiji la Mbeya kama Kata za Swaya na Maendeleo. Je, ni lini hizi kata mbili nazo zitapewa umuhimu wa kupewa umeme?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, subiri hapo hapo, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Frank, halafu utayajibu kwa pamoja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifika Kilolo, tena Kijiji cha Kihesa Mgagao, Kata ya Ng'uruwe, na kuwaahidi vizuri wananchi wa Kilolo kuhusu umeme; na kwa kuwa sasa baadhi ya vijana wameshatenga maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Je, ni nani haswa anayepaswa kusogeza umeme kwenye maeneo ambayo vijana tayari wameshatengewa maeneo, ni gharama za nani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tunduma uko mpakani mwa Zambia na Tanzania na ni mji ambao unapokea wageni wengi wanaotoka nchi za Kusini mwa Afrika lakini huduma ya umeme kwenye Mji wa Tunduma ni haba sana na umeme unakatikakatika mara kwa mara na kusababisha usalama wa wageni na wananchi wa Tunduma kuwa hatarini. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba inaweka umeme wa uhakika katika Mji wa Tunduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa pamoja.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tukushukuru sana kwa namna ambavyo umetambua mahitaji ya nishati na kuwapa fursa Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali mengi. Umenipa fursa ya kujibu maswali ya

Mheshimiwa Njeza, Mheshimiwa Mwamoto pamoja na Mheshimiwa Frank.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Njeza na Mheshimiwa Mwamoto maswali yao yanalingana kwa sababu yamehusisha masuala ya umeme vijijini. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Njeza, tulifanya ziara Mbeya, pamoja na kwamba Jimbo lake ni Mbeya Vijijini, hapa amezisemea kata ambazo zipo ndani ya Jiji la Mbeya, na kama nilivyosema, Serikali imetambua ukuaji wa maeneo katika Miji, Manispaa na Majiji na ndiyo maana tumekuja na mradi huu unaoitwa *Peri-Urban.* Niliombe Bunge lako tukufu, tutakapowasilisha bajeti yetu ya mwaka 2018/2019 ituunge mkono katika miradi mbalimbali ukiwemo Mradi huu wa *Peri-Urban* kuupitisha kwa kishindo kisha tufanye kazi ya kupeleka umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, Mheshimiwa Mwamoto, ni kweli tulifanya ziara tena kwa mara ya kwanza Mawaziri wawili, Mheshimiwa Waziri mwenyewe na mimi Naibu Waziri tulikuwa kwenye kata hiyo aliyoitaja. Nataka niseme sisi lengo letu ni kupeleka nishati kwenye maeneo yenye uhitaji ikiwemo mojawapo ya maeneo ambayo kweli yanahitaji nishati ni eneo la viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze Mheshimiwa Mbunge na vijana hao kwa kutenga eneo la viwanda vidogo vidogo na kwa gharama za Serikali umeme utafika katika maeneo hayo na nitoe rai tu wao waendelee kujipanga kuunganisha lakini umeme utafika kama ambavyo tumeahidi katika ule mkutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la mwisho la Mheshimiwa Frank, ni kweli Mji wa Tunduma ni mji ambao umekuwa na upo mpakani. Nataka niseme Mji wa Tunduma upo katika Mkoa mpya wa Songwe na wakati huo umeme katika Mkoa wa Songwe ulikuwa unatoka katika njia ya kusafirisha umeme ni ndefu kutoka Mbeya. Serikali ina mpango wa kujenga *sub-station* palepale Tunduma kwa ajili

ya kuufanya Mkoa mzima wa Songwe upate nishati ya uhakika na wakati wote. Kwa hiyo, nimthibitishe Mjumbe kwa kuwa yeye Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Nishati na yeye pia atuunge mkono katika bajeti yetu ili mradi huu wa ujenzi wa *sub-station* pamoja na *line* ambayo inatoka Mbeya inayoenda Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi ya *KV* 400 ambayo yote kwa pamoja itachangia kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hongera sana Mheshimiwa Waziri, umejibu kwa ufasaha na kwa uzuri sana, hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, maswali mengine mtakuja kwenye bajeti. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, sema basi wewe ndiyo kwa niaba umesimama tu? *(Kicheko)*

Na. 74

**Fidia kwa ajili ya Mazao Yaliyoharibiwa na Wanyamapori**

**MHE. CECILIA D. PARESSO – (K.n.y. MHE. JULIUS K. LAIZER)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fidia stahiki kwa wananchi ambao mazao yao yaliharibiwa na wanyamapori tangu mwaka 2010 hadi 2017 katika maeneo ya Mswakini, Makuyuni, Naiti, Mbuyuni, Lokisale na maeneo mengine Wilayani Monduli?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanyamapori wakali na waharibifu ni kubwa na linajitokeza katika zaidi ya Wilaya 80 nchini. Uharibifu mkubwa wa mali na madhara kwa binadamu vikiwemo vifo husababishwa na tembo, mamba, nyati, kiboko, simba na fisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu unaotokana na wanyamapori kwa sehemu kubwa unasababishwa na ongezeko la watu na shughuli zao ambazo mara nyingine zinafanyika katika maeneo yaliyo karibu na hifadhi au kwenye mapito ya wanyamapori. Aidha, mabadiliko ya tabianchi yamechangia pia katika kubadili mzunguko na mtawanyiko wa asili wa wanyamapori wakati wa kutafuta mahitaji muhimu, hususani chakula na maji. Hali hiyo kwa ujumla wake imeongeza ukubwa wa tatizo la muingiliano wa binadamu na wanyamapori na kusababisha uwepo wa matukio mengi ya uharibifu wa mali na madhara kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia changamoto zilizopo, Wizara yangu kwa kushirikiana na halmashauri ya Wilaya ya Monduli, inaendelea kukabiliana na tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu kwa kufanya doria za udhibiti wa wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo kulingana na taarifa za uharibifu zinazowasilishwa na wananchi husika. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu ya njia mbadala ya udhibiti wa tembo na wanyamapori wengine katika Wilaya ya Monduli na maeneo mengine, mathalani matumizi ya uzio wa kamba zilizopakwa mchanganyiko wa pilipili na oili chafu, matumizi ya matofali ya kinyesi cha tembo kilichochanganywa na pilipili na mizinga ya nyuki kuzunguka mashamba ambayo tembo huogopa na kuondoka maeneo hayo. Sanjari na hayo, Wizara itaendelea kuelimisha wananchi kuhusu njia bora za kujikinga na wanyamapori wengine kwa kuhimiza ujenzi wa nyumba bora na imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta jasho na Machozi za Mwaka 2011, Serikali imekuwa ikitoa fedha kidogo za kuwafariji wananchi kwa kuwalipa kifuta jasho kwa uharibifu wa mali (mazao na mifugo) na

kifuta machozi kwa madhara kwa binadamu (vifo na majeruhi). Katika kutekeleza mpango huo, jumla ya shilingi 48,015,000 zililipwa kwa wananchi 251 wa vijiji vya Wilaya ya Monduli waliokidhi vigezo vya kulipwa kuanzia mwaka 2010 hadi mwezi Aprili, 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso kwa niaba ya Mheshimiwa Laizer.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kila mwaka wananchi wa Monduli wamekuwa wakipoteza mali lakini pia kupoteza maisha kutokana na uharibifu huu; na Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na takwimu ulizoziwasilisha hapa si kweli kwamba ni vijiji vyote vimelipwa. Kuna vijiji vya Moita, Naiti, Mswakini, Makuyuni na Isilalei wananchi hawa hawajalipwa fidia kwa mwaka 2014/2015, 2015/2016, 2016/2017. Je, ni lini sasa Serikali mtawalipa wananchi hao ambao wamepata uharibifu mkubwa na wamesubiri kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kanuni hii ya Kifuta Jasho na Kifuta Machozi ambayo imekuwa ikitumika kwa wananchi ambao kwa namna moja ama nyingine mazao yao au mali zao zimeharibiwa na wanyamapori katika nchi hii imepitwa na wakati na kwa kweli imewaletea wananchi usumbufu mkubwa sana kwa sababu wananchi hao mali zao zinaharibika kwa kiwango kikubwa na wanachokuja kulipwa hakilingani na uhalisia. Je, Serikali sasa haioni ni wakati mwafaka kuendana na hali ya sasa na thamani ya fedha ya sasa kubadili kanuni hii ili kulipa uhalisia wa uharibifu unaofanywa na wanyamapori?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba si vijiji vyote ambavyo

vimeshalipwa fidia. Hivi sasa naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba madai ambayo yamepokelewa kutoka katika wilaya mbalimbali hapa nchini yalifika takribani 15,370 na madai ambayo yameshalipwa tayari ni 6,185. Kwa hiyo, utaona kwamba kuna madai karibu 9,562 ambayo bado hayajahakikiwa na bado hayajalipwa, hivi sasa zaidi ya shilingi milioni 828 zinadaiwa. Kwa hiyo, baada ya zoezi la uhakiki kukamilika vijiji vyote hivyo vitapata fidia na kifuta machozi hicho ambacho tumekisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba hivi sasa tunafanya mapitio ya Kanuni za Kifuta jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011. Mara tu zitakapokamilika kupitiwa na kuidhinishwa, basi haya masuala yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema yataangaliwa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Boniphace.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, nimshukuru kwanza Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana, lakini kwa ujumla niwashukuru watu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Waziri na viongozi wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la wanyama waharibifu, hasa tembo, katika Jimbo la Bunda na kwa kata tatu ambazo zina vijiji 18 ni kubwa sana. Nikiangalia toka tuanze kulipa haya malipo ya fidia, ni mabilioni ya hela yanaenda na nimeona hapa tumekuwa na mikakati mingi, kuweka ukuta, kuweka pilipili na kuchimba mitaro na wengine huko vijijini kwenye Jimbo la Bunda wanasema tembo hawa hawana uzazi wa mpango, mnasema tembo wamepungua lakini ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza, ni lini sasa mikakati halisi ya Serikali itakuwepo ya kuzuia mnyama tembo ili kutoleta umaskini kwenye maeneo ya kwetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika eneo la Serengeti, na hasa katika Jimbo la Bunda kumekuwa na matatizo hayo na changamoto hizo ambazo zimekuwa zikijitokeza. Suala ni lini hasa tutakuja na mipango, sasa hivi tunakuja na mpango mkakati ambao tutausema tutakapokuwa tunawasilisha bajeti yetu ya mwaka 2018/2019, ni hatua gani ambazo tunategemea kuchukua katika maeneo mbalimbali ya Hifadhi za Taifa na maeneo mengine ya mapori ya akiba ili kukabiliana na changamoto hizi za wanyama waharibifu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba tu aendelee kutusubiri, pale tutakapowasilisha bajeti yetu basi atuunge mkono ilia one hizo hatua ambazo tunakwenda kuchukua ambazo ndizo zitakazokuwa suluhu ya changamoto mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Swali limetuchukuliwa muda mwingi sana. Tunaendela, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

Na. 75

**Miundombinu Mibovu Pori la Akiba Moyowosi/Kigosi**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Pori la Akiba la Kigosi Moyowosi linakabiliwa na tatizo sugu la kutokuwa na barabara za uhakika kwa ajili ya shughuli za utalii na doria.

(a) Je, ni lini Serikali italifufua greda aina ya katapila lenye namba za usajili ST 892 lililosimama kufanya kazi tangu mwaka 2015 ili lisaidie kukarabati barabara?

(b) Kwa kuwa gari aina ya *Grand Tiger* linalotumika kwa shughuli za utawala limekufa, je, ni lini gari hilo litatengenezwa au kuleta gari lingine ili lisaidie shughuli za utawala katika Pori la Kigosi Moyowosi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua umuhimu wa barabara na miundombinu mingine katika hifadhi zetu ili kuimarisha utalii na kufanya kazi za doria ipasavyo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali iliamua kufufua mtambo, hususani greda lililokuwa limeharibika kwa muda mrefu katika Pori la Akiba la Moyowosi Kigosi ili liendelee kutumika kuimarisha barabara zilizopo ndani ya pori hilo. Greda hilo aina ya katapila lenye namba za usajili ST 892 limetengenezwa na linafanya kazi.

Aidha, Wizara ipo katika harakati za kufufua gari aina ya *Grand Tiger* ambalo hutumika kwa shughuli za utawala katika Pori la Akiba Moyowosi Kigosi ambapo mafundi wameshafanya tathmini ya ubovu wa gari hilo na Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya matengenezo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Manyanda.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Kwanza niishukuru Serikali kwa kutengeneza hilo greda ambalo sasa kwa kweli litasaidia sana katika utengenezaji wa barabara kule kwenye Mapori yetu ya Akiba ya Kigosi Moyowosi. Sasa niombe kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia mapori haya ya akiba pesa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya barabara katika mwaka ujao wa fedha ujao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa gari la *Grand Tiger* sasa hivi limeharibika na mapori haya mawili ni

makubwa sana, je, Serikali iko tayari sasa kuyapatia haya mapori magari mawili kwa ajili ya kufanya doria na utawala katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa kazi kubwa ambayo umekuwa ukiifanya. Nakumbuka mwaka jana swali hilihili aliuliza na amekuwa akilifuatilia kwa karibu sana, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu tumeshalitengeneza lile greda sasa hivi tumeshatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati na kutengeneza miundombinu mbalimbali katika ile hifadhi. Kwa hiyo, pale bajeti itakapowasilishwa ataona ni kiasi gani tutakuwa tumetenga katika hilo eneo kwa ajili ya kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu maombi ya gari; ni kweli kabisa hili gari ambalo nimesema kwamba tunaendelea kulitengeneza bado lina changamoto na tutalifufua. Lakini kwa nyongeza zaidi naomba nikuahidi kwamba tutakuongezea gari lingine moja ili yakiwa hayo mawili basi yataweza kufanya kazi nzuri sana katika hilo eneo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Pori la Hifadhi ya Swagaswaga ambalo lipo karibu na Dodoma lina wanyama wengi na kwa kuwa Dodoma sasa ni Makao Makuu ya nchi. Je, Wizara haioni sasa ipo haja ya kuliimarisha pori hili ili liwe sehemu ya kivutio kikubwa cha utalii kwa wageni wanaokuja katika Mkoa wa Dodoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Nkamia...*(Kicheko)*

Kama ifuatavyo; samahani nimekosea jina lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba pori hili la Swagaswaga ni pori muhimu sana katika Mkoa huu wa Dodoma na hasa kwa kuzingatia kwamba sasa hizi hapa imekuwa ni Makao Makuu ya nchi. Kwa hiyo, tutachukua hatua mbalimbali za kuimarisha ili iwe ni kivutio cha utalii katika hili eneo na kuliwekea mikakati ya kutosha kusudi wananchi wengi ambao wanaishi katika Jiji hili la Dodoma waweze kutembelea katika hili eneo. Nikuhakikishie, kesho nitaenda kutembelea lile Pori la Mkungunero. Nikipata muda Jumapili nitapitia kwenye hilo eneo lingine ili tuone ni mikakati gani inaweza kufanyika tuweze kuimarisha utalii katika hili eneo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko halafu Mheshimiwa Marwa na Mheshimiwa Mukasa, wajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi narudi kwenye swali la msingi. Ikolojia ya Kigosi Moyowosi inategemea sana uwepo wa Mto Malagarasi. Mto huu uko kwenye kitisho kikubwa cha kukauka kwa sababu mifugo imekuwa ni mingi. *(Makofi)*

Je, Wizara mnafanya nini kuokoa chepechepe *(wetland)* ya Mto Malagarasi ambayo imevamiwa na ng'ombe wengi na mpaka leo kuna ng'ombe zaidi ya 100,000 kwenye *wetland* ya Mto Malagarasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jibu. Ni swali kidogo liko nje ya swali la msingi, lakini lijibu, wewe ni mtaalam.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Daniel

Nsanzugwanko. Naomba nimhakikishie tu kwamba katika lile eneo la Mto Malagarasi ni eneo muhimu sana kwa ajili kutoa maji na kusambaza katika maeneo muhimu kama ulivyokuwa umesema wewe mwenyewe. Ni kweli kabisa sasa hivi tunaweka jitihada, limevamiwa lile pori, kuna wanyama wengi, kuna mifugo mingi emeenda katika lile eneo, lakini lile eneo ni mojawapo ya maeneo ambayo yako kwenye *Ramsar sites.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi sasa tunakuja na mkakati wa kutosha kabisa wa kuweza kuhakikisha kwamba hatua ya kwanza ilikuwa ni kuweka vigingi katika mipaka yetu ile *Ramsar site.* Bado zoezi halijakamilika, litakapokamilika naamini kabisa tutakuwa tumekuja na ufumbuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili, nitumie fursa hii kabisa kwamba mifugo hairuhusiwi katika maeneo ya hifadhi zozote kwa mujibu wa sheria. Ndiyo maana tukikamata hiyo mifugo, kwa kweli tunaipeleka mahakamani na hatua kali zitachukuliwa kwa watu wa namna hiyo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutachukua hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba mifugo yote katika eneo hilo inaondolewa mara ili kuhakikisha huo mto unaendelea kuwepo na uendelee kutusaidia katika matumizi mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Marwa na Mheshimiwa Mukasa ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Katika hifadhi Serengeti *National Park* pamoja na Ngorongoro, hali ya barabara siyo mzuri na hususan kwenye kipande cha barabara kuanzia Ngorongoro getini mpaka lango la *Serengeti National Park* kuna udongo wa *Volcano* ambao hata watengeneze vipi, kwa muda mfupi unakuta ule udongo unaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haina mpango wowote wa kutengeneza ile barabara hata kwa kiwango cha zege ili kuondoa shida kubwa ambayo tunaipata watu tunaopita kwenye hiyo barabara?

**MWENYEKITI:** Wewe omba barabara, utaalam waachie Serikali. Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Heche kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Marwa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Marwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Marwa Ryoba.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampa hongera sana, amekuwa ni mdau mkubwa sana kwa sababu maeneo mengi, maliasili na hifadhi nyingi ziko katika eneo lake. Nafikiri nitakapokwenda kule, nitajua maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali inapitia maombi mbalimbali, inapitia utaratibu wa kuweka barabara ya kudumu ambayo inaanzia Karatu kupitia Ngorongoro mpaka Serengeti. Mara baada ya taratibu hizo kukamilika na *clearance* zote kufanyika, kwa sababu ni maeneo ya hifadhi, kumekuwa na mabishano makubwa juu ya aina ya barabara ambayo inatakiwa ijengwe.

Sasa hivi tumefikia hatua nzuri, makubaliano yanakuja na ninaamini kabisa kwamba baada ya muda mfupi tutaanza kuweka barabara ya kudumu ambayo ndiyo suluhu ya hilo tatizo ambao Mheshimiwa Mbunge amelisema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tumeshuhudia namna ambavyo Naibu Waziri anasisitiza kwa ukali kabisa kuchukuliwa hatua watu wanaoingiza mifugo hifadhini jambo ambalo ni sawa. Lakini anaongea kwa sauti ya chini na unyonge inapofikia kufidia mwananchi anayeharibiwa mazao na wanyama. Sasa kwa sababu Biharamulo asilimia 50 karibu ya eneo ni hifadhi na kwa sababu vijiji zaidi ya 15 kila mara wanaharibiwa mazao yao, yuko tayari twende tutathimini? Inawezekana akiona hali ile atajua namna Serikali ikae kutafuta namna ya kubadilisha *approach* ili tuwafidie wananchi badala ya kuwapa kifuta jasho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika maeneo yale ya Biharamulo sehemu kubwa ni hifadhi na kumekuwa na changamoto mbalimbali hasa zikiwemo hizo za mifugo pamoja na uharibifu na uvamizi katika maeneo haya ya vijiji. Naomba nimhakikishie tu kwamba niko tayari wakati wowote tupange twende tukaangalie tuone ni maeneo gani na tuone mikakati gani tunaweza tukaifanya kwa kushirikiana na Serikali tuone hatua za kuchukua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Haji Khatibu Kai.

Na. 76

**Matatizo Yanayowakabili Wavuvi wa Tanzania Katika Pwani ya Kenya**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imejenga tabia ya kufuatilia matatizo wanayopata

Watanzania wakiwa nje ya nchi hasa wavuvi ambao wanakwenda kuvua Pwani ya Kenya.

(a) Je, Serikali inatatua matatizo haya baada ya ufuatiliaji?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isishirikiane na Balozi zetu zilizopo Nairobi, Kenya ili kujua changamoto zinazowakabili wavuvi hasa Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, lenye kipengele (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matatizo yanayowakabili wavuvi wanaokwenda kuvua Pwani ya Kenya limekuwa likijirudia mara kwa mara. Hii inatokana na mwingiliano mkubwa wa wavuvi uliopo kutoka Tanzania na Kenya wanaouvua samaki kwenye Bahari ya Hindi. Wavuvi kutoka Pemba wamekuwa wakienda kuvua katika mwambao wa Bahari ya Hindi upande wa Kenya tangu mwaka 1960.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1976 yalifikiwa makubaliano kati ya Tanzania na Kenya ya kuruhusu wavuvi hao wanaokwenda kuvua nchi ya Kenya kwenda kuvua bila matatizo. Hata hivyo, kutokana na kujitokeza kwa changamoto za kiusalama na vitendo vya kigaidi, mamlaka za Kenya zimekuwa zikichukua hatua za kuwakamata mara kwa mara wavuvi siyo tu kutoka Tanzania, bali hata wale wanaotoka nchi za jirani. Ingawa wavuvi wa Tanzania wamekuwa wakikamatwa, huachiwa pindi mamlaka za Kenya zinapojiridhisha kwamba siyo tishio kwa usalama na kwa wavuvi hao na kama hao wavuvi wamefuata sheria na kanuni za nchi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni muhimu kwa wavuvi wa Tanzania wanaovua katika mwambao wa Bahari ya Hindi kuzingatia sheria zilizopo katika shughuli zao za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu maswali ya Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Mambo ya Nje kupitia Balozi zake ikiwemo ya Nairobi, Kenya, imekuwa na utamadumi wa kufuatilia matatizo wanayoyapata Watanzania wakiwa nje ya nchi ikiwa ni pamoja na wavuvi wanaokwenda kuvua Pwani ya Kenya.

Aidha, Wizara inaendelea kufanya mawasiliano na wadau wote ikiwemo Serikali ya Kenya, Ubalozi, Wizara za Kisekta husika ili kufikia makubaliano ya kudumu katika eneo hili. Wakati suala hili likiwa linatafutiwa ufumbuzi, napenda kutoa wito kwa wavuvi wetu kufuata sheria na taratibu za nchi husika ili wasiweze kupatwa na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inafanya kazi kwa karibu sana Ubalozi wetu Nairobi kwa sababu ndiyo inayowakilisha Tanzania nchini Kenya. Kwa kupitia wawakilishi hawa, Serikali inahakikisha changamoto wanazopata wavuvi hao zinashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika maelezo yake amekiri kwamba tatizo hili limekuwa likijirudia mara kwa mara; na kwa kuwa katika maelezo yake amejiridhisha kwamba wavuvi kutoka Pemba wamekuwa wakivua katika mwambao wa Bahari ya Hindi upande wa Kenya kutoka

mwaka 1960; na vilevile katika maelezo yake amejiridhisha kwamba mwaka 1976 Serikali ya Kenya na Tanzania ilifanya makubaliano juu ya wavuvi wa nchi hizi mbili:-

Je, ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kukaa na Serikali ya Kenya kupitia mkataba ambao niliuwasilisha hapa Bungeni ili kulipatia tatizo hili ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wavuvi hawa kabla hawajaenda kuvua katika bahari ya Kenya wamekuwa wakienda kukutana na Maofisa Uhamiaji, *Fisheries* pamoja na *BMUs* za sehemu ambazo wamekuwawakienda kuvua.

Je, ni kwa nini Serikali hii au ni kwa nini Serikali hii au Mheshimiwa Waziri asiwaambie wavuvi hawa leo ili wawe na matumaini kwamba tatizo hili litakuwa halijirudii tena mara kwa mara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema na kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, nimesema kwamba Serikali sasa imechukua hatua ya kuwasiliana na sekta husika ikiwemo Wizara za kisekta kwa maana ya upande wa Tanzania na upande wa Kenya na Balozi ikihusishwa ili kuweza kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto hiyo, siyo tu tunakaa, lakini pia katika kujadiliana ni pamoja na kupitia mkataba ule. Mkataba huu tunajua kwamba ulifanyika mwaka 1976 kabla ya kuvunjika kwa Umoja Jumuiya ya Afrika, kabla ya wa sasa hivi kuundwa upya. Ulikuwa ni wa zamani sana. Kwa hiyo, tumeona hii changamoto na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tumesema tumeanza mazungumzo baina ya wadau wote wanaohusika ikiwemo Serikali ya Kenya, Tanzania kwa maana ya Wizara za Kisekta pamoja na Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba wavuvi hawa kabla hawajaenda kuvua katika upande ule wa Kenya huwa wanakutana na Maofisa Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wamekwenda kuwaona Maofisa Uhamiaji, nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba sisi kama Wizara na tukiwakilishwa na Ubalozi wetu, tunapokuta hawa wametendewa ndivyo sivyo, tunashughulikia jambo hilo. Ila tunawaasa wale ambao wanakwenda kule bila kutumia uratatibu wa kisheria; na ndiyo hao ambao kwa sehemu kubwa wanapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nawaasa kwamba sheria na kanuni zifuatwe kwa sababu suala la kushughulikia uvuvi, kwa maana ya uvunaji wa mazao ya uvuvi hasa samaki, ni masuala ambayo ni makubaliano kati ya nchi husika yaani nchi mbili Tanzania na Kenya. Na sisi tutaendelea kusimamia kuona haki inatendeka kama wavuvi wetu wamefuata utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Kubenea na Mheshimiwa Jaku.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wavuvi kupata matatizo katika nchi za nje, inaendana na tatizo hili ambalo liko ndani ya Jimbo langu la Mtambile katika Kijiji cha Likoni na Chole upande wa Shehia ya Mwambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda wa miezi saba sasa wavuvi hao wako uko Pemba wamewekwa Gerezani, walifuata sheria na taratibu zote, lakini hadi leo wale ambao wanashughulikia wenzao ambao wako Gerezani wamefanya bidii kubwa ya kwenda katika Ubalozi wetu huko Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema nini na ina mkakati gani wa ziada kuhahakisha kwamba wale wavuvi wa Chole pamoja na Likoni wanaotendewa ndivyo sivyo wanapatiwa taratibu zilizo sahihi? Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Jaku na Susan Lyimo wajiandae. Maswali mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimniwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumetoka hapa, tukutane ili niweze kushughulikia hilo kwa karibu zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kubenea. Napenda hilo jibu sahihi kabisa la Kiwaziri na la Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Matatizo ya wavuvi wa Pemba yanafanana na matatizo ya wavuvi wa maeneo mengine ya kKusini mwa Tanzania vikiwemo Visiwa vya Mafia na Mtwara. Matatizo ya wavuvi pia yanafanana na matatizo ya wafanyabiashara wa Tanzania hasa wa malori ambao wanakamatwa katika nchi ya Congo.

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kulinda raia wake waliopo nje wanaopata matatizo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama tulivyosema katika nchi ya DRC Congo tuna Ubalozi wetu na Mabalozi wetu kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba

haki kwa ajili ya wananchi wa Tanzania walioko nje ya nchi inatekelezwa. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba watafanya kazi hiyo na huo ndiyo wajibu wao wa msingi, hatutawaacha na tumefanya hivyo siku zote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jaku na ajiandae Mheshimiwa Susan.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lake, alisema mazungumzo yamefanyika na Serikali ya Kenya. Namwomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri, mazungumzo hayo yamefanyika Tanzania au Kenya? Yamefanyika lini na yatamalizika lini ili wananchi wetu wapate nusura ya kutokuhenyeka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mazungumzo tunafanyia wapi, siwezi kueleza hapa kwamba tunafanyia wapi kwa sababu inategemea na sisi wenyewe tutakavyokuwa tumeamua. Nimesema mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali hizi zote pamoja na Ubalozi baada ya kujua kwamba hili tatizo linafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu ni kuhakikisha kwamba changamoto hii inatatuliwa. Mimi kama Serikali nataka kumhakikishia kwamba mazungumzo yameshaanza, sisi kama Wizara tayari tumeshawaandikia Wizara ya kisekta ambayo inahusika na uvuvi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tayari tumeshakubaliana kwamba sisi kwa upande wetu pamoja na Ubalozi wetu na Ubalozi wa Kenya tutashughulikia hilo jambo. Sasa tunafanya wapi? Hayo ni maamuzi ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan.

**MHE. DKT. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa swali la msingi linahusu matatizo yanayowapata Watanzania wakiwa nchi za nje; na ni kweli kwamba kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo makubwa, Watanzania wanakufa nje ya nchi, lakini unakuta wanaleta picha kwa mfano kutoka Marekani, watu wamekufa, watafutwe ndugu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua Serikali ina kanzidata *(database)* ya Watanzania wanaoishi nje ili angalau pale wanapopata matatizo iwe rahisi kufuatilia? Vilevile hii itasaidia pia *remittance* ya kujua ni watu wangapi wanaishi nchi za nje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Susan kwamba sisi katika Balozi zetu zote na sasa hivi zinafikia 40 kwa zile 35 za mwanzo, tumeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba kila Balozi anahamasisha wale *diaspora* wanaoishi katika nchi husika kuanzisha jumuiya ambazo zinatupa *record* za Watanzania wangapi wako huko na wanafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia hiyo *diaspora* tunaweza kujua kwamba huyu mtu yuko wapi na ni nani? Pale ambapo labda pengine Mtanzania ambaye yuko huku hajaweza kutoa taarifa zake kwenye Ubalozi ndipo tunapopata tatizo. Kule ambako tumeanzisha jumuiya na Watanzania ambao wamekwenda kutoa taarifa kwenye Ubalozi, tunakuwa tuna *data* zao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, suala la mazalia ya samaki yako Mafia. *Indian Ocean Tuna Commission* lazima sasa kuwe na mkakati wa kupata *royalty* kwa maeneo haya ambayo yanazalisha samaki, yanatunza

samaki na samaki hawa wanaenda kuvuliwa nchi nyingine mbali ya Tanzania. Hili nalo mlitazame mjaribu kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa utaratibu wake mpya wa kuingia ndani ya Bunge. Nimeona baadhi ya Wabunge waliokosa maswali ya *REA* wamekasirika na inawezekana kweli tukapigwa wakati tunatoka hapa kwa kukosa maswali muhimu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kutulinda. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni waliopo katika Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika na Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya ambao ni viongozi na watendaji 29 wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Mbeya na Wilaya zake wakiongozwa na Ndugu Jacob Asanwise Mwakasole, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya; Ndugu Wilson Nkahambuku, Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya na Ndugu Steven Mwakajumilo, Mjumbe wa *NEC,* Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Katika kundi hilo pia tunao Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Mbeya Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Humphrey Atanas Nsomba; Wajumbe wa Kamati ya Siasa - Wilaya ya Mbeya Vijijini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Hakim Mwalupindu; Wajumbe Kamati ya Siasa CCM - Wilaya ya Rungwe wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Sam Mwakapalala; Wajumbe wa Kamati ya Siasa wa Wilaya ya Chunya wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Noel Zinganinali Chiwanga; Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Mbarali, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Hashim Mwaliwaya na Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Kyela wakiongozwa na Katibu wao Ndugu Christina Alex Kibiki. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Sasa hii ziara ilikuwa Dodoma au ilikuwa mpango wa jana, Uwanja wa Taifa? Poleni sana kwa kufungwa. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watano wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni familia yake kutoka Liwale, Mkoa wa Lindi, ahsanteni; wageni sita wa Mheshimiwa Hasna Mwilima, ambao ni ndugu zake kutoka Marekani wakiongozwa na mke wa kwanza wa Marehemu Dkt. Aman Walid Kaborou aliyekuwa Mbunge na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kigoma, Mama Sarah Martin Kabourou, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Oscar Mukasa ambaye ni Katibu Mtendaji wa Idara ya Haki za Binadamu, Jimbo la Katoliki, Lulenga-Ngara Padre Anthony Likumulimo, karibu Bungeni; wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili ambao ni familia yake. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambaye ni mwalimu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha, Mwalimu Timothy Kasmiri; wageni 117 wa Mheshimiwa Ritha Kabati ambao ni wanafunzi na walimu wao kutoka shule ya sekondari Tagamenda kutoka Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni Dodoma; wageni wanne wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 40 na walimu 10 kutoka shule ya Viziwi iliyopo Mkoani Dodoma. Karibuni sana na hongereni; wanafunzi 25 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la simu ya *samsung* iliyookotwa kwenye Ukumbi wa Msekwa kwenye kikao kilichopita. Aliyepoteza simu hiyo muda huo, amuone Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja Katibu. Subiri.

Waheshimiwa Wabunge, mlipewa Mwongozo jana kuhusu Kanuni zetu. Mheshimiwa Mwalimu, Mheshimiwa Frank, Mheshimiwa Jaku na Mheshimiwa Kubenea. Mheshimiwa Jaku karibu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa ruhusa hii na kuwa mtu mwanzo kuomba Mwongozo.Tunategema kumaliza hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora. Nimesimama kwenye Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza, hotuba inayofuata, Mungu akituweka hai na uzima ni hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inakwenda na kasi ya kujenga viwanda na kiwanda huwezi kujenga bila mazingira na mazingira yanahitaji muda. Kwa siku moja tu tuliyowekewa ni siku moja ndogo sana na nilipata harufu kwa mbali Muungano na Muungano tuko wengi tunataka kuchangia na wengi kilichotuleta hapa ni Muungano. Kuna hatari ya kuja kupewa watu sita au saba, kiti hakitatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huruma. Kuomba siyo kosa, kuiba ni kosa. Mtufikirie kutupa angalau siku mbili. Nahitaji mazingatio ya kiti chako na mwongozo wako. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunazungumza hapa mara nyingi ndani ya Bunge hili kwamba wapo watu ambao wamepewa mamlaka ya kusimamia Halmashauri; Wakurugenzi lakini pia Wakuu wa Wilaya katika Wilaya zao, imekuwa ni shida na tatizo sana kwa wananchi wetu. Hivi sasa ninavyozungumza, tangu jana soko la Mji wa Tunduma limefungwa bila sababu yoyote ya msingi. Ni kwa sababu tu Mkurugenzi pamoja na Mkuu wa Wilaya wameshindwa kufuata mkataba ambao umeingiwa kati ya wafanyabiashara na Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naomba pia Serikali itoe maelezo ya kutosha ili wananchi wale waweze kujua nini kitakachoendelea kwa baadae? Kwa sababu taharuki kubwa iliyotokea kwenye Mji wa Tunduma inaweza ikasababisha uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka jana hakuna biashara yoyote inayoendelea, lakini pia hakuna makusanyo yoyote yanayoendelea kwenye Mji wetu wa Tunduma. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ajaribu kutoa maelezo kutokana na jambo hili ili wananchi wa Tunduma waendelee na maisha yao ya kawaida. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mwalimu Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kanuni ya 68(7) naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo gazeti hapa la Nipashe la leo ambalo katika ukurasa wa nane, kichwa cha habari kimeandikwa, "Spika abadili njia akihofia kurukiwa."

**MWENYEKITI:** Hebu sema tena.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** "Spika abadili njia akihofia kurukiwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka kupata Mwongozo wako kwamba yale maelezo ya jana ya Spika yaliyotolewa hili neno "kurukiwa" sikulisikia na ilionesha tu kwamba ni utaratibu wa kawiada wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, yanaweza yakaamua kubadili njia wakati wowote na hakuna njia rasmi iliyotajwa kwenye Kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakati unamalizia, na wewe mwenyewe umeridhika, umetamka kwamba kumbe hii njia kubadilishwa imesaidia kwamba kuna watu wana hasira humu, wanaweza wakawarukia kwa kukosa maswali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate Mwongozo wa Kiti, kama hali ya usalama Bungeni ni ya namna hii, imefikia kuwa hata Spika anaweza akaogopa Wabunge wake akabadili njia; na njia yenyewe ninayoiona, pembeni kumejaa watu wa CCM, yaani ndiyo wenzake walio wengi wa chama chake. Sasa nikawa najiuliza, tunakaguliwa kwenye mashine nyingi sana, bado tuna tahadhari kubwa kiasi hicho!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lazima liende sambamba na yale ambayo tumeyazungumza kwamba hali ya usalama nchini siyo nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka. Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) na kwa hoja hiyo

hiyo ambayo Mheshimiwa Mwalimu Bilago ameizungumzia sasa hivi kwamba utamaduni wa Bunge letu kwa ufahamu wangu toka Bunge la Mheshimiwa Mzee Msekwa, limekuwa na utamaduni wa Spika au Wenyeviti wa kuongoza Bunge wanapita hapa mbele; na kwa utamaduni wa sasa na maneno ambayo umeyaeleza sasa hivi, watakuwa wanapita nyuma. Tayari kuna hisia ambazo zimeanza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii juu ya utamaduni huu mpya na ambao tayari umeandikwa kwenye Gazeti la Nipashe na wewe umelisema sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwamba utamaduni huu mpya ambao utalifanya siwa na ile hadhi ya Spika ya kuingia ndani ya Bunge, haupunguzi hadhi ya Bunge letu; na kwamba utamaduni huo unafanana na nchi zipi katika Jumuiya ya Madola?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naanza kwanza na Mheshimiwa Kubenea na baadae Mheshimiwa Bilago. *(Kicheko)*

Kwanza Bunge halifanyikazi na magazeti, la kwanza, lakini la pili, *ruling* ya Spika ametoa jana na Mheshimiwa Kubenea na Mheshimiwa Bilago ni Wabunge wageni, hamjapata uzoefu wa Mabunge mengine. Nendeni mkajifundishe Mabunge mengine.

Mheshimiwa Spika, jana ameeleza vizuri tu hapa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sasa si najibu jamani, mbona mnaanza kunirukiarukia? Subirini. Mtakaa chini sasa hivi hapa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, *ruling* ya Spika haihojiwi na mtu yeyote. Ametoa mfano wa India na Uingereza. Kwa hiyo,

*ruling* ya jana ni *firm* na haibadilishiwi na ndiyo jibu langu na Mwongozo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jaku, kwanza hakuna harufu ya jambo lolote. Mara nyingi dhana hizi zinaleta mpasuko mwingi sana. Ratiba hii inapangwa na Kamati ya Uongozi wa Bunge na viongozi wengi wa pande zote mbili ni Wajumbe wa Kamati hii ya uongozi.

Kwa hiyo, ratiba hii imesimama na ndivyo itakavyokuwa, *unless* kutakuwa na mabadiliko ambayo yatafanywa na mtajulishwa.

Mheshimiwa Frank kuhusu soko lenu, Serikali wamesikia na wao ni sikivu, watalifanyia kazi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Anatropia ajiandae. Mheshimiwa Ruth Mollel dakika kumi na Mheshimiwa Anatropia dakika tano. Mheshimiwa Ruth Mollel hayupo, Mheshimiwa Anatropia dakika tano.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa pole kwa changamoto

ambazo viongozi wa kisiasa wa CHADEMA wanapitia. Muda nilionao ni dakika tano, sitaongea mengi, lakini natoa pole sana na ninaamini katika dhana ya utawala bora watu wengi wanaweza kuongea na wanaelewa nini maana ya utawala bora kama tuna viongozi na Wabunge zaidi ya 15 wa Vyama vya Upinzani wanatakiwa kuripoti polisi karibu kila wiki. Salamu zimefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nishangae Wizara na utamaduni mpya walioanzisha wa kujibu eti hotuba ya *CAG*. Nitaongelea TAMISEMI, mfano waliojibu jana na wakatoa taarifa kwamba mapendekezo aliyoyatoa *CAG* wameyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kufukuza watumishi takribani 4000 na nimei-*quote* vizuri ambao walituhumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kwa mujibu wa *CAG* kwenye *report* aliyoitoa kuna mapendekezo aliyatoa mwaka 2000. Katika kalenda hii ya mwaka 2014/2015 alitoa mapendekezo 15 lakini mpaka mwaka 2017 mapendekezo yenyewe 14 yalikuwa hayajafanyiwa kazi. Kuanzia mwaka 2014/2015 mpaka 2017 aliyoyatoa juzi ndiyo mnaanza kuyajibu kwenye *television.* Inashangaza sana. Ninachoweza kuwaambia, nendeni mkafanyie kazi mapendekezo aliyoyatoa na siyo kwenda kujibu kwenye *television.* Mna kazi kubwa ya kufanya, nendeni mkaangalie upungufu aliouainisha kwenye Wizara zenu, kwenye Serikali za Mitaa ili mtuletee majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kusikitika kwa kuambiwa makusanyo ya Serikali yanapanda kwa asilimia 90 huku Halmashauri zetu mpaka mwezi wa sita mwaka 2017 zikiwa zimepelekewa asilimia 49 tu ya fedha zilizohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ina upungufu wa asilimia 68; Halmashauri ya Kibondo upungufu wa asilimia 88 na Halmashauri ya Kigamboni, upungufu wa asilimia 86. Halafu tunakuja humu Wabunge wenzangu wa CCM mnapongeza. Halmashauri zetu zimepelekewa asilimia 49 tu ya fedha za

maendeleo. Tutabaki kusifiana hapa, lakini mwisho wa siku tutaona aibu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nitaliongelea ni Wakuu wa Wilaya kukosa *instruments.* Hii nai-*associate* na kazi wanayoifanya Wakuu wa Wilaya na Mikoa, wanawakilisha wanaliowatuma. Tumeona mfano mdogo au mfano mkubwa niseme, anachokifanya Mkuu wa Mkoa wa sasa aliyepandishwa, baada ya kutumiwa na CHADEMA kununua Madiwani, akapandishwa kuwa Mkuu wa Mkoa. Sasa ameenda mbali zaidi, anajitangaza hadharani kwamba atawabagua watu wa CHADEMA, atawabagua watu wa upinzani kwa sababu yeye anafanya kazi kwa Ilani ya CCM na hawezi kufanyakazi kwa Ilani ya CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napigia msitari, kwa vile anamwakilisha mtu fulani ambaye ni Rais, kauli ya Mkuu wa Wilaya au kauli ya Mkuu wa Mkoa ni kauli ya Mheshimiwa Rais, kwa hiyo, na sisi tunaweza kusema na hiyo ni kauli ya Rais *unless* kuwepo na kanusho la kauli aliyoitoa Mnyeti kwamba atazidi kuwabagua wapinzani katika maeneo anayoyaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa mbalimbali za fedha kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali zimeonesha upungufu mkubwa sana, mfano, Halmashauri ya Bukoba Mjini ilikuwa na takribani shilingi milioni 60 kwenye madaftari, lakini fedha haijapalekwa benki. Halmashauri ya Kigoma-Ujiji ina zaidi ya shilingi milioni 219 katika daftari, lakini fedha hazijapelekwa benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inaonesha upungufu mkubwa sana na tunakimbilia kujibu kwenye magazeti, nadhani twende kwenye Halmashauri husika tuone chamgamoto ni ipi? Tufanyie kazi mapendekezo yanayotolewa na *CAG,* vinginevyo hatuna haja ya ku-*allocate* fedha kwa *CAG* kama mapendekezo hatuwezi kuyafanyia kazi, tunakwenda kuwajibu waandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa kama nitafanikiwa kulimazilia ni kutotengwa kwa asilimia 10 kwa ajili ya wanawake na vijana kwenye Halmashauri. Nimesikia Mheshimiwa Waziri mmoja hapa akisema na zile asilimia 10 zitakuwa hazitolewi riba, lakini kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali anaonesha takribani Halmashauri 164 hazijatenga asilimia hiyo 10 kwenda kwa vijana na akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui mnavyosema kwamba mnaondoa riba, mnaondoa katika kitu ambacho hakipo? Ni lazima tukae vizuri, tujipange. Kama kweli TAMISEMI iko *serious* inataka Halmashauri zitenge hiyo fedha, iandae *account* maalum katika kila kiasi kitakachokusanywa, basi hiyo asilimia ipelekwe kwa...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel dakika kumi. *(Makofi)*

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ambazo ziko hapo mezani. Kwanza nichukue nafasi kuwapongeza Mawaziri wote wawili na Naibu Mawaziri wao na watendaji wote walioifanya hii kazi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na tamko ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi kuhusu kurudishwa kwa wale watumishi waliomaliza darasa la saba ambao walikuwa wamefukuzwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe masikitiko yangu kwamba tangu awali hawa watumishi hawakutakiwa kufukuzwa kazi, kwasababu waliajiriwa kwa kigezo cha darasa la saba na mikataba yao ilikuwa ya darasa la saba. Kwa hiyo, hawakustahili kufukuzwa kazi na kwa kweli hiyo haikuwa sahihi na Serikali haikuwa sahihi. Sasa wamerudishwa kazini, tukumbuke wamekuwa nje ya utumishi wa umma karibu mwaka mzima, imesababisha familia hizi kupata matatizo ya kifedha, manyanyaso na kutokuwa na *income*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, pamoja na kwamba Serikali imesema walipe mishahara yao yote, lakini je, katika ule usumbufu ambao wameupata kwa muda mrefu karibu mwaka mzima, Serikali inasema nini kuhusu hilo la kuwafidia kwa sababu ya kupata shida kwa kukosa kazi wakati walistahili kuwepo kazini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala linalofuata ninalotaka kuchangia, ndiyo wote ambao walikuwa na vyeti vya darasa la saba wamerudishwa, lakini kuna wale madereva kwa mfano ambao walikuwa darasa la saba na hawakutolewa kazini, lakini kuna madereva ambao walikuwepo kabla ya Mei, 2004 lakini kwa sababu ya shinikizo la kupata vyeti, baadaye walikwenda wakapata vile vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tamko la Mheshimiwa Waziri ni kwamba wale wote ambao waliajiriwa kabla ya hiyo Mei, 2004 kile kigezo cha *form four* hakiwahusu. Kwa hiyo, wanatakiwa wote warudishwe. Napenda kujua, sasa hawa madereva kwa mfano, ambao walikuwepo kabla ya Mei, 2004 lakini baadae ikabidi watafute vyeti, kwa sababu wengine wakwenda kujaribu *form four,* wameshindwa, wakaenda kutafuta vyeti. Je, wanarudi pia? Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee tamko kwa sababu sijaiona kama ameizungumzia katika tamko lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu hawa walioanza kazi baada ya Mei, 2004, ni kweli wameingia kwa vigezo ambavyo siyo sahihi, wamegushi vyeti ambayo kisheria siyo sawasawa, nasi hatuungi mkono, lakini pia ukitazama kwa upande mwingine, wamekuwa wanachangia kodi, *NSSF,* wengine ni *PSPF*, wengine ni *Local Government Provided Fund (LGPF);* je, Serikali inatoa kauli gani kuona kwamba hawa watumishi kweli pamoja na kwamba wame-*forge* vyeti ambayo sio sahihi, lakini pia wamekuwa wanakatwa kodi, wamekuwa wanachangia hifadhi ya jamii? Je, Serikali haioni ni sahihi basi kwa hawa watumishi angalau walipwe basi makato yao ya hifadhi ya jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali langu la nyongeza, alieleza kwamba kulikuwa na majadiliano kati ya Serikali na Vyama wa Wafanyakazi kuhusu jinsi gani ya kufanya ubinadamu kwa ajili ya ku-*compensate* hawa ambao wamefukuzwa kazi kwa makosa ya kughushi vyeti. Napenda kujua hayo majadiliano yamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia watumishi ambao wametumia majina ya watu wengine kusoma, wengine wamepata udaktari, wengine wamemaliza u-*nurse,* wengine wamefanya ualimu; wamesoma hizo *courses* na wamehitimu, lakini kwa majina ya watu wengine. Napenda kusikia tamko la Mheshimiwa Waziri anasema nini juu ya watu hao? Kwa sababu tunao watu ambao wamesoma kwa maina ya watu wengine na ni watu wakubwa na wako kazini, kusiwepo na *double standard.* Lazima Serikali ionekane inatenda haki kwa watu wote bila ubaguzi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sasa kwenye suala la watumishi wa umma kutofungamana na itikadi za kisiasa. Hili jambo nilishalizungumzia siyo mara moja, wala mara mbili na ninaendelea kulizungumza. Labda ni-*declare interest* kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa mtumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na watumishi ambao wanafungamana na itikadi, kuwa na watumishi ambao wakiwa katika utumishi wa umma wanajihusisha na mambo ya siasa kunadidimiza *impartiality* ya utumishi wa umma, inaua *professionalism.* Tunataka utumishi wa umma wafanye kazi zao kwa kuzingataia *professions* zao kwa ajili ya kuendeleza Taifa hili na kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za watumishi wa umma kujiingiza katika siasa ni kukosa *continuity* katika utumishi wa umma. Kwa sababu utumishi wa umma ndiyo *institutional memory* ya nchi. Ikiwa tunakuwa na watumishi katika ngazi za juu ambao wanaletwa wakiwa kwenye

Vyama vya Siasa inaharibu kabisa *integrity* ya utumishi wa umma. Tunaona mahali kama Japan, kila mara Mawaziri Wakuu wanaondoka, wanakuja, lakini utumishi wa umma unakuwa *intact* kwa sababu hauhusiani na chama chochote. Utumishi wa umma unatakiwa utekeleze sera za chama kilichoko madarakani *with impartiality*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtindo wa sasa hivi wa Awamu ya Tano ya kuingiza watu wenye mambo ya siasa kwenye utumishi wa umma, tunaua hiyo *integrity* na tuta-*suffer* kama nchi na itabidi kuja kufanya marekebisho makubwa sana. Kwa hiyo, ni maoni yetu kwamba Serikali sasa iangalie upya na turudi tulikotoka. Enzi zetu watumishi wa umma walikuwa hawaruhusiwi kujihusisha na siasa kabisa wanapokuwa watumishi wa umma. Wakitaka kujihusisha na siasa, watoke katika utumishi wa umma waende wakahangaike na siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la nyongeza za mishahara na kupandishwa vyeo. Watumishi wa umma ndio *engine of growth* ya nchi hii. Awamu hii ya Tano sioni kabisa kama Serikali iko *serious* na kuangalia rasilimali watu. Naona haiko *serious* kwa sababu tangu wameingia madarakani watumishi wa umma hawapati nyongeza zao za mshahara ambayo ni haki yao; hawapandishwi ngazi zao za mishahara, malimbikizo yao bado hayalipwi yakamalizika, kila siku ni hivyo hivyo na maneno mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kuwa na Utumishi wa Umma wenye raha unaojiamini, kwa kweli hata hii dhana ya Tanzania ya Viwanda hatuwezi kuifikia. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa kweli iweze kuangalia rasilimali watu, watumishi wapandishwe vyeo vyao, wapate *increments* zao ambazo wanastahili kwa sababu hizo *increments* za kila mwaka ndiyo zinawasaidia kupunguza makali ya *inflation* katika uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye suala la elimu. Sijaona kama kuna mnyororo mzuri. Tunazungumzia

viwanda, ni jambo zuri; tunazungumzia *standard gauge;* tunazungumzia *Stigler's Gorge;* lakini hatuzungumzii rasilimali watu ambayo itakuja kufanya hizo shughuli. Nikiangalia kwenye mnyororo wa elimu na nimesikia kwamba Serikali ina-*train* walimu wengi wa sayansi na teknolojia, ni jambo zuri. Kama Serikali ina-*train* walimu wa sayansi na teknolojia, ni mkakati gani basi unawekwa kuhakikisha kwamba maabara katika shule za sekondari zinakuwepo kusudi hawa Walimu wanapotoka kufundishwa sayansi na teknolojia, waende hata kwa vitendo kwenye *laboratories* katika vyuo vyetu. Kwa sababu malengo yote ya sayansi na teknolojia ndiyo ambayo inakuwa *complement* katika hiyo Tanzania ya viwanda. Huu mnyororo uendelee mpaka chuo kikuu, uendelee... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maftaha na ajiandae Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hizi mbili za Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia, kunipa afya njema na leo hii niweze kuchangia Wizara hizi ipasavyo. Naomba nianze moja kwa moja na Wizara hii ya TAMISEMI na hasa katika eneo hili la Mipango Miji, kumekuwa na matatizo makubwa sana kwenye suala la upangaji miji. Leo hii tunapopita kwenye Halmashauri zetu na hasa kwenye miji midogo na miji mikubwa katika suala la kupanga ardhi ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo baya ambalo naweza kulisema hapa, watu ambao wanashughulika na upangaji wa ardhi, wanafanya mambo ya ajabu sana kwa wananchi wetu wa Tanzania. Unaweza ukakuta wakati

wanaenda kupima ardhi, wanapima kwa bei kubwa sana, wananchi wa kawaida hawapati ahueni ya kupimiwa viwanja vyao mpaka uweze kuwa na pesa za kutosha. Hii ni kwa sababu gharama zimekuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Jafo kwa kazi nzuri anayoifanya, ahakikishe kwamba Halmashauri zetu hizi zinapewa vifaa vya kupima ardhi na maeneo yaweze kupimwa kwa viwango ambavyo vinastahiki, lakini mwisho wa siku, kiwango kinachotumika kupimia ardhi, basi hata unapotoa fidia, iweze kulingana na viwango halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kuna maeneo yanaweza yakapimwa, lakini kukawa na *double allocation* yaani leo hii kiwanja kimoja kinapewa watu zaidi ya watatu, maeneo mengine kiwanja kimoja watu wanne. Hili ni jambo kubwa sana na kuna changamoto kubwa na migogoro mingi ya ardhi kwenye miji yetu kutokana na sekta hii ya ardhi kwenye Halmashauri, lakini hasa kwenye miji yetu midogo na mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo suala la elimu. Elimu ni jambo ambalo tumekuwa tunazunguza sana kwenye bajeti zetu zote hapa, kwamba maeneo mengi, shule nyingi za mijini na vijijini hazina madarasa ya kutosha. Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba *enrolment* ya wanafunzi wa darasa la kwanza sasa hivi imefikia asilimia 101. *Enrolment* imekuwa ni kubwa sana, kwa hiyo, madarasa hayatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukifika Mtwara Mjini unaweza ukashangaa sana. Shule ina wanafunzi zaidi ya 660, madarasa yaliyopo ni matatu. Shule ya msingi Mbae, watoto 650, madarasa matatu. Kwa hiyo, naomba sana, Wizara ya TAMISEMI ihakikishe inajenga madarasa, inapeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu ili madarasa yaweze kujengwa ili tuweze kuendana na kasi hii ya *enrolment* ya wanafunzi iende sambasamba na idadi ya madarasa tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakati tunasoma wakati ule miaka ya 1990 kule mwanzoni, ilikuwa ukifika shuleni asubuhi ni lazima ukimbie mchakamchaka. Leo hii mchakamchaka haupo, watoto hawafanyi mazoezi. Hata michezo mashuleni imedorora sana. Nalizungumza hili kwa sababu, wakati fulani nilikuwa Mkuu wa Shule Mchinga sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michango mingi sana, inapofika suala la UMISETA na suala la UMITASHUMTA, yaani badala ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya michezo, wanawabebesha Wakuu wa Shule pesa zile ndogo ambazo ni za maendeleo, wanaambiwa wachangie kwa ajili ya michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA. Mkuu wa Shule anakuwa kama kaibeba shule kichwani kama shule yake mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, TAMISEMI itenge pesa za kutosha, zipelekwe mashuleni kwa ajili ya kugharamia michezo. Tunaamnini watoto wakifanya michezo, wakikimbia mchakamchaka asubuhi, wakicheza mpira, *brain* zao zinakuwa na uwezo wa kufikiri sawa kuliko hali ilivyo hivi sasa. Suala la michezo ni suala muhimu sana. Michezo ni afya, michezo ni burudani, michezo ni furaha, michezo ni ajira. Vipaji vingi vinapotea kwa sababu hatuwekezi vya kutosha katika ngazi za Shule za Msingi na Sekondari. Uhakikishe Mheshimiwa Jafo unatenga pesa za kutosha kupeleka mashuleni kwa ajili ya kugharamia UMISETA na UMITASHUMTA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala ambalo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza sana kuhusu posho za Madiwani kwamba hazitoshi. Nami naungana nao. Vilevile posho za Wenyeviti wa Mitaa, unaweza ukashangaa Halmashauri nyingine hizo posho hazipo kabisa. Wenyeviti wa Mitaa wanafanya kazi kubwa sana. Wenyeviti wa Mitaa wanahudumia wananchi sana. Tunaomba sana kwamba posho za Wenyeviti wa Mitaa zipelekwe, ziongezwe, iwekwe sheria maalum, waweze kupewa posho ambayo angalau inafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hali iliyopo Wenyeviti hawa wanapata posho kulingana na maeneo na makusanyo ya Halmashauri. Ukija kwa mfano pale Mtwara, Mwenyekiti wa Mtaa mwezi mzima analipwa shilingi 20,000 tu, ni jambo la ajabu sana. Huyu Mwenyekiti wa Mtaa anahudumia wananchi usiku na mchana, halafu mwisho wa siku, mwezi mzima analipwa shilingi 20,000 kwa hisani ya Halmashauri. Naomba sana tuweke utaratibu wa kutosha kabisa, Wizara ipeleke fedha iweze kuwahudumia Wenyeviti hawa wa Halmashauri kwa sababu wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miradi ni jambo ambalo linashangaza sana. Pesa za kuendeleza miradi haziendi katika Halmashauri zetu. Unaweza ukaangalia ukipitia randama hapa kwa mwaka mzima zimeenda 15% au 16%, ni jambo la ajabu sana. Miradi yetu haiendi kwa sababu pesa hazipelekwi kule kwenye Halmashauri. Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri Jafo kwa sababu tunakufahamu sana, ni katapila, utenge pesa za kutosha zifike Halmashauri ili miradi yetu hii iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine, kwa mfano pale kwangu Mtwara, siku moja *DC* alimuuliza Mkurugenzi kwamba tunataka tukakague miradi ya Halmashauri. Mkurugenzi hana miradi, pesa hazijaenda, anamwambia miradi iliyopo hapa ni Miradi ya Mfuko wa Jimbo tu, ya Mbunge. Twende tu ukakague ujenzi wa kupumzikia wagonjwa pale zahanati na maeneo mengine, lakini Halmashauri miradi imesimama kwa sababu pesa hazifiki. Ni jambo la ajabu sana, tulikuwa tunaomba pesa zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya Halmashauri pesa ziweze kufika na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni afya. Hili ni jambo muhimu sana, kwamba tunaekelezwa sasa hivi kwamba dawa zile tunaita *tresa medicines* zinafika asilimia 94 kwa taarifa za Waziri anavyosema. Bado ukiingia kwenye hospitali na zahanati zetu, tunaambiwa dawa hazitoshi ama dawa hazipo. Leo mgonjwa anatoka huko anaenda

hospitali anaambiwa dawa zimeisha. Bado tatizo lipo sana, tunaomba Mheshimiwa Waziri kama ni tatizo la watendaji basi tunaomba lichukuliwe hatua ipasayo, lakini kama ni tatizo kwamba tunaambiwa pesa zipo, dawa zipo kumbe kule pesa hazijafika, hili nalo ni tatizo lingine. Tunaomba sana kwamba dawa ziweze kupatikana kama taarifa zinavyoelezwa kwamba iwe kweli aslimia 94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la dawa zile maalum ambazo ni za kifua kikuu, ziko dawa za *HIV* na kisukari. Hizi dawa zinatolewa kwenye Hospitali za Mikoa tu, hospitali ambazo zina *specialists.* Ukipita kwenye vituo vyetu vya afya au kwenye zahanati zetu hakuna hawa *specialists* na zile dawa hazitolewi na mtu mwingine, hata yule *Medical Assistant* haruhusiwi kutoa zile dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana, kwa sababu wagonjwa hawa wako wengi sana, wako huko vijijini mbali, wanatembea umbali mrefu sana tunaomba hizi dawa zipatikane kwenye zahanati zetu, zipatikane kwenye vituo vya afya. Kama *issue* ni mafunzo, basi hata wale *medical assistant* kwa sababu wanaokoa maisha ya Watanzania sana, wapewe mafunzo ya kutoa hizi dawa, isiwe tu pale kwenye *specialist* kwenye Hospitali za Mikoa ambazo ziko mbali sana na wananchi. Tulikuwa tunaomba sana hili liweze kupewa upekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la barabara kwenye miji yetu imekuwa changamoto sana. Watu wa *TARURA* wamekuwa ni Mungu watu. Leo ukienda kumwuliza mtaalam wa *TARURA,* ukimwomba mtaalam wa *TARURA* aje kutoa ufafanuzi kwa wananchi ambao anawatumikia, anakuwa hawataki, yaani wako pale kama Miungu watu.

Kwa hiyo, naomba kuwe na usimamizi, sheria hizi ziweze kurekebishwa sawasawa. Hawa watu wa *TARURA* kwa sababu wanawahudumia wananchi wa kawaida, wanahudumia Watanzania, basi waweze kusimamiwa na Madiwani, waweze kusimamiwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati nafanya mikutano ya hadhara pale Mtwara, utamaduni wangu ni kuhakikisha kwamba Wakuu wa Idara wanakuja kutoa ufafanuzi kwa sababu wanawatumikia wananchi, wapo kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. Wote wanakuja, lakini Wakuu wa Idara wa *TARURA* hawataki kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, kama wapo kwa ajili ya wananchi, basi wahakikishe ya kwamba wanawatumikia wale wananchi. Madiwani na Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi. Sasa leo tunashangaa sana kusikia kwamba eti Diwani haruhusiwi kumuuliza mtu wa *TARURA* nini kinaendelea. Mtu wa *TARURA* akiulizwa, anasema mimi sisimamiwi na Diwani wala na Mbunge. Sasa wanafanya kazi kwa ajili ya nani? Tulikuwa tunaomba sana, hawa watu wa *TARURA* wawajibike kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakibete na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami fursa niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara TAMISEMI. Kabla ya yote, kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye ametupa nafasi na tumeweza kuamka salama na kufika ndani ya Ukumbi huu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya katika nchi hii ya Tanzania; na amekuwa *role model* pia wa Marais wengine wa Afrika na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo kusahau, niendelee kuwashukuru Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa namna wanavyofanya kazi vizuri. Kipekee sana, nakushukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Jafo, Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI kwa kazi nzuri na kubwa unayoifanya, nawe ukiwa kijana, umekuwa *role model* pia kwa vijana wenzako. Tunakushukuru sana na pongezi, tumeona namna ambavyo

unapambana kila kona. Vilevile kwa kusaidiwa na wasaidizi wako; Naibu Mawaziri Mheshimiwa Kandege pamoja na Mheshimiwa Kakunda pasipo kuwasahau Watendaji wote wa Wizara hii TAMISEMI, kwa maana ya Katibu Mkuu - *Engineer* Iyombe, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Zainab pamoja na wengine wote na Wakurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite zaidi katika suala zima la *TARURA.* Kwanza naipongeza Serikali kwa kuanzisha chombo hiki cha *TARURA.* Kimekuwa msaada mkubwa sana kwetu Wabunge tunaotoka majimbo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwamba *TARURA* pamoja na kwamba imeanzishwa, lakini bajeti yake ni ndogo kwa maana ya kwamba ina urefu mpana zaidi na uchumi mwingi unatoka vijijini na malighafi nyingi zinatoka kule, lakini bajeti yake ni ndogo. Asilimia 30 kwa 70 kwa maana ya *TANROADS,* hii hakika hawataweza kufanya kazi yao na kufikia lengo tulilokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu kwamba kama itaridhia kupitia Waziri Mpango baada ya kuleta bajeti yake ya Wizara ya Fedha, ingekuwa asilimia 50 kwa 50 tuna uhakika kwamba chombo hiki cha *TARURA* kitaweza kufanya kazi zake sawa sawa na vile ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, kuna changamoto mbalimbali katika Jimbo langu la Busokelo. *TARURA* hii baada ya kuanzishwa mwaka 2017 tuna mahusiano mazuri sana na wale *managers* pamoja na *coordinators* wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mahusiano hayo, barabara ambazo ziko ndani ya Jimbo langu kwa mfumo ambao sasa hivi tuko nao ni kilometa 475 kupitia *District Roads Management Systems (DROMAS)* ambako ndiko zinakuwa *updated* barabara zote 475. Bajeti ambayo

Halmashauri yangu inapata ni shilingi milioni 600.6. Sasa unaweza ukapiga mahesabu hapo kwamba kilometa 475 kwa shilingi milion 606 siyo kitu. Kwa msingi huo, kwa bahati mbaya sana pia hizi fedha ambazo zilipangwa bajeti ya mwaka 2017/2018 hazijakwenda kama ilivyokusudiwa, kwa maana ya kwamba imekatwa nusu kwamba alipe madeni ya zamani kwa maana ya kwamba ile mipango ambayo tulikuwa tumepanga kwa barabara zote hadi hivi ninavyosema, haijaweza kutekelezeka kwa sababu fedha hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naliomba pia Bunge lako Tukufu kwamba kwa umoja wetu hii *TARURA* lazima ipewe fedha nyingi za kutosha. Zaidi pia katika hizi barabara, kuna barabara ambazo hadi sasa hivi ninavyozungumza, wananchi wangu wamenipigia simu tangu juzi, wengine jana kwamba kuna kata ambazo hakuna mawasiliano kabisa. Kuna Kata za Mpata, Isange, Kandete, Rufilyo na maeneo mengine mbalimbali ndani ya jimbo langu, hakuna mawasiliano kabisa kwa maana ya hizi mvua zinazonyesha sasa hivi kipindi hiki cha msimu wa mvua, kumekuwa na changamoto hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yetu kwa sababu ni sikivu, wale *managers* wanapokuwa wanaomba fedha za dharura wapelekewe kwa haraka zaidi kwa sababu kunakuwa hakuna mawasiliano kabisa ya wale wananchi, maana wanaishi kama kisiwa. Wakiwa kama kisiwani maana yake hawawezi kufanya chochote. Ikumbukwe kwamba Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ile tunayoiita *big four* ambayo inazalisha sana *raw materials* pamoja na chakula katika nchi hii. Kwa hiyo, kama hakutakuwa na uwezekano wa kusafirisha mazao yanayozalishwa kule kuja mijini, maana yake hata huku mijini pia tutapata taabu kupata hayo mahitaji tunayohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika jambo hilo hilo la *TARURA,* naiomba Serikali, kwa kuwa Mkoa wa Mbeya, hasa Wilaya za Rungwe, Chunya pamoja na Busokelo, zinapata mvua karibu mwaka mzima, zaidi ya milimita 2,000 kwa

mwaka, tungetamani sana kama suala la kutangaza zabuni kwa wakandarasi zingeanza mwezi wa saba na wa nane ili wa tisa mkandarasi aanze kufanya kazi na wa kumi awe kazini, wa kumi na moja amalizie kazi. Ingetusaidia zaidi, kuliko sasa hivi wakandarasi wengi wamekimbia *site* kwa sababu mvua zinanyesha usiku na mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la afya. Afya ni uzima na roho. Kwa kweli kipekee sana Mheshimiwa Jaffo nikupongeze tena sana, niipongeze sana Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo mmejenga vituo vingi vya afya katika nchi hii ya Tanzania. Historia itandikwa kwamba kipindi fulani ndipo tulijenga vituo vingi vya afya. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, nipongeze pia suala zima katika Halmashauri yangu ya Busokelo, nimeona mmetutengea bajeti ya shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya. Ninawashukuru sana katika jambo hili. Pia ikumbukwe kwamba katika maombi ambayo tuliomba, kuna kituo kimoja najua Mheshimiwa Jafo atakifanyia kazi, kinaitwa Isangi. Tulishaandikiwa barua na Mheshimiwa Waziri wa Afya, lakini hadi leo hii fedha hazijaingia. Ninaamini utalifuatilia na tutaweza kupata fedha hizi ili tuweze kuendelea kufanyia kazi hicho kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la jengo la Halmashauri. Tunashukuru Halmashauri yetu mmeipa shilingi 2,300,000,000 kwa ajili ya kukamilisha jengo. Tunawashukuru sana katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie kuhusiana na suala zima la utumishi. Watumishi wetu katika Halmashauri ya Busokelo limekuwa na shida na changamoto kubwa. Tuna upungufu wa watu takribani 516 katika Halmashauri yetu, kwa maana Halmashauri ni changa na watumishi 516 ni wengi kwa maana hawapo kazini. Wengine ndio hao wamefukuzwa na wengine hawana vyeti. Kwa hiyo,

tunaiomba Serikali kwamba maombi maalum ambayo Mheshimiwa tulikupelekea uweze kuyafanyia kazi na bahati nzuri mzee wangu nilikupelekea uweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, hatuna. Ofisi hii ilijengwa tangu mwaka 1930. Kwa maana hiyo, nazishukuru sana Kamati zote za Bunge ambazo zimepita pale, ninyi ni mashahidi. Kuna Kamati ya *PAC,* lakini pia Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii, mmeona jengo lile kwamba limekuwa la miaka mingi. Tuiombe Serikali, tunajua kwenye mwaka huu hamjatenga fedha, lakini tukuombe Mheshimiwa Waziri kwamba mwakani tuweze kujenga Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikizingatiwa kwamba Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo pato lake la Taifa sasa hivi ni Mkoa wa pili baada ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, ni vizuri tungeweza kuuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala zima la mifumo ya *computer.* Mimi nikiwa mdau, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia mifumo mingi ya *computer* na wana mifumo mingi kweli kweli. Niwapongeze sana kwamba sasa nchi yetu inaenda katika digitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeweza kutoa mapendekezo ama maono kwa maana ya moja, mifumo hii mingi baadhi yake inatoka nchi za nje. Tuna-*import*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu, ajiandae Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo, lakini pia niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika Wizara hii, Ofisi ya Rais, (Utumishi) lakini pia Ofisi ya Rais, (TAMISEMI). Kwanza nawapongeza Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Mkuchika kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na wasaidizi wao, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Kakunda, lakini pia Katibu Mkuu Ndugu Iyombe, Mzee Ndumbaro pamoja na watumishi wote kwa kazi nzuri na ngumu ambayo wanaifanya, lakini kwa kuhakikisha kwamba huduma hii ambayo Watanzania wengi wanahitaji na ambapo ndiyo *engine* nzima ya Serikali, wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niishukuru TAMISEMI kwa niaba ya wananchi wote wa Halmashauri ya Babati kwa fedha tulizopewa kwa ajili ya Kituo cha Afya Ngaiti. Tunashukuru sana, ni kituo ambacho kiko pembezoni na huduma ile itawasaidia watu wengi sana. Tumepata shilingi milioni 400 na kituo kinakaribia kukamilika, pamoja na ahadi ya shilingi milioni 200 kwa ajili ya vifaa, lakini pia fedha za *P4R* pamoja na *ambulance* kwa ajili ya Kituo cha Afya Magogo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Jafo pamoja na timu yako nzima.

Pia tulikuwa na ombi kwamba Kituo cha Afya Magugu pale kinahudumia siyo tu Kata ya Magugu ya watu 30,000, lakini pia Tarafa nzima pamoja na baadhi ya nje ya Tarafa na pale ni *highway,* ikiwa ni pamoja na baadhi ya watu wa Babati Mjini. Tunaomba iongezewe bajeti kwani kile siyo Kituo cha Afya, kile kimekaribia kufanana na hospitali na idadi ya watu wanaotibiwa pale bajeti ikiongezwa itaweza kutoa huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiombea Hospitali ya Mrara pale Babati Mji kwa sababu na yenyewe pia inaendelea kuhudumia watu wengi wa Babati Vijijini, lakini pia sasa hivi Mji wa Babati unakua kwa kasi sana na ni *highway* baada ya kufungua hii barabara kutoka Dodoma kwenda Babati na ile ya Singida. Sasa hivi magari mengi yanapita pale na pindi ajali inapotokea, hospitali ile huwa inazidiwa.

Pia nilikuwa naomba wakati tunapopanga bajeti na baadhi ya miradi, pawe na uwiano kutokana na idadi ya kata na vijiji, kwa sababu kama tunagawa sawa kwa Wilaya zote, unakuta Wilaya kama yangu, Halmashauri yangu ina kata 25, vijiji 102 lakini kilometa za barabara kule ni zaidi ya 1,000 zinazohudumiwa na *TARURA* lakini mgao wa fedha tunaopata unakuta ni sawa na yule ambaye ana robo ya watu wetu, halafu robo ya kata na vijiji. Kwa hiyo, huo uwiano ninaamini kabisa mkijipanga, mtaenda vizuri. Pia nilikuwa naomba kwamba fedha zile za *CDG* tulizoahidiwa za maendeleo kwa mwaka 2017/2018 zije mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa naomba kwenye suala la *TARURA* naipongeza Serikali kwa kuanzisha chombo hiki baada ya Wabunge wengi kukisemea, lakini kama wenzangu wote walivyounga mkono kwamba tunaomba fedha zile asilimia za mfuko wa barabara badala ya kwenda asilimia 30 kwa 70 kama ilivyo sasa, basi iwe 50 kwa 50 ili *TARURA* iweze kufanya kazi yake vizuri. Pamoja na hiyo, tuendelee kuipatia *TARURA* rasilimali watu pamoja na nyenzo nyingine ili kazi yao iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la maji, nilikuwa naomba kwamba Wakala wa Maji Vijijini uanzishwe mapema. Mmeahidi kwamba mpaka mwezi wa Saba itakuwa tayari lakini bado naendelea kusisitiza kwamba ile shilingi 50 tuliyoomba kwa kila lita ya mafuta iendelee kuongezewa ili mfuko ule utune ili suala la maji liende vizuri. Vile vile pamoja na hayo yote, Serikali iendelee kufikiria kwamba bado kwenye suala la maji kuna vifaa kwa mfano vya kuchimba visima vya maji. Ile mitambo inapokuja inakuwa na kodi kubwa. Serikali ingeangalia namna ya kufuta kodi kwenye mitambo wakati inaingia, lakini wakati inapofanya kazi iendelee kutozwa kodi ili mitambo iwe mingi na watu wengi, huduma zisogee katika Wilaya zote na Mikoa yote ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye suala la maji, nilikuwa naomba Serikali iendelee kuangalia suala la *e-water,* mita za maji ambayo inatumia mfumo huu wa kielektroniki.

Babati Vijijini ni eneo la mfano, tayari tuna vijiji vitatu ambapo inaenda vizuri sana na wananchi wote wamezoea kutumia njia hiyo. Tukifanya vizuri naamini kabisa tatizo na changamoto hii ya maji inaweza ikaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu sana, naomba kwa sababu Ofisi ya Rais ndiyo ina Wizara zote hizi mbili ya Utumishi pamoja na TAMISEMI, mwangalie suala la watendaji, yaani kada ya chini, ngazi ya kijiji na kata, watumishi wote wanaohitajika huko, mhakikishe mnatoa vibali vya kutosha ili watendaji kwa mfano wa vijiji, kada ya afya, wale wa sekta ya kilimo wale wote ambao wanatakiwa ngazi ya kata na vijiji wawe wametosheleza badala ya kujaza huku juu. Kwa sababu tukiwa na Watumishi huku juu, ngazi ya Wilaya na Mkoa na huku Taifa na huko chini hakuna na maendeleo yote yanaenda kufanyika kule, unakuta fedha nyingi tunapoteza kwa sababu *OC* zinatolewa za kutosha, lakini kule chini hakuna mtu wa ku-*monitor.*

Kwa hiyo, tungejaza huko chini ambapo huduma ndiyo inakotolewa na mishahara yao ni midogo. Mtu mmoja huku juu ukimwajiri, anaweza kuajiri watu wanne kule chini. Kwa hiyo, mwajiri huko chini wa kutosha halafu huku juu watu wafanye kazi kwa ufanisi zaidi. Lingine ambalo nilikuwa naomba ni suala la kukaimu. Suala hili tungejitahidi pawe na kiwango maalum, kama ni miezi mitatu, isizidi hapo. Baada ya hapo mtu awe amethibitishwa ili ajiamini afanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuangalia *performance.* Siku hizi suala la mtu anavyo-*perform* na utendaji wake, haiendani na shughuli ambazo tunazifanya. Kwa hiyo, naomba tuendelee kuangalia katika sekta nzima ya utumishi katika *performance* ya watumishi ili kutokana na hiyo basi, wawe wanapandishwa madaraja, lakini pia wawe wanalipwa kutokana na *performance* ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la posho za Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji na Mtaa. Najua Serikali haina uwezo wa kuwalipa, kwa nini tusiwe na mfumo

ambapo Madiwani wakikaa huko kwenye vijiji, wakifanya kazi nzuri wakaongeza mapato zaidi kutokana na mapato ya ndani, basi waweze kupatiwa posho zao, posho ziongezeke. Utaona mtu kwa sababu ya *incentive* atakuwa anafanya kazi kubwa zaidi na wataongeza mapato ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hilo pia tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ilikuwa ni suala la Sheria hii ya Manunuzi. Tumefanya vizuri sana, niwapongeze hasa TAMISEMI, mmesimamia vizuri suala la *force account* kwenye sekta ya afya na elimu, imeenda vizuri. Ninaomba hiyo pia mwendele kutumia kwenye maji na pia kwenye *TARURA...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Martin Msuha, ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia na mimi katika hotuba hizi mbili za Mawaziri hawa. Kwanza kabisa, namshukuru Mungu sana kwa ajili ya Tanzania, amani na utulivu uliopo. Namshukuru Mungu sana kwa Rais Dkt. Magufuli na Serikali yake nzima kwa ubunifu wanaoutumia katika kuhakikisha kuwa wanathubutu kuingia katika mikakati mikubwa ya kuiletea maendeleo Tanzania kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumshukuru Rais Dkt. Magufuli kwanza kwa ahadi zake ambazo amekuwa akizitimiza kama sehemu ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kipekee nataka kusema kuwa namshukuru Rais Dkt. Magufuli na Serikali yake kwa sababu kubwa sana kwa ajili ya Ileje. Nataka itambulike kuwa Ileje ni Wilaya Kongwe na imekuwa nyuma kwa miaka mingi sana. Sasa kwa miaka miwili na nusu Ileje inakua kwa kiasi ambacho watu hawawezi hata kuamini. Wale wanaoijua

wilaya ile wanakubaliana nami. Mimi naomba kwa heshima na taadhima nipige magoti hapa. Magoti yangu ni mabovu, lakini naomba kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alikuja akatuahidi barabara ya lami ambayo imepiganiwa karibu miaka 40 na sasa inajengwa kwa kiwango cha lami. Nina kila sababu ya kushukuru kwa sababu miaka 42 unangojea barabara ya lami ya kwanza katika Wilaya, kwa nini nisishukuru? Hivi ninavyozungumza tumepata fedha ya kwenda kumalizia Hospitali ya Wilaya kubwa ya kisasa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja akaweka jiwe la msingi, alijionea mwenyewe jinsi ambavyo ile hospitali itakavyokuwa. Tulikuwa tunatibiwa Malawi, sasa watu watatibiwa Wilayani kwangu Ileje. Tumeenda kupata vituo vya afya viwili na magari yake ya wagonjwa. Hii ni Wilaya ambayo ilikuwa imesahauliwa, kwa nini nisiseme ahsante kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi? Sasa hivi tunaenda kujengewa kituo cha forodha mpakani mwetu na Malawi na Zambia, hii vilevile ni juhudi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ina mpaka mrefu sana karibu kilometa 108 na hizo hazina doria ya aina yoyote, hazina ulinzi wa aina yoyote. Wahamiaji haramu wengi wamekamatwa kule, wengine wamekufa kwenye mabonde yetu kule kwa sababu barabara zetu ni mbaya sana na wengine hawazijui wanapita usiku kutaka kuingia nchi za jirani wanakufa. Tunahitaji sasa gari ya doria, lakini ile barabara itakapojengwa Kituo cha Forodha nacho kikijengwa tuna uhakika Ileje itapanuka kiuchumi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishukuru Serikali kwa miradi mikubwa ya maji inayojengwa Ileje. Ileje tunakunywa maji ya matope. Tuna vyanzo vingi vya maji, tuna mvua nyingi, lakini miradi ya maji ilikuwa hakuna. Sasa hivi tuna miradi mingi ya maji, mmoja mkubwa sana unajengwa pale Isongole, utakaokidhi haja ya shida ya maji yote ya maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru vilevile kuwa sasa hivi *TARURA* wameweza kwa kiasi kikubwa kumudu barabara zetu za milimani ambazo zilikuwa hazipitiki kipindi chote cha mvua. Kipindi hiki japo kidogo watu wanaweza kuwasiliana. Hizi zote ni pongezi na shukrani kwa watu wa Ileje kwa ajili ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeweza kututazama na sisi kwa jicho *special. (Makofi)*

Vilevile nataka kuishukuru Serikali kwa sababu tunaenda sasa hivi kujengewa barabara zinazounganisha vijiji kwa vijiji, kata kwa kata kwa kutumia *TARURA.* Ilikuwa unatoka kijiji kimoja inabidi upite kata nyingine kurudi kwenye kijiji cha Kata yako. Huo ulikuwa ni usumbufu mkubwa na kwa jiografia ya kwetu, hiyo ilikuwa ni adha kubwa lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaenda kutujengea. Ninachotaka kuomba sasa, tunaomba kwa haraka sana tupatiwe gari ya doria kutokana na kwamba sasa hivi uhalifu wa mpakani umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa vilevile tusaidiwe kuongezewa pesa *TARURA;* barabara zetu sisi na jiografia zetu ni ngumu mno; na kwa kuwa ni Wilaya ya pembezoni na ina changamoto nyingi, basi tuangaliwe kwa jicho la huruma zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vilevile kwa *REA.* Ileje ilikuwa ni Wilaya iko gizani lakini *REA* sasa hivi imefunguka. Leo hii unasikia watu wa Ileje wanalalamika mbona leo umeme umekatika? Tulikuwa zamani hatuzungumzii mambo ya umeme, kwa sababu hatukuwa nao. Naishukuru sana Serikali kwa juhudi zao. Naomba hili zoezi la *densification* kwa ajili ya kuhakikisha miradi ya *REA II* inakamilika lifanyike haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa watumishi; na yote hii inachangiwa vile vile na jiografia yetu. Wengi hawapendi kuwa kule, wengine wakija wanatoroka. Tuna upungufu wa watumishi kwenye sekta ya elimu na afya zaidi ya 580. Tunaomba sana zoezi la kuajiri litakapoanza basi na sisi watufikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna tatizo kubwa Kiwira. Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira uko Ileje na nasikitika kwa miaka yote uliokuwa ukifanya kazi Ileje haijafaidika kwa sababu, kwanza ulikuwa unahesabiwa kwamba ni wa Kyela. Mradi ule sasa hivi unatambulika kuwa ni wa kwetu na tunaambiwa kuwa, *STAMICO* wameuchukua na wameshaanza majaribio ya kuchimba makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua sasa mustakabali wake ni upi maana hatujasikia Mkandarasi aliyepatikana ni nani na atauendesha vipi. Tunaambiwa bado kuna mambo ya kupata ile hati ya kukabidhiwa, haijakabidhiwa na yule aliyekuwa mwekezaji wa huko nyuma. Tunaomba hili lifanyike haraka ili wananchi wetu wapate ajira na ule mgodi utuletee faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna daraja pale ambalo limeharibika la kilometa saba ambalo ndiyo linaunganisha Kiwira na Ileje. Sasa hivi inabidi unataka kwenda Kiwira uzungukie Kyela kutokea Kiwira mgodini, hiyo siyo hesabu nzuri kiuchumi. Tunaomba sana hili daraja la kilometa Saba tu lijengwe, ili sasa Ileje na mgodi wake wa Kiwira viunganishwe moja kwa moja kwa mawasiliano. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani ya bajeti ya TAMISEMI pamoja na ya Utumishi na Utawala Bora. Nami niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu Mawaziri wake, pia, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la uhaba wa watumishi katika sekta ya afya. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, ina jumla ya zahanati 42, ina vituo vya afya viwili ambavyo vinahitaji watumishi wa kada mbalimbali

wapatao 324. Waliopo hadi sasa hivi wanaohudumia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ni 112 tu na kufanya upungufu wa watumishi 212. Kwa hiyo, niiombe Wizara iangalie ni namna gani ya kutupatia watumishi ili kuboresha utoaji wa huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbinga walikamilisha ujenzi wa vituo vinne kwa maana ya zahanati za kutolea huduma za afya na hivyo kufanya kuongeza uhaba wa watumishi katika Halmashauri yetu. Zoezi hili lilimlazimisha Mkurugenzi wa Halmashauri yetu ya Mbinga Vijijini kuwatoa watumishi ambao walikuwa wanahudumia kwenye vituo vya afya vinavyomilikiwa na Kanisa Katoliki ili waende kuhudumia hospitali hizi ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilileta mvutano mkubwa sana na kuharibu mahusiano kati ya Jimbo letu la Mbinga, pamoja na uongozi wa Halmashauri. Tunaiomba Wizara ili kurudisha uhusiano huu angalau ituletee watumishi 22 ili zahanati hizi Nne ziweze kufunguliwa na kurudisha mahusiano ambayo yanaelekea kuharibika kati ya Jimbo letu Kuu la Mbinga pamoja na uongozi wa Halmashauri kutokana na mvutano wa hawa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilishapelekwa ofisini kwa Katibu Mkuu wa Utumishi na nina imani atalifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili zahanati hizi nne ziweze kufunguliwa na kutoa huduma zilizokusudiwa. Sambamba na upungufu huo wa watumishi wa Wizara ya Afya tunao upungufu wa watumishi wapatao 755 katika sekta ya elimu kwa ujumla wake. Kwa hiyo, tunaiomba pia, Wizara iangalie ni namna gani inaweza kutuletea watumishi katika sekta ya elimu kwa maana ya sekondari na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wamekuwa wakishukuru sana hapa kwamba, wamepatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya afya, lakini Mbinga Vijijini hatujaletewa chochote mpaka sasa hivi. Nina imani Waziri amepitiwa tu au amejisahau, naomba aangalie

ni kwa jinsi gani ambavyo hata Mbinga Vijijini atatukumbuka ili na tuweze kuletewa fedha kwa ajili ya ujenzi, aidha upanuzi wa vituo vya afya katika Wilaya yetu ya Mbinga. Hususan tunaomba fedha kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya afya vifuatavyo: Kituo cha Afya Matiri, Kituo cha Afya Mapera na Kituo cha Afya Kindimbachini, angalau nasi tuwe na vituo vitatu vya afya katika Halmashauri yenye Kata ishirini na tisa (29). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Serikali kwa kuniletea fedha kwa ajili ya ukarabati wa sekondari kongwe ya Kigotera, ujenzi wa madarasa manne, ofisi mbili za walimu na vyoo 10 katika Shule ya Msingi Maguu. Niishukuru Serikali kwa kuniletea vyumba nane vya madarasa na vyoo 20 katika mtaa wangu ninaotoka wa Msingwa, Kata ya Msigani, Wilaya ya Ubungo ambako mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo tunayo maombi maalum. Tunazo sekondari zetu tano ambazo ziko kwenye mpango wa kupandishwa hadhi kutoka kwenye sekondari za kawaida kwenda kwenye *A – Level.* Kwa hiyo, tunaomba Wizara ituangalie namna gani inaweza kutu-*support* katika kuzipandisha hadhi sekondari zifuatazo: Sekondari ya Hagati, Sekondari ya Mkumbi, Sekondari ya Mahilo, Sekondari ya Langiro na Sekondari ya Kiamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamalizia na suala la *TARURA.* Tunaipongeza Serikali kwa kuunda *TARURA,* ni imani yetu kubwa sana chombo hiki cha *TARURA* kinaenda kutatua matatizo yote ambayo tulikuwa tunakumbana nayo hasa Wabunge wa Majimbo ya Vijijini. Barabara zetu zilikuwa hazihudumiwi kwa kiwango ambacho ni cha kuridhisha kutokana na usimamizi ambao ulikuwa si mzuri kutoka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyochangia Wabunge wenzangu, tumeona *TARURA* ina-*cover* kilometa laki moja na kidogo, bajeti yake bado ni finyu. Kwa hiyo,

naiomba Serikali ione uwezekano wa kutenga huu Mfuko wa Barabara, *Road Fund* asilimia 50 kwa 50 ili kuiwezesha *TARURA* iweze kufanya kazi zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Meneja wa *TARURA* Mbinga. Nilipokuwa ziara mwezi wa 11 aliweza kunipa Mhandisi wake nikazunguka naye Jimbo zima ili kubainisha changamoto zilizoko kwenye upande wa usafiri. Pia, tulibaini kwamba, kuna barabara ambazo zinahitaji matengenezo ya haraka, nyingine zinahitaji kuwekezwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali kupitia Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbinga kwa maana ya *TARURA,* waangalie barabara itokayo Mapera kwenda Mikalanga, inaishia Ilela, barabara hii haijapitishwa *grader* tangu uhuru. Pia, waangalie njia ambayo inahudumia watu wengi na eneo ambalo linazalisha pia njia pacha kutoka Ngima hadi Ukiro pamoja na madaraja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana niiombe Wizara kupitia *TARURA* Ubungo iiangalie Barabara inayotoka kwa Musuguri mpaka kwa Unju ambayo inaunganisha Ilala, pia barabara inayounganisha Maramba Mawili kuunganisha barabara inayotoka Mbezi kwenda Kinyerezi. Barabara hii inahudumia watu wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la ushauri. Barabara zetu zimepewa *code number* ambapo barabara hizi baada ya kupewa *code number* zinaingizwa kwenye mfumo wao wa *dromas,* nashauri kwamba *TARURA* waangalie uwezekano wa kuzi-*grade* hizi barabara kupewa namba kutokana na maeneo yetu ya utawala, kwa maana kwamba wafuate kama ni Kata, ifuate mtaa au kitongoji, ili wasimamiaji tuweze kufuatilia kwa rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukipewa *network* ya barabara kwa mfano ya Jimbo langu la Mbinga unaikuta barabara namba moja inatoka kwenye Kata nyingine, namba mbili inatoka kwenye Kata ambayo ni ya mbali sana.

Inatufanya ufuatiliaji wa hizi barabara kuwa mgumu. Kwa hiyo, nashauri *TARURA* wapange hizi *codification* kutokana na maeneo yetu ya utawala iwe rahisi kufuatilia kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara moja kule Mbinga ambayo ilikuwa inajengwa kwa ufadhili wa *EU,* barabara hii ilikwama kutokana na changamoto walizopata za udongo. Barabara hii inatoka Longa inakwenda mpaka Litoho. Niliambiwa kwamba, barabara hii imechukuliwa na *TARURA.* Niiombe sasa Serikali itenge fedha za kutosha, ili barabara hii imalizike kipande cha kutoka Longa hadi Kipololo ambapo ndipo changamoto kubwa ilijitokeza, lakini pia, niiombe Serikali iunganishe kipande cha kutoka Mbinga Mjini hadi Longa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Japhary Michael, Mheshimiwa Pendo Peneza, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, wajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hizi mbili zilizoko mbele yetu za Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia afya na uzima na ambaye amenipa nafasi hii. Pia, niungane na wananchi wa Jimbo la Ngara, Watanzania, wanajumuiya ya *UDOM* kuonesha masikitiko yangu makubwa kumpoteza kijana Paschal Deogratius Mboyi, ambaye amefariki dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana huyu mwaka jana akiwa Chuo Kikuu cha *UDOM* aliandika kitabu chake cha Diwani ya Pakacha Limetoboka, kitabu ambacho nilimkabidhi nakala yake Waziri wa Elimu na ilikuwa katika mchakato wa kuona namna gani kinavyoweza kuingizwa

kwenye *syllabus* kwa sababu ni vijana wachache sasa ambao wana vipaji. Kwa hiyo, niungane na Watanzania wote kusikitika kwa ajili ya kumpoteza kijana mahiri huyu katika wakati wa ujana na alikuwa na maono makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge wanaopongeza, aisifuye mvua maana yake imemnyea, imemnyeshea au imemnyea yote sawa. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya. Mvua hii ya kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais, mimi na wananchi wa Jimbo langu la Ngara imetunyeshea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata takribani bilioni 1.4 kwa ajili ya upanuzi wa vituo viwili vya afya, Kituo cha Afya Murusagamba, Kituo cha Afya Mabawe, kwa maana ya milioni 400 kwa ajili ya miundombinu, milioni 300 kwa ajili ya vifaatiba, milioni 700 kwa kila kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata milioni 226 kwa ajili ya miradi ya maji ya vijiji 10, lakini Mheshimiwa Rais mwenyewe mwaka jana alitupatia milioni 13 *cash* wakati amekuja Ngara kwa ajili ya kununua *pump* ya maji na milioni 24 tumepata kwa ajili ya maboresho ya huduma za maji. Mwaka jana huo nilimwomba mradi mkubwa wa maji kutoka kwenye vyanzo vya mito, Mto Ruvuvu, Mto Kagera na Mlima Shunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwenye bajeti inayokuja ya maji, kwa taarifa niliyonayo, tunategemea kupata karibu milioni 200 kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu wa mradi huo. Nina kila sababu ya kumpongeza, kuwapongeza Watendaji wa Serikali kwa maana ya Waziri, Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye elimu. Wengi wamechangia na wamesema kwenye elimu, lakini mimi nitaomba nijikite pia kwenye upande wa elimu maalum na watoto wenye vipaji maalum. Nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru Watanzania ambao wamemuunga mkono

kijana wetu Anthony ambaye amesambaa kwenye mitandao ya kijamii nchi nzima na nje ya nchi, anatoka Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wote ambao wameshiriki katika kuchangia kumwezesha ili kijana huyu ambaye ameonekana kuwa na kipaji maalum aweze kuendelezwa. Kwa namna ya kipekee pia, nimshukuru Ndugu Isaack Msuya, ambaye amekubali kumchukua kwenye shule yake anayoimiliki ya Mwanga kumsomesha kijana huyu, pia, wadau wote ambao kwa namna moja ama nyingine wameshiriki katika kumchangia mtoto huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto. Najua kwamba, tumekuwa na shule zenye vipaji maalum, shule hizi ni za sekondari japo nazo pia hazitoshi kama vile Mzumbe Sekondari, Kilakala, Weruweru, Ilboru, Kibaha, shule zisizozidi saba, lakini hatuna shule za msingi, sidhani kwenye *record,* nimejaribu kupitia kwenye mitandao ku-*google,* lakini sijaona kuna mahali ambapo tuna shule za msingi zenye vipaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi za msingi ndizo ambazo zinaweza kulea watoto hawa ambao wana vipaji maalum na tukawekeza kwenye watoto hawa ili kusudi tuweze kuwa na wataalam waliobobea wanaoweza kuleta mabadiliko pia ya kweli na kwenda sawa na kasi ya Mheshimiwa Rais kuwa na uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwamba hii ni changamoto sasa, hivyo tuangalie uwezekano wa kuanzisha shule zenye vipaji maalum, sambamba pia na shule kwa watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kwa watoto wenye ulemavu hasa katika kupata elimu ni kubwa. Nilikuwa nikizunguka kwenye Jimbo langu, wapo watoto takribani mia mbili na kitu ambao wako vijijini na kila nilipokuwa nikipita wanauliza wazazi kwamba, kuna mkakati gani kwa ajili ya kuboresha au kuwapatia elimu hawa watoto wenye

ulemavu. Tunayo Shule ya Msingi Murugwanza ambayo imeanza programu hii japo katika mazingira magumu, lakini niombe Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuona ni namna gani ambavyo tunaweza tukaunga mkono jitihada hizi ambazo zimeanza katika Jimbo la Ngara, hususan katika shule ya msingi Murugwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa *TARURA. TARURA* naiunga mkono kwa asilimia 100. *TARURA* iliundwa kwa maksudi thabiti ya kutaka kuboresha huduma za miundombinu ya barabara kwenye vijiji na miji. Kumekuwepo na ulinganifu kuona jinsi ambavyo Halmashauri zetu zilikuwa zinasimamia programu hii ya matengenezo na ukarabati wa barabara na jinsi ambavyo *TANROADS* wamekuwa wakifanya. Ukijaribu kuangalia asilimia 30 ambayo Halmashauri ilikuwa ikipata ndiyo hiyo ambayo *TARURA* nao wanapata, sasa sitegemei kwamba, kuna kiti kinaweza kikafanyika tofauti kama hatutaweza kuongeza bajeti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jiandae Mheshimiwa Japhary Michael dakika 10, Mheshimiwa Pendo Peneza dakika tano, Mheshimiwa Grace Kiwelu dakika tano na Mheshimiwa Magdalena Sakaya dakika 10.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Nami nichukue fursa hii kupongeza kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Waziri anafanya, Waziri wa TAMISEMI na Naibu Mawaziri wake. Naamini kwamba ana Naibu mzuri ambaye amebobea kwenye mambo ya Serikali za Mitaa, huenda anaweza akamsaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na hayo yote niliyosema ya kumpongeza Waziri, pamoja na jitihada ambazo Waziri anaonekana kufanya, lakini nina hofu kwamba, dhamira ya Serikali hii ya Awamu ya Tano ni kutengeneza Serikali za Mitaa dhaifu, kufanya Halmashauri

zetu ziwe dhaifu na kwenda kinyume kabisa na dhamira ya maboresho ya Serikali za Mitaa yaliyofanywa tangu 1998 mpaka mwaka 2014 na Serikali ya Awamu ya Tatu na Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa sababu *theory* zote zinaonesha kwamba, Serikali zote ambazo zinataka kufanya kazi kama zinavyotaka huwa zinahakikisha kwamba Serikali za Mitaa zinakuwa dhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo sote tuko hapa tunalalamika jinsi ambavyo Wakuu wa Mikoa wanaweza wakaziingilia Serikali za Halmashauri. Tunalalamika jinsi ambavyo Wakuu wa Wilaya wanaweza wakaziingilia Halmashauri kwa sababu ya dhamira inayoonekana yenye mwelekeo wa kufanya yale mawazo yote ambayo yaliwekezwa fedha nyingi sana ya kufanya maboresho ambayo yangezipa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ni mamkala kamili katika maamuzi katika rasilimali yanakuwa hayana nia njema katika Serikali hii ya Awamu ya Tano, kwa maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ili aweze kufanya kazi yake vizuri ni lazima ajielekeze sana katika kujenga Serikali za Mitaa imara. Tukijenga Serikali za Mitaa imara hata hii dhana kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba kila wakati tunadhani kitu tunatakiwa tuombe Serikali Kuu. Barabara za vijijini tuombe kwenye Serikali Kuu, barabara za mitaani tuombe Serikali Kuu itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndio ilikuwa dhamira halisi ya kuimarisha Serikali za Mitaa. Kuzifanya ziwe na maamuzi sahihi ziwe na rasilimali za kutosha rasilimali watu na rasilimali fedha jambo ambalo kwa Serikali hii inaonekana siyo jambo la mkazo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri urejee sana katika hilo la kufanya maboresho yale ya Serikali za Mitaa yaliyozalisha sera ya *D by D* yafanyiwe kazi za kutosha ili kufanya mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa yawe ni ya ushirika na siyo ya Baba na Mtoto. Kwa hali ilivyo

hapa sasa hivi hapa ni kwamba Serikali Kuu inakuwa ni baba, Serikali za Mitaa zinakuwa ni mtoto, kwa hiyo mtoto ni kulalamika kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la maboresho lilikuwa kuzifanya Serikali za Mitaa ziwe na *autonomy* ili ziweze kujitegemea vizuri. Mheshimiwa Waziri naomba sana ajitahidi katika hilo, ni vizuri akaweka sheria itakayozipa uimara, itakayotengeneza taasisi imara ya Serikali za Mitaa itakayoweza kujiendesha ili tuondoe huu mfumo wa watu kutegemea kila saa kuja kuomba, kupiga magoti hapa na ndiyo maana imefika mahala ambapo inaonekana sasa hivi katika nchi hii bila kuvunja heshima na hadhi ya Mheshimiwa Rais na ikionekana kwamba sasa fedha ya nchi hii ni fedha ya Mheshimiwa Rais na siyo fedha ya walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba sasa hivi kila mtu anamshukuru Rais amempelekea hiki, amempelekea kile, amempelekea kile wakati Rais amechaguliwa na wananchi wote kama mtumishi wa wananchi na mabosi wake ni wananchi wanaolipa kodi ili awatumikie. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani kwamba ni eneo muhimu sana la kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya kuhusu Mfuko wa Vijana na Akinamama. Mara nyingi kumekuwa na hoja hizi kwamba fedha hazikusanywi lakini kubwa zaidi ni kwamba hata hizo zinazokusanywa kidogo hizo zinazopatikana zinatumiwaje. Kwa sababu fedha zile zinaingia Hazina, namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi kuwe na akaunti maalum ya Mfuko wa Akinamama na Mfuko wa Vijana ile asilimia 10 iingie kwenye hiyo akaunti, kwa sababu ule mfuko ni *revolving* ili zikitoka kwa wakopeshwaji zirejeshwe kwenye mfuko ule, lakini hela ile ikitoka kwa wakopeshwaji inarejea kwenye Mfuko Mkuu wa Halmashauri, bado inaingia kwenye matumizi mengine ya Halmashauri, kwa hiyo haieleweki ni fedha zipi zimetoka kwa ajili ya bajeti na ni fedha zipi zimerejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri aelekeze

Halmashauri ziwe na mfuko maalum na aushauri Mheshimiwa Rais akubali kuwa na Mfuko maalum kwa ajili ya fedha hizi za Mfuko wa Vijana na Mfuko wa Akinamama ili sasa mwisho wa siku tuweze baada ya muda tuwe tumetengeneza fedha ya kutosha kwenye hizi akaunti na baada ya miaka kadhaa tukazipa viwango maalum Halmashauri, mwisho wa siku tusizipelekee tena fedha ili zile fedha ziwe kwa ajili ya maendeleo, kwa ajili ya vijana na kwa ajili ya akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni vizuri ajitahidi sana na hili kwa sababu zile fedha kwa sasa hivi hapa hazijulikani zinapoingia kwenye matumizi ya kawaida ni wakati zinaitwa za vijana ni wakati zinaitwa za akinamama, ni wakati gani zinaitwa za matumizi ya Halmashauri. Kwa hiyo, nafikiri ni jambo la muhimu sana kwa Mheshimiwa Waziri kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizokuwa zinatengwa za *retention* asilimia 30 za ardhi ambazo leo hazirejeshwi katika Halmashauri na Mheshimiwa Waziri anajua katika nchi hii kila Halmashauri ardhi ndiyo rasilimali yake kubwa. Ile asilimia 30 ilikuwa inasaidia sana Halmashauri kujiendesha leo zile hela hazirejeshwi, ni vizuri angeshauriana na Wizara ya Ardhi zile fedha asilimia 30 zikarejeshwa katika Halmashauri, zikasaidia mambo ya Halmashauri yakaenda. Kwa sababu mambo ya Halmashauri hayaendi na watakuwa wanazi-*commit* Halmashauri wakati hazina uwezo wa kupata fedha na vyanzo vyote wamevichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *spirit* ya kuchukua vyanzo vya Halmashauri ni vema Mheshimiwa Waziri akamshauri Mheshimiwa Rais ambaye ni Waziri akaiondoa. Serikali Kuu ina maeneo mengi ya mapato makubwa tu ina bandari na maeneo mengi. Haya maeneo ambayo ndiyo Halmashauri kwa mujibu wa makubaliano ya maboresho ya Serikali za Mitaa yaachwe yabaki katika Halmashauri ili yaweze kusaidia Halmashauri. Kwa hiyo, naomba asilimia 30 ya Halmashauri iachwe irejee katika Halmashauri ibaki katika Halmashauri isaidie Halmashauri kuliko kuichukua wakaipeleka Serikali Kuu asilimia 30 ya kodi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la posho ya Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Hebu tusifanye wale watu kama vile wao sio miongozi mwa watu ambao ni muhimu katika Taifa hili. Wale watu tunategemea kuwatumia katika mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya nchi hii. Hata wao wanawatumia katika sera mbalimbali, maelekezo mbalimbali na makusanyo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu ni vizuri waelekeze Halmashauri zitenge zile fedha angalau Sh.20,000/= mpaka Sh.50,000/= kwa ajili ya Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji ili waweze kufanya mambo yao. Tumewafanya wale watu wamekuwa kama ni watu ambao hawana mtu wa kuwasaidia. Wamekuwa watu ambao ni ombaomba, wamekuwa wakiishi kwa majamvi ili watu wagombane wapate fedha, lakini wale watu ni watu ambao wamechaguliwa kwa mujibu wa sheria wanapaswa kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji watengewe fedha kwa ajili ya mambo yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pendo Peneza dakika tano, Mheshimiwa Grace Kiwelu dakika tano, Mheshimiwa Magdalena Sakaya dakika 10.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kunipatia fursa hii na kuweza kuchangia katika Bunge hili.

*Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujikumbushe jana Mheshimiwa Zitto Kabwe alipokuwa akitoa taarifa alisema kwamba katika hizi Wizara ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais, Rais mwenyewe ndiye Waziri pia katika Wizara hizo husika na anawajibika moja kwa moja.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika suala zima la utawala bora, tumekuwa na Rais ambaye ameapa kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na amechukua utawala bora ameuweka chini ya ofisi yake, lakini tumekuwa na Rais ambaye yeye ndiye anayetangaza kinyume na sheria kwamba Vyama vya Siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara. Yeye ndiye anayetangaza kinyume na sheria hata Bunge lenyewe anawanyima hata haki wananchi kusikiliza Bunge live. Tumekuwa na Rais ambaye kwa kumsikiliza tunapata matatizo kama Watanzania katika suala zima kwa utawala bora.* ***(Maneno haya iliagizwa na Kiti siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)***

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, ninaomba nitumie Kanuni yako ya 68(1) nitakwenda Kanuni ya 64 (1) (e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anawakilishwa na Mawaziri wake kwa mujibu wa Katiba ndani ya Bunge letu. Kanuni hii ya (*e)* tunakumbushwa kwamba hatutakiwi kuzungumzia mwenendo wa Rais na hasa anapokuwa katika madaraka ndani ya ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo hiyo Kanuni ya 64 (1)(d), hatutakiwi pia kuzungumza jina la Rais kwa namna ambayo inataka kujenga ushawishi ndani ya Bunge katika kufanya maamuzi ya kutoa maamuzi ya hoja yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kama Mheshimiwa Mbunge anaona kuna shida yoyote azungumze na Wawakilishi wa Rais ambao wako ndani ya Bunge ambao ni Mawaziri husika kwa mujibu wa Katiba, lakini kuendelea kuvunja Kanuni na hasa Kanuni hii ya (*e)* ni kuvunja utaratibu wa shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na jambo hilo ambalo ni la kikanuni, naomba ulitolee ufafanuzi na mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kanuni zetu ziko *very clear*, Rais jina lake halitumiki kwa dhihaka, wala Rais halaumiwi na wala Rais hatakiwi kusemwa kama ulivyosema, kwa hiyo, Mheshimiwa Pendo jielekeze kwenye hoja wapo Mawaziri unaweza ukawahoji wao ukauliza utendaji kazi wao. Huwezi kuuliza utendaji wa Rais ndani ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ambazo wewe, sasa nisikilize basi unazungumza na mtu mwingine utashindwa kuelewa ninachokuongoza, halafu utarudia tena makosa, utajiingiza kwenye matatizo. Jina la Rais halitumiwi namna ulivyokuwa unalitumia.

Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo maneno hayo yote uliyomtaja Rais naiagiza *Hansard* wayafute, anza sasa kuwauliza Mawaziri hawa ambao wako hapa hoja zako za msingi za Jimbo lako au za mambo yako. *(Makosi)*

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kauli ambazo zimekuwa zikiendelea ndani ya nchi hii zikisemwa na Mkuu wa nchi kwa namna hiyo, hatuwezi tukaendelea kama Taifa la Tanzania tunaotegemea misingi ya utawala bora ambayo ameapa kuweza kuisimamia hatuwezi tukaitekeleza. Tuna suala zima la Bunge ambapo tuna watumishi…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kaa, Mheshimiwa Pendo kaa chini. Mheshimiwa Pendo natumia Kanuni ya 73 ukae chini hutazungumza tena. Tunaendelea na Mheshimiwa Grace Kiwelu. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Nami niungane na wanachama

wenzangu kutoa pole kwa viongozi wetu wa Chama Taifa, Wabunge, kwa wakati mgumu wanaopitia kipindi hiki, najua wako na kesi Mahakamani. Tunaendelea kuwaombea kwa Mungu awape ujasiri na dhahabu ili ing'ae ni lazima ipite kwenye moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Jafo, kazi yako inaonekana. Nina mambo matatu. Kwanza nizungumzie *issue* ya Wakurugenzi, naiomba Wizara sasa ifanye tathmini kwa Wakurugenzi ambao wameteuliwa ili wale wenye sifa waweze kubaki na wale ambao hawana sifa tuweze kuwaondoa kwa sababu Wabunge wengi hapa wakichangia wameonesha mambo hayaendi kwenye Halmashauri zao. Wakurugenzi wengi waliteuliwa kisiasa. Wengi waliokosa kura za maoni walipewa kama zawadi na walioshindwa kwenye Uchaguzi Mkuu na hii imesababisha ugomvi mwingi kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko baadhi ya Halmashauri Wakurugenzi wanashindwa hata kuendesha vikao vya Mabaraza, wanaitisha vikao vya Mabaraza, lakini ikifika wakati wa vikao wanakaimisha Wakuu wa Idara na hii inasababisha maamuzi mengi kutokufikiwa kwa wakati na maendeleo ya Halmashauri hizo yanarudi nyuma. Kwa hiyo, niombe sana wafanye tathmini kwa hawa Wakurugenzi wenye sifa wabaki, wale ambao hawana sifa waondolewe. Pia tufuate utaratibu wa Utumishi wa Umma wanaotoka kwenye utumishi wa umma ndio waajiriwe katika nafasi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nizungumzie miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zetu; fedha hizi zimekuwa zinachelewa na hazifiki kwa wakati na kibaya zaidi Serikali Kuu ilichukua vyanzo vile vya mapato tena vyenye fedha nyingi wakiahidi kwamba wanakusanya ili waturudishie. Kibaya zaidi fedha hazirudi kwa wakati na zikirudi ni chache, niiombe Wizara sasa kwanza itupe tathmini wakati tulipokuwa tunakusanya wenyewe kama Halmashauri na wao walipoanza kukusanya yale malengo waliyojiwekea yamefikia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hayajafikia ni vizuri sasa vyanzo hivi vya mapato vikarudishwa kwenye Halmashauri zenyewe, ziendelee kukusanya ili kuweza kutekeleza ile miradi ya maendeleo tuliyojiwekea. Serikali Kuu kwa sababu wamechukua vile vyanzo lakini fedha hawazileti. Niishauri Serikali sasa ni wakati muafaka wa kubuni vyanzo vyao vya mapato na kuacha kuchukua vyanzo vya mapato vya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni upungufu mkubwa wa Watendaji wa Vijiji; kumekuwa na upungufu mkubwa sana, unakuta vijiji viwili, vitatu vinakaimiwa na mtu mmoja. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wetu kupata huduma kwa wakati. Kwa hiyo, niiombe Wizara kuhakikisha kwamba Watendaji hawa wanaajiriwa ili wananchi wetu waweze kupata huduma hizi kwa haraka pale wanapofika kwenye hizo ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ofisi za Watendaji hawa, hakuna, hata za kata baadhi ya vijiji hazina ofisi hizo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la upungufu wa Walimu. Tumekuwa na upungufu mkubwa sana wa Walimu katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro na Jimbo la Moshi Vijijini wa shule za msingi. Hii imetokana na kuwa Walimu wengi wamefikia umri wa kustaafu. Tunaomba sana suala la walimu ajira zao zipatikane kwa wakati, pia nyumba za Walimu bado ni tatizo kubwa sana kwa Walimu wetu tuhakikishe nyumba zinajengwa na ajira ipatikane kwa haraka kwa ajili ya watoto wetu hawa ili waweze kupata elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine pia yako matatizo kwa watumishi wetu, wamekuwa wakilalamika hawapati mafao yao kwa wakati, nimwombe Waziri tuhakikishe Walimu wetu tunajua wengi tumefika hapa kwa sababu ya Walimu, kwa hiyo tuhakikishe mafao yao yanapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya dakika 10, jiandae Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi na Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba za Mawaziri hawa wawili. Pia niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo na timu yake nzima kwa kusaidiana na Katibu Mkuu kwa kweli kazi inaonekana. Japokuwa Wizara ni pana sana lakini kwa kwenda *field* kwenda kuona kazi zinazofanyika kule wanaweza kutatua kiasi kikubwa sana cha changamoto ambazo zinaikabili Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Serikali imetenga shule moja ya msingi katika kila Wilaya kuweza kupokea watoto ambao wana mahitaji maalum kwa maana ya watoto walemavu. Kwa bahati mbaya sana shule hizi miundombinu yake siyo rafiki kwa watoto hawa. Pia shule hizi hazina Walimu wenye uwezo wa kufundisha hawa watoto ambao wana mahitaji maalum na kwa sababu watoto wale kuna wengine ni vipofu, kuna wengine ni walemavu wa viungo, wengine ni usikivu wote wamekusanywa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali na fedha ya *capitation* kwa ajili ya shule hizi hazitoshi kufanya chochote kuboresha miundombinu, Serikali ihakikishe inaboresha miundombinu katika hizo shule ili watoto waliopelekwa pale waweze kupata elimu sawasawa na watoto wenzao wanaopata elimu maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upungufu wa Watumishi. Kiukweli tuna shida kubwa ya watumishi katika sekta zote. Ukienda elimu, ukienda afya, ukienda ugani, ukienda Watendaji wa Kata kila kona, kwa hiyo TAMISEMI

bila kuwa na watumishi wa kutosha wananchi hawawezi kupata huduma. Tunaomba Serikali ihakikishe inaongeza watumishi, Mheshimiwa Mkuchika ahakikishe tunaajiri watu, bahati nzuri wasomi tunao, wako wamesoma wako vijijini, wako mijini wanahangaika hawana kazi, kwa nini hatuajiri?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wilaya ya Kaliua Sekta moja tu ya afya tuna upungufu wa asilimia 76, hujaenda elimu hujaenda kokote. Tunaomba sana Serikali iongeze watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni suala la watumishi kutokupanda madaraja kwa wakati. Leo Walimu wanakaa miaka minne hadi sita hawajapanda madaraja. Swali la kujiuliza watakuja kupandaje madaraja kwenda na wakati? Wakati anatakiwa miaka mitatu apande daraja, leo anapokaa miaka saba hajapanda daraja, anapandaje madaraja? Tunaomba watendaji wapande madaraja kuendana na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la watumishi wa Kaliua walihama kutoka Urambo tangu mwaka 2013, mpaka leo mwaka wa sita hawajapata stahiki zao. Mwaka wa sita kuhamishwa na haki zao zote, leo wapo Wilaya ya Kaliua lakini tangu wakiwa Wilaya Urambo mpaka wamehamia Wilaya Kaliua leo miaka sita hawajapata stahiki zao. Waziri Mkuu alikuja Kaliua, akaagiza wapewe haki zao, leo ni mwaka wa sita hawajapewa. Naomba watumishi hawa wa Kaliua ambao walitoka Urambo wapatiwe stahiki zao kutokana na majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la Hospitali ya Wilaya. Wilaya yetu ya Kaliua ambayo ina takribani wananchi laki nne hatuna hospitali ya Wilaya. Tuna vituo vinne tu vya afya, tumeweka kipaumbele chetu ni hospitali ya Wilaya kwa mwaka huu, tukaiomba Serikali itusaidie bahati mbaya sana nimeangalia hiki kitabu hatupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tumeanza

kama Halmashauri tumejenga jengo la *OPD l*enye ghorofa moja, mara nyingi nimeongea hapa Bungeni tumekamilisha tuko kwenye *finishing,* tukawaomba Serikali itusaidie majengo mengine, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie Wilaya ya Kaliua kwa jicho la pekee. Tunazo Kata 26 tuna vituo vya afya vinne (4), tuna vijiji 101 vituo vya afya ni vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanafuata huduma za upasuaji wa akinamama Urambo, tunafuata Kigoma. Naomba sana kwa mwaka huu Kaliua iangaliwe kwa jicho la pekee, kama imesahaulika naomba iingizwe tupate hospitali wananchi wa Kaliua, tuokoe vifo vya akinamama na watoto vinavyotokea kwa kukosa huduma za afya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la uwezeshaji wa vijana na kina mama. Tumeongea sana hapa Mheshimiwa Jenista alituambia tuna mifuko 17. Nashangaa kama kuna mifuko 17 mbona katika Wilaya yangu ya Kaliua kwa miaka mitatu tumepata vikundi vya *SACCOS* vimeletwa vinne tu, vijana viwili, akinamama viwili. Fedha nyingine yote ambayo tunawapa vikundi ni ya ndani ya Halmashauri, hii mifuko 17 inasaidia watu wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine mgawanyo wake siyo sahihi, pengine mgawanyiko hauna uwiano kwenye Wilaya mbalimbali, inawezekana kuna maeneo ambayo zinakwenda zaidi wengine wanakosa. Naomba sana hata fedha inayotengwa na Halmashauri ni kidogo haitoshi, akinamama vikundi viko zaidi ya mia, hatuwezi kuwapatia mtu anaomba milioni 10 unampa milioni mbili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini bado hapa kwa umuhimu wa Wizara hii na kwa kuwa Mheshimiwa Jafo anajua tukiwawezesha akinamama, tumewezesha familia, tumewezesha jamii, haiwezekani kuendelea kusema tunawawezesha wakati ambapo tunawapa kidogo na hatuwezi kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *TARURA*.

*TARURA* anafanya kazi nzuri shida hawana fedha nimeongea jana hapa barabara zimeharibika nyingi *TARURA* wako ofisini hawana fedha ya kufanya kazi. Nakubaliana na Waheshimiwa wengine kwamba tuwape *TANROAD* asilimia 50 na *TARURA* asilimia 50 kwa sababu barabara za vijijini ndiyo barabara za uchumi, mazao yanatoka kule, wananchi wako kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni nyumba ya Mheshimiwa *DC*...

**MBUNGE FULANI:** Seif muachie achangie. *(Kicheko)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya, nyumba imeanza kujengwa tangu mwaka 2013, mpaka leo imekuwa ni pagale haiendelei, imeota majani tunaomba sana nyumba ya Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya wa Kaliua imaliziwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la kuendelea kuwepo mishahara hewa. Nimeangalia kitabu cha *CAG* kuendelea kuwepo na mishahara hewa, hivi jamani ndani ya miaka yote na juhudi zote, bado Halmashauri zaidi ya 29 zinaendelea kulipa mishahara hewa. Tunalia habari ya watumishi, tunalia hatuna watumishi wa kutosha lakini fedha zaidi ya milioni 329 wanalipwa mishahara hewa. Huu ni udhaifu kwa kweli wa hali ya juu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana tatizo la mishahara hewa watu waliokufa wanalipwa mishahara, liwe ni mwisho. Ni aibu kuendelea kuonekana kwenye vitabu vya *CAG* na anashauri anasema mapendekezo anayotoa hayafanyiwi kazi, Serikali amkeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi, wajiandae Mheshimiwa Mlata na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nishiriki katika mjadala wa hotuba hizi za Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana kwanza kumpongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Kakunda na Kandege kwa kazi kubwa sana wanayoifanya. Sifa kubwa waliyonayo Mheshimiwa Selemani Jafo na Mzee George Mkuchika, ni kwamba ninyi ni wasikivu sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Wanawasikiliza lakini pia ni wafuatiliaji wazuri katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Watendaji wanaofanya nao kazi Mhandisi Iyombe, Naibu Makatibu Wakuu wanawasaidia, lakini pia na Ndugu Seif ambaye ndiye mteule katika kusimamia *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa ku-*declare interest* kwamba nimekuwa sasa Mwakilishi wa wananchi kwa miaka 22. Katika miaka 22 hii nimekuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kwa miaka mitano, nimekuwa Diwani kwa miaka kumi, Nimekuwa Meya kwa miaka mitano na sasa ni Mbunge kwa miaka saba. Kwa hiyo nimekuwa TAMISEMI kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye kada ya Wenyekiti wa Serikali za Mitaa na Vijiji na Madiwani. Naishauri Wizara kwamba msingi wa Serikali ni kuanzia kwenye ngazi za vijiji na mitaa, lakini uboreshaji wa maeneo haya umekuwa siyo kwa kasi kubwa. Nashauri kwamba posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ni muhimu sana, kwa sababu viongozi hawa wamekuwa wakifanya kazi kwa masaa 24 na ndiyo viongozi wanaokaa na jamii. Maeneo mengine ambako Maafisa Watendaji wa Vijiji ama Mitaa hawapo wao ndio walinzi wa amani, kwahiyo ni muhimu sana tukazingatia kuhakikisha na maeneo ya hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye maeneo ya Madiwani. Waheshimiwa Madiwani ndiyo wasimamizi wa mabilioni ya fedha tunayoyapeleka kwenye Halmashauri zetu,

lakini posho wanazozipata zinafanya wakati mwingine Waheshimiwa Madiwani sasa wawe ombaomba hata kwa Watendaji. Kwa hiyo, inakuwa ngumu sana kusimamia kikamilifu katika maeneo hayo, nashauri kwamba ni vizuri sana tukaangalia. Pia suala zima la mafunzo ya viongozi hawa wakichaguliwa wanakaa miaka miwili au mitatu hawajapata semina yoyote. Ni vizuri sana viongozi hawa wakapata semina ili kuhakikisha watende kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili napenda kuchangia ni sekta ya afya. Waziri Mheshimiwa Jafo na Watendaji wake na Wasaidizi wako nadhani wameandika na wanaendelea kuandika historia ya kwamba ni Viongozi waliosimamia kikamilifu katika suala zima la kuhakikisha ujenzi wa vituo vya afya, lakini pia ujenzi wa hospitali 67 za Wilaya, lakini pia upatikanaji wa dawa katika mahospitali yetu na zahanati zetu. Haya ni mambo ambayo wote tunayaona na tumpongeze Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimkushukuru sana Mheshimiwa Jafo na Serikali kwa kuwakumbuka wananchi wa Wilaya ya Masasi hususani Jimbo la Lulindi kwa kupata hospitali ya Wilaya, tunawashukuru sana. Katika hilo nina ombi kwa Mheshimiwa Jafo na Serikali kwamba katika kituo cha afya cha Nagaga ambacho nilikielezea kwamba kilipata tatizo la gari lake la wagonjwa kuungua moto miaka saba iliyopita, hakijapata gari tena, hivyo kupelekea tatizo kubwa sana katika maeneo hayo hasa wagonjwa kuwapeleka mbali katika hospitali ya Wilaya. Naomba sana katika mgao ujao wa magari, hebu tufikirie kupeleka gari katika kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *TARURA*. nampongeza Mkurugenzi ama Mtendaji Mkuu wa *TARURA* Ndugu Seif kwa maandalizi ambayo yanaendelea kwenye *TARURA*. Hata hivyo, nitoe angalizo tu kwamba kama hawatapata fedha za kutosha itakuwa ni wakala pekee hapa nchini tuliouanzisha ambao hautaleta tija. Tumeshuhudia wakala zote *REA*, *TANROAD* zinafanya vizuri,

lakini hapa tunahitaji papatikane fedha za kutosha ili waweze kukidhi haja na matarajio ya Watanzania kuhusu eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la watumishi mpaka sasa wameazimwa tu kutoka kwenye Halmashauri wawe pia na watumishi wao ambao wataweza kukidhi kusimamia suala hili. Vile vile kama *TARURA* hatukuwapa fedha za matengenezo ya kawaida za barabara kwa sababu barabara hizi ambazo *TARURA* wanakwenda kuzifanyia kazi ni barabara ambazo nyingi ni za changarawe na mvua ikinyesha huwa barabara hizi nyingi hazipitiki. Kwa hiyo kama hawatapata fedha za *maintenance* maana yake barabara nyingi hapa nchini hazitaweza kupitika hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni eneo la migogoro na kero mbalimbali za wananchi kwenye maeneo yetu. Uzoefu wangu mdogo ndani ya TAMISEMI unaonesha kwamba baadhi ya Halmashauri zetu Watendaji hawafuatilii kero za wananchi na matokeo yake sasa hivi Waheshimiwa Mawaziri wakienda kutembelea, Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais ni mabango chungu mzima yanayoonesha matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana Mheshimiwa Jafo aimarishe kitengo cha ufuatiliaji wa kero za wananchi ili zipungue hata yeye anapokwenda kule asianze kukumbana na mabango kwa sababu huo ni upungufu unaoonesha kwamba watu hawajawajibika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nataka kuchangia ni juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uzoefu unaonesha kwamba liko tatizo kweli la kucheleweshwa fedha na Serikali imejitahidi kwamba wamefikisha asilimia hizo 49,asilimia 50, lakini tukumbuke tu kwamba bado mwaka wa fedha haujausha bado tuna miezi mitatu, tuiombe Wizara ya Fedha ikamilishe ule upungufu wa fedha ambazo zilikuwa hazijaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa pia kwa miradi kunatokana na baadhi ya Watendaji kutoharakisha michakato ya kupelekea uanzishaji wa miradi. Kwa mfano, suala zima la kutangaza *tender*, kuhakikisha kwamba Mzabuni anakuwa *awarded* inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika eneo hilo ni kwamba fedha zingine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kuisha)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlata, wajiandae Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hizi mbili. Kwanza niwapongeze Mawaziri wote Mheshimiwa Selemani Jafo pamoja na Mheshimiwa George Mkuchika, Naibu Mawaziri George Kakunda na Josephat Kandege, Makatibu Wakuu wote katika Wizara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo na Manaibu wake kwa kazi kubwa ambayo tumeiona. Wamekuwa wakitembelea Halmashauri zetu na maeneo yetu yote kuhakikisha kwamba shughuli za maendeleo zinamfikia mnyonge kama Rais wetu ambavyo amekusudia. Nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami niungane na wale wote wapenda maendeleo waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Naomba apelekewe salamu na akubali kwamba yeye kuwa mti ule uzaao matunda yaliyo bora na yaliyo masafi na yaliyo mazuri, kwa sababu mti wa namna hiyo ni lazima upigwe mawe ni lazima upigwe vijiti na ni lazima unenewe maneno yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba akubali kwamba yeye ni mti uzaao matunda yaliyo mema na ndiyo

maana wale wasiopenda mema wanamrushia mawe. Naomba pia apelekewe salamu kwamba wananchi wa Mkoa wa Singida tuko pamoja na yeye, tunamuunga mkono kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea upande wa miundombinu barabara za Mkoa wa Singida nyingi zinapitika hata kama ni za vumbi kwa sababu wale akinamama walioko pembezoni hata wanapotaka kupata huduma za afya kuna bajaji, kuna bodaboda, kuna Noah. Wakifika hospitali wanakuta nidhamu ya watumishi iko safi, dawa ziko nyingi, Rais ameongeza bajeti kubwa, vitendea kazi vipo, wafanyakazi wanafanya kazi nzuri ya kuwahudumia wananchi. Tunamuunga mkono aendelee tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nasikitika sana mpelekeeni salamu Mheshimiwa Rais mwambieni atusaide tupate upinzani utakaosaidia kujenga Taifa hili, Upinzani unaojitambua, Upinzani unaojitambua, Upinzani ulio bora, Msajili wa Vyama awapeleke Wapinzani kwenye nchi zenye Upinzani wenye mfano ambao Mataifa yao yameweza kusimama imara. Nasema hivi kwa sababu hapa Tanzania bado hatujawa na Upinzani ulio imara, Upinzani utakaosaidia katika Taifa hili ili tuwasaidie wanyonge na kulijenga Taifa letu. Mpelekeeni salamu kwamba, bado hatuna Wapinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Rais...

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Vyama vya Upinzani Tanzania ni imara na ndiyo maana Chama Tawala kikawakataza kwenda kwa wananchi kwa ajili ya kutangaza sera zake, kwa sababu ya hofu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa hii kwa sababu Upinzani uko wapi wa kuruhusiwa kwenda kufanya mikutano kwa wananchi, Upinzani unaoenda kuwahadaa wananchi wasifanye shughuli za maendeleo, wakae wanaandamana barabarani, Upinzani unaomkataa Rais, Upinzani usioona yale mazuri, Upinzani ni upi utakaoruhusiwa kwenda barabarani.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata subiria taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji anayezungumza, sisi ni Vyama vya Mageuzi siyo Upinzani. Upinzani ni ule unajenga nyumba huyu anavunja. Sisi ni kioo cha Serikali, sasa usitushambulie kiasi hicho ukasababisha tuseme maneno mengine humu ndani hali ichafuke.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tuendelee taarifa hiyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe Vyama vya Mageuzi, iwe ni Upinzani lakini mimi nasema Upinzani gani hata mambo mazuri wanayakataa? Rais amejitoa kwa ajili ya Taifa hili...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata subiri kwanza. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu. Kanuni ya 64 (1) (b) inatuelekeza Wabunge kwamba hatutazungumzia jambo lolote ambalo halipo kwenye mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara zilizoko hapa mbele yetu leo ni Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Wizara zinazohusika na Vyama vya Siasa ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Sera na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umwelekeze Mbunge aliyekuwa anazungumza arejee kwenye hoja, azungumzie matatizo ya elimu na afya huko Singida, azungumzie matatizo ya maji, Singida ina vijiji havijawahi kupata maji toka uhuru, Singida ina vijiji watu wana...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zitto. Waheshimiwa Wabunge nikikaa kwenye Kiti huwa nasikiliza mazungumzo yote, pale ambapo kuna mtu anakosea Kanuni jambo lolote na mimi nachangia kumzuia ili kumpa fursa ajifundishe kama hajui kujifundisha. Mheshimiwa Mlata mpaka sasa hivi alichokisema ni Upinzani unaokataa maendeleo, Upinzani unaokataa vitu muhimu vinavyojengwa na Serikali, kwa hiyo nafikiri mpaka sasa hivi Mheshimiwa Mlata hujatoka kwenye mstari, lakini usibweteke zaidi ukatoka kwenye mstari, kwa sababu mimi hapa ni *referee* siyo kocha.

Mheshimiwa Mlata endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa kwenye utawala bora lakini sasa nataka kusema mwambieni Rais kwamba yale yote anayoyafanya wako watu watakuja kuyakumbuka kama ambavyo wanamkumbuka Jakaya sasa hivi, asonge mbele aendelee kuwa mti uzaao matunda mema, watakuja kumkumbuka. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sipokei taarifa kwa sababu muda wetu umekwisha na nina wachangiaji wengine wawili. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo ambazo nampa Mheshimiwa Rais, tunamshukuru sana Mheshimiwa Selemani Jafo kwa sababu katika Mkoa wetu wa Singida ametuletea hospitali mbili, hospitali ya Mkalama pamoja na Ilongero. Naomba hospitali hizo zikajengwe mahali ambapo amezipanga. Pia naomba

sana hospitali ya Ilongero itakapokwenda kujengwa pawe ni pale ambapo ndipo maeneo ya Makao Makuu ya Halmashauri ile, hivyo naomba Mkurugenzi ahamie haraka eneo lile ambalo mwaka 2006 ndiyo tulipitisha kwamba patakuwa ni Makao Makuu. Namwamini na naomba atembelee eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nizungumzie suala la afya. Naomba kuuliza, Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi sana kwa ajili ya dawa zile *Delivery Kits* kwa ajili ya kujifungua vile vitu ni vya bure kwa nini wanauza au ni ule mfuko ndiyo wanataka kuuza? Watoe ule mfuko waache vifaa waweke *labor*, wanawake wapate vifaa bure, wasiuze ile *kits* au *set* kwa ajili ya wanawake. Kumbukeni pia kujenga mama ngojea kwa ajili ya kuokoa akinamama wenye matatizo ya uzazi ili waje wasubirie pale, hilo naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba sana hebu tuangalie Kata ya Mwanga kule Mkalama, hata nguzo moja ya umeme haijawahi kupelekwa, kwa sababu tunataka kujenga uchumi wa viwanda na kule ndiko kwenye kilimo cha vitunguu, alizeti na mahindi, tunaomba wapeleke nguzo na hatimaye waweke umeme kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namalizia kwa ajili ya mikopo ile ya fedha za wanawake. Naomba sana ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge namwita sasa Mheshimiwa Lusinde, wajiandae Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Catherine Rugen a jioni tunaanza na Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Ahmed Ngwali.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa uongozi wako na Mungu aendelee kukujalia kwa namna unavyotenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanataka kubomoka lakini leo nataka kusema ukweli sasa, maana yake Tanzania ukweli watu hawaupendi, nami nataka leo niseme ukweli halafu nitatumia kauli ya mdogo wangu Mwenyekiti wa Vijana wa CCM Ndugu Kheri James kuwaomba wanipigie makofi kwa kusema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Waziri mzoefu Kaka yangu Kapt. George Mkuchika. Nawapongeza sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa TAMISEMI, Katibu Mkuu, Mhandisi Iyombe pamoja na timu yako mnafanya kazi nzuri. Wakati nikiwapongeza niwashukuru kwa kunipatia milioni 700 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya pale Mpwayungu, milioni 400 kwa ajili ya ujenzi na 300 kwa ajili ya vifaa. Hii itasaidia sana wakazi wa Tarafa ya Mpwayungu kupata huduma za afya kwa urahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe tu watu wa *TARURA* watengeneze daraja lile la Manda limevunjika kwa mvua, hii inatupa shida sana *ambulance* kupita pale kuleta wagonjwa kwenye kituo cha afya cha Mpwayungu. Kama ambavyo Wabunge wengi wameeleza tunaomba bajeti ya *TARURA* na utendaji wao wa kazi uwe wazi ili Wabunge waweze kuasaidiana nao kuhakikisha kwamba maendeleo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilitolee ufafanuzi kabla sijaingia kwenye utawala bora, nizungumzie kuna baadhi ya Wabunge walikuwa na mashaka juu ya kugawana mali za Chama. Wengine wanafikiri kwamba mali ambazo walizijenga kabla hawajahama CCM wana haki nazo. Ndugu zangu hata Maaskofu hilo mkiwauliza watawasaidieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Muislam ukachangia matofali siku utakayokuwa Mkristo yale matofali ya Msikiti hayatakuhusu tena, wala huwezi kuyadai tena, ukiwa Mkristo ukachangia matofali ya kujenga Kanisa siku utakayohama

kwenda kuwa Muislam matofali yale ukidai ni ugomvi. Kwa hiyo, ndugu zangu muelewe tu kwamba ile michango mliyoitoa wakati wa Chama kimoja kuijenga CCM mkitaka kufaidi rudini CCM ili muweze kufaidi vizuri. Hata kwenye harusi tu, michango ya harusi inaishia mlangoni huingii chumbani kwa maharusi kwa sababu ya mchango uliotoa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo sasa ninukuu tu kwenye Biblia huo mstari siukumbuki. Kuna mstari unasema toa kwanza boriti jichoni mwako ndipo uone vema kibanzi kilicho kwenye jicho la mwenzako. Wapinzani wa nchi hii, tuoeni kwanza boriti iliyomo kwenye macho yenu kabla hamjaona boriti iliyopo kwenye Serikali ya CCM. Nasema hivi kwa sababu nataka niingie sasa kwenye ukweli mtupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye ripoti ya *CAG* ukurasa 266 nanukuu "mkopo ambao haukuthibitishwa mapokezi ndani ya Chama cha CHADEMA, mnamo tarehe 11 Aprili, Menejimenti ya CHADEMA (Mkopaji) iliingia makubaliano na mwanachama wake (Mkopeshaji) kuhusu kukopeshwa kiasi cha bilioni mbili." Mnisikilize hapo, wanakopa hewa yaani deni hewa hilo. Mkopo waliingia makubaliano na mwanachama wake mkopeshaji kuhusu kukopeshwa shilingi bilioni mbili kwa shughuli za Chama. Hakuna nyaraka zinazoonesha kuwa kiasi cha mkopo walichokubaliana kilitolewa na kupokelewa na Chama husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anaendelea tarehe 26 Agosti, kiasi cha shilingi milioni 866 kililipwa kwa mwanachama kwa niaba ya Chama kwa ajili ya mabango ya matangazo yaliyotolewa na kampuni ya *MS Milestone International Company Limited* nje ya deni hilo. Kiasi cha shilingi milioni 715 kililipwa kwa mwanachama kama marejesho ya fedha iliyokopwa kulipia ununuzi wa mabango bila ya kuambatanisha makubaliano ya kisheria. Wajinga ndio waliwao, mmeng'ang'ania maandamano mnaacha wenzenu wanapiga hela. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wangu wa taarifa ya makusanyo ya Chama umebaini kiasi cha Sh. 2,302,305,500 kilikusanywa bila kuingizwa kwenye akaunti ya Wadhamini." Angalia mambo hayo! Hazikupelekwa benki na matumizi yake hayakutolewa kwa ajili ya ukaguzi. Kutokupeleka makusanyo benki kunaonesha Chama kutokuwa na mfumo mzuri wa udhibiti wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi yaliyofanyika, nimebaini kuwa CHADEMA kimefanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh.24,216,625,309 bila kufuata utaratibu." Wajinga ndio waliwao. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kuna taarifa inakuja?

**MWENYEKITI:** Muda wetu jamani hakuna taarifa sasa hivi, endelea Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wajinga ndio waliwao kuna Kwaya imeimba. Badala ya kushughulikia matatizo makubwa ya ufisadi ndani ya Chama chao wameng'ang'ana kila siku kukosoa Serikali, kukosoa Chama chenye Serikali. Ndugu zangu ndani ya Chama chenu kuna wizi na ubadhirifu mkubwa wa pesa, watu wanakula hela na ninyi mpo hapo! Madeni hewa yanatengenezwa, *helcopter* hewa zinakodiwa ninyi mmekaa hapa mnang'ang'ania CCM, toeni kwanza boriti kwenye macho yenu ndiyo muone vibanzi vilivyopo kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Watanzania waelewe kwamba ufisadi mkubwa upo kwenye Chama kinacholalamikia ufisadi kumbe wao ndani hawajikagui. Kwa mara ya kwanza ipo humu na ndiyo maana nasema hakuna mtu atapinga kwa sababu haya ni mawe ya uhakika. Nipigieni makofi kwa ukweli ninaowapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukweli mtupu, ndugu

zangu mkienda mkajisimamia mkawa wakweli kwenye mambo yanayowagusa ninyi mtakuwa na haki ya kutukosoa, lakini kama ninyi wenyewe mnakumbatia ufisadi na wizi wa mabilioni ya pesa yanakusanywa kwa wanachama yanaingia kwenye Chama chenu, watu wanagawana wanakula, michango ya Wabunge inaliwa, mmekaa hapo mmenyamaza kazi yenu kukosoa hii! Nawaambia hamtakaa mfike popote. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimewaambia huu ni ukweli mchungu, nimesema natumia maneno ya Kheri Denice James kwamba ifike mahali kama tunataka kutengeneza Upinzani tutengeneze Upinzani wenye kusema kweli. Ukianza kumulika nyoka anzia kwenye miguu yako ndipo uanze kumulika kule. Niliwaambia hata juzi mna Chama kilichopokea ruzuku zaidi ya bilioni 10 hakina Ofisi hata moja wilayani, hakina ofisi hata moja mikoani, mnataka kufanana na Chama cha Zitto! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnazungumzia utawala bora nataka niwaambie, Mheshimiwa Zitto yupo peke yake anahangaika. Wapo Wapinzani Wazalendo, mimi nataka niseme kwenye Bunge hili mtakuja kunikumbuka, Mheshimiwa Zitto wewe ni hazina lakini badili Chama, njoo CCM uje ufanye kazi ya wananchi, kubaki huko unapoteza muda bure, tutakukosa mtu mzuri kwa sababu ya muda na huko unakopoteza muda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu imeundwa CHADEMA imezaa vyama viwili, imezaa SAU...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Lusinde nimeshasema hakuna taarifa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwambie hivi tangu CHADEMA imesajiliwa, nazungumzia utawala bora, tangu CHADEMA imesajiliwa imezaa vyama viwili. SAU imevunjika kutoka

CHADEMA, ACT imevunjika kutoka CHADEMA, sasa Chama hiki kingekuwa na Serikali si kingekuwa kimeleta vita kubwa sana ndani ya nchi? Kingeleta vita kubwa ndani ya nchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunapozungumzia utawala bora tuanze kujitazama sisi wanasiasa, tutazame miongozo na mienendo ya Viongozi wetu. Kuna Vyama hapa vina Mwenyekiti wa kudumu, kila unapokuja uchaguzi Mwenyekiti wa kudumu, Chama cha namna hiyo hakiwezi kujenga demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, tukikosoa tuanze kujikosoa wenyewe ndipo tuende tuwakosoe watu wengine tunaotaka kuwakosoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hizi zote mbili na naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nimeshasema sipokei taarifa upande wowote mpaka tutakapomaliza saa saba. Mheshimiwa Catherine Ruge nafasi yake anampa Hawa Mwaifunga, kwa hiyo sasa tunaanza na Susan Lyimo halafu ataingia Hawa Mwaifunga dakika tano tano.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii japo fupi. Nitaanza moja kwa moja na TAMISEMI nami kama Mwalimu nitazungumza zaidi masuala ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniuliza kipaumbele namba moja, mbili na namba tatu vyote ningesema elimu, lakini kwa masikitiko makubwa bado Serikali hii haijawekeza ipasavyo kwenye elimu. Ukiangalia takwimu sekta ya elimu mwaka jana bajeti inaisha kwa ujumla wake ilipata trilioni

4.7, lakini trilioni tatu zimeenda TAMISEMI kwenye sekta ya elimu, katika fedha hizo asilimia saba tu ndiyo inakwenda kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba miundombinu ya elimu ambayo wote tunaipigania *including* nyumba za Walimu hazijengwi. Hii ndiyo sababu ukiangalia kwenye hii hotuba hawajaeleza upungufu wa nyumba za Walimu ni ngapi, wamesema tu nyumba za Walimu kwa mwaka huu zimejengwa 290.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya *World Bank* inaonesha kwamba tuna upungufu wa nyumba 186,000. Kama tuna upungufu wa nyumba 186,000 na kwa mwaka mmoja wameweza kutengeneza nyumba 290 maana yake tunahitaji miaka 500 kukamilisha kujenga nyumba za walimu hapa nchini. Hili ni jambo la aibu na halipendezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa mwaka huu ukiangalia, bajeti ya mwaka huu trilioni sita kwa Wizara hii, *only one trillion* ndiyo inaenda kwenye maendeleo, maana yake ni kwamba *only 27%* ndiyo inakwenda kwenye maendeleo, *yet* tunategemea shule, nyumba za Walimu na vyoo vijengwe na kadhalika. Hatuwezi kuwa na elimu bora kama fedha haziendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazungumzia suala la eti kumekuwa na ufaulu zaidi, nataka Serikali ituambie huo ufaulu unapatikanaje wakati Walimu 70% hawako *motivated*, huo ufaulu unaongezekaje wakati hakuna chochote kilichorekebishwa katika elimu. Naomba Serikali iangalie ni jinsi gani fedha za maendeleo zitakuwa angalau zinalingana na fedha za maendeleo katika Wizara hii inayo-*deal* na elimu na afya ili watu wetu wasiendelee kufa kwenye vituo vya afya na ili wanafunzi wetu waweze kusoma *in a comfortable way*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la Meya. Tunajua kwamba Mameya wote wanatakiwa wachaguliwe na Madiwani ambao wamechaguliwa. Leo

Meya wa Manispaa ya Dodoma ameteuliwa na Waziri lakini ndiyo Meya wa Dodoma. Hivi kama tunatunga Sheria yetu ya Serikali za Mitaa, Kifungu Namba 20 kinaelekeza wazi Meya anapatikanaje, lakini inashangaza kuona kwamba mtu anayeteuliwa ndiyo anakuwa Meya wa Manispaa ya Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni kwa nini na hapo Naibu Waziri wa Wizara ya Jenista ni Diwani pale, sasa tunashangaa kwa nini tuna sheria zetu lakini tunazipuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia suala la Walimu wanaoondolewa kwenye shule za sekondari kwenda shule za msingi. Nakubaliana na wazo lakini ni kwa kiasi gani Walimu hawa watapewa mafunzo ili waendane na hali halisi ya kule wanakoenda kufundisha. Haiwezekani Mwalimu aliyekuwa anafundisha kidato cha tano au cha kidato cha nne anapelekwa kwenda kufundisha darasa la kwanza au darasa la pili, ni lazima wawe na mafunzo vilevile tunajua hawa wote hawajapewa fedha za kwenda kule wanakopelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo akizungumza, naomba kujua hawa Walimu watawaondolea adha hii lini wapate fedha ili waweze kufanya kazi zao. Kwa taarifa nilizonazo Walimu karibu wote waliohamishiwa huko hawaendi na kama wanaenda basi wanaenda siku moja moja, kwa sababu maeneo waliyopo ni mbali na kule ambako wanatoka. Hivyo, naomba hilo pia lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kidogo japo limeshazungumzwa, kuhusu suala la Tunduma. Naomba sana Mheshimiwa Waziri alichukue kama *special case* kwa sababu haiwezekani Baraza la Madiwani ambao ndiyo wanapanga maendeleo tangu mwezi wa Agosti mpaka leo hawajakaa, limezungumzwa lakini naomba kusema kwamba sauti ya wengi ni sauti ya Mungu na Mheshimiwa Jafo najua yeye ni msikivu, naomba jambo hili alifanyie kazi haraka

iwezekanavyo ili Madiwani wetu waweze kufanya kazi za maendeleo kama ambavyo miongozo yao inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la elimu ya msingi. Ni kweli wamesema kwamba asilimia 99 ya shule zetu za Serikali zina elimu ya awali, pamoja na uwepo wa shule ya awali Mheshimiwa Jafo hebu atuambie hizi shule… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Susan mengine mwandikie atakujibu. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba nami nichangie haraka. Nilikuwa napitia jedwali la TAMISEMI katika pesa za ujenzi wa hospitali za Wilaya nimeshangaa sana kuona Manispaa ya Tabora haijawekewa hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka Mheshimiwa Waziri Madiwani kutoka Manispaa ya Tabora tulikuja ofisini kwake, moja kati ya maombi ambayo tulimwomba ni kuweza kutusaidia Hospitali ya Wilaya ijengwe. Nafahamu kwa nini amefanya hivi, akiamini kwamba Hospitali ya Kitete itaweza kutusaidia watu wa Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Kitete ina matatizo mengi, hospitali ya Kitete ina changamoto nyingi. Kwanza haina Madaktari, mpaka sasa kati ya Madaktari tisa bingwa wanaotakiwa kuna Daktari mmoja peke yake. Ukimuuliza Daktari huyu ubingwa wake amesomea kwenye nini wala haelewi, lakini ni Daktari Bingwa peke yake ndiye aliyepo katika hospitali ya Kitete. Leo hospitali ya Kitete ni hospitali ya Rufaa, kwa hiyo wale wananchi wote wa Manispaa ya Tabora wanapokuwa wana matatizo

wanakimbilia hospitali ya Kitete, imekuwa na msongamano mkubwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha ajabu pale kuna majengo ya chuo ambayo sasa yameanza kuchakaa, hebu atueleze atakapokuja ku-*wind up* ni lini yale majengo yatamaliziwa na watafungua kile chuo ili tuweze kuondokana na upungufu wa Madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hiyo ya Kitete ina jengo la *ICU* lakini hakuna mashine hata moja katika jengo hilo na ndiyo hospitali ya Rufaa, leo bado mnatuona kwamba watu wa Tabora hatuhitaji kupewa hospitali ya Wilaya tuendelee kutumia hospitali ambayo ina matatizo chungu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Kitete wodi ya wazazi ni ndogo sana, kwa siku katika Hospitali ya Kitete inapokea akinamama 15 mpaka 17 wanaotaka kujifungua kwa kawaida, inapokea akinamama watano mpaka saba wanaokwenda kujifungua kwa operesheni, wodi ile haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo nafasi kubwa kwenye ile hospitali, tunaomba kwa sababu ni hospitali ya Rufaa lijengwe jengo kama lililopo Hospitali ya Mwananyamala ama lililopo pale Sinza ili liweze kusaidia akinamama hawa kuondokana na matatizo ya kuwa na msongamano wa hali ya juu. Wanawake pale wanalala chini, wanawake pale wanaenda kujifungua wanalala wawili na watoto wao, kwa kweli haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba badala ya kutubana, kutegemea hospitali ya Rufaa ambayo ina msongamano mkubwa, tunaomba nasi basi tutengewe fedha ili tuweze kujenga hospitali yetu ya Wilaya. Tunashukuru kwa pesa katika Wilaya ya Uyui na Wilaya ya Sikonge, tunaomba na Tabora Manispaa itengewe fedha ili tupate hospitali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji pia *standby*

jenereta; katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete hakuna jenereta, hata kama mtu anafanyiwa upasuaji kama umeme unakatika na umeme wenyewe huu, haiwezekani na watu wanaweza wakafia na wengi wanakufa wakiwa wanafanyiwa *operation* kwa sababu umeme unakatika mara kwa mara. Tunaomba wamtusaidie hospitali ile angalau basi iwekewe *standby generator* ili kuokoa maisha ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la elimu. Shule za zamani tunashukuru tumepiga kelele angalau zimefanyiwa matengenezo. Shule ya Tabora *Girls,* Shule ya Tabora *Boys* na Shule ya Mirambo, tunawashukuru sana kwa hilo lakini bado zipo changamoto. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri Tabora *Girls* wasichana wanalala chini kwa sababu vitanda vingi pale vimevunjika, wanaomba wasaidiwe angalau vile vitanda viweze kutengenezwa waweze kulala kwa nafasi. Pia Tabora *Girls* ina uhaba wa Walimu. Kwa hiyo, tunaomba watusaidie Ofisi ya Utumishi waajiri Walimu, wale waliowandoa wasiokuwa na vyeti waturudishi Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba na bado tutaendelea kuomba kama wanawake angalau kwenye shule kama hizi, basi wanawake wale mabinti waweze kusaidiwa taulo, kwa sababu waliopo katika shule hizi wengi ni wale ambao wazazi wao hawana uwezo, kwa wale ambao wazazi wao hawana uwezo waweze kusaidiwa taulo ili angalau wanapofika kwenye kipindi chao cha hedhi waweze kuwa salama na waweze kuendelea na masomo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unga mkono hoja basi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha mchana kimekwisha, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilishataja majina mawili ya kuanzia; Mheshimiwa Mussa Mbarouk, ajiandae Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitaanza na hotuba ya bajeti ya Utumishi. Sekta ya Utumishi ni sekta muhimu na vile vile katika kila nchi basi sekta hii inakuwa na changamoto, lakini kwetu niseme imezidi. Kwa nini nasema hivyo; kwa sababu kwanza kuna tabia ya kuwacheleweshea watumishi wetu michango yao ya Mifuko ya kijamii katika *NSSF, LAPF, WCF, GEPF* na kadhalika. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi suala hili ili hii michango iwe inapelekwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale wafanyakazi au watumishi wanapostaafu kumekuwa kuna tabia ya kucheleweshewa mafao yao. Sasa wale wanaohusika na malipo ya mafao wajijue na wao pia kwamba ni wastaafu watarajiwa, kwa hiyo wanavyowafanyia wenzao na wao wakija wakistaafu wajue watakuja kufanyiwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, miongoni mwa changamoto ni kwa wale ambao walifukuzwa kazi. Katika Bunge hapa tumeambiwa kwamba Serikali imesema watarudishwa kazini, lakini mara tu jambo lolote linapotoka juu likienda kule chini kuna tabia unaambiwa kwamba waraka bado haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano hai katika mambo mbalimbali; kwa mfano mwaka jana tulipitisha hapa kwamba *road license* isamehewe, lakini ukienda

ukafanya *transfer* kule unalipishwa na *TRA,* ukiwauliza wanakwambia kwamba bado waraka haujafika. Jambo likiwa la kuwasulubu wananchi hawaulizi waraka, moja kwa moja linafanyiwa kazi, kwa hiyo hii tabia nayo naomba iachwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wafanyakazi ambao waliachishwa kazi kwa kisingizio cha vyeti feki au hawana vyeti vya darasa la saba; kuna wengine wameachishwa kazi wakiwa tayari katika *QT,* wamefanya mitihani na wanasubiri vyeti vile vya *form four,* lakini wameachishwa kazi. Sasa hili la kuwarudisha ni jambo jema lakini pasiwe na kisingizio cha kwamba waraka haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni vibali vya ajira katika halmashauri. Zoezi hili pia limetuathiri katika baadhi ya vituo vya afya, zahanati na maeneo mengine ya huduma muhimu, watu wamefukuzwa kazi; matokeo yake vituo vya afya havina manesi, hata baadhi ya Madaktari hakuna. Hata katika halmashauri tumepata tatizo kubwa la kuwa na watendaji ambao wanakaimu kwa muda mrefu; hili la kukaimu nalo pia lifanyiwe kazi. Mtu kukaimu zaidi ya miaka miwili inakuwa sio vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri yetu ya Jiji la Tanga tuna mitaa 181, lakini watumishi waliopo ni 123, na tuna upungufu wa watendaji wale wa mitaa 58. Pia tunazo kata 27, tuna watendaji 13 tu, bado tuna upungufu wa watu 14 kama watendaji kata. Kwa hiyo hilo naomba lifanyiwe kazi. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba vibali vya ajira pia vipelekwe katika halmashauri ili tuweze kujaza nafasi za wale watendaji ambao hawapo, hiyo ni kwenye utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye suala zima a TAMISEMI sasa. Kabla sijaanza, najua TAMISEMI inaendana na shughuli nyingi, ni idara au ni taasisi pana ambayo inabeba mambo ya watu wengi. Pamoja na yote katika suala zima la utawala bora kuna kipengele kimeeleza kwamba

mazingira ya utulivu na amani ni fursa adhimu katika kujenga uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote ile. Sasa sisi bado kuna baadhi ya maeneo yamekuwa yanatupa shaka kidogo; huu mpango wa watu kukamatwa halafu hawajulikani walipo lakini familia zao zinahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna tatizo lililotokea tarehe 3, Aprili, 2018 kule Pemba kuna vijana sita walikamatwa, watatu wameachiwa ambao walikuwa ni; Juma Abdallah Kombo (miaka 16), Abdallah Hamisi Abdallah (miaka 19) na Said Shaabani Mohamed (miaka 16), hawa waliachiwa. Bado kuna wengine watatu hawajulikani walipo, mmoja wapo ni Thuwein Nassoro Hemed (miaka 30), Hamisi Abdallah Mattar (miaka 25) na Khalid Hamisi Abdallah (miaka 30). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna mambo mengine, kama alivyozungumza mzungumzaji mmoja jana, kuna baadhi ya mambo yakifanyika ni kama kuitia doa Serikali. Ni bora wale vijana huko walipo wakaachiwa...

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji ambaye anaendelea kwamba vijana hao waliotekwa, ni kwamba sisi tumetoa taarifa kwa Kamanda wa Polisi Kaskazini Pemba na inaonesha kwamba amegonga mwamba. Tumetoa taarifa kwa Kamanda wa Polisi wa Kusini Pemba, hadi sasa amegonga mwamba. Tumetoa taarifa kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar akaahidi kwamba ataweza kulishughulikia lakini hadi sasa hakuna kitu. Tumetoa taarifa kwa Kamishna wa Operesheni Tanzania nzima, Afande Marijani, akasema atashirikiana na sisi, Tumetoa taarifa kwa...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Masoud unachangia au unatoa taarifa? Unachangia sasa... haya maliza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa taarifa kwa Waziri anayeshughulika na mambo ya Utawala Bora, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika, tumetoa taarifa kwa Waziri Mkuu mwenyewe, lakini hadi sasa vijana hawa hawajapatikana; naomba nikupe taarifa mzungumzaji uelewe hali ya ugumu ulivyo, kwamba watu, sio wasiojulikana, ni watu wanaojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Haya. Sasa ulitaka hiyo taarifa yeye aijibu vipi?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, taarifa nimeipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwenye suala la Serikali za Mitaa, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Waziri wetu wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, lakini Mheshimiwa Kapteni Mkuchika sijamsahau, ukizingatia alikuwa ni Mkuu wetu wa Mkoa wa Tanga; nampongeza, lakini haya niliyoyasema ayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika TAMISEMI naanza kwenye elimu. Wanafalsafa mmojawapo, bwana Nelson Mandela, amesikika akisema; *education is the most powerful weapon which we can use to change our world;* lakini pia wapo wengine waliosema *education is the key of life.* Sasa kwa nini natoa mfano huu; Mheshimiwa Jafo katika elimu yetu Tanzania tumekuwa na mitihani mingi sana, bado kuna matatizo ya ukosefu wa walimu wa masomo ya sayansi kama *biology, chemistry, physics* na *mathematics.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pia bado kuna uhaba wa matundu ya vyoo. Mwaka jana nilisema hapa kwamba kuna tangazo la Haki Elimu linaonesha kwamba

mwalimu na wanafunzi wanasukumana kuingia chooni, choo ambacho kiko wazi juu hakina paa, kumejaa maji machafu, wanakanyaga kwenye mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado inahitajika bidii kubwa ya Serikali kuwekeza. Kama vile tulivyonunua magari ya maji ya kuwasha, basi tuhakikishe tunapeleka hata vile vyoo vya bei nafuu katika shule zetu ili kuepukana na tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mitaala yetu ya kielimu; tumekuwa na matatizo ya mitaala kuanzia kwenye *nursery schools, primary schools, secondary schools, colleges* na *universities;* bado kuna matatizo makubwa ya hii mitaala. Kwa mfano katika *nursery* kila mtu anafundisha anavyojua mwenyewe, yaani Serikali haikuweka mtaala maalum, kwamba *nursery* wanatakiwa wafundishwe kupitia nyanja hizi, hakuna hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naishauri Serikali kwamba ni lazima tuwe na utaratibu mzuri. Haiwezekani katika nchi zote za Afrika Mashariki sisi Watanzania mfumo wetu wa elimu, mimi kwa maoni yangu naona tumepitwa na wenzetu wote. Kwa sababu ukienda Rwanda na Burundi leo ni *one child one laptop.* Ukienda Kenya kwa wenzetu wametangaza kwamba elimu bure lakini ni kuanzia *standard one* mpaka *university,* tena hakuna mambo ya mikopo ya wanafunzi wala hakuna matatizo, wanafunzi kazi yao ni kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kwetu kwa sababu mifumo yetu imekuwa ikiingiliana na mambo mbalimbali, matokeo yake kumekuwa na migomo ya mara kwa mara, wazazi wanashindwa kulipa ada kwa baadhi ya watoto wa familia za maskini. Tumetangaza elimu bure lakini kisiasa, kwa mantiki hiyo wengi wana akili, wamefaulu lakini wanabaki nyumbani. Naamini Wabunge wenzangu ni mashahidi hapa; kama hawakufuatwa na watoto 20 basi 30, kila mtoto amefaulu lakini hana *school fees,* hana viatu, hana madaftari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, kama tunasema elimu bure basi angalau kidogo tuwaige wenzetu wa Kenya ili watoto wetu wapate elimu. Unakuta mtoto ananyongeka, yeye amefaulu amefanya kazi ya kusoma lakini familia haina uwezo, mtoto anakaa nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, juzi tarehe 11 Rais Uhuru Kenyatta amesaini sheria kwamba wanafunzi wote wa kike Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Kenya itakuwa inawapa taulo za kike *(pads)* bure, *free, no charge.* Sasa najiuliza; ukiitazama Kenya Mbuga ninazozijua mimi ni Tsavo na Maasai Mara. Sisi tuna mbuga za wanyama, tuna bandari tatu, Kenya wana bandari moja, tuna Mlima Kilimanjaro Kenya hawana, tuna mkonge, katani, pamba, pareto, alizeti na mambo mengine... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Unga mkono hoja, ahsante; unga mkono hoja; kengele ya pili hiyo, umeanza saa kumi na moja kamili wewe, tazama saa ngapi pale. Mheshimiwa Ngwali, ajiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, anafanya vizuri, lakini Katibu Mkuu, mzee Iyombe, ni miongoni mwa watu mahiri ambao wanalazimu watambulike katika utumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na *e-Government,* Wakala wa Serikali Mtandao *(eGA).* Kabla ya kusema chochote napendekeza moja kwa moja kwamba Serikali ituletee Muswada wa sheria hapa Bungeni tuibadilishe *eGA* kuwa mamlaka. Nayasema hayo kwa sababu kama wakala hana uwezo wa ku-*enforce,* yeye kazi yake ni kushauri, hawezi kudhibiti wala hawezi kufanya kitu chochote ambacho hata mlaji anapokataa kufuata zile *regulations* na ile miongozo; kama wakala hana uwezo wa ku-*enforce* sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali ilete Muswada wa sheria hapa tubadilishe. Kwa sababu gani; kwa sababu katika dunia ya sasa ukitazama *research* iliyofanywa na *cyberspace,* inavyofika 2025, *internet users* watakuwa *4.7 billion,* wanafunzi waliohitimu kwenye hisabati, sayansi, *engineering, technology,* watafika milioni kumi na sita kwa mwaka. Ongezeko hilo linahitaji uwepo wa chombo ambacho kitaweza kukabiliana na mabadiliko hayo *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *eGA* ikiendelea kubaki kuwa wakala haiwezi kabisa kukabiliana na mwendelezo huo mkubwa wa teknolojia. Kwa hiyo, niiombe Serikali ilete hapa Muswada na kama Serikali hawakujibu hili jambo tunaweza kupambana. Kadri teknolojia inavyoongezea ndivyo uhalifu unavyoongezeka. Idadi ya watu inavyoongezeka na uhalifu wa mtandao unaongezeka, hatujui sasa *eGA* wametengewa kiasi gani cha kuwawezesha kukabiliana na hali ya teknolojia inavyobadilika; hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya ambapo tunawazidi kwa idadi ya watu ambao wanakwenda kwenye milioni 50 sasa hivi watumiaji wa intaneti ni asilimia 85, wana *about* watu milioni ishirini na tisa. Uganda ingawa wana watu milioni arobaini lakini wanakwenda kwenye asilimia 42, Tanzania bado tumebaki kwenye asilimia 38, jambo ambalo linatufanya; kwanza *eGA* yenyewe ipo kwenye Serikali, haipo mahali popote, haipo *nationwide.* Kwa hiyo, hiyo ni sababu ya kwamba kama hatukuwekeza mapema, kama hatukuwekeza leo, tutajuta kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimalize hili nije kwenye Usalama wa Taifa; na hapa ndipo ambapo mara zote huwa nalisemea suala la Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa nafikiri hawana Kitengo cha *Economic Intelligence Unit.* Mheshimiwa Rais anasema katika mkutano na wafanyabiashara kwamba kuna kiwanda cha sukari hewa kilichokuwa kikiagiza sukari, Usalama wa Taifa hawajui. Baada ya kiwanda kuagiza na kuleta ndipo habari zinapatikana, kabla hawajaleta Usalama wa Taifa haukuiarifu Serikali kwamba jambo hili halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaingia mikataba ambayo inaumiza nchi, *why* Usalama wa Taifa hauiambii Serikali? Au, je, kitengo hiki kwanza kipo na kama kipo kina uwezo gani? Je, teknolojia ipi ambayo inatumia? Mtuambie. Kama ni hivyo kimetengewa kiasi gani kwa ajili ya kuokoa uchumi wa nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapa mfano; kwenye tenda hizi za Serikali, mfano *flow meter* Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda kule kwenye *flow meter* bandarini, akasema kwamba hii *flow meter* itafanya kazi baada ya wiki mbili, *flow meter* haijafanya kazi hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais akasema *flow meter* hii lazima ifanye kazi, *flow meter* haikufanya kazi. Tenda ya kwanza imepelekwa, mtu mmoja kapeleka kampuni sita, kampuni sita zikawa saba wakati wa *submission* akaondoa kampuni zote tano ikabakia moja; Serikali haijui. Wafanyabiashara wale wa mafuta wanachezea, tenda ikafutwa ikawekwa tenda nyingine, *consultant* akapewa bilioni mbili tenda ikaenda ikafutwa, Usalama wa Taifa sasa hivi wao ndio wameichukua tenda ili wafanye wao, haiwezekani. Haiwezekani hivyo, lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama wa Taifa, Mheshimiwa Waziri, nishauri kwamba hiki kitengo kisishughulike na haya mambo madogo madogo huyu kaandika nini yule kaandika nini, mambo madogo, wasimamie maslahi mapana ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na Usalama wa Taifa nije kwenye hoja yangu ya tatu ambayo ni Shirika la Elimu Kibaha. Shirika hili liliingia mikataba mitatu na ndiyo maana nasema Usalama wa Taifa wana matatizo. Katika mkataba wa kwanza ulikuwa na hekta 310 ambazo Serikali imepangisha Shirika la Elimu Kibaha kwenye ile ardhi kwa miaka 66 kwa shilingi milioni 120. Sasa ardhi inapangishwa kwa miaka 66 kwa milioni 120, kweli jamani? Hizo pia zilipwe *cash* ili dola isije ikapanda kwa sababu iko *in terms of dollars.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkataba wa pili wa Kisarawe, kwa Mheshimiwa Waziri Jafo, pamoja na Kibamba, kuna hekta 110 umeingiwa pale na huyu Mkurugenzi kachukuliwa hatua kaondolewa tu; pamoja na yote haya aliyoyafanya lakini kachukuliwa kaondolewa kawekwa pembeni, hakuna hatua yoyote iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama wa Taifa sasa itabidi tusaidie sisi; pale *Tanzania Internal Logistics Center,* Kurasini, pale Serikali imelipa fidia hela nyingi, nasahau kichwani kidogo, lakini baada ya kuwekeza hayo makubaliano na China mwisho wamewekwa kiwanda cha misumari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelipa bilioni sitini, niziache, lakini sasa *logic* yangu ni hii kwamba *why* unawekeza kiwanda cha misumari badala ya kuwekeza ile *hub* ambayo Mheshimiwa Mwijage alituambia Afrika Mashariki ndiyo itakuwa *hub* kubwa; kwa sababu Usalama wa Taifa hawajui kwamba hizo pesa zilizotolewa na Serikali bilioni mia moja kwamba zinafanya kazi anapewa nani. Zilikwenda kwenye mifuko ya watu na sasa kwa taarifa nilizonazo wamewekeza kiwanda misumari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme kuhusu hili ambalo tunalizungumza, juu ya vijana wetu wa Pemba waliochukuliwa. Tuiombe Serikali ya Muungano, sisi ni wenzenu, tukae pamoja tuone hili jambo, ni jambo dogo sana, hakuna sababu ya jambo kama hili tukapiga kelele kila wakati kuwaambia jamani hivi na hivi, hebu tukae pamoja tuone tunalitatuaje; kwanza ni kupatikana hawa watoto.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sophia, jiandae Mheshimiwa Marwa Ryoba.

**MHE. SOPHIA. H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Kwanza kabisa nitazungumzia utawala bora kama wenzangu walivyosema. *CAG* mara nyingi alikuwa akitoa ripoti na ripoti zake nyingi sana zimeeleza ubadhirifu wa mali uliofanywa na Serikali ya CCM. Ninachotaka kushangaa kuna msemaji aliyepita amezungumzia habari ya Chama cha CHADEMA lakini nikaona huyu mwenzangu labda hajasoma kitabu chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wa Chama cha Mapinduzi wamechukua pesa za watu ambao walitakiwa walipwe *pension* kwa *cheque number* 156424 wakazitumia vibaya. Mpaka CAG anakagua hesabu mwezi wa Pili hizo pesa hazijarudishwa. Anazungumzia tujitoe boriti kwenye jicho letu, huwezi kuwa nyoka ukazaa mjusi. Ili uweze kuwa safi pia lazima uzae mtoto safi, makosa ni ya CCM, si ya CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia utawala bora wewe kama kweli ni chama tawala na uko vizuri na unafanya kazi sawasawa na ilani ya chama chako kwa nini unatumia nguvu ya kuzuia upinzani ambao tayari ulipita kihalali na uliusaini na ukakubalika? Huwezi kuwa mzazi, watoto wawili wanagombana mmoja umemshika mkono halafu unajiita wewe ni mshindi, hiyo siyo kweli. Tupewe uwanja sawa, twende viwanjani na sisi tukazungumze, tuone zile kule milioni sita feki mlizotupa kama hatujawapiga 2020. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Wizara sasa, maana na mimi nilikuwa najibu ndugu aliyezungumza. Soko la Kariakoo lilijengwa kwa makusudi ya kusaidia wakulima na kuuza vifaa na pembejeo kwa ajili ya wananchi. Najua ni miaka mingi imepita soko lile kuwa pale, lakini tuna Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inayozalisha mazao mengi; huu ni wakati sasa mngejenga masoko hayo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, Mkoa wa Mbeya ni mkoa ambao uko katikati, una mazao mengi sana,

tunashauri mtupatie masoko ya kimataifa yanayoweza kusaidia wanawake ambao wanalima kwa nguvu zao zote waweze kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiunga na Afrika Mashariki lakini cha kushangaza wenzetu wa Kenya, Waganda wanakuja hadi vijijini kununua maparachichi bila utaratibu unaokubalika. Tukiwa na masoko haya tunaweza tukafanya kazi nzuri na tukasaidia uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia habari ya masoko hayo hayo. Leo hii Mheshimiwa Jafo, Tunduma wamefunga masoko; sijaelewa wanaposema ninyi mnatetea wanyonge, mmepoteza hela ngapi kwa siku ya leo kufunga soko la Tunduma? Sijajua ni kwa nini tunawaachia Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa waamue mambo bila kutumia utaratibu na *professionalism?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri kama kiongozi wa Wizara hiyo, tunaomba Soko la Tunduma lifunguliwe. Tunadaiwa madeni mengi, kwa sababu mwishowe wafanyabiashara wamesema wanatupeleka mahakamani; ni nani atalipa pesa hizo? Halmashauri hii wameifungia Madiwani, kazi haziendi kisa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya. Hapa ndipo ninapoushangaa huu utawala bora Mzee Mkuchika. Naomba ninyi wazee ambao bado mpo na mpo kwenye *system* shaurini Serikali ifanye kazi sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija upande wa mikopo, ilitengwa bilioni sitini na moja kwa ajili ya wanawake na vijana, lakini bilioni kumi na tano ndizo zilizotumika. Idadi ya wanawake ni wengi lakini pesa zilizotoka ni kidogo. Tunaomba waachilie vyanzo vya mapato kwenye halmashauri ili tuweze kukusanya pesa nyingi na kusaidia wanawake na vjiana kwa ajili ya ahadi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ugawaji wa mikopo hii unakwenda kiitikadi... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Marwa Ryoba, jiandae Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anisikilize kwa makini maana Jumatatu nitaondoka na shilingi yake. Mheshimiwa Waziri wa Afya alinipa barua inayoonesha Kituo cha Iramba, Kijiji cha Nyagasense, Kata ya Kenyamonta inapata milioni mia saba; na Waziri wa Afya alituma wataalam wakaenda kule wakahamasisha wananchi wakachangia viashiria wakapeleka mchanga wanasubiria milioni mia saba. Mpaka leo TAMISEMI wamepindua milioni mia saba wamepeleka kwenye jimbo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kenyamonta walimpa Mheshimiwa Magufuli kura, wanataka kutwambia 2020 wasimpe, si ndiyo? Kwa hiyo, nataka majibu Jumatatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka jana Mheshimiwa Jafo ulikuja Serengeti tukampeleka Hospitali yetu ya Wilaya ya Serengeti tunayojenga kwa nguvu za wananchi na wadau mbalimbali na tumemaliza *wing* ya kwanza; akatuahidi na akaniahidi tutapata milioni mia saba, lakini hatukupata. Mwaka huu tena sijaona chochote ingawa ameniahidi kwamba ameweka vizuri na kwamba tutapata milioni mia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja pale Mheshimiwa Waziri, tumempeleka kwenye ile hospitali na ameona jitihada zetu. Amekuja Mheshimiwa Makamu wa Rais tumempeleka pale akaahidi kutusaidia; juzi tumempeleka Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijaona chochote. Hebu naomba Mheshimiwa Waziri aseme kwamba katika Hospitali ya Wilaya ya Serengeti ambayo itahudumia mpaka watalii hawaoni sababu ya kutenga chochote kwa ajili ya wilaya ile? Kwa hiyo, nataka majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye elimu, naomba niongelee elimu bure. Serikali ya CCM sasa hivi kila mtu akisimama anasifia elimu bure. Wametenga na wanapeleka shilingi bilioni mia moja sabini na mbili kwenye elimu. Ukienda kuna matatizo chungu nzima kwenye shule zetu za msingi, watoto kwenye darasa moja wamerundikana, hakuna madarasa ya kutosha. Tuna upungufu nchi nzima wa madarasa laki 264,594.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vyumba vya madarasa ni mbaya. Kwa nini wasingetumia pesa hizi kujenga madarasa? Ukienda kwenye shule zetu hali ya elimu ni mbaya, hakuna Walimu, wameamua kutoa Walimu wa sekondari wanawapeleka katika shule za msingi, kweli wataweza ku-*deliver?* Wata-*deliver* nini? Watafundisha nini? Hali ya Walimu ni mbaya na ukienda kwenye hali ya Walimu wa sayansi ni tatizo kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba tumpigie makofi Mheshimiwa Kikwete, alifanya kazi kubwa sana. Mimi ni mojawapo ya matunda ya Mheshimiwa Kikwete, nilienda *crush program* baada ya kumaliza *form six,* nikasoma mwezi mmoja nikaenda kufundisha. Baada ya miaka miwili nikaenda chuo kikuu nikafanya *Bachelor of Science and education* nikamaliza nikaenda kufundisha, nilikuwa nafanya vizuri na nina wanafunzi wangu sasa hivi ni madaktari; nilifanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kikwete alikuwa *very creative* kwenye suala la ualimu; ndipo Mheshimiwa Kikwete alipoona kwamba kuna tatizo la Walimu wa sayansi akaanzisha *program* maalum chuo kikuu cha *UDOM* ili kukabiliana na tatizo la Walimu wa sayansi. Serikali ya CCM; yuko hapa ndugu yangu Mwalimu wangu Mheshimiwa Ndalichako, hivi kweli wanawapenda watoto wa nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekondari ukienda hakuna Walimu wa hesabu hakuna wa fizikia, hakuna wa kemia, hali ni mbaya, *are you serious,* mko *serious* kweli? Mimi ni

Mwalimu, wakati wa likizo nakwenda kufundisha kule, hali ni mbaya. Wanasema Serikali ya viwanda wanatoa wapi Walimu? Lazima muwe na *special program* kwa ajili ya Walimu wa sayansi, lazima watengeneze *incentives* za kuwavutia wanafunzi kusoma sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hata ukiwa Mwalimu wa sayansi haina maana, ndiyo maana hata mimi niliondoka huko, mimi ni Mwalimu wa kemia na baiolojia. Yaani Mwalimu wa sayansi ukienda kwenye shule za sekondari, Mwalimu kwa mfano wa kemia ni Mwalimu mmoja, labda kemia na baiolojia; unafundisha kuanzia *form one* mpaka *form four*, wanafunzi karibu 2,000, wewe mwenyewe, hakuna *incentives* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, akina Mheshimiwa Jafo washauri Mheshimiwa Rais aje na *special program* kwa ajili ya sayansi. Ndugu zangu tunawashauri bure mkiona ni la muhimu chukueni mkiona halina maana... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimwa Nsanzugwanko, jiandae Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Albert Obama.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natumaini nina dakika kumi leo. Nami kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu nianze kwa kuwapongeza sana wenzetu katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiitazama TAMISEMI kama Serikali ndani ya Serikali yenyewe. Mheshimiwa Jafo na timu yake hongera sana kwa kazi nzuri, yeye na Naibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu wake, Alhaji Iyombe, wanafanya kazi nzuri sana na Naibu Makatibu Wakuu, mama Zainab na Naibu mwingine anayeshughulikia masuala ya elimu, hongera sana kwa kazi nzuri na kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze haraka haraka na hili la hili la takwimu. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Jafo ukurasa wa 58, anazungumzia habari ya *program* ya kuijengea uwezo miji 18, ameitaja pale. Katika ile miji 18 aliyoitaja sikuona Mji wa Kasulu kwa sababu baadhi ya miji aliyoitaja imesajiliwa sanjari na Miji wa Kasulu na Mji wa Kasulu ni mji wa siku nyingi sana. Kwa hiyo, naomba sana katika kumbukumbu zao waweke Mji wa Kasulu katika *program* ile kwa sababu miji ambayo imesajiliwa pamoja na Mji wa Kasulu wameiainisha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 59, Mheshimiwa Jafo amezungumzia juu ya kitu kinachoitwa *program* ya kuendeleza miji 18; bahati nzuri ile miji hakuitaja na amezungumzia habari ya kuboresha na kupanga na uandaaji wa mipango ya *master plan* katika miji. Ni kweli jambo la kupanga miji yetu ni jambo la msingi sana ili miji yetu isiharibike. Sasa ile miji hakuitaja pale, sasa sikuelewa kama hiyo miji ndiyo ile miji 18 au ni miji mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 115, ameendelea kusisitiza juu ya *program* ya ujenzi wa barabara za kuimarisha miji 18. Sasa hoja yangu iko hivi; ukurasa wa 58 anazungumza miji 18, ukurasa wa 59 anazungumza miji 18, ukurasa 115 anazungumza miji 18. Sasa nataka kujua ni miji ipi hiyo? Ni hiyo hiyo? Kama miji ni hiyohiyo pengine wanatumia *criteria* gani kwamba mji huu tunaupanga na mji huu tunauboresha na huu mji tunajenga barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kwamba hoja hii inahusu halmashauri za miji na si halmashauri za vijiji; na pale ukurasa wa 59 amekiri kwamba takribani billioni tisini na moja zitatumika kwa kazi hiyo. Sasa naomba sana; Mji wa Kasulu ni mji wa siku nyingi uko mpakani mwa nchi yetu na ni mji uliosajiliwa tangu mwaka 1974, ni mji wa siku nyingi sana; usiachwe kuingizwa kwenye *Town Authority* ambayo imefanywa sanjari na miji mingine kama Bariadi, Geita na Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana, ule ni mjini wa siku nyingi, naomba watuingize kwenye *program* na hasa hizi *program* mbili, hii ya kupanga miji *(master plans)* na hii ya kuboresha miji, kwa maana ya kujenga barabara za mijini.  Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nijielekeze alikoishia rafiki yangu huyu, kuhusu hoja ya Walimu. Nichukue *line* kwamba kwa Walimu lipo tatizo kubwa la msingi, wana madai mengi sana. Labda nitoe mfano, Walimu wa shule ya msingi katika Mji wa Kasulu wanadai malimbikizo yao tangu Juni, 2016, shilingi milioni mia tatu tisini na sita, *almost* milioni mia nne, hawajalipwa. Fedha za likizo, masomo, matibabu, uhamisho, kujikimu na kadhalika. Kama alivyosema ndugu yangu Ryoba pale, hawa Walimu wanakuwa hawana *incentive* jamani, matokeo yake ni lazima elimu itashuka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia ile hoja aliyokuwa anaijenga Rais wetu Mstaafu Mzee Mkapa ya kuwa na mjadala wa kitaifa kuhusu elimu, lakini yako mambo hata kabla ya mjadala huo tunaweza tukaanza nayo. Huwezi kuwa na Mwalimu anadai matibabu yake tangu Juni, 2016 hajalipwa, hiyo ni kwa msingi.

Mheshimiwa Spika, ukija sekondari kwa sekondari zilizopo katika Mji wa Kasulu wana madai yao ya shilingi bilioni sabini, hawajalipwa hawa. Kama anavyosema mwalimu aliyetangulia hapa, kuna Walimu wa sayansi humu hawana *incentives* hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri, nadhani Mheshimiwa Kakunda ndiye anayeshughulikia sekta hii, kuna mambo ambayo wanaweza wakayafanya sasa ambayo nina hakika kama Walimu wakilipwa mafao ambayo ni stahili zao nina hakika kabisa suala zima hili la elimu tunaweza tukapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, pamoja na shida zote hizi niwapongeze sana Walimu nchini, niwapongeze Walimu wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu, wanafanya kazi

kubwa sana katika mazingira magumu. Nafikiri wakati umefika kabisa Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, wa Utumishi na TAMISEMI kwa kweli kuangalia namna ya kuwapa *incentives* watu hawa, wanafanya kazi kubwa iliyotukuka. Watu hawa kwa kweli ndio wanaolea Taifa letu pamoja na mazingira yote magumu wanayokumbana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa niliseme ni kuhusu suala la afya. Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Kasulu na bahati nzuri alinikuta tukamtembeza, tunamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Kandege. Ushauri wake tuliuzingatia na kile Kituo cha Afya alichokitembelea cha Kiganamo kinakaribia kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nilimweleza jambo moja mahsusi kabisa, sisi katika mji ule tumepata kituo kimoja cha afya na Mji wa Kasulu una wakazi 270,000, yaani Kasulu Mjini na viunga vyake. Naomba sana. Viko vituo vya afya tumeanza kujenga katika Kata za Murufiti, Heru Juu pamoja na Muhunga, tunaomba sasa nguvu ya Serikali ijumuike na nguvu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli mimi hata Mfuko wangu wa Jimbo nimeu-*surrender* kwa kazi hiyo ili akinamama hawa wasipate shida kusafiri kilometa 30 mpaka 35 kufuata huduma katika maeneo ya kutolea huduma Kasulu Mjini, naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyeketi, kuhusu sekta ya afya, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia masuala ya kujenga vituo vya afya; jambo jema sana, jambo lenye afya jambo lenye akili kabisa. Hata hivyo, sikuona hata sentensi moja waliyozungumzia kukarabati hospitali za wilaya kongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hospitali za siku za nyingi, kwa mfano Wilaya kama za Kasulu, Kibondo zina hospitali za siku nyingi na hizo hospital zimekuwa ndizo zinazotoa huduma kwa kweli; na zimekuwa zikitoa huduma

hata kwa halmashauri za jirani ambazo hazina hospitali ambazo ndizo wanazijengea sasa hivi. Kwa mfano Hospitali ya Wilaya Kasulu ambayo ndiyo ya Mji wa Kasulu inatoa huduma Buhigwe, Kasulu DC pamoja na Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo bado ni hospitali ya siku nyingi. Nafikiri kuliko tu kutuachia ile *CDG* Mheshimiwa Waziri ambayo inatusaidia kwenda kurabati kuwe na *program* maalum kama ilivyofanyika 2009 ya kukarabati hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnakumbuka, Waziri wa Afya atakuwa anakumbuka na TAMISEMI watakumbuka walitoa takriban milioni mia sita kwa hospitali nyingi za mikoa kwa ajili ya ukarabati. Ziko hospitali za wilaya, nina hakika ziko wilaya nyingi ambazo zina hospitali kongwe ambazo zinahitaji ukarabati na wangekuwa na *special program* kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Waganga na Madakrati, nalo hili wangeliangalia kwa umakini sana, hasa kwa mikoa ile ambayo ni *disadvantaged,* mikoa ya pembezoni, mikoa yenye shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze Mheshimiwa Waziri, sisi watu wa Kigoma *referral hospital* yetu ipo Bugando-Mwanza ukiacha ile *regional hospital...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tuna Wabunge wenzetu ambao kesho wana uchaguzi Arusha, ni Wanasheria na wamo kwenye orodha, kwa hiyo nitawapa wao wachangie mwanzo ili wawahi kwenda kwenye majukumu ya Arusha.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja naomba Mheshimiwa Jafo ayatilie maanani yote niliyozungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani, baada ya Mheshimiwa Obama ataingia Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais katika Wizara hizi mbili kama zilivyotajwa. Nataka niende moja kwa moja kwenye masuala makubwa yanayohusu eneo langu la utawala, nalo si lingine, ni Halmashauri ya Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha bajeti iliyopita, Serikali ikishirikiana na halmashauri imeweza kufanya mambo mengi makubwa, ikiwemo kusaidia kuimarisha maeneo ya afya, maeneo ya elimu na maendeleo ya vijiji vyetu kwa ujumla wake. Pamoja na jitihada hizo bado yapo mapengo ambayo leo hii ninaposimama hapa nataka nimkumbushe hasa Mheshimiwa Waziri Jafo; kwa sababu kwenye eneo huko la Ofisi ya Rais upande mwingine sina mengi; lakini eneo la TAMISEMI ndiko nina mengi mengi kidogo; nataka nimkumbushe juu ya mapengo machache ambayo naamini tukishirikiana kwa kasi ambayo ameendelea kufanya kazi, tutaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na eneo la afya. Kwanza nianze kushukuru maana tunaelekezwa kwamba usiposhukuru kwa kidogo huwezi kushukuru kwa kikubwa. Katika kipindi cha bajeti iliyopita ndani ya Halmashauri yangu ya Chalinze nimeweza kuletewa zaidi ya shilingi milioni mia saba kwa ajili ya maendeleo ya afya. Katika shughuli hizo tumeweza kufanya mambo makubwa sana kwa mfano kwenye zahanati yetu kule Kibindu, mambo yanakwenda vizuri, naishukuru sana Serikali yangu. Vile vile pale Lugoba nako pia mambo ni mazuri sana na naendelea kuishukuru Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo, upande wa watumishi imekuwa sasa ni kizungumkuti kikubwa sana. Tumeweza kufanikiwa na kama tunavyoendelea kufanikiwa kujenga miundombinu mizuri

lakini kuna upungufu wa Wauguzi na Wakunga imekuwa ni shida kubwa sana. Vifo vya akinamama na watoto vimeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kwa sasa hivi tumevipunguza sana, lakini kwa kweli kukosekana kwa watu hawa ambao ni viungo vizuri sana katika kutimiza eneo zima au lengo zima la Serikali kwa upande wa afya mambo yameendelea kuwa si mazuri sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama aseme neno kidogo ili watu wa Chalinze waweze kufurahi juu ya mikakati mizuri ambayo Serikali imepanga katika kuhakikisha kwamba anatupatia wauguzi na waganga ili mambo ya afya yaweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia mahitaji makubwa ya sasa ni mahitaji ya gari za kupakia wagonjwa. Kama anavyojua Mheshimiwa Waziri alipokuja kwa mara ya mwisho tulimwonesha tulikuwa na magari mengi lakini Mungu naye ana yake. Magari yetu mawili ambayo tulikuwa tunayategema yamepata ajali na sasa hivi imekuwa ni tabu kweli kweli, hasa inapofika wakati wa kuwasafirisha wagonjwa kutoka katika vituo vya afya kwenda katika hospitali kubwa za rufaa; kama ambavyo anazifahamu, kule Tumbi, Bagamoyo na nyingine ambazo zinakwenda Msoga pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika eneo la elimu kilio kinafanana kidogo na kilio cha afya. Jitihada kubwa tumeendelea kuzifanya katika kuhakikisha kwamba madarasa, tunaendelea kujenga nyumba za Walimu. Hata hivyo, ukweli ni kwamba upungufu wa Walimu pia umeendelea kutusumbua. Kwa mfano, kama anakumbuka vizuri katika ile zoezi letu la kukagua vyeti feki tumepata shida sana kwa sababu baadhi ya Walimu walionekana kupungukiwa na sifa na kuondolewa, lakini sasa hivi kwa jinsi ambavyo tunakwenda nina imani kabisa kwamba kama katika bajeti yake mzee atatuangalia vizuri, basi mambo kule nako yataendelea kuwa mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya bajeti sikumbuki ukurasa wa ngapi lakini upo ukurasa anaozungumzia mradi wa uendelezaji wa miji kimkakati. Katika eneo hili sihitaji kusema mengi sana. *Geographical position* ya Chalinze inajieleza, wala sihitaji kueleza kwamba kuna maji, kuna kitu gani. Sielewi wanapozungumzia mikakati ya uendelezaji wa miji kimkakati, maana hapa ni *strategical development* ambayo tunaizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji kama wa Chalinze ambao sasa hivi umeendelea kupanuka na idadi ya watu imeendelea kuwa kubwa, viwanda vimeendelea kushamiri na maendeleo ya mmoja mmoja yameendelea kuwa makubwa; mipango miji, mahitaji ya kijamii kuanzia kwenye upande wa mahitaji ya masoko, afya, elimu na miundombinu yameendelea kuwa ni mahitaji ya muhimu sana kwa mji ule. Hata hivyo, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri niliposoma ametaja maeneo mengine lakini Chalinze sijaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tu kujua ni mkakati gani alionao Mheshimiwa Waziri katika miji kama hii ambayo kwangu mimi naona kama ndiyo sehemu ya kupumulia kwa Mji mkubwa kama wa Dar es Salaam kwa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo, lipo jambo ambalo pia limekuwa kizungumkuti na nafikiri kwa namna moja ama nyingine tumelizungumza sana katika vikao vya maendeleo ya Mkoa, hili jambo la *TARURA.* Ni kweli *TARURA* imeanza kufanya kazi na matunda katika baadhi ya maeneo tumeyaona. Hata hivyo, sisi ndani ya halmashauri ambako ndiko tunakoibua miradi ile mara nyingi tunapokuja kutekelezewa miradi ile na *TARURA* hatuoni ile tija ya yale ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja; iko barabara inayotoka kwa Ruombo mpaka Kijiji kinachoitwa Kwa Mduma. Barabara hii umbali wake unakaribia kufika kilometa 12, lakini ilipopelekwa katika *TARURA,* ilipokamilika

zilizokuwa zimetengenezwa ni kilometa nane tu. Sasa tunaomba tujue, hii mipango ya *TARURA* inakaakaa vipi? Wanajipangaje na je, ni lini tunaweza tukafikia malengo tajwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia tunatambua uchache wa fedha katika eneo hili. Kwa hiyo nafikiri siku nyingine tukikaa na *TARURA* wetu hawa, tukaenda kwa pamoja, tujadiliane nao juu ya vipaumbele ambavyo wananchi wanavitaka halafu wao watuambie. Sisi tunaposema barabara ya kutoka kwa Ruombo kwenda kwa Mduma maana yake tunaelewa umuhimu wa barabara ile. Sasa mtu akija akitengeneza barabara ile ya kilometa nane halafu yale malengo ambayo tunayakusudia sisi kama Halmashauri hayafikiwi nina uhakika kabisa hata malengo hayo ya Serikali Kuu pia hayatafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo pia, niendelee kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayoendelea kufanya katika kuhakikisha kwamba tunahakikisha halmashauri zetu zinapata mapato ya kutosha. Mheshimiwa Waziri katika hatua hizi ningeomba sana tuendelee kuangalia vyanzo vipya tena, tuendelee kuhamasisha halmashauri zetu ziendelee kupata maendeleo katika kutatua au kuamsha vyanzo vilivyo vipya. Wameeleza waliotangulia hapa kwamba katika fedha ambazo zimepelekwa ndani ya Halmashauri zetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Obama jiandae Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hizi mbili ambazo zimewasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba niwapongeze na hasa nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendesha Serikali yake vizuri, lakini wakisaidiana na Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nitoe pongezi kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Jafo na Naibu Mawaziri wake wawili, Kandege na Kakunda lakini na Mzee wetu Mheshimiwa Mkuchika, hongereni kwa kazi nzuri sana. Vile vile tuwape pongezi Makatibu Wakuu wao wanaowasaidia kwenye shughuli zao, Mungu awape wepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mkuu wangu wa Wilaya, Kanali Gaguti ambaye ameteuliwa jana kuwa Brigedia Jenerali; amefanya kazi nzuri sana kwenye Wilaya yetu, sasa Rais na Amiri Jeshi Mkuu amempandisha hadhi na ameambiwa aweze ku-*report* Makao Makuu ya Jeshi. Kwa hiyo Wilaya yetu itabaki bila kuwa na Mkuu wa Wilaya lakini tunamtakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo amefanya kwenye Jimbo la Buhigwe. Kazi nyingi zimefanyika katika muda mfupi na huku Wilaya yenyewe bado ni changa. Naomba niwapongeze kwamba tunajenga Ofisi ya Mkurugenzi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inaendelea vizuri, kwa hiyo hiyo ni *complementary* yao. Ujenzi wa hospitali ya Wilaya unaendelea ambapo wametupatia milioni mia nne hamsini, wametupatia milioni mia tano na sasa wametupangia bilioni 1.5, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo ch afya milioni mia nne, nashukuru sana Mheshimiwa Jafo kwa kutupatia kituo hiki. Pia nimpongeze Mheshimiwa Kandege kwa kwenda kukikagua na kukiona na niwashukuru sana kinaendelea vizuri na wananchi wanafurahia, wanabaki wanasubiri tu watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunacho Kituo kingine cha Afya cha Muyama ambacho tulisaidiana na *World Vision* ambacho sasa nacho kimeshaimarika na kinaendelea na upasuaji. Hiyo yote ni juhudi ya Serikali, tunaomba tuwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari za wagonjwa kwenye Jimbo la Buhigwe zinatosha kwa sababu kila kituo kilichopo kina gari jipya, kwa hiyo tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi ya maji inayoendelea ambayo ni juhudi zenu, lazima niziseme kama Mwana CCM. Tunayo miradi ya Nyamugari inaendelea, Nzeze, Kirungu, Mbanga, Myegela, Mgela, Kasumo, Nyanga hii yote ni miradi ya maji ambayo inaendelea kwenye Jimbo langu, kwa hiyo kwa kweli kwenye maji bado tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunao mradi mmoja wa Mnanila unaokwenda Mkatanga na Kata ya Mwayaya; huu ni kati ya ndugu zetu Wabelgiji ambapo kwa kweli wa mradi huu bado hauja-*take off,* tungeomba Ofisi ya *RAS*-Mkoa ambayo ndiyo *link* na hawa Wabelgiji ili tuweze kuendelea na mradi huu kwa sababu watu wa Manyovu na Mnanila wanauhitaji huu mradi. Vile vile tunaendelea, kwa kibali chenu, tunaendeleza kupeleka maji Kilelema na Migongo, Wakandarasi bado wanaendelea kutafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasambaza maji, tumepeleka andiko kwa Mheshimiwa Waziri na kupitia Waziri wa Maji, maji ya Mji wa Buhigwe ambao utaweza kusaidia Vijiji vya Songambele, Kavomo, Mlela, Buhigwe, Bwelanka na Kibande, hilo andika tunasubiri majibu tuweze kuona kwenye bajeti ya 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya ningependa kuomba yafuatayo:-

Tulikuwa na mkataba wa hospitali yetu ya Heri *Mission* ambayo iliingia mikataba na halmashauri kwa ajili ya kusaidia akinamama, watoto na wazee, kwa sababu yale

maeneo hatukuwa na kituo cha afya, lakini kwa maelezo yao walileta mkataba wa kusitisha ili huduma hii isiendelee. Sasa wananchi wanapata adha kwa sababu hakuna hopsitali ya karibu kwa sababu hospitali ya wilaya sasa ndiyo tunajenga. Tungeomba waturudishie hii huduma, ule mkataba ambao Katibu Mkuu aliandika ili akinamama hawa waendelee kupata huduma la sivyo, tutapata shida, lakini tutakapomaliza hospitali ya Wilaya wanaweza waka-*cancel* mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishukuru Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, tumetengewa bilioni mbili na milioni mia nne kwa ajili ya kujenga soko zuri la Kimataifa pale Mnanila. Hili ni soko ambalo litakuwa na vyumba 300 vya kuuzia bidhaa, tutakuwa na vizimba vya kuuzia bidhaa 500, kutakuwa na vyumba vya Benki, kwa hiyo ni jambo kubwa. Tunachoomba, hiki kitakuwa ni chanzo cha mapato ya halmashauri lakini pia wafanyabiashara watapata eneo la kufanyia biashara. Tunaahidi kwamba tutautendea haki mradi huu, tunahitaji, tungependa tuone fedha hizi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu; naomba tu pamoja na changamoto zote zilizopo kwenye Wilaya yangu ya Buhigwe; Wilaya yangu ya Buhigwe kwenye ufaulu katika nchi hii ni ya 21 katika Halmashauri 189. Kwa hiyo ningependa tu niwapongeze Walimu kwa changamoto zilizopo lakini Buhigwe sisi kwenye ufaulu katika nchi hii ni watu wa 21 kati ya 189. Kwa hiyo nawapongeza na waendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma, kwa wale ambao hamna taarifa ni Mkoa wa 10 katika mikoa ya Tanzania hii. Kwa hiyo msije mkafikiri tuko nyuma sana mkafikiri kwamba watu hawafanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya maboma ya madarasa kuezekwa; tungependa kuwe na *special program*. Wananchi wamejitolea, tunayo maboma karibu 17 kwenye Jimbo langu sasa tungependa kupata nguvu angalau tuweze kuezeka. Ilani ya Mheshimiwa Waziri

ilisema kwamba tukiweza kufikisha kwenye lenta wao wanaweza wakatusaidia kuezeka. Kwa hiyo, nalo hilo tungeomba watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu tunataka kupandisha shule nne ili ziwe kidato cha tano. Shule ya Myama, shule ya Buyenzi, shule ya Mkoza, pamoja na shule ya Munzeze tungepanda nazo zipande kuwa kidato cha tano kwa sababu sasa watu wanafaulu vizuri ili waweze kupata sehemu ya kwenda kusomea elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* miundombinu. Mheshimiwa Rais JPM alikubali kwamba kwa kuwa wilaya yetu tumehamisha makao makuu, vijiji namna ya kuungana imekuwa ni tatizo; alikubali kwamba ataweza kutupasulia barabara mpya ili ziweze kuunganisha vijiji na vijiji na Sheria ya *TARURA* inasema kwamba wao hawawezi kupasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapeleka ombi na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais; tunayo ya kutoka Kijiji cha Nyakimwe kwenda Muhinda, Munzeze kwenda Kwitanga, Rusaba kwenda Nyarubanda, Myegera kwenda Songambele, Kilelema kwenda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu ya mwisho. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa, jiandae Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii na kwa niaba ya Wandengereko wote duniani

tunakushukuru sana na tunakuombea dua kwa kuwa Mbunge wao sasa ameweza kusimama na kuzungumza mbele ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamewasilisha taarifa zao, Mheshimiwa Suleiman Jafo kaka yangu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa kweli niseme tu kwamba wanafanya kazi nzuri. Hata hivyo, pamoja na kwamba wanafanya kazi nzuri Watanzania wanaendelea kuwaombea dua pamoja na kuiombea Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi iendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tunatambua kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano sasa imeridhia kuwarejesha baadhi ya watendaji wale ambao wana vigezo maalum kuweza kurejea kazini. Hii ni pongezi kubwa sana, kwa niaba ya watendaji wote nchi nzima wanaishukuru sana Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akumbuke kwamba miaka ya 2000 walikuwepo Watendaji wa Vijiji ambao walifanya kazi kwa kujitolea ambao kabla ya tamko la mwaka 2003 watendaji hawa mwaka 2004, Waziri wa Utumishi aliyekuwepo wakati ule, Brigedia Ngwilizi alitoa tamko la kutoa ajira kwa Watendaji wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora aweke kumbukumbu zake vizuri sana. Wakati wa tamko lile la mwaka 2004 ambalo lilipelekea kuajiriwa watendaji wengi wa vijiji hususani vijiji vyangu karibu vyote vya Wilaya ya Rufiji, watendaji wale hawakuwa na sifa ya kuwa na vyeti vya utumishi. Mwaka 2006 tamko lililofuata liliwataka watendaji waajiriwe kwa kuwa na vyeti vya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tumshauri vyema Mheshimiwa Rais atambue kwamba wapo watendaji walioajiriwa mwaka 2004 bila ya kuwa na vyeti vya utumishi. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu iwapo leo hii tunasema kwamba watendaji wale waondolewe kazini kwa kuwa hawakuwa na vyeti, lakini vigezo vya ajira mwaka 2004 havikuwataka wao wawe na vyeti vya utumishi.

Mheshimiwa Waziri iwapo tutaamua kuwaondoa kazini watendaji hawa tunavunja mambo mengi ya kisheria hususan Sheria za Kazi. Pia niwashauri watendaji wote nchini wale ambao wanaangukia kwenye tatizo hili; iwapo barua zao za ajira zinaonesha kabisa kwamba hawakupaswa kuwa na vyeti vya utumishi, basi wasilalamikie katika mioyo yao, wasisite kwenda kwenye Mahakama za kazi ili waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu watendaji hawa hawana makosa, kosa ni letu sisi wenyewe viongozi wa Serikali ambao tulitoa tamko la ajira kwa watumishi ambao hawakuwa na vyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwa Ndugu yangu Mheshimiwa Suleiman Jafo, nimshukuru sana kwa kazi nzuri aliyoifanya; lakini kipekee kabisa nimshukuru kwa kiasi cha fedha alichokitoa kwa ukarabati mkubwa wa Kituo chetu cha Afya cha Ikwiriri, tulipokea shilingi milioni mia saba. Hata hivyo nimwombe na nimkumbushe, aliwaambia wananchi wa Rufiji kwamba atawapatia kiasi cha shilingi milioni mia saba nyingine kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kule Mwaseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, nimwombe Katibu Mkuu kama maagizo haya anayo basi kuhakikisha kwamba kiasi hiki cha fedha kimekwenda; na wananchi wa Kata ya Mwaseni tayari walishaandaa mazingira ya ujenzi wa kituo cha afya kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Kata ya Mwaseni ndipo tutakapozalisha umeme wa *Stieglers' Gorge.* Kwa hiyo utoaji wa fedha hizi milioni mia saba ni muhimu sana, kwa sababu tunategemea kwamba *population* ya wananchi wa Kata ya Mwaseni itakuwa kubwa sana. Kwa kuwa sasa Mbunge wao amepambana kuhakikisha kwamba *Stieglers' Gorge* sasa inarejea na sisi tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais. Tumwombe sana Mheshimiwa Waziri, kiasi hiki cha fedha sasa kiweze kufika na wananchi wetu wa Kata ya Mwaseni waweze kupata kituo cha afya kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatambua kazi ya Waziri, Mheshimiwa Suleiman Jafo ni nzuri sana. Yeye ni mchapakazi kwa ajili ya wanyonge; wananchi wa Rufiji wanaomba nyongeza ya *ambulance* kwa ajili ya Kata hii ya Mwaseni pamoja na Tarafa nzima ya Mkongo, pia katika Kata ya Mbwala kuna uhitaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea katika elimu nimwombe Mheshimiwa Waziri atambue kwamba Rufiji tumetoka katika matatizo makubwa sana mwaka 2017, matatizo ambayo yalitisha nchi nzima katika maeneo ya Rufiji, Mkuranga pamoja na Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue matatizo haya yalisababishwa na mambo mengi, lakini miongoni mwa mambo haya lazima tutambue kwamba wananchi wengi asilimia karibu 90 ya wananchi wa Rufiji, vijana wanaoanza darasa la kwanza hawaendelei kidato cha nne, hawaendelei kidato cha sita. Niseme zaidi ya asilimia 95 ya vijana wanaoanza darasa la kwanza hawaingii chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, yako mengi yanayosababisha vijana kushindwa kuendelea na shule, yako mambo mengi sana. Pia katikati ya mambo haya ni mazingira ya shule, umbali wa shule zenyewe tulizonazo na pia ziko baadhi ya kata ambazo hazina shule zetu za kata kwa mfano Kata ya Ngarambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Ngarambe kuelekea Utete ni zaidi ya kilometa 68. Huwezi kuamini kwamba kijana anayefaulu kidato cha nne anapaswa kwenda kusoma Utete ambako anatakiwa atembee kwa kila siku kilometa 68. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, upendeleo na dhamira ya Serikali kuona umuhimu wa kunyanyua elimu katika maeneo ambapo mwamko wa elimu ni mdogo; si dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ipo hata katika Katiba ukiisoma ibara ya nane (8) ya Katiba inazungumzia umuhimu wa Serikali kunyanyua ustawi wa maisha ya wananchi wake. Tunapokwenda kunyanyua ustawi wa maisha wa wananchi tunazungumzia umuhimu wa maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atambue kwamba nchi yetu hii ipo jamii ya tabaka la wananchi wenye maisha duni na dumavu. Tabaka hili ni miongoni mwa tabaka la wananchi wa Rufiji pamoja na maeneo mengine ya Kibiti. Pia yapo maeneo ya tabaka la wananchi wenye maisha endelevu, yako maeneo hayo, ameyazungumzia katika ukurasa wa 56 wa hotuba yake katika mchakato wa kuboresha miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tunapokwenda kuboresha miji tuangalie maeneo yenye matatizo makubwa, maeneo ambapo kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara. Kwa mfano, Rufiji mwaka 2007 yalitokea machafuko makubwa kati ya wakulima na wafugaji, lakini mwaka 2017 kumetokea matatizo makubwa ya amani kila mmoja anafahamu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati amedhamiria kwenda kutatua matatizo haya na tunaipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya, tuangalie sasa uwezekano wa Serikali kwenda kubadilisha kabisa hali ya maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liliwahi kufanywa na Mwalimu Nyerere miaka ya 70 ambapo aliongeza mwamko wa kutoa elimu na kuwasaidia wananchi wenye matatizo makubwa ya elimu na ya kiuchumi. Miongoni mwa watu

walionufaika tunaye Profesa Kabudi alinufaika na mpango wa Mwalimu Nyerere wa mwaka 1973 na niiombe Serikali sasa kipekee kabisa...(*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha, Mheshimiwa Joram Hongoli, jiandae Mheshimiwa Omary Badwel.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hizi mbili TAMISEMI na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa shughuli anazozifanya za kuhakikisha kwamba anatetea maisha ya Watanzania na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pia kwa namna ya pekee nichukue fursa hii nimshukuru sana kwani katika jimbo langu aliweza kutoa vitanda 25 , vitanda 20 vikiwa ni kwa ajili ya wagonjwa wa kawaida na vitanda vitano kwa ajili ya *labour,* nashukuru sana .

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Suleiman Jafo kwa jinsi anavyojituma katika kuhakikisha kwamba anaisimamia vizuri Wizara yake ya TAMISEMI. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Mkuchika pia naye anajitahidi kusimamia kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. Niwapongeze pia Naibu Mawaziri wote Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege; niwapongeze Katibu Mkuu injinia Musa Iyombe, niwapongeze Naibu Makatibu Wakuu kwa namna wanavyofanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba wanawaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi wanazofanya Wizara hizi zote mbili ni kazi zinagusa maisha ya Watanzania, zinagusa maendeleo ya wananchi. Maana sote tunajua kwamba Wizara hizi hasa Wizara ya TAMISEMI inahusika sana na huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, vituo vya afya, ujenzi wa barabara na hakuna eneo ambalo shughuli hizi hazifanyiki, kila kijiji na kila eneo kama ni mjini na vijijini kote shughuli hizi zinaendelea. Kwa hiyo wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanyonge wanapata maendeleo, kwa hiyo nawapongeza wote kwa maana ya mawaziri lakini pia na watumishi wote wa Wizara zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kazi wanazofanya zinagusa maisha ya watu, niombe sana Mwenyezi Mungu awasaidie ili kuhakikisha kwamba wanasimamia vizuri hasa *recourses.* Pesa wanayoiomba ni trilioni 6.58, ni fedha nyingi lakini ndogo kutokana na jinsi matatizo yaliyopo huko kwenye maeneo yetu yalivyo mengi, kwa hiyo niwaombe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana hasa kwenye zile fedha za maendeleo hasa zile zinazotokana na wafadhili, tujitahdi kusimamia vizuri kwa sababu tusipozisimamia vizuri zinaweza zikasababisha manung'uniko katika baadhi ya maeneo. Halmashauri yetu sisi ya Wilaya ya Njombe ipo Mkoa wa Njombe na ni Halmashauri mama ya Mkoa. Mkoa wa Njombe una halmashauri sita na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ndiyo iliyozaa halmashauri hizi zote; na sasa hivi *resources* zake zote zimekuwa zikigawanywa kwenye halmashauri nyingine na imebaki halmashauri mzee ambaye hana kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri hii pamoja ni kwamba ni halamashauri mama ni halmashauri pekee ambayo haina hospitali ya wilaya, halmashauri zote tano za Mkoa wa Njombe zina hospitali za wilaya lakini Halmashauri hii ya Wilaya ya Njombe haina hospitali hata moja ya Serikali lakini pia hata ya binafsi hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo vya afya vinne tu; tuna Vituo vya Lupembe, Matembwe, Kichiwa na Sovi. Vituo hivi vyote vilikuwa havina huduma ya upasuaji. Mpaka mwaka 2015 tulikuwa na kituo hicho kimoja cha Lupembe tukaongeza vikawa baadaye vinne na sasa hivi tunajenga kituo kingine cha pale Ikuna ambacho tupo kwenye umaliziaji *(finishing),* kwa hiyo si muda mrefu tutakuwa pengine na vituo vitano vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2016 nilivyoingia Bungeni hapa, nimekuwa nikiomba Kituo cha Afya cha Lupembe kipewe fedha kwa ajili ya kujenga *theater,* kutoa huduma ya *theater* na kujenga wodi. Kituo hiki ni cha muda mrefu sana, mwaka 1985 ndipo kilipoanza kazi yake, kwa hiyo ni kituo ambacho kimeshachakaa. Hata hivyo, bahati mbaya hatujapata hizo fedha pamoja na kwamba tulikuwa tumeahidiwa muda mrefu, lakini hatujapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa kuwa na sisi tulianza kujipanga kuhakikisha kwamba wananchi wetu wale wanapata huduma ya upasuaji, baada ya kuona akinamama wanafariki wanafia njiani kwa kukosa huduma ya uzazi. Kwa hiyo kwa uchungu huo tukaamua kujipanga na mimi Mbunge kwa kushirikiana na halmashauri tukajenga jengo la mama na mtoto. Mimi nilichangia bati katika lile jengo kwenye fedha binafsi nje ya Mfuko wa Jimbo na halmashauri imesaidia wananchi wamefyatua tofali na tukajenga lile jengo ambalo Mheshimiwa Kigwangalla alikuja na akalaifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla alipokuja tulimwomba fedha kwamba tupate angalau fedha kidogo kwa ajili ya huduma hii ya upasuaji lakini mpaka leo hatujapata. Hata Kituo kingine kila cha Kichiwa tuliomba tupate fedha na wananchi wameshafyatua tofali tayari, lakini mpaka leo hii hatujapata fedha yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mwezi wa Pili tumeambiwa kwamba tukae kikao kuna fedha milioni mia sita zitakuja, tukakaa vikao vyote Kamati zikakaa kwenye

halmashauri yangu na Baraza la Madiwani likakaa, tumetuma Mkurugenzi na Mwenyekiti wamekuja hapa lakini wamerudi bila fedha. Nitaomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atakaposimama basi tuweze kupata ufafanuzi angalau wa hizi fedha milioni mia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Jafo, katika bajeti tumeona kuna hospitali ya wilaya itaaanza kujengwa na wametutengea shilingi bilioni 1.5 nashukuru sana. Hata hivyo pamoja na kutenga hizi fedha tunaomba hizi fedha kwenye hivi vituo ili tuweze kujenga chumba cha *theater room* na vyumba vingine vinavyohitajika ili hatimaye wananchi wetu hawa wasiendelee kufa kwa sababu ya kutekeleza jukumu lao la msingi la kuongeza wanadamu hapa duniani, kwa hiyo namwomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya barabara kwa maana ya *TARURA. TARURA* kwangu wanafanya kazi nzuri sana lakini wanakwamishwa na fedha, bado fedha haziendi za kutosha. Sisi kwenye halmashauri yetu tuna mtandao wa barabara ambao una kilometa 586 na zaidi, lakini fedha kwenye bajeti mwaka jana tulipangiwa biloni 1.1, tukapata miloni mia saba na milioni mia nne zimeenda kulipa madeni ya mwaka wa fedha ulioisha, kwa hiyo tumebakiwa na milioni mia tatu. Sasa ukiangalia mtandao wa barabara ulivyo na kiasi cha fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Badwel na jiandae Mheshimiwa Zakaria Isaya naona hayupo nafasi yake dakika tano Mama Sitta na dakika tano Mheshimiwa Flatei, kwanza Mheshimiwa Badwel.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara hizi mbili ambazo ziko mbele yetu. Kwanza naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri pamoja na Naibu Mawaziri wao na wasaidizi wao mbalimbali ambao wamekuwa wakishirikiana nao katika kufanya kazi mbalimbali za maendeleo za nchi yetu kupitia Wizara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi ambao serikali baada ya kuwaondoa katika utumishi na baadaye imekubali kuwarudisha. Kwa kweli nawapongeza sana, lakini pia nawapa pole kwa madhira waliyoyapata katika kipindi kila cha miezi mitatu ambao hawakuwepo kazini. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa kusikia ushauri wa Wabunge na kuwarudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri maamuzi magumu na yanayolenga maisha ya watu kama hivi wakati mwingine kwa kweli Serikali itafakari kwa kina kabla haijachukua maamuzi magumu kama haya. Pengine sisi Wabunge wakati mwingine isitoshe tu kuishauri Serikali kufanya maamuzi tofauti na waliyoyafanya awali, lakini pia wakati mwingine tuelekeze pia kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini viongozi waliohusika walishauriwa pia na watendaji ambao hawakuwashauri vizuri mpaka wakachukua maamuzi haya. Nao wawajibike wakati mwingine waone uchungu wa kutoka kazini na namna ambavyo walikuwa wakitegemewa na watu mbalimbali na dhoruba ambayo wanaipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nashukuru mpango amaboa umeletwa na Wizara juu ya fedha za *CDG* kutumika katika miradi michache ambayo itaweza kukamilika kwa wakati na kuweza kutoa huduma tofauti na miradi ambayo tulikuwa tunafanya kidogo kidogo. Huo

ni mpango mzuri na sisi Bahi tumeiga hata kwenye bajeti hii ambayo tumependekeza sasa kuwa na miradi michache lakini ambayo itaweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachokiomba Serikali izileta hzi fedha. Ukiangalia fedha hizi za *CDG* kwa mfano Wilaya ya Bahi tumepangiwa bilioni moja na milioni mia mbili, na sasa imebaki miezi mitatu muda wa mwaka kwisha, lakini hakuna hata senti tano ambayo imekuja. Kwa hiyo ni vizuri sasa hizo fedha zikaletwa, tukiwa bado tupo Bungeni hizi fedha tuzione zimekwenda kwenye Wilaya zianze kufanya kazi ambayo kwa kweli tulikuwa tumekusudia na kuipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunakubali miradi mingine ya Kitaifa inakwenda. Ukiangalia kila mahali miradi ambayo inasimamiwa kitaifa inakwenda, lakini miradi ya halmashauri haiendi halmashauri hazina fedha. Tuna watumishi wengi kule mpaka unafika mahali nasema tunawalipa mishahara bure kwa sababu hakuna fedha ambazo wanaweza kuzisimamia kuleta maendeleo kwenye halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kweli imeweka watumishi wengi na ni wataalam na wana sifa mbalimbali na wakipewa fedha wanaweza kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo wakishirikiana na wananchi; basi fedha ziende pia kwenye halmashauri zetu. Isiwe baba tu sasa anaonekana Serikali Kuu anafanya kazi lakini halmashauri ambayo sasa inachukuliwa kama watoto hawafanyi kazi. Hata sisi wazazi tunakwenda kazini na watoto tunawapeleka shule, kwa hiyo pia wazazi na watoto wapewe haki sawa katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za bajeti katika maendeleo mbalimbali ukiacha hizi fedha za *CDG* nazo pia zinapashwa kwenda katika halmashauri zetu ili ziweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa. Kuna miradi mingi ya wananchi ambayo wameifanya kule ya kujenga zahanati, nyumba za Walimu, madarasa na tuliwaaambia wajenge

mpaka hatua fulani halafu Serikali itakwenda kuwasaidia. Tunasubiri fedha hizo wazipate ili waweze kufanya hiyo kaiz ya kumalizia majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboma haya yamekaa muda mrefu, mahali pengine hata sisi viongozi kama Wabunge tunaona hata aibu kwenda katika baadhi ya vijiji. Umewahaidi wananchi mwaka huu kwamba tutatenga fedha, tunatenga kweli halmashauri lakini fedha zile haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mifano mimi kwangu kule Bahi kuna kujiji cha Mayamaya wamejenga zahanati mpaka wamefika hatua ya visusi huu mwaka wa tano. Kuna kijiji cha chonde wamejenga zahanati wamefika hatua ya visusi huu ni mwaka wa tano na Mbunge unakwenda kila mara unafanya mikutano unabaki na hadithi ile ile, mwaka huu tumewatengea fedha milioni arobaini, unakwenda mwakani tumewatengea fedha milioni arobaini. Mwisho wanatuona na sisi ni watu ambao tunawadanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Serikali ifanye tathimini, iwatake Wakurugenzi kufanya tathimini ya miradi yote ya wananchi ambayo imekwama kwa muda mrefu. Uandaliwe mpango kabambe wa kwenda kumalizia haya magofu, yatatuletea shida wakati tunakwenda kwenye uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa, lakini pia itatuletea shida kwenye uchaguzi tunaokwenda wa mwaka 2020. Ni vizuri Serikali ikachukua hatua madhubuti kama ambavyo inachukua ili kukamilisha hii miradi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Bahi imegawanywa miaka 10 iliyopita, lakini watumishi waliotoka hapa Dodoma wakati huo tunakaa hapa Dodoma kama Makao Makuu ya Wilaya ikiwa Dodoma Vijijini mpaka leo huu mwaka wa 10 wamehamia Bahi hawajalipwa mafao yao ya uhamisho. Kwa kweli ni kitu cha ajabu sana. Watu wanasubiri miaka 10, wako waliostaafu, wako waliokufa, wako waliohama kwenda wilaya nyingine, wako waliobaki pale Bahi mpaka leo hawajalipwa fedha zao za uhamisho, miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na wakati wa kushika shilingi nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri mpaka aniambaie ni lini atawalipa hawa watumishi wa Bahi milioni mia nane sabini wanazodai kwa kipindi cha miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*. Tunaipongeza Serikali na sisi Wabunge wenyewe ndio tumetunga sheria ile ya *TARURA* hapa, lakini upo upungufu katika ufanyaji kazi wa *TARURA*. Ukiangalia katika mchango wa Waheshimiwa Wabunge hapa wako Waheshimiwa Wabunge ambao wameshukuru sana namna ambavyo unashirikiana vizuri na *TARURA*, lakini wako Waheshimiwa Wabunge wameonesha tu kasoro katika namna ambavyo *TARURA* inashirikiaa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali pengine wako Mameneja wa *TARURA* wamejisifu wanasema sisi ni chombo pekee, sisi ni chombo maalum, lazima Mheshimiwa Waziri kauli hii waiondoe waelekeze kwamba wao ni wakala na mimi najua wakala yeyote anafanya kazi kwa niaba ya mtu fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa kama ni wakala ina maana wanafanya kazi kwa niaba ya halmashauri na ndio wenye barabara wanapashwa kuripoti, wanapashwa kushirikiana na Mkurugenzi, wanapashwa kuhudhuria vikao mbalimbali vya halmashauri ili Madiwani ambao ndio wenye hizo barabara, ndio wanatekeleza ilani, ndio waliowaahidi wananchi kutengeneza barabara nao waweze kutoa ushauri katika utengenezaji wa barabara na kusimamia katika utengenezaji wa barabara zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa mara ya kwanza kututengea fedha katika bajeti hii za hospitali ya wilaya, jambo hilo tunalishukuru sana. Hata hivyo, nashauri, kama ambavyo tumetumia *force account* kwenye miradi ya vituo vya afya ambavyo pia wametupatia pesa na tumeona ufanisi mkubwa katika kutumia *force account* kwenye

ujengaji wa vituo vya afya. Hizi fedha Wizara ielekeze nazo pia zitumike kwa mtindo wa *force account.* Hizi bilioni moja na nusu zinaweza kufanya kazi kubwa na kama upungufu unaweza kuwa kidogo tu kabla ya kukamilisha hizi hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI wamekuwa wakitupangia watumishi na wamekuwa wakituletea watumishi, tunaomba waache kutupangia vituo, watuletee watumishi kwenye halmashauri, Mkurugenzi ndiye apange vituo vya hawa watumishi. Leo wanaleta Walimu 20 halafu wanawaandikia na majina ya shule wakati pengine shule ile wanayompelekea haina upungufu kama ambavyo shule ambayo hawakuitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri katika maeneo ya watumishi Walimu, watumishi wa hospitali na watumishi wa kada zingine wamletee Mkurugenzi, wamwambieni hawa ni wataalam fulani, yeye atawapangia vituo vya kazi kulingana na yeye anavyoona wapi pana mahitaji muhimu, kuliko kutupangia moja kwa moja kutoka Wizarani. Kwa kweli wamekuwa hawatutendei haki na mara nyingine wanakwenda kurundika watumishi mahali ambapo tayari walikuwepo na shule ya pili au ya tatu inakuwa haina watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza kwa kuondoa riba ya asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya akinamama na vijana, lakini wahakikishe inafika. Kuondoa riba tu peke yake bila fedha hizi kutengwa haiwezi kusaidia kwa sababu wako Wakurugenzi katika kutenga hizi fedha wanaamua wanavyotaka, akijisikia kutenga anatenga... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Mama Sitta dakika kumi.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie. Kwanza, namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi lakini pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Mkuchika na Naibu wao; Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege na Makatibu Wakuu; Mhandisi Iyombe na Dkt. Ndumbaro na Naibu wao; Dkt. Chaula na Ndugu Nzunda pamoja na watendaji wote wa taasisi za *TASAF,* MKURABITA na Mfuko wa Rais, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Mungu awasaidie na naomba Serikali iwaongezee fedha waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ni muhimu kwangu kwa niaba ya wananchi wa Urambo kuishukuru Serikali kwa kutupa *ambulance,* ahsante sana itatusaidia kukimbiza wagonjwa pale inapobidi. Pia nashukuru kwa kupewa wafanyakazi kumi na nne na kutembelewa na Waheshimiwa Mawaziri, ahsanteni sana kwa kufika kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kupewa milioni 400 ambayo inasaidia kumalizia Kituo cha Afya cha Usoke ambacho kilikuwa ni kiporo cha mradi wa *ADB.* Wakati huo huo, niiombe Serikali yetu sikivu itusaidie kumalizia *theatre* ambayo pia ni kiporo cha mradi wa *ADB,* iliyoko katika Wilaya ya Urambo kwani itakuwa na manufaa sana kwa sababu bado tunasaidia wenzetu wa Kaliua na maeneo mengine kutoka Wilaya ya Uyui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani za kupewa milioni 400 ya kusaidia kituo cha afya bado tuna uhaba mkubwa sana wa vituo vya afya. Tunaiomba Serikali yetu itusaidie kupata Kituo kingine cha Afya cha Vumilia ambacho kipo katika barabara ya kwenda Sikonge ili ajali zinapotokea kisaidie. Pia kituo hiki kitasaidia ajali zinazotokea kati ya Kigoma na Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo kingine cha Afya cha Usoke nacho tunaomba kisaidiwe. Kwa hiyo, tunaomba msaada wa kupata vituo vya afya cha Vumilia na Kata ya Usoke kwa sababu mpaka sasa tuna kituo kimoja tu cha afya kati ya kata 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuiomba Serikali iangalie sana suala la wafanyakazi wa afya. Sisi Urambo peke yetu tuna uhaba wa wafanyakazi zaidi ya 300, lakini ili angalau kupooza makali tunaomba wafanyakazi 75. Tutashukuru sana tukipata haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iajiri na hasa hasa Wakunga. Tunapozungumzia kupunguza vifo vya mama na mtoto tunaangalia sana uwepo wa Wakunga. Kwetu sisi kuna zahanati ambazo zina mfanyakazi mmoja tu, sasa anapougua au anapokwenda kwenye semina mama mjamzito anapokuja pale inakuwa ni vigumu sana kupata huduma. Tunaomba Serikali iajiri wafanyakazi na kwa kuanzia waanzie Wakunga ambao tunaamini kabisa watatusaidia kupunguza vifo vya akinamama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhaba mkubwa sana pia kwa upande wa elimu. Orodha ya mahitaji yetu sisi kama Urambo tulishapeleka TAMISEMI. Kwa hiyo, tunaomba Walimu wa shule za sekondari na shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuunda *TSC* ilikuwa ni kuangalia jinsi gani tunaweza kuwapunguzia Walimu adha katika kupata haki zao. Ombi langu kwa Serikali ifanye tathmini, kweli *TSC* iliyopo inakidhi mahitaji iliyoundiwa? Kwa sababu mpaka sasa hivi matatizo bado ni mengi tu, Mwalimu anapodai haki zake au anapotaka kuhama na kadhalika. Tunaiomba Serikali ifanye tathmini, je, *TSC* kweli inafanya kazi zake ilizokusudiwa? Naamini Serikali inaweza kuchukua hatua za kurekebisha ili Walimu waweze kupata huduma kwa wakati hasa hasa mahitaji ya kupanda daraja na wakati huo huo kurekebishiwa mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa upande wa elimu lakini hasa kwa kugusa mtoto wa kike. Naomba niseme wazi kabisa mimi nimo katika Kamati ya Utawala na TAMISEMI na naiunga mkono kabisa taarifa ya Kamati yangu kwenye ukurasa wa 37 ambapo inasema, naomba kwa ruhusa yako nisome, kutokana na kushindwa kumudu gharama za taulo za kike, wanafunzi wa kike wamekuwa wakikumbwa na athari za kushindwa kuhudhuria masomo kwa siku kati ya tatu mpaka tano kwa mwezi na hivyo kuathiri mahudhurio yao na wakati mwingine kuacha shule kabisa hasa wanaotoka katika familia duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni muhimu sana. Naiomba kwa heshima na taadhima Serikali kuliangalia suala hili kwa undani na kuona jinsi gani ambavyo itaweza kumsaidia mtoto wa kike. Suala hili kama nilivyosema tunaiomba Serikali iliangalie kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna tatizo moja sugu kwenye Kamati yetu tulilitilia sana mkazo na tulimwambia Mheshimiwa Waziri husika wa TAMISEMI kuangalia suala la vyoo. Suala la vyoo pia limekuwa likisababisha wakati mwingine watoto wa kike kushindwa kuvitumia kutokana na kukosa milango na vilevile na Walimu kuchangia vyoo na watoto yaani wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kwa heshima kabisa kuangalia jinsi gani wanaweza kuweka mkakati ambao utaondoa kabisa tatizo la vyoo na wakati huo kuiomba Wizara ya Elimu kwa kupitia taarifa hii hii, shule zisisajiliwe kabla ya kujenga vyoo. Vyoo vianze halafu ndiyo majengo mengine yakaguliwe. Nadhani jambo hili linahitaji mkakati wa karibu kabisa ili iweze kusaidia kuondoa tatizo la vyoo visitajwe kabisa tena kwa sababu ni jambo la kusikitisha kwamba tunazungumzia choo katika karne ya 21 kwa sababu tunaamini kabisa mtu ni afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza nikaongea mengi zaidi ya hayo lakini hasa hasa ni kuomba kwa heshima kabisa vituo vya afya kama nilivyosema Vumilia na Usoke;

kuomba *theatre* yetu Urambo ambayo ni kiporo cha *ADB* imaliziwe, lakini wakati huo huo kuiomba kabisa Serikali yetu kwa heshima na taadhima kabisa kuangalia upatikanaji wa wafanyakazi wa Idara ya Afya na hususan Wakunga ambao watasaidia kuondoa vifo vya akinamama au kupunguza kwani hali ilivyo sio nzuri tunahitaji huduma haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nikiamini Serikali yetu nzuri itasikia haya niliyoyasema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu, Mheshimiwa Bura na Mheshimiwa Dkt. Mollel wajiandae.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa kwa heshima kabisa nianze kwa kuzishukuru Wizara zetu hizi mbili, TAMISEMI na Wizara hii inayoshughulikia mambo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru sana kaka yangu na mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika. Mzee Mkuchika nampongeza kwa sababu miongoni mwa Mawaziri wasikivu yeye ni miongoni mwa Mawaziri wasikivu sana. Nakumbuka lilipotokea tatizo la watumishi kuondolewa kazini mimi binafsi nilikwenda ofisini kwake na alipopata taarifa kupitia kwa aliyekuwa anakaimu kama Katibu Mkuu pale Wizarani ambaye pia alinihudumia niliona *public service* pale, Mheshimiwa Mkuchika nataka nimpongeze sana na watumishi wake wa Wizarani hakika ni watu ambao wana *commitment* ya kazi. Naomba hilo nilitambue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka nimpongeze Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Jafo nampongeza sana kwa sababu kwa muda mfupi katika Wizara ambayo Mheshimiwa Rais amemweka kuweza kulitumikia Taifa letu amekuja Jimboni kwangu na Wilaya yangu ya Ikungi zaidi ya mara mbili, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kwa Mheshimiwa Jafo naelekeza ushauri wangu kwa taasisi ambayo Rais amemweka kuiongoza. Taifa letu linakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa nyumba za Walimu wa shule za msingi na sekondari. Nataka nimshauri kaka yangu Mheshimiwa Jafo, kama tulivyofanya mikakati ya kulisaidia Taifa kuondokana na uhaba wa madawati nchi nzima, natoa rai ni wakati muafaka kwa Serikali yetu kuamua kwa makusudi kukomesha tatizo la ukosefu wa nyumba za Walimu nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Jimbo la Singida Magharibi. Kuna maeneo unakwenda Walimu wanatembea zaidi ya kilometa saba mpaka nane hawana mahali pa kukaa. Changamoto hii inapelekea utulivu wa Walimu ku-*concentrate* katika kuwafundisha watoto wetu kuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuliweza kutatua changamoto za madawati kwa kipindi kifupi namwomba Mheshimiwa Jafo, kaka yangu, nina imani na yeye bado ni kijana mwenzetu namwomba akae na Wizara yake, akae na watendaji, wafanye tathmini ya upungufu wa nyumba za Walimu nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa sababu ya uzalendo wetu na kulipenda Taifa letu tutakuja kumuunga mkono atakapoleta mapendekezo ya kujenga nyumba za Walimu nchi nzima hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niongelee suala zima la afya. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza kujengwa kwa zahanati katika vijiji vyote na vituo vya afya katika kata zote katika Taifa letu. Mimi katika Jimbo langu nimeshaanza kujenga zahanati vijiji vyote kwa nguvu za wananchi na kwa kushiriki mimi Mbunge binafsi na kwa kutumia fedha za Jimbo. Mpaka sasa hivi tunavyoongea, kuna changamoto ya kumalizia pale ambapo wananchi wamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Mheshimiwa Jafo, Jimbo la Singida Magharibi sasa hebu alitumie jimbo hili kama mfano wa majimbo katika Taifa hili kwa sababu sisi hapa tunapozungumza vijiji vyote vya jimbo tumeanza kujenga zahanati. Mimi juzi nimegawa zaidi ya vitanda 85 na nimevipeleka hata pale ambapo zahanati bado hazijakwisha lengo ni kuipa Serikali changamoto ili waone ya kwamba tuna kila sababu ya kuhakikisha wananchi hawa wanafikiwa na huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuna maeneo ambapo wananchi wamemaliza kujenga maboma kwa zaidi ya miaka mitatu. Tuna kijiji cha Mnang'ana pale Sepuka wamejenga boma mpaka leo Serikali bado haijapeleka nguvu kwenda kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri na changamoto ambazo Mheshimiwa Jafo anakabiliana nazo katika sekta hii lakini bado kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba zahanati ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi, mimi mpaka sasa hivi tuna maboma zaidi ya 17 ambayo tumeanza kuyajenga kipindi mimi nimeingia hapa kama Mbunge lakini bado msukumo wa halmashauri kwenda kumaliza ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mheshimiwa Jafo akitoka hapa leo, akifanya mawasiliano na Mkurugenzi wangu atamwambia ni maboma mangapi tumeyasimamisha. Mheshimiwa Naibu Spika anapiga makofi kwa sababu alikuja jimboni kwangu akajionea. Kwa hiyo namwomba kaka yangu Mheshimiwa Jafo maboma ambayo tumeshayasimamisha watuletee fedha tuweze kuyamaliza ili tuweze kuwaunga mkono na kuwatia moyo wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, nakwenda kuzungumza habari ya vyumba vya madarasa. Nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Jafo. Amefanya kazi kubwa ya kutuunga mkono pale ambapo wanafunzi wetu walikuwa wanatembea umbali mrefu, sisi tumeanzisha programu ya

kuanzisha shule za msingi ikiwezekana hata shule tatu katika kijiji. Kwa mfano, Kata yangu ya Minyuge tumeanzisha shule mpya za msingi katika maeneo ya Mayaha, Minyughe na Misake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ni kwamba kuna baadhi ya maeneo watoto wanatembea kilometa 14 kwenda kutafuta shule katika makao makuu ya kijiji. Sasa maeneo ambayo tayari sisi kama Wabunge kwa kushirikiana na wananchi wetu tumeanzisha ujenzi wa shule mpya, tunaomba Serikali isichelewe kwenda kuweka nguvu kuhakikisha kwamba madarasa haya yanapauliwa na kumalizwa. Hilo ni la msingi sana katika kuwasaidia watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna Kata moja inaitwa Mwaru, kuna eneo linaitwa Mtakuja, watoto wanatembea umbali wa kilometa 16 kipindi cha mvua mito inakuwepo, watoto hawawezi kwenda shule, lakini sisi tumejenga shule pale Mtakuja tumeshamaliza. Kwa kushirikiana na wananchi tumeshamaliza kuipaua. Namwomba Mheshimiwa Jafo anapofanya *location* ya Walimu Jimbo la Singida Magharibi aliangalie kwa jicho la karibu sana kwa sababu tumeweka *commitment* na tumeweza kuwasaidia watu wetu katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, nizungumze kuhusiana na barabara. Ombi langu kwa Mheshimiwa Jafo na Serikali yangu kwa ujumla, Serikali yangu sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba Mfuko wa *TARURA* ikiwezekana asilimia waliyoiweka waiongeze kwa sababu idadi kubwa ya barabara ambazo zinahudumiwa na halmashauri changamoto ya barabara bado ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nina barabara yangu ambayo haijafanyiwa ukarabati wa kutosha kwa takriban miaka miwili inayotoka Puma - Ihanja - Muintiri - Igeransoni. Halmashauri yangu ya Ikungi sehemu kubwa ya mapato inategemea kutoka katika hizi kata ambazo ziko

mpakani wa Tabora ikiwemo Igaransoni. Kwa hiyo, naomba kaka yangu Mheshimiwa Jafo chonde chonde...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bura ajiandae Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu, lakini nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Jafo pamoja na wasaidizi wake. Mheshimiwa Jafo anafanya kazi kubwa mno na sijui kama familia yake anakaa nayo saa ngapi kwa sababu kila wakati tunamwona kwenye vyombo vya habari akiwa kwenye shughuli za Kitaifa. Nawaomba Wabunge wenzangu tuwaombee Mungu hawa Mawaziri kwa sababu wanatumia vyombo vilivyotengenezwa kwa mikono ya wanadamu. Wakati wowote wanaweza wakapata hatari za barabarani na tulishuhudia juzi juzi tu Mheshimiwa Kakunda alipata ajali mbaya, tunamshukuru Mungu kwamba hakuumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuuliza swali moja ambalo limenisumbua, nimesikia baadhi ya Wabunge wa upande wa Upinzani wakisema kwamba hawaruhusiwi kufanya mikutano. Mimi ninavyojua ni kwamba kila Mbunge anaruhusiwa kufanya mkutano katika jimbo lake. Sasa sijui pengine tuje tupate ufafanuzi kwamba ni mikutano ipi wanayoilalamikia kwa sababu hata sisi tunaruhusiwa kufanya mikutano katika maeneo yetu. Kama wewe siyo Mbunge wa Dodoma Mjini unataka uje ufanye mkutano katika Jimbo la Dodoma Mjini unataka nini Dodoma Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokijua ni kwamba Mbunge anaruhusiwa kufanya mikutano kwenye eneo lake. Kama lipo jambo lingine Mheshimiwa Waziri naomba Serikali ije itoe ufafanuzi, lakini ndivyo ninavyojua. Pengine lisiwe kwa ajili ya kuwapotosha wananchi kwamba wamekatazwa kufanya mikutano iwe dhahiri kwamba Mbunge yeyote anaruhusiwa kufanya mkutano katika eneo lake la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la Mungu linasema aombaye hupewa, atafutaje huona na abishaye hufunguliwa. Sisi watu wa Dodoma tumeomba sana, tuliomba sana Serikali ihamie Dodoma na namshukuru Mheshimiwa Rais na Serikali yake ya Awamu ya Tano ametimiza lengo lile, yale maombi yetu tuliyoomba siku nyingi ameyatimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi mvua za masika zikinyesha watu wanaotoka Kilosa kwa njia ya reli kuja Dodoma wanaweza wakalala wiki nzima njiani hawajafika Dodoma kwa sababu ya mafuriko. Sasa hivi reli inatengenezwa *Standard Gauge* kitu ambacho sisi Watanzania hatukutegemea kwamba tungepata kwa muda mfupi hivi. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wa kujenga *standard gauge* tena kwa fedha zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani ukitaka kuja Dodoma lazima ukodi ndege yako au ndege za kukodi, sasa hivi *Air Tanzania* inakuja Dodoma mara tatu kwa wiki, hatukulitegemea kwa haraka hivyo. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio tunayoyapata Mkoa wa Dodoma. Sasa hivi mikutano mikubwa inafanyika Dodoma na hivi sasa tuna Bunge la Afrika Mashariki hapa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Maafisa Mipango Miji wazuri na naamini Mji wa Dodoma utakuwa mji mzuri katika Afrika nzuri kama tutafuata utaratibu na ujenzi ambao tunaelekezwa na maafisa wetu ambao tumepata kutoka

kwa Mheshimiwa Lukuvi. Kitu ambacho nakiomba ni kwamba kama kuna changamoto zozote kwa mfano ulipaji wa fidia kwa wananchi uende kwa wakati ili wananchi wapishe na makao makuu yaendelezwe kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kitu kimoja pia kwa Serikali yetu sikivu, Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali imeamua Makao Makuu yaje Dodoma, lakini bila sheria itakayoweka msingi kwamba Makao Makuu ya nchi hii ni Dodoma itaweza kuwa shida baadaye. Sijui mbele ya safari baada ya Mheshimiwa Magufuli kumaliza muda wake, atakayekuja simjui, lakini anaweza kuja mtu ambaye hapapendi Dodoma, kama hakuna sheria inayotamka kwamba Dodoma ni Makao Makuu kunaweza kukatokea mtafaruku mbele ya safari. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwamba walete basi Muswada wa Sheria hapa Bungeni na tuufanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ujio wa watu au ujio wa Makao Makuu nimeanza kuona changamoto kama upungufu wa maji, hasa maeneo ya *UDOM* kule, maji hayatoshi na kule kuna wanafunzi wengi wanaosoma kule. Niombe *DUWASA* wapate fedha za kutosha kwa ajili ya maji ili wageni wanaokuja basi wasiwazie tena Dar-es-Salaam wajue kwamba wamekuja mkoa wa asali na maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkoa wetu kabla ya ugeni huu haujaja tulikuwa na mahitaji ya Walimu wa sayansi 373, waliopo ni 258. Niiombe Serikali watuletee Walimu wa sayansi. Tuna maboma 116, tuna mahitaji ya maabara 116, yaliyopo ni 11 tu. Niiombe Serikali kukamilisha maboma ya maabara yaliyopo ili wanafunzi wapate elimu kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kukarabati na kujenga Kituo cha Afya Makole. Kituo kile kinahudumia zaidi ya wagonjwa 300, wauguzi hawatoshi, waganga hawatoshi, naomba tufikiriwe katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile jengo la Halmashauri ya Chamwino lina zaidi ya miaka 10 halijakamilika. Sasa hivi tunajitahidi kukamilisha *ground floor* lakini haitawatosha wafanyakazi wa Halmashauri ya Chamwino. Naomba fedha zitolewe kwa ajili ya kukamilisha jengo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Chemba wanaomba magari mawili tu ili yawasaidie kutoa huduma ya afya na elimu kwa sababu magari waliyonayo ni machakavu. Mkitusaidia katika hilo tutashukuru sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, wajiandae Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa TAMISEMI pamoja na Naibu wake. Mheshimiwa Waziri ninachoweza kusema kuhusu yeye ni kusema tu yeye ni mzalendo. Vile vile nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipa Wizara yake Katibu Mkuu mahiri, Mzee wetu Iyombe pamoja na wasaidizi wake ambao wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kwa kuishukuru Serikali kwa niaba ya watu wa Siha kwa ajili ya shilingi bilioni 52 za barabara, shilingi bilioni mbili kwa ajili ya hospitali ya wilaya, shilingi milioni 700 kwa ajili ya Zahanati ya Umakiwaru, shilingi milioni 680 kwa ajili ya kumalizia miradi ambayo ilikuwa haijamaliziwa, shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya maji na shilingi

milioni 931 kwa ajili ya daraja. Hiyo nimesema ili watu wajue kwamba watu wa Siha hawakukurupuka, walijua wanafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu wetu mwaka huu wameotesha kuanzia mwezi wa Nne na wengine sasa wanalima kwa juhudi sana kwa ajili ya kuzalisha. Kama watu wetu wanafanya hivyo ni muhimu sana Wizara husika kuanzia sasa kwa sababu tunataka tunyanyue uchumi wa watu wetu basi waanze kutafakari ni namna gani kilimo ambacho wanakifanya watu wetu sasa hivi kitakuwa na tija watakapofikia wakati wa mavuno. Kwa sababu imekuwa ni utaratibu wa kawaida kwamba inapofika wakati wa mavuno na mauzo mahindi yanafungwa na mipaka inafungwa ili wasiuze nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tutafakari namna mpya ya kufanya hilo kwa sababu kwa muda mrefu unaweza ukafikiri unadhibiti mfumuko wa bei kwa kuzuia mahindi yasiende nje, lakini kwa muda mwingine unaweza ukasababisha wananchi wakaacha kuzalisha mazao ya chakula wakaanza kuzalisha mazao mbadala. Matokeo yake hata ile bei ya mazao tuliyofikiri tunaidhibiti ikapanda na ikawa tu umefanya kazi ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile soko la mbaazi. Nafikiri ni mapema sasa tuanze kushughulika na soko la mbaazi. Tumeambiwa kwamba nchi ya India ndiyo imekuwa ikinunua mazao yetu ya mbaazi, ni vizuri kwa sababu na sisi tunanunua dawa kutoka kwao tuanze kuzungumza sisi tunachukua dawa kwenu nyingi kwa ajili ya watu wetu na nyie mnachukuaje mbaazi yetu na tunaanza kujadili kuanzia hapo ili tuweze kufanya biashara yenye tija kwa ajili ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Wilaya yangu ya Siha kuna ardhi kubwa sana, kuna ardhi ya *NARCO* zaidi ya heka 56,000 na ya *TALIRI* zaidi ya heka 14,000. *TALIRI* na *NARCO* wana ng'ombe kidogo sana na *TALIRI* wanafanya

*research* ya mifugo bora lakini utaona *NARCO* wanataka kufuga mifugo waanze kuwa wachungaji. Nashauri *TALIRI* wafanye *research* ya mifugo na wazalishe mifugo mizuri sana, *NARCO* wafuge hiyo mifugo lakini wajenge kiwanda ndani ya *NARCO* na ile mifugo mizuri wapewe wafugaji wetu waweze kuzalisha mifugo na kiwanda ambacho kitakuwa pale Siha kiweze kutumika kwa ajili ya kuvuna hiyo mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende kwenye eneo la utawala bora. Nimesikia rafiki zangu wengi wamekuwa wakiongea na kukosoa kuhusu utawala bora, lakini utawala bora unaanzia kwenye nyumba yako. Namshukuru rafiki yangu Mheshimiwa Lusinde leo ameanza vizuri kwenye kuelezea eneo moja lakini nimesikia habari moja ikisema kwamba Mheshimiwa Lusinde hajasoma kitabu kizima. Naomba nitoe mifano ambayo haihitaji usome kitabu kizima ili uelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge walioko hapa kuna Wabunge wanachangishwa zaidi ya Sh.500,000/= na wengine wanachangishwa zaidi ya Sh.1,500,000/= na ukipiga hesabu kwa mwezi mmoja ni zaidi ya Sh.73,000,000/= kwa mwaka mzima ni zaidi ya Sh.876,000,000/=. Nilisema juzi kidogo kelele nyingi zikapigwa lakini nikawa najiuliza Wabunge hawa leo wanakosa nafasi ya kufanya siasa kwenye Bunge hili kwa sababu imekosekana kuajiriwa tu wafanyakazi wanne lakini Wabunge hawa wamechumwa zaidi ya shilingi milioni 876. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa wao kuhitaji watumishi hao...

**TAARIFA**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Dokta Mollel.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji, ya kwanza, mipango ya ndani ya chama haikuhusu tena. Aidha, tunachangishana au hatuchangishani na ni bajeti yetu ya chama. Kila chama kinachangishana na tunaelewa kwamba chama tawala pia wanachangishana. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya pili…

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nimwelimishe labda niwaambie na wengine wapate kuelewa. Sekretarieti ya Bunge upande wa KUB wako kihalali. Sisi ni Bunge ambalo tunaenda sawasawa na Mabunge yote ya *Commonwealth* na kuna Kambi Rasmi ya Upinzani na wako kihalali na kazi yao inajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yangu ni hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mollel, taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakubali kabisa sihitajiki kuingilia mipango ya chama chochote, lakini ukweli tu ni mmoja kwamba ni *logic* ya kawaida kama unapata milioni isiyozidi 460 kwa mwezi na unashindwa hata kuweka programu ya ndani ya nyumba yako vizuri…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine wakipiga makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu unamtaka Dokta Mollel apambane na wewe ili uweze kutimiza azma yako ya …

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, *order, order please.*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unataka Dokta Mollel ashirikiane na wewe ili muweze kumiliki Benki Kuu, wazalendo kama sisi hatuwezi kuwakabidhi Benki Kuu kama milioni 400 hamuwezi kusimamia. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine wakipiga makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwambie dada yangu kwamba mimi namtetea kwa sababu Wabunge wa Majimbo wanachangishwa Sh.500,000/= na Viti Maalum wanachangishwa Sh.1,500,000/=

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wabunge wa Majimbo wana hela ya Jimbo, waliniambia niseme lakini wakaniambia...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi hapa tunapojaribu kuonesha, watu hapa tunazungumzia...

**MWENYEKITI:** Taarifa.

Mheshimiwa Dkt. Mollel muda wako umekwisha. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel, nilifikiri kengele ya pili, ni kengele ya kwanza, lakini kuna taarifa, subiri. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi huyu Dokta pengine ni Dokta wa vidonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pilipili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara kaa chini, hiyo sio taarifa, Mheshimiwa Mollel endelea. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Pilipili iko shambani yamwashiani? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwege kaa chini, kaa chini.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Pilipili iko shambani yamwashiani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwege kaa chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dokta endelea.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru amenipa heshima kubwa kwa sababu daktari wa vidonda ndiyo anaona Watanzania wale wa chini na masikini zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme hapa tunazungumzia suala la utawala bora na watu wamekuwa wakitoka mapovu kwa ajili ya kujitahidi kuonesha kwamba Serikali iliyoko madarakani imeshindwa kujipanga na kuendesha mambo na wakijionesha kwamba wao ni Serikali inayotakiwa kuja kuwa Serikali mbadala kwa ajili ya nchi hii, lakini imeshindwa kusimamia milioni hizo nilizozitaja, basi kuna sababu kubwa ya kusema Watanzania wasiwaamini na hawana uwezo. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukafikiri shilingi bilioni mbili alizozitaja Mheshimiwa Lusinde hapa ni nyingi, ni nyingi kuliko zilizoko Serikalini kwa sababu ndiyo hela pekee walizokuwanazo. Kwa hiyo, hela 100% zimeenda mikono...

**MBUNGE FULANI:** Wewe ni bidhaa inayonunuliwa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia suala la usalama. Vilevile limekuwa likizungumzwa suala la usalama kwenye Bunge hili, usalama sio suala la tu la vyombo vyetu vya usalama peke yake vilevile ni suala la watu wote na viongozi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuna kikundi kidogo ambacho kimekuwa kiki-*remote* watu ambao wanapiga kelele hapa wasiojua wanachokifanya baada ya mirija yao kufungwa na wamekuwa wakitaka ku-*propagate* kwamba kuna usalama na wao wenyewe wakitumia...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dokta Mollel muda wako umekwisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea na wengine walipiga makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni limeletwa sasa hivi, inaelekea wageni wenyewe na wao wanataka kuondoka. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ana mgeni wake Ndugu Hellen Lifiga, mwanafunzi wake wa zamani kutoka Jiji la Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Wageni 100 wa Mheshimiwa Edward Frank Mwalongo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Iringa kilichopo Mkoani Iringa ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendeshwa. Karibuni. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Kitandula, Mheshimiwa Mipata, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu wajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja zilizoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amezidi kutupa baraka zake na hatimaye tunaweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye mambo matatu. Nitajielekeza kwenye suala la elimu, afya na lishe. Nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa kutupatia fedha za kujenga mabweni na madarasa kwa Sekondari zetu mbili za Maramba na Mkinga ambazo zimekuwa *high school,* nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo bado sekondari hizi ambazo zimekuwa *high school* zina changamoto nyingi kwani kuna uhaba mkubwa wa nyumba za Walimu. Sekondari ya Mkingaleo hakuna nyumba za Walimu na *high school* ile inachukua wasichana, kwa hiyo, unaweza kuona hatari iliyopo. Nawasihi sana Serikali tuchukue hatua za haraka kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Sekondari ya Maramba, sekondari ile tulipoianzisha tulichukua majengo ya yaliyokuwa mashamba ya mkonge. Kwa hiyo, nyumba wanazotumia Walimu ni nyumba zile za wafanyakazi wa mkonge, za chini kabisa. Kwa hiyo, unaweza kuona picha Walimu wetu tunawaweka katika mazingira gani. Nawasihi sana, tumezipandisha hadhi shule hizi, basi tuziboreshe na kuzipa hadhi inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile shule hizi zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa Walimu, taarifa tumekwishapeleka naomba waziangalie. Pia shule hizi zinakabiliwa na tatizo la maji, naomba waangalie. Wingi ule wa wanafunzi katika shule zile halafu shule hazina maji ni changamoto kubwa kwelikweli. Vilevile lipo lingine, shule hizi hazina usafiri, tumewaweka vijana wetu pale, lakini shule hizi hazina usafiri ni changamoto kubwa kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunayo madai ya Walimu. Tuna Walimu takribani 271 wanadai madai mbalimbali, ukiacha mishahara, wanadai takribani shilingi milioni 312. Hata orodha ile ya malipo ilipotoka kwa Wilaya ya Mkinga walikuwa ni wafanyakazi wawili tu, naomba waliangalie vizuri jambo hili, halitupi hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu yangu Mheshimiwa Waziri atakumbuka niliwahi kuja na timu ya Madiwani kutoka Mkinga, wanastahili posho zao baada ya kumaliza muhula uliopita wa Bunge. Mpaka leo madai yao bado hayajatimia, naomba tuwalipe fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kwenye afya. Hapa naomba vilevile niipongeze na niishukuru sana Serikali, imetupatia shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga kituo cha afya. Kituo kile kimekamilika, tunaomba zile shilingi milioni 200 zilizobaki ili kufika shilingi milioni 700 kwa ajili ya vifaa tiba, naomba watupatie ili tuweze kukamilisha kituo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ombi langu liko palepale la kuhakikisha Wilaya ya Mkinga tunapatiwa fedha za kujenga hospitali ya wilaya. Wilaya ile tuna kata 22, sasa hivi tuna vituo vya afya vitatu. Kwa hiyo, unaweza kupata picha kwa wilaya yenye kata 22, haina hospitali ya wilaya ina vituo vya afya vitatu, unaweza kujua ukubwa wa tatizo ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilisema hili muda mrefu, naomba ifike mahali sasa Serikali isikie. Tunawashukuru *World Vision* kwa kutusaidia kujenga jengo la kisasa la upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mkingaleo, tunaomba na wahisani wengine waige mfano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa kwenye sekta ya afya, tuna mahitaji ya watumishi 395 waliopo ni 183, tuna uhaba wa karibu asilimia 58 ya watumishi. Maombi haya tumekwishayapeleka muda mrefu, tunaomba wayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nihamie kwenye lishe. Hapa nataka ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Ma-*champion* wa Lishe katika Bunge letu. Niishukuru Serikali juzi imetoa *commitment* ya kutoa semina kwa Wabunge wote juu ya tatizo tulilonalo la lishe katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwamba kwa ukubwa wa tatizo tulilonalo katika nchi yetu ingekuwa busara sana kama Wabunge wote mngeona umuhimu wa kujiunga na kikundi hiki cha lishe. Mwaka jana tulifanya jambo kubwa, tulipitisha hapa shilingi bilioni 11 ziende kwenye halmashauri kwa ajili ya kutatua tatizo la lishe. Lilikuwa ni jambo kubwa kweli kweli lakini cha kushangaza na imenisikitisha kidogo kwamba nimeisikia hotuba ya Waziri Mkuu sikusikia chochote kuhusu lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisikiliza hotuba ya ndugu yangu Mheshimiwa Jafo hakuna sehemu imetajwa lishe. Ndugu zangu tuna tatizo kubwa kwenye lishe, wala

tusimumunye maneno, tuna tatizo kubwa. Haiwezekani kwamba takribani asilimia 45 ya vifo vya watoto katika nchi hii vinahusishwa na utapiamlo, haiwezekani asilimia 57 ya watoto katika nchi hii wana upungufu wa damu, haiwezekani asilimia 34 ya watoto wetu wamekuwa *stunt* halafu hotuba zetuhazigusii jambo hili, si sahihi, si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo yeye alikuwa miongoni mwa Wabunge tulioanzisha kikundi cha lishe, najua *passion* yake kwenye jambo hili, Waziri wa Fedha najua *passion* aliyonayo kwenye jambo hili, hebu tuchukue hatua. Taarifa zilizopo ni kwamba katika shilingi bilioni 11 tulizoidhinisha *it's only eight percent* ya fedha hizo ndiyo zimekwenda. Taarifa hii ni ya mwezi wa Pili. Katika shilingi bilioni 11 tumepeleka shilingi milioni 888, hii haiwezi kuwa sawa. Nawasihi sana tuchukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua changamoto tuliyonayo ni kwa sababu fedha hizi tunazipitishia kwenye *Health Basket Fund*, fedha hizi tunataka zitoke kwenye *own source*, fedha hizi tunataka zitoke kwenye *OC.* Njia hii haitatufikisha, tuangalie uwezekano wa kutumia njia ya ku-*ring-fence* fedha hizi, kuzi-*page* kwenye *GDP* asilimia fulani ili tuhakikishe fedha hizi zinakwenda moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitumia bajeti za halmashauri kule tukategemea tutaenda kutatua tatizo kubwa kama hili tunajidanganya. Tumekubaliana kwenye *vision* 2020-2025 kwamba tutaweka kipaumbele kwenye kuboresha *human capital* na *productivity* haya hayawezi kupatikana kama hatutahakikisha tunaondokana na tatizo la lishe duni na lishe iliyopitiliza.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea sasa kwamba ripoti ya *Human Development* ya mwaka 2014 inaonesha kwamba nchi kila mwaka inapoteza takribani shilingi bilioni 600 kwa nguvukazi ambayo ina ukosefu wa lishe bora *(malnutrition)*. Sasa hiyo nguvukazi ukiiweka katika *monetary term* ndiyo inakuwa takribani shilingi bilioni 600 inapotea katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa lakini hali ni mbaya zaidi ya hapo. Tathmini inaonesha kwamba kama hali ikiendelea hivi ikifika mwaka 2025 Taifa litakuwa limepoteza nguvukazi ya shilingi trilioni 28.8, *this is very serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha taarifa yake atueleze, tulikubaliana kwamba tutaajiri Maafisa Lishe 600, nini kimetokea mpaka sasa hatujaweza kuajiri? Vilevile mpaka kufikia kipindi hiki ni fedha kiasi gani tunazipeleka kwenye lishe? Nawasihi sana tunapofanya mabadiliko ya miundo katika Wizara tujitahidi Kitengo cha Lishe kisije kikamezwa tukahatarisha jitihada hizi tulizozianza. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate, jiandae Mheshimiwa Oran.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kuchangia hoja ya TAMISEMI pamoja na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nitaenda moja kwa moja kwenye suala la mgao wa wilaya. Halmashauri

yetu ya Wilaya ya Tunduru ni kubwa sana na kilio chetu kimekuwa cha muda mrefu. Pamoja na kwamba Rais amesema hatutakuwa na mgao lakini hali yetu ya kiutawala ni ngumu kutokana na ukubwa wa eneo letu tulilokuwa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tunduru imeanzishwa tangu mwaka 1905 lakini mpaka leo haijawa na wilaya nyingine na ukubwa wake ni zaidi ya Mkoa wa Mtwara ambao sasa una wilaya zaidi ya sita (6). Kwa hiyo, utakuta kimaendeleo kuhudumia wananchi wetu inakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kulingana na idadi ya watu tuliokuwa nao, ukubwa wa eneo uliokuwepo na umbali wa makao makuu kuhudumia maeneo mengine yaliyokuwepo tunaomba sana mtufikirie kwa hali na mali ili tuweze kupata wilaya nyingine kwa ajili ya kuwahudumia watu wetu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitalizungumzia ni suala la elimu. Kama nilivyozungumza juzi tunashukuru sana elimu bure lakini tuna changamoto nyingi sana upande wa Tunduru ambazo kwa kweli ni aibu, mpaka leo tuna madarasa ya nyasi katika maeneo mengi ya shule zetu za msingi. Pamoja na madarasa ya nyasi lakini bado hata vyoo hatuna. Kulingana na idadi ya watoto ilivyokuwa utakuta shule ina watoto 840 matundu ya vyoo ni saba, kumi ambayo hayaendani na hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi kwenye nyumba za Walimu ndiyo usiseme, walimu ni wachache kupita kiasi hata nyumba zao hazipo. Kwenye eneo langu nimetembea karibu jimbo zima na shule zote za msingi nimezitembelea, shule ina watoto 840, Walimu watano, sita au watatu. Asilimia 60 ya shule za msingi zilizopo kwenye jimbo langu zina Walimu chini ya watatu, jambo ambalo ni gumu hata tukifikiria namna wanavyofundisha na kufaulisha Walimu wale wanastahili pongezi kubwa sana kwa sababu Walimu ni wachache na madarasa yamekuwa mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimeliona miaka hii kunakuwa na *session* katika madarasa ya kwanza mpaka darasa la saba. Kwa kweli wale watu wanastahili kupewa hata *overtime* kwa sababu wanafunzi ni wengi, madarasa ni mengi lakini wanafundisha Walimu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nitazungumzia juu ya ujenzi wa vituo vya afya. Naishukuru kwa mara nyingine Serikali kwa kutupatia Kituo cha Afya Nkasale lakini eneo la Tunduru kwa maana ya halmashauri yote tuna kata 35. Katika kata 35 tuna vituo vya afya vitano (5) tu na hivyo kwenye jimbo langu kuna vituo vya afya vitatu (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kituo cha Afya Nalasi, Rais wa Awamu ya Nne Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi ya kujenga kituo hiki. Nalasi ni mji mkubwa una zaidi ya wakazi 30,000 ambao wako kwenye kata mbili katika kijiji hicho hicho kimoja. Kwa hiyo, alivyokuja kwa mara ya mwisho aliahidi kwamba angeweza kujenga kituo cha afya katika kata ile na aliahidi kutoa gari la wagonjwa lakini ile ahadi mpaka leo haijatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014 kwenye bajeti waliweka shilingi milioni 80, wananchi walifyatua tofali za kujenga boma. Bahati nzuri shilingi milioni 80 ilipatikana wakaanza ujenzi ule lakini tofali zile sasa zimekuwa kichuguu, tangu umejengwa huo msingi kwa maana ya *foundation* mpaka leo ahadi ile haijatekelezeka na halmashauri imejitahidi kila mwaka kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa halmashauri yetu ni kubwa kama nilivyozungumza tuna kata 35, tuna Madiwani 52, tukijumlisha sisi Madiwani kwa maana Wabunge halmashauri yetu ina Madiwani 55 yaani ni darasa kubwa ambalo hata kusikilizana inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, bajeti ya afya haitoshi na ya elimu inakuwa haitoshi kwa sababu mapato yetu hayawezi kukidhi kuweza kuhudumia vituo vya afya vyote kwa maana ya kupata fedha za majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la maji. Tuna miradi mingi sana ambayo inasimamiwa na halmashauri yetu kwa maana ya maji. Tunayo miradi ya muda mrefu, Mradi wa Mtina mpaka leo haujakwisha. Juzi bahati mbaya halmashauri imesitisha mkataba na mkandarasi yule lakini naomba waende wakaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetembelea ule mradi kwa macho yangu na kwa *scope* ya kazi niliyoona inaonekana mradi ule umefikia zaidi ya asilimia 80, lakini kwa matakwa ya watendaji wetu naweza kusema kwa maslahi binafsi wameweza kusitisha ule mkataba tangu Desemba mwaka jana mpaka leo mkandarasi mwingine hajapatikana, wakati wangeweza kumuachia ndani ya mwezi mmoja kama alivyoomba mradi ule ungekuwa umeweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tabia nchi ya ukame katika maeneo mengi, Tunduru tulikuwa na mito mingi lakini bahati mbaya mito hii imeendelea kukauka. Kwa hiyo, tunahitaji miradi ya maji mingi kwenye vijiji vyetu kwa ajili ya visima vifupi na virefu ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ningependa kuchangia juu ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Halmashauri yetu kama nilivyozungumza ni kongwe na ni imezeeka lakini ina watumishi wachache sana. Watumishi waliokuwepo ni wachache mno ukizingatia na namna ambavyo kazi zile zinafanyika. Mbaya zaidi kuna watumishi wanazeeka na halmashauri ile, wana zaidi ya umri wa miaka 20 kwenye halmashauri moja, kwa hiyo, wanafanya kazi kwa mazoea kiasi kwamba kila wanachokifanya wanafanya kwa namna ambavyo wao wanaona siyo kwa matakwa ya masharti ya kazi kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba basi ikiwezekana watusaidie angalau kufanya *internal transfer* kwa maana ya kutoka halmashauri moja au nyingine ili wale waliokaa muda

mrefu ambao sasa imekuwa ni mazoea kufanya kazi zao ikiwezekana na wao waweze kupelekwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna jambo linanisikitisha kwenye halmashauri yetu. Tumekuwa na tabia sisi ya kusomesha wataalam wetu katika halmashauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Oran, jiandae Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza nianze kwa pongezi za dhati kabisa, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kazi kubwa aliyoifanya hasa kwenye jimbo langu. Ameleta mageuzi makubwa sana kwenye sekta karibu zote, kwenye miundombinu, maji na pia sasa hivi hata kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege Naibu Mawaziri, wamefanya kazi kubwa sana na kweli kazi imeonekana. Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini wamenituma nizilete pongezi zenu hizo pamoja na wataalam wenu katika Wizara zenu ikiwemo na Wizara ya Utumishi wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazitoa hizo pongezi kwa sababu moja tu. Jimbo la Mbeya Vijijini tunategemea sana kilimo lakini tulikuwa hatuna barabara kabisa huko vijijini, mazao tulikuwa tunashindwa kuleta mjini. Leo hii tuna kilomita za mtandao kama 1,007, tulikuwa hatuna barabara kabisa za kuaminika. Tulikuwa na kilomita moja tu ya barabara ya lami ukiachilia mbali zile barabara za *TANROAD* kwa barabara yetu ya *TANZAM* ya kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia. Hivi navyozungumza kutokana na jitihada

alizofanya Mheshimiwa Jafo na timu yake pamoja na matunda mazuri ya ziara yake, leo hii kuna maandalizi ya kilomita 37 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizo kilomita 37 lakini leo hii kuna *design* ya kilomita 126 ambazo nazo tunategemea zitajengwa kwa kiwango cha juu. Kwa vile pesa zipo wakimaliza *design* tu hizi barabara zitatangazwa na wananchi wameshaliona hilo kwa sababu wameshaziona *survey* zinazofanyika, kwa kweli kazi ni nzuri na timu ya *TARURA* tuliyonayo ya *Country Manager* wa Mbeya Vijijini ni kijana mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Jafo huyu kijana anachohitaji pale ni motisha, hana gari. Utatembelea vipi mtandao wa kilomita zaidi ya 1,000 wakati huna usafiri? Vilevile ukiangalia hii kazi iliyoko mbele yake kilomita 163 ata-*supervise* namna gani akiwa hana usafiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hizo, tunaomba vilevile wenzetu wa *TANROAD* kuna barabara ya mchepuko ambayo inaingiliana na hizi barabara waweze kuimalizia. Kwa hiyo, itategemea ni kiasi gani watafanya haraka kuijenga ile barabara ya kuanzia Mlima Nyoka kuja mpaka Songwe ili ziende pamoja kwa vile kiuchumi hizi barabara ni muhimu sana na ndiyo zitatuongezea *mileage* sana kwa ajili ya ushindani na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi barabara naomba waangalie ni namna gani wataipandisha hadhi barabara ya kuanzia Mbalizi kwenda Shigamba mpaka Isongole. Hii barabara Mheshimiwa Mbena asubuhi alipiga magoti, ni barabara muhimu sana kiuchumi kwa vile hizi barabara ndiyo zinakuja kutuunganisha sisi Tanzania na majirani zetu wa Zambia. Kwa hiyo, tumeomba hizi kilomita 96 za hii barabara, wenzetu wa *TANROAD* wafanye mchakato wazipe bajeti za upendeleo kabisa ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizi barabara, Mbeya sisi pale tuko kimkakati, biashara ya bandari inategemea zaidi nchi za Zambia, Congo, Malawi na kwa kiasi fulani Zimbabwe. Bila kuboresha *TAZARA* na bila kuwa na bandari kavu pale Mbeya biashara yetu ya bandari hasa kwa nchi za nje kwa kweli itapata mtikisiko sana. Nilizungumzia juzi ni namna gani wenzetu Msumbiji wamejiandaa kuchukua soko hilo, wameshaanza ujenzi tayari wa reli na wanaboresha bandari yao ya Nakao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya haraka na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu wasipochukua uamuzi wa haraka kwa sababu eneo limeshatolewa, wananchi wameshatangaziwa bila kujenga bandari kavu pale soko lote kwa ajili ya hizo nchi litachukuliwa na wenzetu wa Msumbiji. Pamoja na hilo, naiomba Serikali iangalie namna gani itajenga reli ya kuanzia Mbeya mpaka Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri ni suala zima la maji. Nililalamika sana hapa kuhusu miradi ya maji lakini leo hii kwa ajili ya ubunifu wake tulikuwa tunadanganywa kuwa hela hazitoki lakini amekuja kutuambia Waziri wa Maji kuwa pesa zipo na leo natoa ushuhuda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Chikota, jiandae Mheshimiwa Susan Kiwanga dakika tano.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri ambayo wamewasilisha nikianza na kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika vilevile na Mheshimiwa Jafo na timu yake wakiwepo na Naibu Waziri Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege, hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze Watendaji Wakuu, kuna Dkt. Ndumbaro wa Utumishi lakini pia Kaka yetu Injinia Iyombe wa TAMISEMI; Dkt. Chaula pia na kaka yangu Nzunda, Naibu Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa pongezi kwa sababu asiyeshukuru kwa moja hata akipewa tano hatashukuru. Niishukuru TAMISEMI kwa uratibu mzuri wa ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za wilaya. Wote mtakuwa mashahidi katika hotuba zilizopita tulikuwa tunauliza Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kila kijiji kutakuwa na zahanati, kila kata kutakuwa na kituo cha afya, lakini mtekelezaji ni nani? Wizara ya Afya hawakuwa na mpango na TAMISEMI hawakuwa na mpango. Leo ukienda ukurasa wa 25 utaona mpango wa ujenzi wa vituo vya afya, hongereni sana TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo 208 ambavyo vinajengwa na vinakarabatiwa na mwezi Aprili vitajengwa vingine 25. Haya ni mapinduzi makubwa na wasikate tamaa kwa wale ambao wanawabeza kwamba watachukua sijui miaka mia tano kukamilisha nchi nzima, hiyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mipango ya maendeleo tunapanga kulingana na rasilimali zilizopo, mwaka huu wameweka fedha ya vituo 208, mwakani unaweza kuweka fedha ya vituo 1,000. Kwa hiyo, siyo sahihi kwamba kwa idadi ya vituo vya afya vilivyopo nchini tutakarabati kwa muda mrefu inategemea na upatikanaji wa rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivi hata elimu ya msingi, *PEDP* tukajenga madarasa, *SEDP* tukajenga madarasa na tukajenga maabara. Kwa hiyo, wasikate tamaa waendeleze kuweka mipango mizuri, watafute fedha kwa wafadhili ili tuongeze kasi. Tunatarajia bajeti ya mwakani tutaona ukarabati na ujenzi wa vituo zaidi ya 1,000 ili wale wanaowabeza wakose cha kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru kaka yangu Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Kakunda wote mmefika Jimbo la Nanyamba na waliona hali halisi. Walipofika kulikuwa hakuna kituo hata kimoja cha afya na tukawaambia mikakati yetu kwamba hatusubiri fedha za Serikali, tunaanza kwa fedha zetu za korosho. Wakati tumeanza ujenzi wa *OPD* pale Dinyecha, namshukuru sana Mheshimiwa kaka yangu Jafo kwa sababu ametupa fedha shilingi bilioni moja na milioni mia nne kwa ajili ya ukarabati wa vituo vitatu vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa sababu tuliona kwamba hakuna kituo cha kukarabati tukaanza na ujenzi, tumesimamia vizuri na yale majengo ambayo walisema tujenge tumeongeza mengine. Mheshimiwa Kakunda atakuwa shahidi pale Dinyecha walituambia tujenge wodi ya akinamama sisi tumejenga wodi mbili, tumejenga wodi ya akinamama na wodi ya jumla lakini tumejenga na *OPD* kwa fedha za korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na fedha za TAMISEMI lakini na sisi kwenye mipango yetu tumeongeza fedha. Pale Majengo wametupa shilingi milioni mia nne na sisi tumeongeza shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa *OPD*. Nimshukuru vilevile ametupa *ambulance*, Mheshimiwa Jafo amefanya kitu kikubwa sana kwa mara ya kwanza *ambulance* imeingia Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu Mheshimiwa Waziri amesoma Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ni miongoni mwa halmashauri zitakazopata fedha za ujenzi wa hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, namshukuru na nampongeza kwa sababu ameangalia mahitaji halisi ya halmashauri yetu na jinsi sisi wenyewe tunavyotumia rasilimali chache tulizonazo kuwekeza katika afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye suala la Madiwani. Ukisoma Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 1977, Ibara ya 145 na 146

inazungumzia kuanzishwa kwa majukumu ya Serikali za Mitaa. Madhumuni ya kuanzisha Serikali hizi ni kupeleka madaraka kwa wananchi na kuna Diwani ambaye ni mwakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sasa *package* ya Madiwani hawa. Madiwani hawa wana majukumu mengi, wana kazi nyingi lakini bado *package* yao hairidhishi. Madiwani wana malalamiko, wana matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Jafo, awasikilize Madiwani hawa. Aunde Tume afanye tathmini ya majukumu ya Madiwani aangalie ukubwa wao wa kazi na si vibaya sasa kupitia posho zao na maslahi yao kwa sababu posho yao ambayo wanayo sasa hivi ina zaidi ya miaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tusiwajibu majibu mepesi mepesi kwamba uwe na kazi nyingine au uwe na shughuli nyingine ndiyo uombe udiwani, Diwani ana majukumu mengi, kumlipa shilingi laki tatu kwa mwezi na Diwani huyu unategemea asimamie miradi ya maendeleo, asimamie fedha za halmashauri lakini kwa mujibu wa sheria zetu Baraza la Madiwani ndiyo mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa halmashauri, kwa posho ya shilingi laki tatu uhukumu kesi ya Mkuu wa Idara ambaye ana mshahara wake ni shilingi milioni mbili ni rahisi kuwa *corrupted.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutengeneze vizuri *package* ya Madiwani ili wafanye kazi kwa uaminifu, kwa uadilifu ili kusukuma maendeleo ya halmashauri zetu. Kama ninavyosema Mheshimiwa Jafo wana matarajio makubwa sana na yeye, awasikilize, atengeneze timu ikawasikilize, afanye tathmini tuje na kitu kipya kwa Madiwani wetu kama anavyofanya *reform* katika maeneo mengine pale TAMISEMI na mimi nina matarajio na Mheshimiwa Waziri na najua hatawaangusha Madiwani wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, kuna fedha zinaitwa *payment for result* ambazo zinakwenda kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa na zinakwenda kwenye sekta zote za elimu, afya nafikiri na maji. Fedha hizi

TAMISEMI sijaona kwenye kitabu chao, nikawa najiuliza fedha hizi wanatoa TAMISEMI au Wizara ya Elimu. Kama zipo Wizara ya Elimu naomba nishauri fedha hizi ziende TAMISEMI ili Wizara ya Elimu ibaki na mambo ya sera tu. Hawa ambao wanakwenda *field* na TAMISEMI sasa hivi wana kitengo kizuri cha ufuatiliaji wa fedha kwenye Serikali za Mitaa na Mkoani, hizi fedha ziende kwao lakini vilevile zionekane kwenye vitabu. Wenzao wa Wizara ya Maji mwaka jana walionesha kabisa fedha za *OC* na fedha za *P for R*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao pia Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu waige wanavyofanya Wizara ya Maji, inaonekana kabisa na zile *key performance indicators* zionekane kwamba halmashauri inapata fedha nyingi kwa sababu ipi. Wizara ya Maji walitengeneza vizuri kabisa na hata sasa hivi wameshatoa matokeo ya halmashauri na TAMISEMI waige kitu kama hicho ili tusije tukawa tuna hisia tu kwamba zimepelekwa nyingi Nanyamba kwa sababu Mheshimiwa Kandege na Chikota ni marafiki, hapana. Tupeleke kwa vigezo vilivyowekwa na vya wazi na halmashauri ziwe zimeshindanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la *TARURA*. Nami niungane na wenzangu kuwapongeza TAMISEMI kwa kuanzisha *TARURA* na *TARURA* inafanya vizuri. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge tuipe muda *TARURA* tusianze kuwalaumu, huwezi kumlaumu mtoto wa mwaka mmoja ukasema hawezi kutembea. *TARURA* imeanzishwa na imeanza kufanya kazi vizuri, tuipe muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* wana changamoto ya rasilimali fedha, watumishi na usafiri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo natarajia kwa kipindi hiki atapunguza haya matatizo ambayo *TARURA* wanakabiliana nayo. Suala kubwa ambalo tunamwachia Mheshimiwa Jafo na hili ningependa kusikia kauli yake wakati wa kuhitimisha ni kile kilio chetu cha Wabunge kwamba mgao ubadilishwe, wa fedha za *Road Fund* ambazo zinakwenda *TANROAD* na hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majukumu mengi *TARURA* wanayo na *network* ya barabara za vijijini ambazo mwananchi wa kawaida, mpiga kura akiamka anakutana na barabara za *TARURA* halafu ndiyo anakwenda za *TANROAD*. Kwa hiyo mgao ubadilishwe...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Nagu.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa dakika hizi tano. Moja kwa moja naenda kwenye hiki kitabu cha TAMISEMI, ukurasa wa 12 - 13 katika masuala ya utawala bora inaonesha kwamba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Maafisa Utumishi na Mipango pamoja na Makatibu Tawala wamepewa mafunzo kuhusu utawala bora. Sasa sielewi hayo mafunzo waliyowapa yalikuwa yanahusu nini? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utawala bora kuna misingi. Misingi ya utawala bora moja ni utawala wa sheria *(rule of law),* waliwafundisha nini? Katika misingi ya utawala bora ninachojua mimi uwajibikaji *in English (accountability),* waliwafundisha nini? Katika misingi ya utawala bora uwazi katika uongozi yaani Bunge, Mahakama, vyombo vya maamuzi, *transparent in English,* waliwafundisha nini? Katika misingi ya utawala bora uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa watu kutoa mawazo yao bila vitisho. Sasa tukiangalia nchi yetu hivi sasa hivi kuna utawala bora ama bora utawala? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Wakuu wa Mikoa wame-*prove failure.* Wakuu wa Wilaya baadhi yao na Wakuu wa Mikoa wameonesha hawajafaulu huo mtihani wamepoteza hela za Serikali za kodi za wananchi kwa kuwapa mafunzo halafu wakienda kule hawafanyi walichojifunza. Labda wangeniita mimi mwenyewe ni Mwalimu wa utawala bora vilevile na maendeleo ya uchumi nije nitoe mada halafu wangepewa mitihani huko *field*, wale wanaofeli wanawatoa katika uongozi.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan taarifa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwalimu wa utawala bora lakini nilitaka kumwomba aanze kutoa hiyo elimu kwenye chama wakikomaa ili na sisi aweze kutusaidia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake ampelekee mkewe. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu kaa chini. Mheshimiwa Susan Kiwanga, hebu futa hilo neno, futa mwenyewe.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta lakini ujumbe kapata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mkuu wa Mkoa wa Morogoro safari hii kafanya maajabu, Dkt. Kebwe tena alikuwa Mbunge huku, eti leo hajaitisha *RCC*, hajaitisha *Road Board,* vitabu kaleta TAMISEMI, huo ndiyo utawala bora? Wabunge hatujahusishwa katika mipango yetu ya Mkoa wa Morogoro, mkoa mkubwa, hivi kwa nini wanamkabidhi mtu kama yule mkoa mkubwa kama ule? Wananiambia ukisema

ndiyo watamwacha pale pale, muacheni lakini CCM inaenda kuondoka, mimi nawaambia, anaenda kuwadondosha jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mkoa mkubwa kama Morogoro na tulikwishaomba jamani mtupunguzie huu mkoa, mtupe Mkoa wa Kilombero mpaka leo hamna kitu. Tutaona kwenye bajeti hii, kuna majimbo wamewapa hela kama mkoa ndiyo tutakuja kushughulika na ninyi. Sisi Mkoa wa Morogoro mkoa mkubwa hamna chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja Mlimba sasa. Mlimba halafu Mheshimiwa Jafo alipokuwa Naibu Waziri...

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba misingi ya utawala bora anayosema Mbunge mwenzangu ameitaja lakini nidhamu ya kuzungumza pia inaweza ikam-*define* aina ya mtu ambaye anaweza akasimamia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, taarifa hiyo.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nidhamu hii...

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka, Mheshimiwa Susan taarifa hiyo.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alipe madeni benki huyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi Mlimba. Jimbo la Mlimba liko ndani ya Wilaya ya Kilombero.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto kaa chini, endelea Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe dakika zenyewe ni tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlimba, Mheshimiwa Jafo aliniahidi atakuja Mlimba ndugu yangu mpaka leo Mlimba hawajaja wanataka nini? Kwa nini hawaji Mlimba kuangalia wakija wanaishia Ifakara na Morogoro, Mlimba ni hatari. Hivi ninavyozungumza barabara karibuni, nawashukuru *TANROAD* kidogo wanajitahidi kutengeneza tengeneza barabara lakini barabara imekuwa ni tatizo. Mito inayokatiza...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mollel kaa chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mawaziri, Waziri wa TAMISEMI mimi siwezi kusema sana hapa nawaomba waje Mlimba. Kwa mfano, tulikuwa tunategemea mwaka huu tutapata hela katika Kituo cha Afya cha Mngeta, cha Mchombe lakini hamna hata shilingi. Kilometa 265 mpaka kwenda kwenye hospitali ya wilaya akinamama wajawazito wanakufa njiani jamani, watoto wanakufa, tatizo ni nini? Kwa nini hawaji wakaangalia mazingira halafu waone maeneo ambayo yalikuwa muda mrefu hayana huduma ili watuletee hizo huduma angalau, barabara tukose....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja. Mheshimiwa Dkt. Nagu. *(Kicheko)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unga mwenyewe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto muda wetu ni mdogo sana, *we only have ten minutes please, please* kaa chini Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Zitto kaa chini. Mheshimiwa Dkt. Nagu endelea.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hizi Wizara mbili ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais. Kwa kuanza kabisa, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge pamoja na kusimamia na kushauri Serikali ni muhimu sana kuchangia kwa busara na bila ugomvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa agizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kufuatilia kwa karibu sana na kikamilifu nia ya Mheshimiwa DC wangu kutaka kuniweka ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru sana Wabunge wa Mkoa wa Manyara, Wabunge wote ambao wamefuatilia suala langu hususani Mheshimiwa Abuu kuona kuna nini kumbe nataka kuwekwa ndani kwa sababu niko karibu sana na wananchi wa Wilaya ya Hanang. Nawashukuru sana kwa uvumilivu wao nilivyowaomba wasiandamane kuja kule hawakufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waendelee kushirikiana na mimi, ushirikiano ambao unawapa hofu watu

ambao wanataka kuvamia wilaya yangu, napenda niendelee kushirikiana nao na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Dkt. Nagu subiri kidogo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa anayezungumza, jana amesema hapa kwamba hajawahi kuwekwa ndani, leo anasema kwamba anawashukuru wananchi hawakuandamana wakati amewekwa ndani. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kaa chini, Mheshimiwa Dkt. Nagu endelea na kuanzia sasa hamna taarifa tena. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa kwa sababu ni kweli sijawekwa ndani na nimemshukuru Rais kwa agizo lake. Kama walikuwa wanataka niwekwe ndani sijawekwa ndani na ni wao ndiyo chimbuko la matatizo hayo.

**MWENYEKITI:** Mama Nagu endelea na mchango wako.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana na kumshukuru Waziri Jafo, wakati nia hiyo ikitaka kutekelezwa yeye vilevile alisaidia sana kuisimamia vizuri TAMISEMI ili wanaofanya kazi chini yake wafanye kazi vizuri. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa sababu kwa kweli wanajaribu sana kusimamia utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mambo ya wilaya yangu. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba agizo lake la elimu msingi bure linatekelezwa vizuri ambalo limezaa uandikishaji wa watoto mara mbili ya uandikishaji wa awali kabla ya agizo hilo. Pamoja na agizo hili zuri nataka niwaambie kwamba sasa watoto walioandikishwa wameongezeka, madarasa yanatakiwa zaidi na vilevile nyumba za Walimu zinatakiwa zaidi na zaidi ya yote tunahitaji walimu wengi zaidi kwa sababu watoto wameongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano tu wa Wilaya yangu ya Hanang kwamba kabla ya agizo lake tulikuwa tunaandikisha watoto laki moja na elfu kumi lakini mwaka huu wa 2018 waliandikishwa elfu kumi na mbili na mia nne themanini na sita. Utaona jinsi watoto walivyoongezeka, kwa hivyo, madarasa mengi yatahitajika, Walimu wengi watahitajika na nyumba nyingi za Walimu zitahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wananchi wa Hanang wameliona hilo na wanamuunga mkono Rais wao kwa kujenga madarasa mengine lakini naomba tushirikiane nao. Kwa mfano, mahitaji ya madarasa kwa shule za msingi ni mia saba sabini na mbili na sekondari ni sitini na nne, kwa hiyo, wao wako tayari kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwe na utaratibu mzuri, nyumba zinazohitajika sasa hivi ni mia nane ishirini na tano kwa shule za msingi, mia tatu sabini na saba kwa shule za sekondari na madawati mia tisa kumi na mbili kwa shule za msingi na mia tano tisini na tisa kwa shule za sekondari. Haya yote yametokana na kuandikisha watoto wengi zaidi. Wananchi wako tayari kusaidiana na kuunga mkono Serikali yao, wanachoomba utaratibu mzuri wanapoona kwamba wananchi wamejenga mpaka kwenye lenta basi mimi Mbunge wao nipo lakini Serikali za Mitaa pamoja na Serikali Kuu tuone ni namna gani tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, Serikali ina utaratibu mzuri kama kusaidia wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya. Hanang wanajitahidi sana, wana vituo kama saba walijitolea wao wenyewe kuvijenga na napenda kuishukuru TAMISEMI kupangia na kutoa shilingi milioni mia tano kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Simbai ambacho kipo kwenye kata ambayo iko pembezoni na kitasaidia watu wengi sana hata wale wa Kondoa watakuja kwenye kile kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuendelee kuungana na wananchi kwa sababu afya ni muhimu sana. Watu wanaokwenda kwenye kilimo, wanaokwenda katika ufugaji, wanaofanya biashara ni wale wenye afya. Kama hatuna misingi mizuri ya afya itakuwa ngumu sana kutekeleza hata ilani yetu na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za vijijini, naishukuru na kuipongeza Serikali kuunda *TARURA* kwani itasaidia barabara za vijijini. Tujue kwamba barabara kuu na za mikoa hazitafanya kazi kubwa kama vijijini hakuna barabara. Naomba sana ugawaji wa fedha za Mfuko wa Barabara uwe hamsini kwa hamsini na ikiwezekana tutilie mkazo vyanzo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia *REA*, Serikali imefanya kazi kubwa kwani wananchi wa vijijini walikuwa hawategemei umeme lakini sasa umeme umefika vijijini, naipongeza sana Wizara. Hata hivyo, kuna upungufu mwingi ambao na kwa hakika usipofanya jambo upungufu hautaonekana, naomba Waziri aweze kufanya tathmini kila wakati ili aondoe upungufu ule kama kuruka taasisi au vijiji njiani wanapopeleka kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nichukue nafasi hii kwa sababu mwaka 2004 nikiwa Waziri wa Utumishi ndiyo tuliotoa ule Waraka kwamba wale watendaji waliomaliza darasa la saba kabla ya muda huo waendelee. Nimeishukuru sana Serikali kuchukua hatua hiyo, nampongeza sana Waziri Mkuchika kuweza kuelewa Waraka

ule na kuwaelekeza watendaji waone kwamba ule Waraka unasimamiwa vizuri na watu wasionewe ila pale ambapo wamegushi hatuwezi kusema neno lolote. Napenda kuwashauri watendaji wa Serikali wasipende kughushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie hakuna mahali ambapo panatakiwa *job security* kama Serikalini kwa sababu ndiyo uamuzi ambao unahusu maisha ya watu unapotoka. Watumishi wa Serikali wanapaswa wajisikie salama, wanapaswa wajisikie kwamba wanaaminika ili waweze kutenda haki ambayo inaweza ikasaidia maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana Wizara ya Utumishi iweze kusimamia sana usalama wa kazi kazini kwa sababu kwa kweli wasipokuwa salama hawatakuwa na uhakika katika kufanya uamuzi na mambo mengi yatasimama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mama Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hotuba ya Mawaziri wote wawili, naiunga mkono Ofisi ya Rais kwa kazi nzuri inayofanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, orodha iliyokuja mezani kwangu ya wajumbe wote wa CCM wamechangia, wajumbe wote wa CHADEMA wamechangia na wajumbe wote wa *CUF* wamechangia.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi katika maeneo ya pembezoni, mazingira yao ni

magumu. Kutokana na jiografia ya Ukerewe ambapo ina visiwa (38) Watumishi wengi wanakuja kuripoti na kuondoka, hali ambayo inasababisha upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika maeneo ya afya na elimu. Zahanati zetu, vituo vya afya pamoja na shule zina upungufu mkubwa wa watumishi katika Visiwa vya Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi au ushauri wangu ni kwamba, moja; pamoja na Halmashauri zetu kuwa na mipango mbalimbali ya motisha kwa watumishi wanaopangwa kwenye Halmashauri zetu, Serikali iwe na mpango maalum wa kuhakikisha kuwa watumishi wanaofanya kazi katika maeneo kama ya Ukerewe wapate *package* fulani ya mazingira magumu ili wasijione kama watu waliopewa adhabu na hivyo kutafuta kila njia kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kutokana na changamoto ya watumishi kuripoti na kuondoka katika maeneo kama Ukerewe, katika mgao wa watumishi Visiwa vya Ukerewe viangaliwe kwa mtazamo wa pekee na hivyo kupewa idadi ya kutosha ya wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa na Vitongoji; wananchi ndiyo injini kubwa ya maendeleo kwenye Halmashauri zetu lakini wanaweza kuwa na tija pale wanaporatibiwa na kusimamiwa na viongozi wetu wa ngazi za chini, mfano, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji lakini viongozi hawa wamekuwa na mfumo mbovu na malipo duni wakati wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza au nashauri kuwa, mfumo wa malipo kwa viongozi hawa ubadilishwe ikiwezekana basi Serikali Kuu iweze kuwalipa moja kwa moja badala ya kupitia Halmashauri kwa sababu nyingi zimekuwa haziwalipi viongozi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango kinacholipwa kwa viongozi hawa kiongezwe ili kiendane na hali halisi ya maisha ikizingatiwa kwamba wanatumia muda wao mwingi

kuhamasisha na kusimamia shughuli za maendeleo, muda ambao wangetumia katika shughuli zao binafsi za uzalishaji.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kuharakisha urasimishaji wa hati za maeneo ya wananchi ili kuwezesha kupata mikopo kiurahisi na kupunguza umaskini. Nashauri zoezi la utoaji huduma kwa wahitaji kupitia *TASAF* kuchunguzwa, kwani wataalam wengi hawana weledi katika utendaji. Watendaji wamesababisha misaada hiyo kuwaacha walengwa na kupewa wenye uwezo na hivyo zoezi hilo kukosa maana ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuwalipa watumishi waliostaafu stahiki zao kwani ajira inapokoma ni dhahiri mtumishi anakuwa na mipango yake ya kujikimu baada ya kustaafu. Hivyo, nishauri Serikali kuliona hilo kwani inaharibu taswira ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali kufungua milango ya uhamisho kwa watumishi wale ambao wanahitaji kuungana na familia pale mwenza mmoja anapohamishwa hivyo kuleta usumbufu kwa watoto ambao hawaelewi wabaki na mzazi yupi. Kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa mtumishi anapotaka kuhama, kuambiwa atafute mtu wa kubadilishana naye, je asipopatikana huyo mtu hivyo mtumishi anakosa haki ya kuhama? Je, huo ni wajibu wa mtumishi au Serikali kutafuta jinsi ya kujua ni wapi mtumishi huyo atapangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watumishi wapate kozi fupi za kujengewa uwezo ili wapate uelewa mpana katika sehemu zao za kazi.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Kwanza ni mgao wa Wilaya. Wilaya ya Tunduru ina eneo kubwa sana la utawala ambalo linalingana na eneo la Mkoa wa Mtwara wenye Wilaya Sita. Tunaomba Serikali ifikirie suala la kugawa Wilaya ya Tunduru ili kurahisisha shughuli za kuhudumia wananchi kwa kuleta huduma karibu na wananchi. Kila eneo la Jimbo liwe Wilaya kamili inayojitegemea kutokana na wingi wa watu na umbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tatizo la watumishi wa Halmashauri. Tuna upungufu mkubwa wa watumishi wa Halmashauri katika sekta zote za afya, elimu na kada zingine za kilimo. Tuna upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi zaidi ya 1,000 na Walimu wa Sayansi wa Shule za Sekondari zaidi ya 100 na kuna upungufu wa watumishi wa afya zaidi ya 700, tuna watumishi asilimia 26 tu katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wa Halmashauri wamekuwa na muda mrefu katika Halmashauri ya Tunduru na wanasababisha kudumaa kwa kazi za Halmashauri na wanafanya kazi kwa mazoea. Hivyo, tunaomba watumishi waliokaa muda mrefu wahamishwe, wapelekwe Halmashauri zingine ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya afya. Halmashauri ya Tunduru ina Kata 35 ina vituo vya afya vitano tu. Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kituo cha afya Nalasi lakini mpaka leo kuna msingi tu. Wananchi walifyatua tofali za udongo lakini tangu 2014 mpaka leo hamna kinachoendelea. Halmashauri inatenga fedha kila mwaka lakini hazipatikani kabisa, hivyo naomba Kituo hicho cha Afya Nalasi ambacho kitahudumia Kata mbili za Nalasi Magharibi na Nalasi Mashariki zenye wakazi zaidi ya 30,000 kijengwe na Serikali ili kuheshimu ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kituo hicho naomba Serikali isaidie Halmashauri kujenga vituo vya afya

angalau vinne zaidi kupunguza adha ya huduma kwa akinamama na watoto. Kata hizo ni Malumba, Lukumbule, Ligoma, Misechela na Tuwemacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni maji. Kuna tatizo kubwa la maji katika maeneo mengi ya Jimbo la Tunduru Kusini, kutokana na mabadiliko ya tabianchi mito mingi imekauka kabisa hasa katika Vijiji vya Mchoteka, Likweso, Mnemasi, Molandi, Mdumba, Misyaje, Mbesa, Uliwana, Chukano, Nasumba, Wenje, Mkapande, Nuwemecho, Nasya, Namasadau, Miseula, Ligoma, Chemchem, Makade, Kozango, Likada, Senei, Azimio, Angalia na kadhalika. Tunaiomba Serikali kutuchimbia visima virefu na vifupi ili kutoa huduma ya maji safi kwa wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya maji miwili ya Mbesi na Mtina ni ya muda mrefu bado inasuasua katika ukamilishaji wake na mradi wa Mtina Mkataba wa ujenzi Halmashauri umekatishwa wakati mradi umefikiwa zaidi ya asilimia 60, kufanya mradi ule uendelee kuchelewa zaidi kukamilika. Vile vile tunaomba miradi mipya ya maji ili kupunguza adha ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu. Upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa na vyoo pamoja na nyumba za Walimu. Kuna tatizo kubwa sana la vyumba vya madarasa kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule za msingi, hivyo tunaomba Serikali isaidie kutoa fedha kuongeza jitihada zilizofanywa na wananchi ambao wanaweza kufyatua tofali 100,000 kwa ajili ya madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Tunduru Kusini halina *high school* hata moja, tumeomba angalau shule mbili za Kata zipandishwe hadhi ili ziwe *high school.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia hoja ya hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa Wilaya, Wilaya ya Tunduru ina eneo kubwa sana la utawala kulinganisha na eneo la Mkoa wa Mtwara wenye Wilaya sita. Tunaomba Serikali ifikirie suala la kugawa Wilaya ya Tunduru ili kurahisisha shughuli za kuhudumia wananchi kwa kuleta huduma karibu na wananchi. Kila eneo la jimbo liwe Wilaya kamili inayojitegemea kutokana na wingi wa watu na umbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watumishi wa halmashauri; tuna upungufu mkubwa wa watumishi wa halmashauri katika sekta zote za afya, elimu na kada zingine za kilimo. Tuna upungufu wa Walimu wa shule za msingi zaidi ya 1,000 na Walimu wa sayansi shule za sekondari zaidi ya 100 na kuna upungufu wa watumishi wa afya zaidi ya 700, tuna watumishi asilimia 26 tu katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watumishi wa halmashauri wamekaa muda mrefu katika Halmashauri ya Tunduru na wanasababisha kudumaa kwa kazi za halmashauri na wanafanya kazi kwa mazoea. Hivyo, tunaomba watumishi waliokaa muda mrefu wahamishwe wapelekwe halmashauri zingine ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vituo vya afya, halmashauri ya Tunduru ina kata 35 ina vituo vya afya vitano tu. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga Kituo cha Afya Nalasi lakini mpaka leo kuna msingi tu. Wananchi walifyatua tofali za udongo lakini tangu 2014 mpaka leo hamna kinachoendelea. Halmashauri imetenga fedha kila mwaka lakini hazipatikani kabisa, hivyo naomba Kituo hicho cha Afya Nalasi ambacho kitahudumia Kata za Nalasi Magharibi na Nalasi Mashariki zenye wakazi zaidi ya 30,000 kujengwa na Serikali ili kuheshimu ahadi ya Rais Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na kituo hicho naomba Serikali isaidie halmashauri kujenga vituo vya afya angalau vinne zaidi kupunguza adha ya huduma kwa

akinamama na watoto. Kata hizo ni Malumba, Lukumbule, Ligoma, Msechela na Tuwemacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la maji katika maeneo mengi ya Jimbo la Tunduru Kusini. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi mito mingi imekauka kabisa hasa katika Vijiji vya Mchoteka, Likweso, Mnemasi, Molandi, Machemba, Misyaje, Mbesa, Chiwana, Chikomo, Nasomba, Wenje, Mkapunda, Tuwemacho, Nasya, Namasalau, Misechela, Ligoma Chemchem, Mkandu, Kazamoyo, Lukala, Semeni, Azimio, Angalia na kadhalika. Tunaiomba Serikali kutuchimbia visima virefu na vifupi ili kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya maji miwili ya Mbesa na Mtina ni ya muda mrefu bado inasuasua katika ukamilishaji wake. Mradi wa Mtina mkataba wa ujenzi halmashauri umekatishwa wakati mradi umefikia zaidi ya asilimia 60 na kufanya mradi ule kuchelewa zaidi kukamilika. Vilevile tunaomba miradi mipya ya maji ili kupunguza adha ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu, kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa na vyoo pamoja na nyumba za Walimu. Kuna tatizo kubwa sana la vyumba vya madarasa kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi katika shule za msingi, hivyo, tunaomba Serikali isaidie kutoa fedha kuongeza jitihada zilizofanywa na wananchi ambao wameweza kufyatua matofali 100,000 katika kila kijiji kwa ajili ya kujenga vyoo, madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Jimbo la Tunduru Kusini hamna shule ya *high school* hata moja. Tunaomba angalau shule mbili za kata zipandishwe hadhi ili ziwe *high school.*

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutupatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara yake kwa kuandaa na kuiwasilisha hotuba yake kwa ufasaha na umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ni Mfuko wenye madhumuni ya kuwapunguzia wananchi makali ya kiuchumi. Naipongeza Serikali sana kwa mfuko huo na naomba uendelee zaidi. Hata hivyo, imeonekana kuwa bado kuna matatizo katika utambuzi wa kaya zinazohusika, kuna udanganyifu katika kuwatambua walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, Serikali iwashirikishe Walemavu, Wabunge katika zoezi la kutambua kaya husika ili kuondoa mkanganyiko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Mfuko huu ni mzuri sana, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko huu. Bado hakuna uwiano wa kiwango cha wahitimu wanaomaliza shule za *VETA*. Kiwango cha wanaomaliza shule za *VETA* ambao ni miongoni mwa walemavu ni mkubwa kuliko kiwango cha fedha zinazotolewa kwa mkopo. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iongeze kiwango cha fedha za mikopo kwa Mfuko huu ili dhamira ya Mfuko huu iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuchangia katika hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa umahiri wanaoonesha katika kuongoza Wizara hii nyeti katika nchi hii. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Afya ya Jamii; katika ulimwengu wote afya ni jambo muhimu sana kwa

mwanadamu. Naipongeza Wizara kwa kuanzisha utaratibu mzuri wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika utaratibu huu ni kuongeza kasi ya kuwapatia kadi za afya wananchi husika. Bado idadi ya wanachama 12,278,406 ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo; naipongeza Wizara kwa ubunifu wanaoonesha kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo lakini bado inaonekana kuna utegemezi mkubwa wa fedha katika utekelezaji wa baadhi ya miradi, bado Serikali inategemea misaada kutoka taasisi za nje. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iongeze *speed* ya kutafuta vyanzo vya mapato ili tuweze kuendesha miradi yetu kwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema pia naendelea kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga kwa kunichagua na nawaahidi kuwatumikia kwa utumishi na uwakilishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *education is the most powerful weapon which we can use to change the World (By* Nelson Mandela Madiba) *education is the key of life.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, semi zote hizi zimetumiwa na Wahenga wetu zikiwa na maana kubwa sana. Katika miaka ya 1970, Tanzania ilikuwa katika *level* moja ya kiuchumi au hata sarafu yetu ilikuwa na thamani kuliko sarafu ya nchi za Singapore, Malaysia, Indonesia, China, Vietnam na Kenya lakini leo hii 2018, nchi zote hizi zimetuacha kiuchumi na kielimu na sababu kubwa wenzetu hawa waliwekeza katika elimu kuanzia *nurseries, primaries, secondaries, colleges and universities*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi za East African *Communities* tunaishinda Southern Sudan tu, nchi nyingine zilizobaki zimetuacha nyuma. Nchi nilizozitaja zimefikia uchumi wa dunia ya kwanza na dunia ya pili sababu waliwekeza katika elimu, hiyo ndio siri ya mafanikio. Kenya walipoamua elimu bure waliamua kwa dhati ya moyo wa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, Serikali iwekeze katika elimu ili tuepuke shida na matatizo yaliyopo katika elimu ya Tanzania kuanzia mitaala, chakula mashuleni, mikopo vyuo vikuu. Tanzania uchumi wake ukue *practically* badala *theoretically* kama nchi nilizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana 11 aprili 2018 Rais wa Kenya Uhuru Kenyata alisaini sheria kwa niaba ya Serikali kuwapatia huduma ya taulo za kike kwa wanafunzi wote wa kike nchini Kenya kupatiwa huduma hiyo bure (*free of charge).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure bado katika ngazi za chini haieleweki na Walimu wetu wamechanganyikiwa maji na umeme vinakatwa, walinzi hakuna na shule zinaibiwa vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, naipongeza Serikali kwa kutoa katika halmshauri mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Tanga kutupatia shilingi 1.4 bilioni kwa ajili ya Vituo vya Afya vifuatavyo:-

Makorora 500 milioni, Mikanjuni 400 milioni na Ngamiani 500 milioni na shughuli za ujenzi sasa hivi zinaendelea katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga hatuna hospitali ya Wilaya, katika bajeti ya halmashauri, Baraza la Madiwani tumetenga shilingi milioni300, *regardless* shilingi milioni 400 ambazo zimeshajenga *administration block* ambapo kwa sasa baadhi ya vyumba vinatumika kutoa huduma kwa wananchi kama zahanati. Naiomba Serikali itupatie shilingi

bilioni 1.6 ili tuweze kujenga *Out Patient Department (OPD).* Kwa kufanya hivi tutaipunguzia mzigo mkubwa wa wagonjwa toka Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Bombo ni hospitali ya rufaa ambayo ina upungufu mkubwa wa vifaa tiba, Madaktari Bingwa lakini hata miundombinu, *lift* ina muda mrefu zaidi ya miaka mitatu ni mbovu na *old model* inahitajika *lift* mpya Bombo.

Mheshimiwa Mwenyekitim, nimefanya utafiti na ufuatiliaji katika kampuni maarufu ya *lift ya OTIS- FRANCE* zinahitajika *euro* 126,000 ambazo ni sawa na shilingi milioni 400 kuweza kupata *lift* mbili mpya kwa ukubwa wa jengo la *lift* lililopo. Naiomba Serikali itoe hizi *euro* 126,000 ili kutatua tatizo la *lift* na kuondoa adha ya mabaunsa kubeba wagonjwa na pia tunaomba Madaktari Bingwa wa mifupa, vichwa na magonjwa ya akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, nawapongeza wakulima wote Tanzania. Tanzania miaka 57 baada ya uhuru bado kilimo chetu ni cha jembe la mkono 80% na bado kilimo kipo katika propaganda za kisiasa na misamiati kibao. Kilimo cha ushirika, kilimo cha kufa na kupona, kilimo kwanza, kilimo cha bega kwa bega, lakini Serikali bado haipo *serious* na hata pale wakulima wanapofanya bidii ya kulima na kupata mazao ya kutosha kwa chakula na biashara wanakatazwa kuyauza kwa soko wanalotaka wenyewe. Mfano, zao la mahindi, Mbaazi na zao la Karafuu Zanzibar. Baada ya Bunge kuchachamaa mahindi ruksa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, Tanga *City Council*, tunazalisha muhogo na matunda kwa wingi katika Kata za Kirare, Tongoni, Mabokweni, Pongwe, Mzizima na Chongoleani lakini hakuna soko la uhakika. Ni aibu kwa Tanzania kuagiza *juice* za *orange*, *mango*, *guava*, mastafeli tena tunaagiza kwa fedha za kigeni kutoka nchi za Saudi Arabia, South Africa na Kenya *juice* za *Ceres* na *tropical*. Serikali ijenge viwanda vya kusindika *(processing)* matunda Tanga kulingana na wingi wa matunda yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo; ufugaji katika Tanzania imekuwa ni balaa wafugaji wanateseka wao na mifugo yao, hawaruhusiwi kuchunga mifugo yao katika mapori ya hifadhi wala ranchi za Serikali kwa kisingizio kuwa wanavamia hifadhi za Taifa. Mifugo ni uchumi na biashara, nchi kama Botswana, Swaziland na Ethiopia zinafaidika kiuchumi na kutumia fedha hizo katika miradi ya maendeleo. Tanzania wafugaji wetu wananyang'anywa mifugo yao na kutiwa umaskini hali inayosababisha wafugaji kukimbia familia zao kutokana na umaskini baada ya kunyanga'anywa mifugo yao. Wananyang'anywa mifugo ng'ombe 500, 700 hadi 2,000 habaki na hata ng'ombe mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka alama kwa moto, huu ni ukatili wa kupindukia kwa kuwa chuma cha moto ni maumivu makali kwao. Waziri wa Mifugo anazindua uwekaji alama kwa kumchoma mnyama kwa moto. Ushauri Serikali itoe elimu ya ufugaji wa kisasa kwa kuweka *pin* masikioni badala ya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi na zana za kisasa, wavuvi wamesahauliwa na kubwa kwao ni kulipishwa ushuru wa samaki, kunyang'anywa nyavu na boti zao. Hii sio haki inahitajika elimu na *replacement* za vifaa vinavyokubaliwa kisheria na sio kuchoma moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA (Tanzania Rural and Urban Road Agency);* katika Bunge la mwaka jana bajeti tulipatiwa taarifa na kupitisha *TARURA,* tunajua nia njema ya Serikali lakini *TARURA* haijafahamika kwa Wabunge na Madiwani hata kidogo. Tuliomba Serikali itufanyie semina Wabunge, kisha Madiwani lakini hadi leo ni mwaka bado hakuna semina. Ushauri wangu, Wabunge tupatiwe semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za vijana na akinamama asilimia kumi; kila halmashauri inatakiwa kutenga 10% za vijana na akinamama, lakini kutokana na vyanzo vya mapato vya *property tax* na mabango kuporwa na Serikali Kuu (*TRA*), halmashauri kwa sasa zina hali mbaya

kifedha. Hii ni moja ya sababu za kutotengwa kwa fedha hizi. Ushauri wangu ni kwamba, naomba Serikali irudishe vyanzo vya *property tax* na mabango ya biashara ili makusanyo haya yaweze kuziwezesha halmashauri kutenga fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utumishi ni sehemu muhimu katika nchi yetu ambayo ina changamoto nyingi ikiwemo watumishi na wafanyakazi kucheleweshwa michango yao katika Mifuko ya kijamii kama vile *NSSF, LAPF, GEPF* na kadhalika. Miongoni mwa changamoto nyingine ni mtindo wa kuwahamasisha Walimu toka sekondari kuwarudisha kufundisha shule za msingi bila ya kuwalipa stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo na tunaona ni jambo jema kwa kisingizio cha kuboresha tatizo la upungufu wa Walimu katika shule za msingi, lakini hili ni tatizo ambalo Walimu hawa wanafanya mgomo wa kimya kimya na matokeo yake wanaoathirika ni wanafunzi kwa kuwa Walimu hawafundishi kwa moyo, wanafunzi wanafeli na ushahidi wa hili shule zinazoongoza kwa ufaulu ni za *private.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira kukosekana katika halmashauri, kufuatia zoezi la uhakiki wa vyeti feki watumishi waliokosa vyeti vya *form four* pamoja na Serikali kutangaza kuwa walioathirika na zoezi hili warudishwe kazini, lakini kuna tabia kule chini likitoka agizo la Serikali katika utekelezaji wanasema hatujapokea waraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, waraka huo ushushwe ngazi za chini *immediately,* wale ambao wamefariki kufuatia *pressure* na mshtuko ingawaje kufuatia zoezi hili pia athari zimepatikana katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya, Madktari na wauguzi baadhi wamekosekana na vituo, zahanati zimekosa watumishi na ajira mpya vibali havitolewi bila ya kuelezwa sababu zenye kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu, bado kuna upungufu mkubwa sana katika sekta ya Walimu (shule za msingi, shule za sekondari na vyuo). Mfano, Mamlaka ya Maji Tanga wafanyakazi wengi wamefukuzwa katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, tunazo kata 27 na mitaa 181; Watendaji wa Mtaa katika mitaa 181 waliopo 123 na pungufu ni 58. Watendaji Kata katika kata 27, waliopo ni watendaji 13, pungufu ni 14. Pia kuna mitaa ambayo kuna makaimu ni zaidi ya miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, vibali vya ajira vitolewe haraka ili kuondoa upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapa pole viongozi wa CHADEMA zaidi ya 15 wakiwemo Wabunge wa Upinzani ambao wana kesi katika Mahakama zetu, kesi za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe pole na Mungu amponye Mheshimiwa Lissu ili aweze kurudi aendelee na majukumu yake. Pamoja na kwamba mpaka sasa ripoti ya tukio la Mheshimiwa Lissu Bunge halijaleta ripoti hii na malalamiko mengi yaliyopo nchini. Mfano, kupotea Ben Saanane na Mwandishi Azroy, kifo cha Aquilina, vifo vya watoto Kibiti na Tundu Lissu kupigwa risasi. Ni kwa nini Serikali inatoa majibu tata na kuacha wananchi wakibaki na sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali kuendelea kukaa kimya inapelekea wananchi waamini kwamba Serikali hii ni Serikali isiyojali wanyonge na Serikali inayowaonea watu bila kuwasaidia wananchi na matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa kufanya mikutano ya hadhara. Serikali ina hofu gani kuzuia mikutano ya siasa. Hii inaonesha kuwa katika Serikali hii ya Awamu ya Tano inaogopa kufichuliwa udhaifu uliopo ndio maana inaogopa ukweli.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja zifuatazo kwa Wizara mbili zilizowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijinasibu kuwa inashughulikia rushwa. Manispaa ya Morogoro ujenzi wa barabara ya kilometa nne kutoka Kichangani – Tubuyu. Barabara hii imejengwa kwa fedha za mkopo wa *World Bank* ambayo tunatarajia fedha hizo zitalipwa na kodi za jasho la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza barabara hiyo kilometa moja imejengwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.4 kwa kilomita nne, hivyo imegharimu 13.8 bilioni, wakati haina mto, korongo wala milima imenyooka kama rula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Madiwani walihoji matumizi mabaya ya barabara hiyo kwa fedha, matokeo yake rushwa za wazi zilianza kutolewa kwa Madiwani wa CHADEMA na CCM. Kuna kigugumizi gani katika kufuatilia ubadhirifu wa fedha waziwazi zilizotafunwa na wakandarasi wakishirikiana na watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii niliileta Bungeni nikamuuliza swali Waziri wa TAMISEMI ambaye wakati huo alikuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Jafo mwaka jana aliendа kuitembelea barabara hiyo na akaunda Kamati ya kufuatilia baada ya kutoridhika na pesa zilizotumika ikilinganishwa na thamani ya barabara yenyewe lakini cha kushangaza hadi sasa hakuna kitu kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi huu wa wazi wazi Serikali imeuona lakini hakuna hatua zozote zimechukuliwa. TAKUKURU wamehoji Madiwani wa Manispaa wamekiri kupokea rushwa kwa nini Serikali haichukui hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro wamevunja nyumba za wananchi Mtaa wa *CCT*

Mkundi kwa madai ya kujenga kwenye hifadhi ya lami lakini wananchi hawa wana hati halali za viwanja pamoja na vibali vya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika Serikali ilipeleka huduma za maji, umeme, ujenzi wa shule, Ofisi ya Mtendaji wa Kata na wana vitambulisho vya makazi na walipiga kura. Sasa hivi Serikali inawahamishia wananchi wa Mtaa wa *CCT* katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero. Haki haikutendeka kwa wananchi na imesababisha usumbufu na taharuki.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu wafanyakazi wanaolipwa kwa kifungu 5000 (mapato ya ndani) katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga (Mafinga *TC*). Kufuatia kugawanywa kwa Halmashauri ya Mufindi na kupatikana Mafinga *TC*, wafanyakazi wengi wanaolipwa kwa mapato ya ndani walipelekwa Mafinga *TC*. Mafinga *TC* tunatumia *around* Sh.12,000,000 kila mwezi kulipa wafanyakazi hao ambao miongoni mwao wako ngazi ya uandamizi. Hali hii imekuwa na changamoto kubwa mbili kwa Halmashauri ya Mafinga Mji na kwa watumishi.

(i) Kwa halmashauri, tunajikuta tunatumia kiasi cha Sh.120,000,000 kwa mwaka kulipa mishahara ya watumishi. Kama watumishi hao wataingizwa katika mfumo wa Hazina, fedha hiyo itasaidia katika shughuli za maendeleo.

(ii) Kwa watumishi, kutokana na mishahara yao kutegemea makusanyo ya ndani, wafanyakazi hawa wamekuwa wakichelewa kupata mishahara, hali hii imekuwa ikiathiri hata huduma zao za afya. Mara mbili mfanyakazi ameshindwa kupata huduma Hospitali ya Ikonde kwa sababu ilionekana kuwa michango ya bima ya afya haijawasilishwa. Baadhi yao waliokopa benki, marejesho yanacheleweshwa na kujikuta wakipigwa penati. Hali hii inawaathiri sana wafanyakazi hao, wanajihisi ni *second citizen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itusaidie kuwaingiza watumishi hawa ili walipwe na Serikali Kuu. Yawezekana ni jambo ambalo lipo katika halmashauri nyingi, lakini naomba Mafinga *TC* tutazamwe kwa macho mawili. Kuna hoja kuwa Mafinga tuna mapato ya Msitu wa *Sao Hill,* lakini ukweli ni kuwa *beneficiary* wa Msitu wa Sao Hill ni Mufindi *DC*, hivyo, naomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu kupandishwa madaraja/vyeo watumishi. Kuna manung'uniko makubwa sana kuhusu kubadilishwa kwa tarehe za wao kupanda vyeo, baadhi yao walipanda mwaka 2015. Ni kweli kuwa maelekezo ya kuhakiki vyeti na suala zima la watumishi hewa, suala hili lilisitishwa, aidha, mishahara yao haikubadilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, waraka ulitoka kuwa barua au kupanda vyeo kusomeke kuanzia 1/11/2017 na wengine kuanzia tarehe 1/4/2018. Nafahamu yawezekana kutokana na suala la kibajeti Serikali inaona kuwa itakuwa na mzigo mkubwa wa kulipa malimbikizo. Hali hii inaweza kushusha morali ya watumishi. Kama Serikali haitawalipa malimbikizo ni miaka *almost* mitatu itapotea na hivyo kuathiri hata *pension* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hekaheka nyingi za kuweka sawa masuala ya watumishi wa umma, nashauri na kupendekeza kuwa watumishi hao waangaliwe upya na vyeo vyao vizingatie tarehe ya awali ya kupanda vyeo. Ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuongelea kuhusu utawala bora. Utawala bora ni nini? Je, nchi yetu inazingatia utawala bora? Tumeona matukio mengi hapa nchini yasiyokidhi utawala bora wenye kufuata sheria na kujali haki za wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uhuru wa kutoa maoni na kupata habari. Hii ni moja ya msingi wa utawala bora kwa wananchi kupata habari lakini tumeona kwa sasa Serikali

imezuia hata wananchi kufuatilia majadiliano yanayoendelea ndani ya Bunge *(live on TV).* Baadhi ya waandishi ya habari wamekuwa wakipotea, wengine kupigwa na baadhi ya magazeti kufungiwa kisa ni kwa kutoa maoni yao dhidi ya Serikali. Hata vyama vya siasa vilivyoanzishwa kisheria kwa Sheria Na.5 ya mwaka 1992 bado haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara ili kuwaeleza wananchi sera zao badala yake viongozi wengi wa upinzani wamekuwa wakifunguliwa mashtaka kwa kisingizio cha uchochezi. Je, huu ndiyo utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ukiukwaji wa haki za raia. Sasa hivi katika nchi yetu panakuwepo na kundi la watu wasiojulikana wanaoteka watu. Mara nyingi watu wamekuwa wakiokotwa pembezoni mwa bahari ya hindi wakiwa wamefariki. Mfano, Mwandishi wa Gazeti la Mwananchi, Ndugu Azovi Gwanda na Msaidizi wa Mwenyekiti wa CHADEMA, Ndugu Ben Sanane, mnadhimu wetu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu alipigwa risasi mchana kweupe lakini mpaka leo Serikali haijatoa taarifa yoyote kuhusu matukio hayo yanayoendelea hapa nchini. Je, usalama wa raia uko wapi hapa nchini? Ni lini Serikali itatoa maelezo ya kina juu ya hatua iliyofikia katika kukomesha matukio haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ajira. Utawala bora ni pamoja na kuwaongezea watumishi mishahara lakini kwa miaka miwili sasa watumishi hawajaongezewa mishahara kama sheria inavyoelekeza. Huu siyo utawala bora kabisa. Hii ni pamoja na kuwapandisha madaraja watumishi wa umma kwani haijafanyika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo kutoka kwa wakati katika Halmashauri; fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu haziendi au hazitumwi kwa wakati kwenda kwenye Halmashauri na kupelekea Halmashauri kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe siku za nyuma Halmashauri zilikuwa na vyanzo vya mapato vya kukusanya kodi za ardhi na ada mbalimbali ambazo zote hizi zinakwenda Serikali Kuu. Ni vizuri sasa katika makusanyo hayo Halmashauri zikate asilimia 30 ya makusanyo ili zibaki kwa ajili ya maendeleo. Halmashauri nyingi zimeshindwa kutenga hata zile asilimia10 kwa ajili ya vijana, akinamama na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; ili mwanafunzi aweze kufaulu vizuri na Mwalimu akubali kufundisha bila kuchoka ni lazima mazingira ya kufundishia na miundombinu ya kufundishia iwe mizuri. Tumeshuhudia shule nyingi tukianza na shule za awali, nyingi hazina Walimu wa kutosha, hakuna nyumba za Walimu, zaidi vijijini, hakuna Walimu wanataka kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Walimu wa hisabati na sayansi ni mkubwa takribani 22,460 ni pungufu na shule za msingi ni takribani 186,003 ni pungufu sawa na asilimia 83.1. Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha upungufu huu unajazwa kwa kuajiri Walimu? Baada ya hayo ni lazima Serikali ihakikishe:-

(a)Walimu wanalipwa posho zao;

(b)Pawepo na mashimo ya vyoo ya kutosha; na

(c)Maabara zikijengwa ihakikishwe zina vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; Serikali imekuwa ikitoa kauli ya kujenga zahanati na vituo vya afya katika kila kijiji na kata lakini ikumbukwe kuna zahanati zilizopo lakini bado zina upungufu mkubwa, hazina Wauguzi wa kutosha, dawa hazipelekwi kwa wakati, hazina *ambulance* ya kupeleka mgonjwa aliyezidiwa pengine anahitaji rufaa kwenda ngazi ya juu. Mfano, kutoka zahanati kumkimbiza hata hospitali ya Wilaya wanashindwa na mara nyingine kupelekea wagonjwa kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha mahali kama Moshi Manispaa hakuna Mfamasia, aliyepo ni *technician* tu, hivi huyu anaendaje kukagua Mafamasia walio juu yake kitaaluma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; katika Hamashauri yetu bado kilimo hakijathaminiwa ila Serikali imekuwa ikija na mbwembwe za maneno tofauti kama vile kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kwanza na kadhalika, lakini kilimo bila watalaam hakiwezi kuwa na tija. Kuna uhaba mkubwa wa Maafisa Ugani na uhaba wa pembejeo. Mfano, sasa hivi mbolea ni ghali sana mfuko Sh.53,000, mkulima wa kawaida anaweza kununua? Hata wakilima na kufanikiwa kuna uhaba mkubwa wa kuuza mazao yao. Sasa hivi mbaazi ziko tu nyumbani kwa wakulima na mahindi mengi yanaharibika na hata wakulima wakitaka kuuza nje Serikali inazuia na hata wakitaka vibali ni ngumu kuvipata.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ukurasa wa saba, tunaona ufafanuzi wa fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka 2017/2018 ni trilioni 6.57 kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hiyo tunaona mishahara ni trilioni 4.27 ila jumla ya fedha zilizopokelewa kufikia Februari, 2018 ni trilioni 3.33 sawa na asilimia 50.68 ya bajeti yote iliyoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, utoaji wa fedha iliyobakia utatolewa ndani ya kipindi hiki kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, sababu tukiangalia muda uliotumika kutoa fedha iliyotolewa ni mwingi na fedha iliyotolewa inaonesha haitoweza kutosheleza hata bajeti ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira ni la muhimu katika Taifa, hasa tunaposema tunahitaji nchi ya viwanda, tutaendaje kupata *product* ya wataalam wa kuendeleza hivi viwanda siku za mbele endapo Walimu mashuleni hakuna, Walimu wa sayansi hakuna wa kutosha. Je,

tutapataje *product* yetu wenyewe ya kuendeleza viwanda vyetu endapo hatuajiri Walimu wa kutosha kutoka ngazi ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifanye mikakati ya makusudi ya kuajiri walimu kuanzia ngazi ya msingi na pia kuwatengenezea mazingira mazuri Walimu sehemu wanazopangwa kwenda kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la utawala bora nchi yetu inatakiwa isimamie kwenye misingi ifuatayo:-

Kuzingatia utawala wa sheria, kuzingatia busara na kuzingatia heshima. Ila kwa mwenendo wa sasa unaoendelea wa kila mtu anasema anachokifikiria yeye italeta shida. Mfano tumeshuhudia Wakuu wa Wilaya wakiwaweka Wabunge ndani na kuwafukuzisha watu kazi bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Waziri mwenye dhamana, Wakuu wa Wilaya, Mikoa na Wakurugenzi wanaochukua hatua bila kujali taratibu wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** sasa nizungumzie Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kama ifuatavyo:-

Suala la ajira ni la muhimu katika Taifa hasa tunaposema tunahitaji nchi ya viwanda tutaendeleaje kupata *product* ya wataalam wa kuendeleza hivi viwanda siku za mbele endapo Walimu mashuleni hakuna? Walimu wa sayansi hakuna wa kutosha, je, tutapataje product yetu wenyewe ya kuendeleza viwanda vyetu endapo hatuajiri Walimu wa kutosha kutokea ngazi ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifanye mikakati ya makusudi ya kuajiri Walimu kuanzia ngazi ya msingi na pia kuwatengenezea mazingira mazuri Walimu sehemu wanazopangiwa kwenda kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la utawala bora nchi yetu inatakiwa isimamie kwenye misingi ifuatayo:-

Kuzingatia utawala wa sheria; kuzingatia busara na kuzingatia heshima. Kwa mwenendo wa sasa unaoendelea wa kila mtu anasema anachokifikiria yeye italeta shida. Mfano tumeshuhudia Wakuu wa Wilaya wakiwaweka Wabunge ndani na kufukuzisha watu kazi bila kufuata utaratibu. Nashauri Waziri mwenye dhamana, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wanaochukua hatua bila kujali taratibu za ajira wachukuliwe hatua za kisheria.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba hii na kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwa wasikivu. Waziri ametoa tamko Bungeni kuwa watumishi walioajiriwa kabla ya mwaka 2004, waliosimamishwa kazi sababu walikuwa na cheti cha darasa la saba hawana cha kidato cha nne warudishwe kazini. Nawapongeza Serikali kwa kuwarudisha kazini na kuwalipa mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo sasa ni wale walioajiriwa tangu mwaka 2004 na kuendelea wamesimamishwa, hawa hatma yao ni nini? Hawa ni watu wa hali za chini na kawaida, ni maskini, ni wanyonge, wametumikia nchi hii kwa zaidi ya miaka 10, je, Serikali itawasaidiaje kwa sababu hawa wa darasa la saba hawaajiriki tena. Fedha zao zilikatwa zikawekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii mfano *NSSF*, uwezekano wa kuajiriwa haupo sababu ni darasa la saba. Naomba ili kuwasaidia warudishiwe michango yao iliyo kwenye hii mifuko, Serikali inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la utawala bora; naomba kutumia fursa hii kuikumbusha Serikali ya CCM misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali na taasisi za umma kutekeleza majukumu yake kwa kufuata Katiba, Sheria na taratibu zilizowekwa. Taasisi za Serikali kusimamia rasilimali za umma kwa manufaa ya wananchi, kutengeneza mfumo wa kutoa haki bila upendeleo, kulinda demokrasia, kulinda amani, kulinda haki za binadamu, uwajibikaji, uwazi, utawala wa Sheria kufuta *chain of command.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeonesha upungufu mkubwa katika kufuata misingi ya utawala bora. Kwa mfano, sasa hivi kila kiongozi anatoa matamko kuanzia Rais, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Polisi wa Mikoa, Wakurugenzi bila kufuata misingi ya utawala bora; tena matamko mengine yamekuwa hayatekelezeki na ya kudhalilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wakuu wa Mikoa na Wilaya wamekuwa na mamlaka makubwa mpaka kufikia kuwaweka Wabunge ndani kwa *personal interest.* Napenda kuishauri Serikali kuzingatia misingi ya utawala bora ili tuweze kulinda amani, demokrasia na kutoa haki sawa kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia hotuba ya TAMISEMI; nimesoma hotuba ya TAMISEMI na nimegundua upungufu katika sehemu tatu. Moja, hotuba hii haina jicho la kijinsia; pili, haina mnyambulisho wa *data;* tatu, haina *consistency.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukurasa wa 12 wa hotuba hii inaonesha asilimia 49 ya pesa za maendeleo hazikwenda kwenye halmashauri. Napenda Waziri atakapokuja ku-*wind up* atueleze ni kwa nini pesa hizi hazikwenda wakati Serikali imekusanya mapato kwa asilimia 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la vijana na wanawake. Taarifa ya ajira kutoka *National Bureau of Statistics* inaonesha jumla ya watu 2,334,969 na *youth employment rate is 13.7 percent* kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2015/2016. Naomba kufahamu mkakati wa Serikali juu ya ajira kwa vijana. Serikali inasema vijana wajiajiri wakati hawana mitaji watajiajiri vipi? Mapato ya ndani ya halmashauri hayatoshi kuwapa vijana asilimia tano na wanawake asilimia tano. Ukiangalia ukurasa wa 23 wa hotuba ya TAMISEMI ni asilimia 15 tu ya vikundi vya vijana na wanawake waliweza kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; Serikali iwa-*guarantee* vijana ambao wamemaliza vyuo vikuu ili waweze kupata mikopo kutoka taasisi za fedha ili waweze kujiajiri kwa kutumia vyeti vyao.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Walimu wa sayansi, Sekondari Kakonko. Nchi nzima ina uhaba wa Walimu wa sayansi wa sekondari zaidi ya 15,000. Kwa mantiki hiyo sera ya uchumi wa viwanda ni ndoto nchini maana wataalam watakuwa hawapo kutokana na ukosefu wa sayansi. Kakonko kuna upungufu. Ushauri ni Serikali iajiri Walimu wa sayansi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya mashuleni; kuna uhaba mkubwa mashuleni wa miundombinu, kama ifuatavyo: Nyumba za Walimu, vyumba vya madarasa, vyoo vya wanafunzi na Walimu, madawati, maabara, viwanja vya michezo na vifaa vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu; Walimu wana madai mengi yasiyolipika. Hali hii inakatisha tamaa Walimu na kushusha morali ya kazi. Ushauri ni Serikali ilipe madeni yote ya Walimu ili waongeze tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa Hospitali ya Wilaya Kakonko; Wilaya ya Kakonko haina hospitali ya wilaya na sasa Kituo cha Afya cha Kakonko kimeelemewa sana. Kituo hicho kinapata dawa kwa hadhi ya kituo cha afya

wakati kinahudumia wagonjwa kwa ngazi ya wilaya, hivyo kuishiwa dawa mapema. Pia, dawa muhimu zinaletwa kwa *level* ya kituo cha afya. Nashauri kwamba, Serikali ijenge Hospitali ya Wilaya Kakonko mwaka 2018/2019. Pia Kituo cha Afya Gwanumpu kifanyiwe ukarabati, kwani kilitengewa fedha 2017/2018 lakini fedha hazikutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Watumishi wa Afya. Kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya, jambo linalotishia afya za Watanzania sambamba na vifo vya akinamama wajawazito na watoto wachanga. Nashauri Serikali iajiri watumishi wa sekta ya afya. Ukosefu wa watumishi wa sekta ya afya kwenye vituo vilivyojengwa na *Bloombergy* vipatavyo vitano kwa ajili ya baba, mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji ya *World Bank* iliyokwama. Kuna miradi mitano ya maji ambayo imekamilika, lakini haitoi maji. Miradi hii ilishalipiwa fedha zote mpaka za *retention,* lakini hakuna maji. Miradi hiyo ya *World Bank* ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Maji Nyagwijima, Kata ya Mugurunza;
(ii) Mradi wa Maji Kiduduye, Kata ya Nugunza;
(iii) Mradi wa Maji Katanga, Kata ya Katanga;
(iv) Mradi wa Maji Muhange, Kata ya Muhange; na
(v) Mradi wa Maji Kiga, Kata ya Ruyeye una nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ichunguzwe haraka. Nashauri wasimamizi na wakandarasi waliohujumu miradi hii wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie Ofisi ya Rais, Utumishi kama ifuatavyo:

Upungufu mkubwa wa watumishi; uhaba wa Walimu shule za msingi *about* 95,000, uhaba mkubwa wa Walimu wa Sayansi (sekondari) zaidi ya 15,000, uhaba mkubwa wa

watumishi wa Sekta ya Afya. Nashauri Serikali itoe ajira Wizara ya Elimu na Afya ili kukidhi mahitaji ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utawala bora; utawala wa sheria *(rule of law);* kuna ukiukwaji mkubwa wa sheria za nchi na Katiba ya nchi kwa ujumla. Mfano, kuzuia mikutano ya hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusiana na uhuru wa mawazo. Wanaoikosoa Serikali au kuishauri wanapata misukosuko na wengine kupotezwa. Mfano Azori, Ben Saanane na kadhalika; watumishi wa kiroho kupata misukosuko baada ya kuhoji kuwepo kwa Katiba mpya au Serikali kukosolewa kwa maslahi ya Taifa. Mfano, Maaskofu Niwemugizi na Kakobe kufikia kuhojiwa uraia wao kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu tena za kikatiba. Magazeti yanafungwa na Waandishi wa Habari kukosa uhuru wa kuandika taarifa zao; *TV* kutozwa faini kwa sababu ya kutoa taarifa zisizoipendeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana haki ya kuishi; tumeshuhudia wananchi wakipoteza maisha na maiti zao kuonekana zinaelea baharini na Serikali iko kimya; mauaji ya mwanafunzi Akwiline Akwilini; mauaji ya Daniel, kiongozi wa CHADEMA, Kata ya Hananasifu na maiti yake kutupwa Fukwe za *Coco Beach*.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Ofisiya Rais, Utumish na Utawala Bora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie katika utawala bora; kumekuwa na tatizo la Wakuu wa Wilaya kuwanyanyasa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Mfano; Mkuu wa Wilaya ya Njombe amekuwa anaingilia vikao vya Madiwani na kutoa amri zisizo na tija kinyume na

kanuni. Naomba wakuu hao wapewe maelekezo wasivuruge Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utumishi; watumishi kutopewa maslahi stahiki; kuna watumishi ambao wamepandishwa madaraja lakini mishahara yao imebaki ile ile, mfano Wlimu. Naomba Serikali iwapandishe madaraja, lakini pia wapandishwe mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri wa TAMISEMI kwa moyo wake wa kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu Bure/Bila Malipo; kumekuwa na mkanganyiko mkubwa katika utekelezaji wa matamko ya viongozi wa juu wa Serikali. Matamko hayo yamekuwa yakitolewa bila kufanyiwa utafiti; matamko hayo yamekuwa yakiathiri wananchi. Mfano, Rais alipotamka kuwa wanafunzi wasitozwe kitu chochote, wazazi walikwenda shuleni na kudai fedha zao za michango na vyakula ili kurudishiwa. Hivyo, naiomba Serikali ihakikishe inapotamka ifanye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa sekondari kwenda kufundisha shule za msingi; kumekuwa na changamoto kubwa kwa kuhamisha Walimu wa sekondari kwenda kufundisha shule za msingi. Kwanza walimu hawa waliandaliwa kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wakubwa na siyo watoto wadogo. Hivyo, inakuwa vigumu sana watoto hawa wadogo kuwaelewa Walimu hawa wa sekondari na hii itasababisha watoto kufeli. Naiomba Serikali iajiri Walimu wanaolingana na ufundishwaji wa shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya mapato vya halmashauri kuchukuliwa na Serikali Kuu; Serikali Kuu imechukua vyanzo muhimu vya halmashauri. Kwa mfano,

ardhi ndiyo rasilimali pekee ambayo kila halmashauri inamiliki; ardhi ndicho chanzo cha mapato cha uhakika kwa kila halmashauri ya nchi hii. Halmashauri zinatakiwa kuchukua asilimia 30 ya kodi ya ardhi, lakini Serikali imechukua kodi hiyo na fedha hizo hazirudishwi na zikirudishwa zinarudi kwa kuchelewa. Naiomba Serikali kurudisha baadhi ya vyanzo vya mapato katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; wananchi wamehamasika wamelima mazao ya mahindi, matunda, nazi na mazao mengine. Wamejitoa kununua mbolea, dawa za wadudu na kutunza mazao yao kwa gharama kubwa na hatimaye wamevuna kwa wingi lakini hakuna soko. Kwa mfano, wananchi wa Ludewa katika Mkoa wa Njombe wanategemea sana zao la mahindi ambalo limekuwa likichukuliwa na watu *NFRA,* lakini mwaka huu hawajachukua mahindi hayo. Naiomba Serikali itafute soko kwa ajili ya wananchi wetu kwa kufungua mipaka ili mazao hayo yauzwe nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji; miradi ya maji katika halmashauri nyingi inasuasua; mfano, katika Halmashauri ya Mji wa Njombe kuna Miradi ya Maji ya Lugenge na Hagafilo, inasuasua. Naiomba Serikali ifuatilie miradi hiyo na kubaini tatizo linaloikwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bili za maji zimekuwa ni tatizo kubwa; zinaletwa bili kubwa wakati maji yanayotumika ni kidogo. Pia kumekuwa na uchakavu wa mabomba, mfano maeneo ya Kisasa mabomba yanapasuka ovyo. Naiomba Serikali ifuatilie suala hili la uchakavu wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote na Makatibu wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia sasa Ofisi ya Rais, TAMISMI kama ifuatavyo:

Nianze na sekta ya elimu; sekta hii kwa ujumla wake ina changamoto nyingi sana, elimu yetu haijawahi kuandaa wahitimu kuweza kujitegemea hata wale wa elimu ya juu. Changamoto kubwa ni mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara ambako hakuendani na mafunzo kwa Walimu juu ya hiyo mitaala mipya na hata vitabu wakiandaa havitoshi hasa kwa shule za msingi. Vilevile hata miongozo inayotolewa kila kukicha kunachangia kuwavuruga Walimu mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya uhaba wa Walimu ni kubwa sana nchini, mfano, katika Halmashauri ya Liwale kuna shule nyingi zina Walimu chini ya watano. Shule ya Ndapata, Mtungunyu, Nambinda shule hizi zina Walimu watatu tu kila moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kujenga miundombinu ya shule limeachwa kwenye Halmashauri jambo hili limefanya shule nyingi kuwa na miundombinu mibovu sana kwani Halmashauri nyingi zinashindwa kumudu jukumu hili hasa baada ya vyanzo vingi vya mapato vya Halmashauri kuchukuliwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; changamoto zilizopo kwenye sekta ya afya zinafanana kwa kiasi kikubwa na zile za elimu. Uhaba wa watumishi na miundombinu mibovu ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya hali ni mbaya sana hasa kwenye zahanati na hospitali za Wilaya. Mfano, Halmashauri ya Liwale yenye Kata 20, Vijiji 27 kuna Zahanati 34 tu ambazo zote zinahudumiwa na Manesi Wasaidizi, hazina matabibu wala Madaktari Bingwa wala mmoja na mpiga picha wa *x-ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, shida ya gari la wagonjwa kwenye hospitali ya Liwale ni kubwa sana. Mapato ya Halmashauri kununua gari ni jambo lisilowezekana kwenye Halmashauri ambayo hata zahanati zilizopo ni chache na miundombinu yake ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri licha ya kupokwa vyanzo vya mapato, lakini Serikali imekuwa bado ikiwapa mzigo mkubwa wa kuhudumia jamii Wakurugenzi wa Halmashauri hizo. Serikali imekuwa haitoi fedha za maendeleo kwa kisingizio cha Halmashauri kutumia mapato ya ndani wakati ikijua kwamba kwenyewe haipeleki fedha za matumizi ya kawaida yaani *OC*. Jambo hili linafanya halmashauri kushindwa kupanga mapato yake ya ndani kwa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imekuwa haipeleki fedha za miradi ya maendeleo hadi mradi huo uanze kutekelezwa kwa ngazi ya Halmashauri. Jambo hili limekuwa likiongeza umaskini kwenye Halmashauri nyingi hasa zile zisizokuwa na mapato ya kutosha kugharamia miradi hiyo, hivyo Halmashauri kuendelea kubaki nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo huu wa Serikali hauwezi kuleta mgawanyo ulio sawa kwa nchi nzima. Kuna Halmashauri itakayopata fedha nyingi na zingine zikawa hazipati fedha kabisa. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale haina jengo la hospitali ya Wilaya, jengo la Polisi Wilaya. Miradi hii yote ni miradi ya fedha nyingi na ni miradi muhimu. Kama Halmashauri tukishindwa kuanzisha miradi hii maana yake Serikali haiko tayari kugharamia miradi hii. jambo hili ni vyema Serikali mkaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo; pamoja na kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watu wetu ni wakulima, lakini sekta hii haijapata msukumo wa kweli. Wakulima wetu bado wanaishi maisha duni sana licha ya kutumia zana duni kwenye kilimo bado hata hayo mazao wanayopata hawana uhakika wa masoko.

Matamko mengi ya Serikali juu ya kilimo yanachangia kwa kiasi kikubwa kudumza kilimo. Mfano kuzuia watu kusafirisha mazao kufuata soko ni unyanyasaji mkubwa. Ni nani mwenye jukumu la kutunza chakula cha akiba kwa nchi, ni mkulima au Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa pembejeo za kilimo ni kikwazo kingine cha kumkwamua mkulima. Mfano, hadi leo pembejeo za korosho hazijulikani zitaingia lini nchini wakati mwezi Mei ndiyo mwezi wa kuanza kuweka dawa kwenye mikorosho na hata bei za pembejeo hizo hadi leo hazijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Maafisa Ugani pamoja na vyombo vya usafiri kwa hawa wachache waliopo kunachangia kwa kiasi kikubwa watu wetu kulima bila kuzingatia kilimo cha kisasa kwani wananchi wengi hawafikiwi na watalaam hao. Hivyo, ni vyema Serikali ikahakikisha inakuwa na Maafisa ugani wa kutosha na wawe na vitendea kazi. Vilevile sekta ya kilimo cha umwagiliaji ndiyo kimetupwa kabisa. Miradi mingi ya umwagiliaji nchi nzima imekuwa haikamiliki na fedha zake kuliwa kama hazina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuhudumu kwenye Wizara hii, Mungu ampe umri mrefu ili aweze kuendelea na jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utumishi na watumishi hapa nchini ni hali mbaya sana. Hali ya watumishi nchini kwenye kada mbalimbali ni mbaya. Kilio cha uhaba wa watumishi nchini ni kikubwa sana na hata hao wachache tulionao hali na mazingira yao ya kazi ni mbaya sana kwani walio wengi malipo yao hayalingani na kazi zao. Walio wengi wanafanya kazi kwa sababu tu hawana namna ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linapunguza ufanisi na ari ya kazi. Ikumbukwe kwamba baada ya punguzo kubwa la wafanyakazi hapajatokea mkakati maalum wa kuziba pengo hilo. Mishahara ya watumishi wengi, hasa wa kada za chini bado ni midogo sana na ni miaka miwili kama si mitatu haijafanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengi hasa wa sekta ya elimu na afya wanafanya kazi chini ya kiwango kwa kuwa kazi zao hazithaminiwi, hivyo walio wengi hufanya migomo baridi, jambo ambalo halina tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mipaka ya kazi sasa haiko wazi kwa wakuu wengi wa mahali pa kazi, wanafanya kazi kwa matamko zaidi kuliko weledi wa kazi. Jambo hili linachagizwa zaidi na kutokuwapa mafunzo au semina kwa watumishi wengi wa umma. Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri walio wengi hawajui mipaka ya kazi zao ndiyo maana kuna migongano mingi kazini. Ubabe ni mwingi kuliko weledi, watumishi wanajazwa hofu badala ya kutiwa moyo na ari ya kazi, kazi za kitaaluma zinafanywa kwa matamko badala ya kitaaluma, hivyo kuondoa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwenye sekta binafsi ndiko kumeoza kabisa. Wafanyakazi huko hawana taasisi yoyote inayowasimamia, tumeacha watu wa chini wapambane na matajiri wao. Katika mazingira haya ya uhaba wa ajira tunatarajia nini kitatokea kama si watu wetu kunyanyasika na matajiri tunaowaita wawekezaji? Hali ya ajira kwenye sekta hii ni mbaya sana, hakuna anayesimamia mikataba ya ajira zao wala hali bora ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora; dhana ya utawala bora ni pana sana na ili itekelezwe ipasavyo kuna haja watu waliopewa dhamana ya kusimamia dhana ya utawala bora waelewe maana ya utawala bora na utawala wa sheria kwani mahali ambapo sheria hazifuatwi hakuna utawala bora. Utawala wa sheria ni dhana nyingine inayowataka viongozi au watawala kufuata sheria kwa mujibu wa Katiba wakijua kuwa roho ya amani ni haki na haki ni kufuata sheria/Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya sasa dhana ya utawala bora imeanza kutokomea kwani watoaji haki wameanza kukiuka dhana ya utawala bora. Sasa hivi

tumeanza kujenga Taifa la watu waoga na si watii wa sheria kwani kuna tofauti kubwa kati ya kutii sheria na woga. Mtii wa sheria siku zote atabaki na utii wake, lakini mtu mwoga siku akibadilika akaacha woga basi hapo amani huwa mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, roho ya amani ni haki na wala haitakuwa woga, kulea watu waoga ni kulea bomu katika jamii. Ni vizuri Serikali ikaanza sasa kuwafanya watu watii sheria badala ya kuwajengea woga ambao ipo siku utakwisha. Vitendo vinavyoendelea nchini sasa havina mwelekeo mzuri, vitendo vya watu kutekwa, kupotea na hadi kuuawa ni hatari sana, hasa pale Serikali inapokaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matamko ya Viongozi. Uongozi wa Awamu ya Tano umekuja na namna mpya ya kuongoza. Kumekuwa na matamko mengi kutoka kwa viongozi na mara nyingi yamekuwa yakipingana kutoka ngazi moja hadi nyingine. Vile vile kuna viongozi ambao hawafanyi kazi wakisubiri maagizo kwani wakifanya bila maagizo wanaweza wakaondolewa kwenye nafasi zao hata pale anapofanya jambo lililo chini ya mamlaka yake. Watendaji wako ofisini wakisubiri maagizo tu. Uwajibikaji wa pamoja nao umeanza kutoweka, viongozi walio wengi wanaogopa dhana ya uwajibikaji wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki na amani; watu wa kwanza watakaowajibika kwa Mungu siku amani ya nchi yetu ikitoweka ni wale wanaosimamia utoaji haki ambao ni pamoja na polisi, mahakama, Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi na Usalama wa Taifa. Taasisi hizi ni muhimu sana wakatenda haki na jamii wakaona haki ikitendeka na haki hiyo lazima iende na wajibu. Hakuna amani bila haki na hakuna haki bila wajibu, naishauri Serikali kusimamia haki ili kulinda amani yetu.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu mpo salama. Natoa pole kwa Wabunge wote kutokana na matukio na ajali ya *power*

*bank.* Natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Jafo, Mheshimiwa Waziri Mkuchika na Makatibu Wakuu wote na Watendaji kwa kazi nzuri ya kusimamia Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ambapo uzito ndani ya tani moja hakuna tozo unaposafirisha kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine. Pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Rais waliweza kueleza nafuu hiyo, lakini mwongozo au sheria hiyo haikuzingatia mazao yanayodumu katika muda mfupi *(perishable goods)* ambayo mkulima hawezi kuhifadhi na inamlazimu kupeleka sokoni moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali katika hitimisho la bajeti itoe tamko juu ya tozo kwenye mboga mboga *(perishable goods)* kwa kuwa wakulima wengi wa Jimbo la Nsimbo wanasafirisha kwa kiwango chini ya tani moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona maeneo mengine wanategemea *perishable goods* kama *own source* kubwa. Basi, nashauri mtu mwenye mzigo chini ya kilo 50 asilipe ushuru ili kutoa nafuu kwa wakulima wadogo wadogo. Pia *produce cess* 3% *on value* inavyotozwa na Halmashauri, ipo tofauti na sheria kwani *Councils* wanatoza *fixed amount* mfano shilingi 1,000/= kwa tenga, lakini ukitathimini kwa bei ya soko inakuwa chini ya shilingi 1,000/=. Serikali pia iangalie eneo hilo ingawa kwa kudhibiti *fixed charge,* itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Serikali hususan Walimu wanadai pesa nyingi ingawa Serikali hivi karibuni ililipa kiasi. Kwa mfano Walimu wa Mkoa wa Katavi kwa madeni yasiyo ya mshahara wanadai kiasi cha shilingi bilioni 1.3. Naomba Serikali ifanye tena malipo ya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkoa wa Katavi kuna madai ya kupanda madaraja mfano mwaka 2016, Februari

Tume ya Utumishi ya Walimu ilitoa barua lakini kufikia Novemba, 2016 Walimu waliambiwa warejeshe barua hizo. Mpaka sasa hakuna waliopanda, lakini kwa wale wachache ambao hawakutii agizo hilo walipanda madaraja. Tunaomba Serikali iangalie Walimu hawa ili wapande madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wapo Walimu ambao wanatakiwa kupanda mishahara, lakini bado *Lawson* haiwatambui ingawa Halmashauri zimeshawasilisha madai yote Utumishi, naomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie maombi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*, wazo la kuanzisha *TARURA* ni jema, lakini mgao wa *road fund* kwa uwiano wa 3:7 na *TANROADS* bado hauna tija kwa kuanzishwa kwa *TARURA.* Kuna ongezeko la gharama za utawala ambazo zinapunguza fedha za maendeleo. Ukiangalia hiyo asilimia 30 itakuwa imepungua; fedha za maendeleo inaenda asilimia 20 na nyingine utawala. Hivyo mgao na uwe uwiano wa 4:6 *TARURA Vs TANROADS* ili fedha za maendeleo zibaki kama ilivyokuwa kabla ya kuanzisha *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ilifanya kikao na madeni, Afisa Mipango na Wenyeviti wa Halmashauri 2018, Februari mwishoni ikiwa ni mkakati wa kuhakikisha miradi inafanyika kwa ukamilifu na kutumia chini ya fedha za ruzuku. Tunaomba Serikali itoe fedha angalau asilimia 50 ili miradi iliyorekebishwa katika bajeti. Halmashauri zilifanya mawasilisho upya Machi, 2018. Kwa kutoa fedha kiasi itawezesha Halmashauri zianze kutekeleza miradi ya maendeleo iliyo chini ya *LGCDG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Halmashauri nyingi nchini zina Wakuu wa Idara ambao wamekaimu kwa muda mrefu. Aidha, kutokana na kutotimiza masharti au uzembe katika mchakato wa kuthibitisha. Naomba Serikali iangalie upya vigezo vya Utumishi kama Wakuu wa Idara mfano kupunguza miaka saba mpaka mitano, ikiendana

sambamba na kupandisha cheo. Hii itasaidia watumishi kufanya kazi kwa hali na mori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Jimbo haina uwezo mkubwa na kati ya Kata 12 tuna Vituo vya Afya vitatu tu. Hivyo kwa kuwa mwaka 2018/2019 hatuna mgao wa Hospitali ya Wilaya, basi tunaomba msaada wa fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Kapalala, chini ya Kijiji cha Songambele ambapo kituo hicho cha afya kitasaidia jumla ya Kata nne ambazo ni Kapalala, Nsimbo, Urwira na Mtapenda. Tunaomba sana Serikali itupatie msaada huo wakati tunasubiri bajeti ijayo kwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kutupatia gari la wagonjwa *(ambulance)* Maruti Suzuki, itasaidia kwa kiasi changamoto ya usafiri. Hivyo basi, tunaomba tena gari la wagonjwa aina ya *Land Cruiser Hardtop*, ambalo linaendana na mazingira ya msingi kwani miundombinu bado mibovu sana na pia matukio ya vifo vya mama na mtoto bado yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Nsimbo bado ina uhaba mkubwa wa Walimu na Watumishi wa Idara ya Fedha. Tunaomba TAMISEMI katika ajira za Walimu zinazokuja mwangalie Halmashauri ya Nsimbo. Pia Wahasibu hawatoshi mpaka inapelekea kutofanya kazi kwa ufanisi katika kusimamia mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TEHAMA, Serikali imefanya kazi nzuri katika TEHAMA upande wa kukusanya mapato, lakini changamoto iliyopo ni kwenye *POS,* hakuna udhibiti wa kutosha kwa kuwa mtozaji ndiyo anachagua aina ya tozo na idadi za bidhaa. Hivyo, upotevu wa mapato bado upo. Nashauri Serikali ihimize Halmashauri ziwe na takwimu ili kulinganisha na makusanyo halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutoa shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jafo kwa kuweza kutoa kwa Nsimbo fedha za Kituo cha Afya na

*ambulance,* pia fedha za *Equip, P4R, TEA*, Shule za Msingi na nyingine nyingi.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza Serikali kwa jinsi wanavyojitahidi kuhakikisha kila wilaya inapata huduma stahiki kama vile elimu na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu ni mtu ambaye inapaswa Serikali imuangalie kwa jicho la huruma sana. Mwalimu hana muda wa kufanya kazi nyingine ya kujitafutia riziki. Anafundisha darasani, wakati mwingine lina wanafunzi karibu 70 na anaporudi nyumbani hapumziki ana kazi ya kusahihisha madaftari mpaka anapomaliza keshachoka hawezi tena kufanya kazi nyingine. Hivyo basi, Mwalimu wa nchi yetu anabakia na umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni pamoja na kuheshimu kila mmoja anafanya kazi ambayo inamhusu. Nakusudia kuwa kama wewe sio kiongozi katika nafasi fulani basi huwezi kufanya kazi ile ambayo sifa yako kwa mujibu wa sheria na kanuni ya vyama vya siasa. Kuna Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992, Kifungu cha 8B(2) ni marufuku kujitambulisha kwa vyeo ambavyo sio vyako.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni pamoja na kuheshimina na kuhakikisha kila mmoja anafanya kazi ambayo inayomhusu. Nakusudia kuwa kama wewe sio kiongozi katika nafasi fulani, basi huwezi kufanya kazi ile ambayo siyo yako kwa mujibu wa sheria na kanuni ya vyama vya siasa. Kuna Sheria ya Vyama vya Siasa ni ya mwaka 1992 kifungu 8B(2) ni marufuku kujitambulisha kwa vyeo ambavyo siyo vyako.

Mheshimiwa Spika, tunaowaona baadhi ya watu wanasema vyama kwa nafasi ambazo siyo zao na Serikali haiwachukulii hatua stahiki. Hapa utawala bora ndiyo unakosekana. Tunaishauri Serikali, watu hawa wapo na wanajulikana wachukuliwe hatua za kisheria ili utawala bora upatikane.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema. Napenda kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu hospitali za wilaya 67; naomba kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ilivyosema juu ya ujenzi wa hospitali za wilaya nchini. Napenda kupongeza mpango huo na sisi Wilaya/Manispaa ya Mtwara mjini hatuna hospitali ya wilaya kabisa. Naomba Mtwara Mjini tupewe hospitali hivyo kwa kuwa tuna shida sana ya hospitali na hasa ukizingatia hata hospitali ya kanda hatuna Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubovu wa barabara Mtwara Mjini; kuna barabara ambazo hazipitiki kabisa wakati wa masika (kifuku). Barabara hizo ni Mbae –Mbawala chini, Mtawanya- Namayanga na Mikindani – Dimbuzi kupitia Lwelu. Naiomba sana Wizara barabara hizi za mjini Mtwara zijengwe kwa lami ili kuondoa usumbufu wa kukarabati kila mwaka kwa kuwa maji huharibu wakati wa mvua na wananchi wanakosa mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, stendi za kisasa Magomeni na Mikindani Mtwara; kumekuwa na ahadi za muda mrefu sana juu ya ujenzi wa stendi Mtwara Mjini eneo la Magomeni, Mkanaledi na Mikindani Mtonya. Naomba pesa ziletwe mwaka huu wa fedha kwa ajili ya ujenzi huo kwani wananchi wengi wamehamishwa kupisha ujenzi huo eneo la Magomeni lakini Mikindani Mtonya wananchi wanaishi kwa wasiwasi juu ya kupewa fidia majumba yao ili kupisha ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TARURA* Mtwara Mjini; watu wa TARURA ni viburi sana na hasa Mtwara Mjini. Wakati mwingine wanakaa na fedha kwa mfano Mtwara Mjini walikuwa na Milioni 20 za halmashauri lakini hawachongi barabara na miundombinu ya mjini inaharibika sana wakati wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; *TARURA* wanakataa kutoa taarifa kwa wananchi pamoja na mimi Mbunge kuwaandikia barua kuja kutoa ufafanuzi juu ya ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye mikutano ya hadhara lakini *TARURA* pekee walikataa kuwapa taarifa wananchi juu ya mpango kazi wao wakati wanafanya kazi na wapo kwa ajili ya wananchi wa Mtwara Mjini. Watendaji wa aina hii hawatufai Mtwara kwani wananchi lazima wapewe taarifa za maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ubadhirifu mkubwa wa fedha za halmashauri nchini. Kwa mfano Mtwara Mjini Mwekahazina na *syndicate* yake walitafuna milioni 800 na ushee. Cha ajabu Mwekahazina kahamishwa lakini hajachukuliwa hatua za kupelekwa kwenye Mahakama ya Mafisadi, pia wenzake waliohusika bado wapo Mtwara Manispaa na wanafanya hujuma juu ya Mkurugenzi kwa kusimamia vema halmashauri ya Mtwara Manispaa. Naomba wahusika wote wachukuliwe hatua stahiki na kuhamishwa mara moja Halmashauri ya Mtwara Mikindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa; upatikanaji wa dawa bado siyo mzuri sana Mtwara Mjini, wananchi wengi wanaambiwa hamna dawa kwenye zahanati zetu na hospitali ya Mkoa wa Mtwara. Naomba dawa ziongezwe na Mbunge nipewe taarifa juu ya kiwango cha dawa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara ya TAMISEMI kuhusu elimu. Katika halmashauri ya Lushoto na Bumbuli kuna takribani shule za msingi 168 ambazo ni kiasi kikubwa sana. Tunao uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa vipatavyo 228 kwa Halmashauri ya Lushoto, lakini pia kuna uhaba mkubwa wa Walimu wapatao 836. Hivyo kukosa ikama bora kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto na Tanga kwa jumla kuna shule nyingi sana kulinganisha na mikoa mingine. Wakati Mkoa mzima wa Tanga una shule za msingi 1,032 mikoa kama Simiyu zipo 571, Katavi 177 ambao ni zaidi ya

Wilaya ya Lushoto kwa shule tisa tu, Songwe 406, Njombe 499, Lindi 502 utaona uwiano huu hauwezi kuleta tija na ulinganishi kwa sababu mamlaka za usimamizi zinapata mzigo mkubwa kusimamia, itapendeza kama Mkoa wa Tanga utapewa uangalizi maalum ili kusimamia elimu kutokana na ukubwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala; lengo la ugatuzi wa Serikali za Mitaa ni kuboresha utawala bora na kupeleka madaraka karibu na watu. Mkoa wa Tanga ni mkoa pekee wenye halmashauri nyingi ambazo ni 11. Hivyo kuhitaji muda, rasilimali fedha na watu ili kusukuma maendeleo. Halmashauri 11 wilaya nane (8) na majimbo 12 ni mzigo mkubwa hivyo kuhitaji kutazamwa kwa jicho la kipekee ili kuboresha maeneo ya utawala na kuleta utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa kama ya Geita ina halmashauri sita (6), Katavi tano ()5, Iringa tano (5), Lindi sita (6), Rukwa sita (6) utaona kwamba Mkoa wa Tanga sasa unahitaji angalau kugawanywa na kupata mkoa wa zaidi. Wilaya ya Muheza, Kilindi na Korogwe ni kubwa mno kuweza kuzalisha wilaya ya ziada. Hali kadhalika Wilaya ya Lushoto inaweza kupatiwa halmashauri tatu yaani Mlalo, Lushoto na Bumbuli kwa sababu takribani robo ya wakazi wa Mkoa wa Tanga wanaishi Lushoto, idadi kubwa ya watu huhitaji usimamizi wa huduma za kijamii ni suala linalohitaji jicho la karibu kutafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *performance based audit,* napendekeza ufanyike ukaguzi mahsusi juu ya utendaji wa Maafisa Ugani *(Extension Officers)* katika halmashauri zetu nchini. Watumishi hawa wanaonekana wenye kuzurura hawajulikani wanafanya kazi gani, hivyo kuwa mzigo kwa Taifa kuwalipa mishahara wakati hakuna tija yoyote inayopatikana kutokana na uwepo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*; Mamlaka hii mpya iishie pale ambapo halmashauri zimeishia, hata hivyo shughuli zao ziendane na mpango wa Taifa wa mwaka mmoja na miaka mitano ili kuleta uwiano wa usawa kuweza

kwenda pamoja na sekta nyingine (mfano lengo la usambazaji umeme kijijini *(REA)* ni ifikapo 2020/2021 ifike mwisho. Je, kwa vijiji visivyokuwa na barabara *TARURA* wanahusianishaje zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika halmashauri ya Lushoto hakuna hata gulio moja ambalo lina miundombinu ya vyoo wala vizimba vya kuhifadhia bidhaa, hivyo kuleta kero kwa wananchi na kusababisha magonjwa ya milipuko kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2018/2019. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo mengi muhimu ndani ya kipindi kifupi cha miaka miwili na nusu cha uhai wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo wananchi wa Wilaya ya Mbogwe ni uhaba wa miundombinu ya majengo ya halmashauri pamoja na makazi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Tunaiomba Serikali itusaidie kuhakikisha hospitali yetu ya Wilaya ya Mbogwe inaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanambogwe tunaiomba Serikali itusaidie kutupatia huduma ya maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria maji ambayo tayari yako katika Wilaya jirani ya Kahama ambayo ni wilaya mama ya Wilaya za Bukombe na Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya mpya ya Mbogwe tunaipongeza Serikali kwa kutupatia jumla ya Sh.800,000,000 kwa ajili ya Vituo vya Afya vya Iboya na Masumbwe. Kila kituo kimepewa Sh.400,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, wilaya yetu ya Mbogwe tayari inaendelea na ujenzi wa shule ya sekondari ya kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mbogwe, hata hivyo shule hii imeshindwa kufunguliwa

kutokana na uhaba wa upatikanaji wa maji. Tunayo matumaini makubwa kuwa Serikali itasaidia juhudi za uongozi wa wilaya katika kuhakikisha kuwa shule hii ya pekee ya kidato cha tano Wilayani Mbogwe inafunguliwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuongeza juhudi za kutupatia watumishi katika sekta za afya na elimu kwani tunao upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta hizi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ambao ni Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini unafanya kazi zake vizuri, kinachotakiwa ni kuongeza ushirikiano baina ya idara hii na uongozi mzima wa wilaya ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na Baraza la Madiwani ili kujenga umoja na mshikamano katika kutatua kero na matatizo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakala wa Maji Vijijini na Mijini ni wazo jema hasa ikizingatiwa kuwa wakala mbalimbali za Serikali zimeonesha mafanikio makubwa na kuwa na ufanisi wa kuwahudumia wananchi katika sekta hii muhimu ya maji hasa ikizingatiwa msemo usemao maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira ni jambo mtambuka kwani mabadiliko ya tabia ya nchi yamekuwa na athari mbaya kwa maisha ya mwanadamu na kusababisha ukame, uharibifu wa vyanzo vya maji, ukosefu wa mvua. Ni wajibu kwetu kama Taifa kuhakikisha tunatunza mazingira yetu kwa kuanza jitihada za kupanda miti na kuihifadhi na kujiepusha na tabia ya ukataji miti ovyo. Aidha, naishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi kuongeza matumizi ya nishati mbadala ya kuni na mkaa kwa kuwekeza zaidi katika matumizi ya umeme, umeme jua na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uti wa mgongo wa Taifa letu limekuwa likitilia mkazo yaani kilimo, naishauri Serikali kuweka mkazo zaidi katika uwekezaji wa viwanda

vya mbolea nchini hasa ikizingatiwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na hazina kubwa ya gesi asilia ambacho ni chanzo muhimu cha malighafi ya utengenezaji wa mbolea. Mbolea ikipatikana kwa bei nzuri itasaidia kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo ambacho ni chanzo muhimu cha malighafi katika sekta ya viwanda ambayo imekuwa ni kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia kidogo kwenye Wizara hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipouliza swali mara kadhaa hapa Bungeni kuhusu ni lini Serikali itajenga daraja muhimu la Mto Ruhembe lililopo kwenye Kata ya Ruhembe Jimboni Mikumi, aliyekuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI ambaye sasa ni Waziri aliahidi kututengea Sh.700,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo kwa kuwa wanatambua umuhimu wake na vifo vingi vinavyosababishwa na maji mengi ya mto huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha mpaka leo bado hakuna kinachoendelea maana mpaka sasa hata yale machuma ya daraja yaliyoletwa kutoka Chekeleni yamewekwa chini na hakuna kinachoendelea na madhumuni yake yalikuwa yaletwe ili lijengwe daraja la muda wakati tunasubiri kuletewa fedha za ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu aweze kutujibu ni lini pesa hizo Sh.700,000,000/= zitaletwa na je, vyuma vya daraja la muda ni lini vitaweza kuunganishwa na kusaidia wananchi kwa muda muafaka maana vinapokaa pale kwa muda mrefu vinasababisha hali ya wananchi kuwa mbaya na pia watu wenye nia mbaya wanaweza kuviiba na kuitia hasara kubwa sana Serikali na wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa

ujumla. Tunaomba sana tupate majibu ni lini Serikali italijenga daraja hili muhimu la Ruhembe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kumalizia ujenzi wa barabara ya lami kuanzia Dumila – Kilosa mpaka Mikumi ambayo imekuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa Awamu ya Tano kuwa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Mji Mdogo wa Mikumi unakua kwa kasi sana na ni mji wa kitalii, je ni lini Serikali itajenga kituo cha afya kwenye Mji Mdogo wa Mikumi? Maana Zahanati ya Mikumi ni chakavu sana na imezidiwa kabisa uwezo na idadi kubwa sana ya watu wengi pale Mikumi na vitongoji vyake, hivyo tunahitaji sana kuwe na kituo cha afya ili kiweze kuhudumia wananchi na watalii na wanaotumia barabara ya Tanzania - Zambia ambapo kuna ajali nyingi sana maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kunipa nafasi ya kusimama na kutoa mchango wangu katika hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na timu yote ya Serikali kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya CCM. Jambo ambalo limesababisha kila unapofanyika uchaguzi mdogo, CCM inapata ushindi wa kishindo, dalili hizi ni nzuri na kama kura zingepigwa leo ushindi wa Rais, Wabunge na Madiwani ungekuwa wa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu naomba kujielekeza katika hoja nitakazozitilia mkazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI: Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti na ukusanyaji wa Mapato na Maduhuli. Upelekaji fedha katika Halmashauri; pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali Kuu kupeleka fedha katika halmashauri zetu kiasi cha trilioni 3.33, sawa na asilimia 50.63 fedha hizi hazikufikia lengo lililokusudiwa. Naiomba Serikali katika mwaka huu wa fedha tuiangalie sekta ya TAMISEMI katika macho mawili hasa katika kupeleka fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani ya halmashauri pamoja na kwamba halmashauri zimekusanya zaidi, ukilinganisha na mwaka jana tofauti Sh.90/= ziliongezeka na makusanyo yote ni asilimia 50 kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, ukurasa wa tisa (9). Bado kazi ya ukusanyaji wa mapato si ya kiwango cha kuridhisha katika baadhi ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri katika kukusanya mapato; naishauri Serikali kuzielekeza halmashauri zetu kuendelea na kubuni miradi ya uwekezaji na kubuni vyanzo vya mapato ambavyo havitaleta kero kwa wanawake na wananchi. Hapa pia ningependa Waziri atuambie je, Serikali imejipangaje kuzisaidia halmashauri zetu kufanya uwekezaji mkubwa utakaoleta tija na kuongeza vyanzo vya mapato na kuziondoa halmashauri katika tatizo la kuwa tegemezi kwa Serikali kuu hata kwa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa; kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017 na Taarifa ya Waziri ukurasa wa 15 inaonesha kati ya Halmashauri 185 zilizokaguliwa, halmashauri 166 sawa na asilimia 90 zimepata hati safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake yote, Wakurugenzi wa Halmashauri zetu na Madiwani kwa kukubali maagizo ya Rais wetu ya usimamizi wa fedha za Serikali. Lengo likiwa kila kinachopatikana kiingie katika Mfuko wa Serikali na

kinatumika kwa kuzingatia taratibu za fedha za Serikali yetu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuendelee kuiwezesha Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani katika kila Halmashauri ili waweze kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kuhakikisha wanapewa ulinzi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao ili wasipoteze ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia nipende kujua Serikali imejipangaje kuimarisha vitengo vya ndani vya ukaguzi ili watekeleze jukumu la kufanya ukaguzi wa ndani kwa uhuru na haki bila ya kuingiliwa na mamlaka zao za ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi; Mfuko wa asilimia 10 ya Wanawake na Vijana; pamoja na kuzipongeza halmashauri zilitengewa bilioni 15.6 na kutoa mikopo kwa vikundi 8,672 vya wanawake, vijana na walemavu kati ya 18,233.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema wazi kuwa bado lipo tatizo kubwa la baadhi yetu kutotenga, kutoa hata kufuatilia urejeshaji wa mikopo, ushahidi unathibitishwa na Taarifa ya Waziri kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Wanawake ulitengewa Shilingi bilioni 61.6 kiasi kilichotolewa ni Shilingi bilioni 15.6 na ilipangwa vikundi 18,233, vikundi vilivyopata ni 8,672.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa kuwa Mfuko huu wa Wanawake na Vijana katika Halmashauri ndio mfuko pekee ambao ndio mkombozi kwa mwanamke mnyonge asiye na uwezo wa kufikia taasisi nyingine za fedha kutokana na masharti yake, naomba hapa Waziri atupatie majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi huu Muswada wa Sheria wa kuweka utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa kutaja na kutoa asilimia kumi ya wanawake na vijana utaletwa lini hapa Bungeni kwa sababu ni maoni ya Kamati mbalimbali hapa Bungeni. Je, Serikali Kuu ina mpango gani wa kupeleka

fedha katika halmashauri kuunga mkono Mfuko huu kwa sababu fedha hazitengwi kikamilifu na hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa huduma za afya; kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri ukurasa wa 24 – 29 umeonesha kwa ufasaha kuwa hospitali za wilaya zilizopo 120 zinazohitajika 184 sawa na asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya afya vilivyopo ni vituo 696 sawa na asilimia 15.7 lengo likiwa ni kuwa na vituo vya afya 4,420 na Serikali iendelee na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 208.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Zahanati; kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, Zahanati zilizopo nchini 6,440 sawa na asilimia 53, lengo ni kuwa na zahanati 12,543.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kuendelea kujenga, kukarabati hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati. Tatizo la kusogeza huduma ya afya kwa wananchi bado ni changamoto kubwa sana, wanawake bado wanafariki kwa uzazi na watoto chini ya miaka mitano (5) wanafariki dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri; kabla ya kuja hapa Bungeni nilikutana na baadhi ya wanawake na wananchi na hasa wanawake ninaowawakilisha walinituma nije nilete kilio chao cha kuomba kusogezewa huduma za hospitali kama ambavyo Serikali imejenga shule kila kijiji na sekondari kila kata na ili niweze kuwasilisha maombi yao Bungeni nikianza na TAMISEMI kutaka kujua mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya TAMISEMI chini ya Mtendaji wake mahiri Mzee Iyombe na Chaula walinieleza mipango yao ambayo ni mizuri sana, wanachohitaji Ofisi ya TAMISEMI ni kupatiwa fedha. Ofisi ya TAMISEMI wameishaandaa bajeti ya ujenzi wa zahanati 2,277, vituo vya afya 156 na ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa na wananchi 1845 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa vituo vya afya 156 na ununuzi wa vifaa tiba 156 x 850,000,000 = 132,600,000,000/=. Ukarabati wa zahanati angalau nusu ya mahitaji 2,277 x 100,000,000 = 227,700,000,000/=. Ukamilishwaji wa maboma 1,845 = 934,000,000,000/= hivyo Jumla kuu 1,294,300,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; naiomba Serikali ya CCM itafute fedha hizo Sh.1,294,300,000,000 na kuzikabidhi TAMISEMI kwa ajili ya ujenzi wa miradi hii na kuboresha huduma za afya, kupunguza vifo vya watoto na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Elimu. Usimamizi wa elimu ya msingi na sekondari nchini; naishukuru Serikali kwa mpango wa kuendelea kuboresha elimu hapa nchini pamoja na pongezi nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mpango mzuri wa kuwaandaa Walimu wa shule ya awali kwa baadhi ya shule wanaofundisha shule za awali hawana taaluma ya elimu ya awali. Serikali iandae vitabu vya kufundisha na kujifunza kwa wanafunzi wa shule ya awali. Shule za sekondari na msingi zina upungufu wa Walimu na hasa Walimu wa sayansi. Serikali kwa kushirikiana na wananchi wajenge madarasa yatakayopunguza msongamano wa watoto wetu katika shule zetu. Serikali kwa kushirikiana na wananchi itafute fedha kwa ajili ya matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe Kitengo cha Ukaguzi ili kitekeleze wajibu wake kikamilifu. Serikali iendelee kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za Walimu. Ningependa kujua pia mpango wa Serikali wa kukabiliana na changamoto nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utumishi; pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kuajiri watumishi katika kada mbalimbali upo upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali za umma mfano; Walimu wa shule za awali, Walimu wa shule za msingi na sekondari hasa Walimu wa Sayansi na Hesabu. Maafisa Ugani, Maafisa Maendeleo ya

Jamii, Sekta ya Afya, Madaktari, wataalam mbalimbali, Sekta ya Afya TAMISEMI, upungufu ni wafanyakazi 62,976 sawa na asilimia 55. Hapa ningependa kujua hawa wafanyakazi watakaoajiriwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 ni wa kada gani na ni wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*; napenda kuchukua nafasi hii kuupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF* kwa kazi nzuri ya kutoa huduma za jamii na kuzitambua kaya maskini 1,363,448 tangu kuanza kwa mpango huu na kaya 1,118,751 zenye watu watano na shilingi bilioni 185 zilizotolewa kwa kaya maskini Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nashauri, Serikali ifuatilie kwa karibu viongozi wanasiasa katika vitongoji, vijiji na kata kwani yapo malalamiko ya baadhi ya wananchi kuwa baadhi ya viongozi wanasiasa wanatambua watu wahitaji kwa upendeleo bila kuzingatia vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya usalama na TAKUKURU: Usalama; nawapongeza kwa kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama na amani endelevu na kazi ya kuhakikisha usalama wa viongozi, wananchi na Taifa letu la Tanzania linaendelea kuwa salama na amani na kuwa mfano wa kuigwa katika mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, nashauri vyombo vyote vya ulinzi na usalama viendelee kuimarisha ulinzi na usalama na katika nchi yetu na Tanzania iendelee kuwa kisiwa cha amani na utulivu, kwani amani itakapotoweka watakaoumia ni wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU; nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya ya kudhibiti vitendo vya rushwa na kuwezesha kuokoa fedha nyingi ambazo zilipotea. Ushauri wangu waendelee na kazi ya kupambana na rushwa kwa nguvu na bidii zaidi kwa manufaa ya Taifa letu. Sisi wanawake wa Tanzania tunawaunga mkono katika jitihada hizo za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na miradi ya maji ambayo imeshindwa kukamilika katika Mkoa wangu wa Mwanza, nitazungumzia mradi ulioko katika Halmashauri ya Buchosa Jimbo la Buchosa Wilaya ya Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Lumeya-Kalebezo Nyehunge wenye thamani ya shilingi bilioni 1.69; mradi huu ulianza Desemba, 2012 na ulitarajiwa kumalizika ndani ya miezi sita hadi leo ni miaka sita, mradi huo haujakamilika na mkandarasi alishalipwa bilioni 1.3 ambayo ni asilimia 90 ya fedha ya mradi mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ungekamilika kwa wakati ungesaidia kuondokana na matatizo ya maji kwa wakazi zaidi ya 16,000 katika halmashauri hiyo. Pamoja na mradi huo kutokamilika kwa wakati Serikali imekuwa ikitoa matamko ambayo mpaka sasa hayajasaidia mradi huo kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, terehe 30 Aprili, 2016, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema alisema Serikali imeunda Tume ya kuchunguza uzembe na madudu yaliyosababisha mradi huo kutokamilika huku mkandarasi akiwa ameshalipwa pesa karibu zote na maji hayatoki. Mwezi Juni, 2016, Mkuu huyo wa Wilaya akasema kuwa ripoti ya timu aliyoiunda imebaini u badhirifu mkubwa kwenye mradi huo na kuziomba mamlaka za juu kumchukulia hatua aliyekuwa handisi na Mkurugenzi wa Wilaya ya Sengerema kwa kumlipa mkandarasi pesa nyingi wakati kazi hajamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, terehe 5 Aprili, 2017 aliyekuwa Naibu Waziri wa TAMISEMI akijua kabisa muda wa kukamilika mradi huo umepita na pesa nyingi zimelipwa, akasema kuwa utakamilika na maji yatatoka ifikapo Juni, 2017, lakini mpaka sasa maji hakuna na watu wanahangaika.

Tarehe 15 Februari, 2018 Waziri wa Maji alitoa agizo akiwa hapa Dodoma akiwaagiza TAKUKURU kuchunguza mradi huo wa maji baada ya kuona Waziri Mkuu ambaye ni bosi wake akiwa Mwanza. Tarehe 15 Februari, 2018 Waziri Mkuu naye akaagiza TAKUKURU na Serikali ya Mkoa wa Mwanza walichunguze suala hilo na kuchukua hatua lakini mpaka leo hakuna majibu yaliyotolewa na maji hayatoki na wananchi wanazidi kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wahusika wanapokuja kuhitimisha wawaeleze wananchi wa Buchosa ni lini mradi huo utakamilika na ni hatua gani zitachukuliwa kwa watu waliochelewesha mradi huo mpaka sasa wananchi wanateseka huku watu wengine wakitafuna kodi zao. Ni aibu kubwa kwa Halmashauri ya Buchosa iliyoko Nyehunge kilometa chache kutoka ziwani kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie miundombinu ya barabara ya Halmashauri ya Buchosa, wananchi wa maeneo haya walitaja mojawapo ya neema ambayo wangeipata kwa kuwa na halmashauri ni kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara. Barabara ya kutoka Nyamadoke ulipo mpaka wa Mwanza na Geita kuelekea Nyehunge Kalebezo, Bukokwa, Nyamazugo hadi Sengerema ni mbovu kwelikweli miaka yote na hata inapofanyiwa matengenezo au marekebisho yamekuwa yakifanyika kwa kiwango cha chini na kuifanya kutodumu kwa muda mrefu na kuwekewa molamu ngumu inayoweza kudumu hata zaidi ya mwaka haina mitaro ya kupitisha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ikileta usumbufu kwa wafanyabiashara wa magari( vyombo vya usafiri) kwa magari kuharibika sana na hivyo kuongeza adha na shida ya usafiri hasa wagonjwa wanaokwenda kutafuta matibabu hospitali za Sengerema wakiwemo akinamama wajawazito. Pia wafanyabiashara na wakulima wa mananasi wanaotokea Nyamadoke, wavuvi wa kutoka Kahunda, Kafunzo, Kanyara, wasafishaji wa mazao ya misitu kutoka Bihindi, Bupandwa wanapata shida sana kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahusika wanapokuja kuhitimisha wawaeleze wananchi wa Buchosa na Sengerema ni lini barabara hiyo itawekewa lami na kuwa barabara bora, pia wanataka kusikia ni lini barabara hiyo itaboreshwa kuanzia njia panda ya Nyamazugo- Sengerema ili wapite Katunguru wanapoelekea hadi Kamanga. Aidha, wananchi waelezwe ni kitu gani hasa kinasababisha barabara ya kuanzia Sengerema kuelekea Manga pamoja na umuhimu wake haijawahi kuwa katika hali inayostahili kwa shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nata kujua je, ni kwa sababu gani Serikali inagombania mapato ya vivuko na wale wawekezaji kule Kamanga kwa sababu Serikali nayo inamiliki vivuko Busisi, hivyo haitaki wananchi wavuke Kamanga hali inayowaathiri wananchi wa maeneo ya kuanzia Sengerema kuja Kasunganile, Lubondo hadi Kamanga kwa sababu hawawezi kwa vyovyote kwenda kurukia Busisi. Wanataka kusikia Serikali ina mipango thabiti kwa barabara hii badala ya kufanya ukarabati wa kuweka mchanga wa mfinyanzi, lini itaweka lami au molamu iliyo imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali sasa ituambie lini itaipandisha hadhi barabara hizi za Buchosa hadi Sengerema kutokana na matumizi muhimu na unyeti wake wa shughuli za kiuchumi na kijamiii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Kigoma Ujiji ina changamoto kubwa ya mapato ya ndani. Mfano, mwaka 2016/2017 makadirio yalikuwa shilingi bilioni 3.3, lakini makusanyo yao yalikuwa bilioni 1.4 tu sawa na asilimia 42. Mwaka 2017/2018 makadirio ni billion 2.3 na mpaka sasa tumekusanya asilimia 33 tu na miezi imebaki miwili tu kabla ya mwaka wa fedha kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ushuru wa masoko haukusanywi kwa sababu Katibu Mwenezi wa CCM amekataza wafanyabiashara kulipa tozo ya 50,000 kwa

mwezi na Serikali ipo kimya. Serikali itoe kauli hapa Bungeni ili watendaji waende kukusanya ushuru. Shughuli zimesimama. Serikali ielekeze watendaji kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana asilimia 10. Kwa miaka 24 sasa *MSM* zimekuwa zinatenga asilimia 10 kutoka mapato ya ndani lakini changamoto bado ni nyingi na zile zile, nadhani tubadili mfumo. Napendekeza kuwa fedha hizi zitekelezwe kupitia mfumo wa Hifadhi ya Jamii ambapo vikundi vya vijana na wanawake wanufaishwe na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kupitia fedha hizi *MSM* zichangie asilimia 50 ya michango ya mwezi na vijana na wanawake wachangie asilimia 50 iliyobaki. Hii ingejenga tabia ya kuweka akiba na pia kuwezesha vijana na wanawake hawa kuwa na bima ya afya kupitia mifuko hii. Hii pia ingewezesha kuwepo na fedha za uwekezaji wa miradi ya kimkakati kati ya *MSM* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2016/ 2017, *MSM* zilikusanya shilingi bilioni 544 ambapo asilimia 10 ya hizi ni bilioni 54 ambazo zingewekwa akiba kwenye mifuko. Kwa kuwa vijana na wanawake wangechangia asilimia 50 ya michango yao, jumla ya fedha za michango zingefika bilioni 108. Hizi zingekuwa zinaongezeka kila mwaka (2017/ 2018 shilingi bilioni 687, mwaka 2018/2019 bilioni 735) na hivyo kujenga mfuko mkubwa ambao fedha zinatunzwa vizuri kuliko sasa ambapo fedha nyingi hupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tufanye hili ili kulinda fedha hizi kwani zingekuwa na uhakika kwani mifuko ingefuatiliwa, ingejenga utamaduni wa kuweka akiba kwa watu wetu na ingewezesha watu wetu kupata bima ya afya na kupata mikopo yao kupitia mifuko hii. Wataalam walitazame hili jambo la kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa fedha MSM; kuna changamoto kubwa kuhusu uwezo wa watendaji wetu kufanya kazi na Madiwani, hawasikilizi, hawajali na dharau. Manispaa ya Kigoma Ujiji ni ushahidi tosha wa uzembe wa

watendaji kupelekea kupata hati chafu. Rejea barua ya Meya wa Manispaa kwa TAMISEMI tarehe 30 Juni, 2017 kumb na. A20/448/*Vol*.11/7) na majibu kutoka TAMISEMI (15 Septemba, 2017) kumb. *RALG(PCF*.5211).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua hizi pamoja na barua nyingine zote zilionesha malalamiko dhidi ya watendaji. Manispaa iliomba Taasisi ya Wajibu ya Bw. L. Utouh kutusaidia kupata ufumbuzi. Watendaji hawakutekeleza kabisa ushauri. Ukisoma ukurasa wa 270-272 wa Taarifa ya *CAG* utaona sababu za hati chafu zote zinahusu ufuatiliaji wa watendaji. TAMISEMI haikumsikiliza Meya wa Manispaa. Nashauri uchunguzi unaofanywa sasa uwe mpana, utazame uwezo wa watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani kwa mujibu wa *CAG MSM* zilishindwa kukusanya 17% ya makadirio (shilingi 104 bilioni) mwaka 2016/2017 wastani wa miaka ya nyuma ni 10% tu. Pia *property tax* kuchukuliwa na *TRA* ni changamoto. Hii maana yake ni kuwa fedha za vijana zitakuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe maelezo kuonya wanasiasa kuingilia sheria. Katibu Mwenezi wa CCM Bwana Polepole alikuja Kigoma kuagiza ushuru usikusanywe na kuvunja sheria. Kwa nini TAMISEMI haikemei mambo haya? *CAG* ametaka tuongeze mapato lakini wanasiasa wanazuia?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu bado nilisahau kuhusu msongamano wa wanafunzi na kwa makusudi kabisa wananchi wa Tarime pamoja na wadau mbalimbali tumeamua kujenga shule nyingi za msingi, mbili za sekondari, lakini cha kusikitisha Shule ya Msingi Rebu ilikuwa ikitumiwa na Shule ya Msingi Buguti pamoja na Shule ya Msingi Mturu, ambapo tumejenga shule Bufuti na imekamilika, tumejenga shule ya Mturu kwa ushirikiano wa Mitaa ya Uwanja wa Ndege na Mkuyuni ambapo tulijenga vyumba sita na ofisi hadi usawa wa renta, lakini Mkurugenzi amesimamisha ujenzi kwa sababu zisizo na

msingi. Wakati Waziri Mkuu amekuja alisema *DC* ashughulikie hiyo shule, tunaomba sana tupate suluhisho ili wanafunzi wetu wasisome zaidi ya 120-200 kwa darasa au wengine kukaa chini ya mti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa ukaimishaji wa idara zote zilizopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tarime ili kuweza kuweka ufanisi wa kazi na kuleta maendeleo ndani ya halmashauri ya mji. Tupate rasilimali watu wenye uweledi na wanaomudu kazi zao. Tusibebane kwa maslahi ya watu wachache bali tuangalie Taifa. Halmashauri ndio wasimamizi wa miradi mbalimbali kutoka wizara zingine. Hivyo watendaji wazembe ni msiba kwa halmashauri na maendeleo hayatakuwepo. Mfano ni Idara ya Maji, miradi yote ya maji tulikosa kwa uzembe, Idara ya Mipango ndio ime-*paralyze* kabisa, idara zingine zimekwisha, si sawa. Tunaomba waajiriwe kama wanafaa au watafutwe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni fedha za jengo la utawala hatujapewa hata senti tano. Tunaomba *review* ifanyike ili na sisi tuweze kujenga jengo letu la kukamilika kuliko pale tulipo ili hata mandhari ya mji wetu yawe mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni mnada wa Magena, tunaomba sana Wizara hii ifanye *follow up* na Wizara ya Mifugo ili ule mnada ufunguliwe na kuwe chanzo cha mapato kuliko kupotea kwa kupeleka mnada wa mpakani kwa nchi ya Kenya (Mabara). Kwa nini sisi Magena isifunguliwe kwa makubaliano ya kikao cha 2016 kilichojumuisha Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Kamati ya Ulinzi na Usalama; wananchi na kuridhia kuwa minada yote ifanye kazi maana Magena ni wa mpakani na ule wa Kinimi *Check point* ni wa upili. Hii yote italeta tija ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kuniwezesha kuchangia hotuba

iliyoko mezani. Nianze kwa kuzungumzia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu ambao unatengwa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kuwapongeza sana Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanazozifanya, nimpongeze Mheshimiwa Jafo na wasaidizi wake kwa kazi nzuri na zinazoonekana. Ninachotaka kushauri ni kwamba Mfuko huu utengewe akaunti yake maalum katika halmashauri zetu ili kufanya usimamizi mzuri wa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Serikali ni kila halmashauri kutenga fedha asilimia 10 kutokana na mapato ya ndani. Jambo hili ni jema sana iwapo litaratibiwa vizuri kwa kuwa litasaidia ajira kwa makundi haya hasa kwenye ujasiriamali. Naomba kuishauri Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Kusimamia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu. Mfuko wa Walemavu 2% utungiwe sheria inayozielekeza halmashauri kutenga kiasi hiki kwa ajili ya walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijijini *(TARURA).* Lengo ni kuhudumia barabara zote zilizokuwa zinahudumiwa na halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji. Kumekuwa na changamoto mbalimbali katika *TARURA* kukubaliana na majanga kama mafuriko ambayo hupelekea uharibifu wa madaraja, makalavati na mashimo makubwa kwenye barabara vijijini, mijini na mitaa mingi nchini. *TARURA* inatekeleza majukumu yake kupitia fedha za Mfuko wa Barabara za mwaka wa fedha 2017/2018. Wakala waliidhinishiwa shilingi bilioni 230.8 kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 34,024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2018 *TARURA* imepokea bilioni 98.5 ambazo zimetumika kutengeneza barabara yenye urefu wa kilomita 4,183.3 tu. Naomba Waziri atakapohitimisha atuambie ni kwa nini fedha hizi hazitolewi kwa wakati ili kukamilisha barabara hizi kwa mwaka wa fedha unaoishia 2018. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri Mkuu ni kwamba barabara zilizopo chini ya *TARURA*

ni kilomita 108,946.2. Mwaka huu wa fedha *TARURA* imesimamia matengenezo ya barabara ya kilomita 4,183.3 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miradi ya maendeleo kutofika kwa wakati katika halmashauri zetu. Katika kujiletea maendeleo rasilimali fedha toka Serikali Kuu ni muhimu sana, lakini kuna tatizo la Serikali kushindwa kupeleka fedha kwa ukamilifu na kwa wakati kiasi kwamba utekelezaji wa miradi unashindikana na utaratibu wa manunuzi kutofanyika kwa wakati na kutofuata Sheria ya Manunuzi ambayo inahitaji kutimizwa kwa masharti hivyo kupelekea fedha kurudi Serikalini.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa TAMISEMI pamoja na Manaibu Mawaziri wake. Wananchi wengi wamejenga maboma mengi ya zahanati, shule, nyumba za Walimu pamoja na vituo vya afya na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, maboma haya yamekaa muda mrefu bila kuendelezwa na kama Serikali inavyosema kuwa wananchi wanapojenga maboma na wakafikia kwenye mtambaa wa panya (lenta) Serikali inaendeleza, lakini mpaka leo kuna maboma mengine yanakuwa magofu. Kwa hiyo niiombe Serikali ipeleke fedha za kutosha ili kumalizia maboma haya ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna vituo vya afya viwili vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi, vituo hivyo ni Kituo cha Gare na Gwelo. Kituo cha Gare tayari kimeshajengwa maboma manne ambayo yako kwenye hatua tofauti. Jengo la kwanza ni *OPD* hili limeshapigwa bati, *ward* mbili nazo zimeshapigwa bati na *ward* nyingine mbili zipo kwenye kujengwa msingi. Kituo cha Afya Nawelo hiki kina jengo moja la *OPD* ambalo lipo kwenye mtambaa wa panya (lenta). Kwa hiyo niiombe Serikali itupatie fedha kama vinavyopatiwa vituo vya afya vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lushoto lina kituo cha afya kimoja tu ambacho kipo Mlola na niishukuru Serikali yangu tukufu kwa kutupatia shilingi milioni 700 kwa ajili ya kupanua kituo pamoja na kupata vifaa tiba. Hata hivyo, kituo cha afya kile kina changamoto ya gari la wagonjwa na ukizingatia kituo cha afya kile kina zaidi ya kilomita 53 kufika katika hospitali ya wilaya. Kwa hiyo gari hii itakuwa ni muhimu ili kuokoa vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida kabisa kwa halmashauri kutotenga 10%. Kwa hiyo niiombe Serikali ihakikishe halmashauri zinasimamiwa ipasavyo kwa suala zima la kutoa 10%. Kwani halmashauri nyingi hazitengi pesa hizi kwa viburi walivyokuwanavyo watendaji wachache wasiolitakia Taifa letu mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zilizotengwa kwenda *TARURA* 30% ni ndogo sana wakati mahitaji ya barabara ni makubwa hasa kwa vijijini. Kama unavyojua uchumi mkubwa wa wananchi unatoka kwa wakulima ambao wapo vijijini kwa hiyo wananchi hawa wanatakiwa waboreshewe miundombinu. Serikali iongeze ifike 50% ili angalau barabara zetu ziwe zinatengenezwa kwa wakati muafaka na kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali 20% kikamilifu kwa ruzuku inayotengwa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mamlaka za chini yaani vijiji na Serikali za Mitaa. Kwani hii pesa ikitengwa itasaidia kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Niishauri Serikali ianzishe Bodi ya *TARURA* ili Bodi hii isimamie kuanzishwa kwa Mfuko wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Serikali iwezeshe halmashauri fedha ili ziweze kununua magreda kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu za vijiji hasa kukiwa na dharura kuharibika kwa barabara hasa vijijini. Niiombe Serikali pamoja na kuishauri ifanye haraka iunde haraka mamlaka ya maji vijijini, kwani kuna uovu mkubwa sana unaofanywa na watendaji wetu na ndio maana miradi hii ya maji haimaliziki kwa wakati na mingine haifiki hata kwa robo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takribani miaka saba sasa toka iundwe Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lushoto, lakini cha kushangaza mamlaka ile haijapewa mamlaka ya kujiendesha mpaka leo. Niiombe Serikali itoe kauli ili mamlaka ile iweze kupewa madaraka yake.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nipongeze kazi nzuri sana ya Serikali ya Awamu ya Tano na Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana ambazo anafanya kwa Watanzania. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri, hongereni sana kwa kazi nzuri ya kujenga nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto chache za shule za msingi hususan madarasa pamoja na matundu ya vyoo. Naomba sana Serikali ielekeze mpango mkakati kwa ajili ya mambo muhimu sana hayo kwa ajili ya watoto wetu ili waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Walimu wetu ni wachache sana hususan vijijini pamoja na wahudumu wa zahanati zetu, Manesi, Madaktari, Watendaji wa Vijiji, Kata vilevile kada ya kilimo na Maendeleo ya Jamii. Tunaomba sana Serikali iweke nguvu katika maeneo hayo kwa sababu ndio wanaosimamia maendeleo yetu katika vijiji vyetu pamoja na kata zetu kwa ajili ya wananchi kwa ajili ya huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji vijijini bado wananchi wa Mkoa wa Katavi kupitia vijiji vyake maji bado shida sana. Huo ndio ushauri wangu. Ahsante.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la masomo ya sayansi katika sekondari. Mahitaji Walimu 35,136, waliopo 19,459 upungufu 15,677; je, Tanzania ya viwanda itafanikiwa kwa hali hii? Serikali imefanya sensa ya Walimu wa sayansi wanaoacha kazi katika shule za sekondari na kujua sababu zilizopelekea kuacha kwao na kujua namna ya kuzitatua kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mfuko wa Wanawake na Vijana. Kwa nini katika Halmashauri hakuna akaunti maalum kwa ajili ya fedha hizi, mwisho wake lini Halmashauri kuchangia Mfuko huu kwa sababu huu Mfuko fedha zake zinazunguka. Ni matarajio yangu kwamba baada ya muda Mfuko huu uweze kujiendesha na fedha zinazotolewa na Halmashauri ziweze kufanya au kutoa huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila halmashauri ina chanzo kimoja cha uhakika ambacho ni ardhi, lakini Serikali Kuu imekuwa ikichukua fedha hizo na kushindwa kurudisha 30% inayotakiwa kwenye halmashauri. Je, hapa Serikali Kuu inatenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati yanasema halmashauri nyingi zimeshindwa kukusanya mapato hata chini ya 25% na kushauri Halmashauri hizo zitafute vyanzo vingine vya mapato. Je, vyanzo hivyo vinatoka wapi ikiwa kila chanzo halmashauri zinazobuni Serikali Kuu inachukua? Je, vyanzo hivyo vipya vya mapato ya Halmashauri vinavyotakiwa kubuniwa ni kama vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa utekelezaji wa Manispaa ya Mtwara Mikindani. Taa zilizofungwa katika barabara ya Zambia haziwaki, naomba ufafanuzi wa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha ujenzi wa stendi ya kisasa katika eneo la Mkanaledi, Manispaa ya Mtwara Mikindani. Stendi iliyopo sasa ni ndogo haikidhi mahitaji, naomba ufafanuzi kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopandisha watumishi madaraja licha ya kuwa na sifa stahili mfano kuna watumishi 8,369 katika mamlaka 18 hawajapandishwa kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mpaka 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi katika Halmashauri 161 ambao ni takribani 155,013 sawa na 32% ya huhitaji ambao ni takribani 500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopelekwa 10% ya *own source* (mapato ya ndani) katika Halmashauri 143. Ushauri wangu kuwepo na akaunti maalum na hii pesa iwekwe huko kwanza hata kabla ya matumizi ya kawaida mengine kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kuja na hoja binafsi kuishawishi Serikali kuleta Muswada wa kuzibana Halmashauri ili pesa hii ipelekwe kwa kundi hili maalum katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kuendelea kupanga bajeti zisizo halisi, ndio maana Halmashauri nyingi zimelazimika kuongeza bajeti zake. Mfano Ilala 10%, Mlele 51% na ya kusikitisha ni Newala 81%, kweli bajeti ina-*burst* kwa 81%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopelekwa fedha za maendeleo, hata zile zilipelekwa zimechelewa. Hii inarudisha nyuma juhudi za wananchi kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri tatu kuendelea kufanya vibaya. Je, watumishi waliopo hawaendelezwi kielimu au ni wezi?

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ipandishe madaraja Walimu waliofundisha kwa zaidi ya miaka mitatu ili kuweza kuwa- *motivate* na kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho wa Walimu; kumekuwa na changamoto kwa Walimu pindi ambapo anataka kuhama kutoka eneo (Mkoa, Wilaya) kwenda sehemu nyingine. Aidha, kumfuata mwenza wake au kwa matatizo ya kiafya. Suala la Mwalimu husika kutafuta Mwalimu mwingine wa kubadilishana nae ni gumu. Hivyo, nashauri Serikali isimamie zoezi hilo na sio kuachiwa Mwalimu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya mazingira magumu; kuna baadhi ya Walimu hususan wa vijijini, vituo vyao vya kazi vipo mbali sana na huduma za kijamii mfano mabenki na ofisi za Serikali hivyo hulazimika kutumia fedha nyingi kwa usafiri. Hivyo, naishauri Serikali itenge fungu maalum la posho kwa Walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu kuongeza ujuzi (elimu); naishauri Serikali itenge fedha katika bajeti hii 2018/ 2019 ili iwasaidie Walimu ambao watahitaji kwenda kusimama katika vyuo vyetu. Maana elimu hiyo itasaidia kuwajengea uwezo zaidi wa kuwafundisha watoto wetu wa kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa madarasa na uhaba wa shule katika Wilaya ya Temeke, Mkoani Dar es Salaam. Hususan shule za sekondari kutokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza mwaka 2018. Hivyo, naishauri Serikali itusaidie kutatua upungufu huo uliojitokeza ili kuondokana na wanafunzi hao kusoma kwa *session* yaani asubuhi na jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa nyumba za Walimu katika sehemu mbalimbali katika nchi yetu. Naishauri Serikali iwajengee nyumba bora ambazo zitawekwa na umeme ili kumsaidia Mwalimu kuweza kuandaa andalio la somo, azimio la kazi na kusoma mada mbalimbali ambazo atawafundisha wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa samani (meza, viti na kabati *(shelves),* katika Ofisi za Walimu. Katika

Shule ya Msingi Yombo Dovya Kata ya Makangarawe, Jimbo la Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, katika ofisi za Walimu hakuna meza, makabati na viti. Hivyo, Walimu hulazimika kutumwa madawati kwa kukaa na kufanyia shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iweze kutenga fedha katika bajeti 2018/2019 kwa ajili ya kutengeneza samani hizo ili ziweze kutumika katika shule mbalimbali ikiwemo Shule ya Msingi Yombo Dovya. Pia shule hiyo ina uhaba wa vyoo vya Walimu, Walimu hulazimika kutumia vyoo vya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika Shule ya Yombo Dovya kuna wanafunzi walemavu nao pia hawana choo ambacho kitawasaidia kulingana na walemavu. Hivyo basi kutokana na changamoto hizo, naishauri Serikali itenge fedha ambazo zitasaidia kutatua tatizo hilo la kujenga matundu ya vyoo vya Walimu na wanafunzi walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ushauri wangu atauzingatia.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa hotuba nzuri. Vile vile pongezi kwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni juu ya utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais katika Jimbo la Busanda. Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara ya lami yenye urefu wa kilometa tano katika mamlaka ya Mji Mdogo Katoro na kilometa tano Buseresere wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2015. Mpaka sasa ni miaka mitatu hakuna kinachoendelea. Ningependa kujua ni lini ujenzi wa barabara hizi utaanza rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa barabara katika Jimbo la Busanda kuna kero kubwa sana ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kwa kuwa mamlaka ya Mji Mdogo Katoro kuna idadi kubwa sana ya watu na suala la maji ni kero kubwa ambapo tumezungukwa na Ziwa Victoria. Naomba Serikali iwe na mkakati maalum wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria ili kupata suluhu juu ya changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kwa maneno machache naomba kuwasilisha ili Serikali iweze kutafutia ufumbuzi changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi na msimamo wa Serikali katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza ina upungufu wa Walimu wa shule ya msingi 487, kwani waliopo ni 846 na mahitaji ni 1,333. Je, Wizara ina mkakati gani kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza Walimu hao 487 ili kujenga msingi imara wa kielimu kwa watoto wetu wa shule za msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa nyumba za Walimu ni mkubwa sana Wilayani Muheza, Serikali imejipangaje kuanzisha mpango mkakati wa haraka kusaidia kutatua changamoto ya makazi ya watumishi. Makazi ya askari polisi ni duni, chakavu na hayatoshi. Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto hiyo kubwa inayopunguza morali ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; upungufu wa watumishi katika hospitali teule Wilayani Muheza, Serikali tunaomba mtufikirie. Katika hospitali ya Muheza (Teule) dawa ya nyoka ni 250,000 x3 na dawa ya mtu aliyeng'atwa na mbwa ni 50,000x3. Mheshimiwa Waziri, kung'atwa na mbwa na kung'atwa na nyoka ni ajali ambazo asilimia kubwa ni wananchi waishio vijijini (mashambani). Je, Serikali haioni ni

wakati muafaka dawa hizi kuziingiza kwenye kundi la dawa muhimu ili wananchi wazipate bure. Serikali iliahidi katika mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga milioni 20 kwa ajili ya *ambulance* na mpaka sasa gari huko la wagonjwa halijafika Muheza katika Hospitali Teule. Je, ni lini tutapata gari la wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumishi; katika Wilaya ya Muheza wapo watumishi waliosimamishwa kazi na Serikali kwa sababu mbalimbali. Wapo wengi wa darasa la saba walinzi, madereva na watendaji wengine. Je, Serikali imejipangaje kuwalipa stahiki zao kwa wakati na kuwarudisha kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kwani wanafanya kazi kubwa ya kuwahudumia wananchi lakini hawapati chochote. Je, Serikali imejipangaje kuwapa posho ili nao wapate utulivu wa kufanya kazi zao.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana tena sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya na Mola ampe maisha mema na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo ni Waziri wa kuigwa kutokana na jinsi anavyofanya kazi kwa kushirikisha zaidi na walengwa hadi ngazi ya awali, hafanyi kazi za mezani. Mola ampe nguvu na afya atimize azma yake. Pamoja na timu yake ya Wizara yake wanashirikiana vyema na waendelee hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mkuchika kwa kazi nzuri sana, ingawa bado ana jukumu kubwa kwa mazingira ya upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mengi kufanyika vizuri, bado tunahitaji kazi ifanyike na hasa kwa mikoa ya

pembezoni na kufuatiwa na miji kupanuka na wananchi kuibukia kujenga majengo yao kwa maendeleo yao na kuwaonesha kasi yao kubwa na kuacha Serikali nyuma. Mfano Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba TAMISEMI ishirikiane na Wizara husika kupatikana kwa vyombo vya upimaji ardhi, ili miji ipangwe na tusiwe na maeneo yasiyo na mpangilio. Zoezi la matumizi bora ya ardhi kwenye mikoa yetu lifanyiwe kazi na kutathmininwa kila mwaka ili tuondokane na migogoro ya wakulima na wafugaji, pia na hifadhi zetu na miji yetu isivurugike kimpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba TAMISEMI kuona umuhimu wa kuongeza asilimia ya fungu la fedha za maendeleo ya ujenzi wa barabara za vijijini kwa *TARURA.* Barabara hizo ni nyingi na zinaongezeka siku hadi siku, kwa jinsi wananchi wanavyoongezeka kwenye maeneo na kuibuka vitongoji na vijiji kupanuka. Hivyo tunahitaji *TARURA* kuwa na nguvu kubwa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia barabara za vijijini ni za muhimu sana kwa wakulima, kusafirisha mazao yao kuwapeleka sokoni na viwandani. Akinamama ndiyo wazalishaji hasa wanahitaji barabara kuwawezesha kufika sokoni, hospitali na kupunguza vifo vyao na watoto. Bora *TARURA* kupata asilimia 65 angalau kwa kuanzia kwani *TANROADS* hupata wao na wafadhili na marafiki wa nchi na mikopo ya nchi kuendeleza barabara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tena sana pamoja na kutokuwa na mapato ya kutosha na kutoa nguvu ya mwelekeo wa bajeti kuwa yenye matumaini makubwa kwa maendeleo. Bado tunaomba Wizara kuona uhitaji wa watumishi kwenye maeneo ya awali waliko wananchi wetu ambao wazalishaji wa mazao ya chakula na malighafi ya viwanda vyetu. Wanahitaji zahanati, vituo vya afya, majengo yapo na yanaendelea kujengwa lakini watumishi hawapo, wanahitajika wataalam husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure; inatuhitaji kujenga madarasa, tunaomba Serikali kuwaunga mkono wananchi kuyakamilisha madarasa haya na miundombinu yote ya shule. Maafisa Maendeleo wa Mitaa/Vijiji na Kata na Maafisa Ugani kuhakikisha wataalam hawa kuwepo katika maeneo hayo kwa nchi nzima kwa maendeleo ya wananchi wetu. Pia, wapewe usafiri kurahisisha kazi yao ya kuwatembelea walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto kwenda shule kutokana na elimu bure, Wizara tunahitajika kuajiri Walimu wa shule za msingi na kuwapeleka Walimu kuwa na watoto (wafanyakazi) 45 kuliko ilivyo sasa zaidi ya 100 siyo vyema. Utaratibu wa ujenzi wa nyumba za Walimu ufanyike kwa kila mkoa kwa kuigwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado halmashauri zetu zinafanya vikao vya Mabaraza wakati wa ratiba ya Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge. Hali hii inasababisha Wabunge kutohudhuria vikao hivyo, waskati mwingine inamgharimu pakubwa Mbunge kuhudhuria. Pia tunaomba posho ya Madiwani kuangaliwa upya na wasaidizi wao Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, kwani kazi yao ni kubwa kwa usimamizi wa ufuatiliaji wa miradi na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwarudisha kazini wale wote ambao waliachishwa kazi kwa sababu ya kuwa na elimu ya darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iangalie kwa jicho la huruma hospitali ya Rufaa ya Mtwara. Katika hospitali hii kuna upungufu mkubwa wa Madaktari pamoja na Wauguzi. Hospitali hii inahudumia wagonjwa wengi sana kutoka maeneo mengi sana ya Mkoa wa Mtwara. Katika hospitali pia kuna upungufu mkubwa wa dawa.

Naomba hospitali hii iongezewe bajeti ili wananchi wa Mkoa huu wa Mtwara waweze kupata dawa na huduma za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za vijana/ akinamama. Kwa mujibu wa sheria, kila halmashauri ina majukumu ya kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vijana asilimia tano na akina mama asilimia tano. Hata hivyo, kwa kuwa vyanzo vya mapato ya kodi za majengo *(property tax)* na ushuru wa mabango vimechukuliwa na *TRA,* Halmashauri haziwezi kutoa fedha za mikopo kwa akinamama na vijana. Hii inasababisha vijana na akinamama kuchukua mikopo *BRAC, FINCA* na kadhalika. Taasisi hizi zina riba kubwa na akinamama wanachukuliwa vyombo vyao vitanda, makochi, *TV,* radio na kadhalika pale wanaposhindwa kulipa riba hizo

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na pongezi. Sina budi kuipongeza Wizara ya TAMISEMI, Waziri Jaffo, Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege pamoja na Makatibu wao wote kwa kazi zao nzuri na usikivu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini tumepewa milioni 900 za *force account* na Serikali. Fedha hizi tumezigawa katika kata mbili; Kata ya Katoro milioni 500 na Kata ya Kishage milioni 400. Katika Kata hizo wanajengewa nyumba za mama na mtoto, nyumba za Waganga kila kata nyumba moja moja na mochwari moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo, tuna shida ya Wahandisi wa Ujenzi, tunaomba Serikali itusaidie wahandisi hao maana Wahandisi wa kujitegemea gharama zao ni kubwa sana. Tuna Wahandisi wa *TARURA* tukiwaomba wanasema wao ni wa barabara. Tunaomba sana watuonee huruma katika shida hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru zahanati tunazo, vituo vya afya angalau tunavyo na dawa zipo, shida

hatuna Manesi, pia na Waganga ni wachache sana, tunaomba na eneo hilo tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; tuna shida sana na Walimu wa shule za msingi na sekondari kwani tuna upungufu sana. Vile vile tusaidiwe nyumba za Walimu ni shida, vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake, basi aiangalie Wilaya yetu ya Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, nashukuru.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wachangiaji waliotangulia kuwapongeza Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Nianze na kuchangia kuhusu Walimu. Walimu wanafanya kazi nzuri na ni walezi wa pili katika familia baada ya wazazi/walezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mwingi Walimu wanashinda na watoto wanaotoka katika malezi mbalimbali lakini wanapofika shuleni wao huwa ndiyo walezi, Madaktari, Manesi, Mahakimu, Polisi na kadhalika. Kazi zote hizi Walimu wanakuwa kama ndiyo mbadala wa watajwa hapo juu kutokana na majukumu wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ndiyo chimbuko la wafanyakazi wa fani zote katika nchi hii. Kama Mwalimu angeacha kumpatia mwanafunzi msaada wa kumudu kusoma vizuri darasani akafaulu vizuri na hatimaye kufika hadi chuo kikuu na kuweza kupata kazi nzuri ya kumwendeshea maisha yake au hata kuweza kujiajiri mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu huyu yuko katika mazingira magumu sana lakini bado wanaendelea na

mikakati ya kufundisha ili kujenga Taifa la wasomi. Naiomba Serikali angalau iwarudishie Walimu ile posho waliyokuwa wakipewa miaka ya 80 yaani *teaching allowance.* Hii *teaching allowance,* ilikuwa ni asilimia 25 ya mshahara wa Mwalimu. Hii ingewasaidia Walimu katika kupunguza makali ya maisha na kumudu kufanya vizuri kazi yao ya kuwafundisha watoto.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya, ni nzuri na zinaonekana. Niwapongeze pia Makatibu Wakuu wa Wizara kwa kuendesha vyema Wizara. Naomba changamoto zifuatazo tuzifanyie kazi:-

Ujenzi wa barabara ya Nzasa-Kilungule-Buza; barabara hii ni muhimu sana, Serikali imelipa fidia kwa wananchi kwa lengo la kuingia mradi wa *DMDP,* lakini mradi huo inasemekana hauwezi kuingia katika *DMDP*. Je, zile fedha za fidia si tungeweza kujenga barabara angalau kwa nusu kilomita? Je, nini hatima ya barabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweka maslahi wazi, mimi nilikuwa Mwalimu; Walimu kuwahamisha kutoka msingi kwenda sekondari ni jambo jema, lakini halijazoeleka katika nchi yetu. Zamani ukirudishwa msingi kutoka sekondari ni *demotion.* Je, Serikali imewapa elimu Walimu watambue Mwalimu anaweza kufanya kazi msingi au sekondari kwa ngazi ya mshahara ule ule? Je, Serikali imejipanga vipi kuweka *Counselors* katika Halmashauri zetu kwa kutoa ushauri nasaha kwa makundi mbalimbali yanayofanyiwa mabadiliko ya kimfumo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa vibali vya ujenzi katika Halmashauri zetu; kweli Serikali imefanya vizuri kwa kufupisha muda wa kupata kibali cha ujenzi, lakini kibali kinachotoka Halmashauri hakipewi heshima kama kimepitishwa na wataalam mbalimbali matokeo yake wanakuja wahindi na Ma-*architect* kutoka maeneo mengine

kuvitengua na kudai malipo upya. Kwa nini hawa wanataka kupitia wasiungane na Halmashauri, mwananchi akipata kibali aendelee na ujenzi badala ya kusimamishwa kila mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabasi yaendayo kazi; napongeza Serikali kwa mradi huu ni mzuri na unasaidia. Naomba sasa angalau uanze ujenzi wa mwendokasi Mbagala kwa kuwa hatua iliyobaki ni ulipaji wa fidia ya stendi ya Mbagala Rangitatu. Naomba sasa tuanze ujenzi wa barabara huku tukiendelea na zoezi la stendi, ni jambo jema, nalitakia heri lifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza juhudi za Serikali kwa maboresho ya barabara za Mitaa ya Kariakoo, Gerezani na Upanga kwa kweli inapendeza na kazi ni nzuri kwani maeneo hayo yalikuwa na barabara mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawapongeza viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala, Wakurugenzi wa Halmashauri zangu zote za Mkoa wa Dar es Salaam na Wakuu wa Wilaya wote, Ma-*DAS* wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kuweza kutekeleza majukumu yangu bila kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TARURA waongezewe nyezo za kufanyia kazi kama magreda, makatapira na vifaa vingine vya ujenzi. Kwa kuwategemea wakandarasi wa kukodishwa linapotokea tatizo, hakuna wa kuli-solve haraka sana. *TARURA* pia waangalie wakandarasi wa kuwapa kazi, kuna tofauti kubwa kati ya barabara za *TANROADS* na *TARURA* kwa zile za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za wanawake na vijana, benki wanazitoza riba lakini halmashauri wana Wahasibu. Kwa nini utaratibu usifanyike fedha zikatolewa katika Halmashauri zetu na kama ni benki kusiwe na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, bajeti ipite, maendeleo yafanyike, tupate matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa miongoni mwa washiriki katika mjadala wa bajeti 2018/2019. Naipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa kufanya kazi vizuri chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona juhudi za Serikali katika suala la afya na kuongeza juhudi katika ujenzi wa zahanati. Naiomba Serikali iendelee kutoa mchango wake katika zahanati na maeneo ya visiwani. Naomba nielezee zilizopo Mkoa wa Pwani Wilaya ya Rufiji, Kibiti, Mkuranga na Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii inayoishi kwenye visiwa inahitaji huduma zote muhimu katika maeneo yao ikiwemo afya na usafiri wa uhakika ambao ni haki yao kwa kuwa maeneo mengine kuna aina mbliambali za usafiri. Naomba Serikali iongeze nguvu au kupeleka usafiri wa boti la wagonjwa kwa wananchi wa Kisiwa cha Koma na Kwale vilivyopo Wilaya ya Mkuranga ili kuokoa na kurahisisha usafiri kwa wagonjwa hususani kwa wajawazito, watoto na wengine wanapougua ukizingatia mama mjamzito anapotoka kujifungua hajui muda gani wala siku. Kusipokuwa na huduma sahihi na za haraka hupelekea kupoteza maisha na hivyo inatokea sana kwenye visiwa vyetu vya Mkoa wa Pwani. Chondechonde naiomba Serikali itupatie huduma hiyo au kupeleka vifaa vyote muhimu vya tiba na wahudumu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya TAMISEMI izielekeze Halmashauri zote ziweze kutenga fedha kwa ajili ya taulo za wasichana mashuleni ili kuwawezesha wale wasio na uwezo wa kuzipata na kushindwa kuhudumia masomo pia kuwa na ufaulu usioridhisha kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana kwani Halmashauri ya Kisarawe imeanza kutenga fedha hizo kwa

mantiki hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na nyingine ambazo zimekuwa zinatenga fedha. Nimelisema hilo kwa kuwa ni tatizo kubwa sana kwa baadhi ya wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa fedha na kukarabati shule Kongwe nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali katika juhudi zake za kusogeza maendeleo jamii na kuziwezesha. Suala la kupunguza riba kwenye mikopo ni jambo jema sana, hivyo basi mchakato wake ukamilike kwa haraka ili ulete unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*; iwezeshwe ili iweze kufanya kazi zake kwa wepesi. Mkoa wa Pwani unahitaji barabara zake ziwe za kupitika mwaka mzima kwani zitarahisisha maendeleo na pia kuwezesha kusafirisha malighafi na bidhaa zinazotoka kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.Kwanza naunga mkono hoja iliyo mbele yetu na nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika shughuli za maendeleo. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Dokta John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na bila kumsahau Mheshimiwa Waziri Jafo na Manaibu wake wote wawili, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuamua kwa dhati kuboresha huduma za Mama na mtoto katika vituo vyetu vya afya Mkoa wa Shinyanga. Tumepata vituo sita ambavyo kwa sasa kazi ya ujenzi inaendeleea ukingoni. Tunashukuru sana kwa niaba ya wanawake wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na shukurani zangu hizo kwa sekta ya afya, nina ombi maalum ambalo kila ninapopata nafasi ya kuongea lazima niseme chondechonde, Mheshimiwa Waziri naomba sana mwaka huu wa fedha Serikali iweze kuiona Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa jicho la huruma. Naomba tupatiwe fedha ya kutosha katika ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambao umeanza kwa muda mrefu sana ili kuweza kuunga mkono jitihada na nguvu za wananchi hatimaye hospitali hii ianze kutoa huduma zilizokusudiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI wakati anajibu swali humu Bungeni alisema, kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, hospitali 67 zitajengwa; naomba sana miongoni mwa hizo 67 na hospitali ya Wilaya ya Shinyanga iwekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ipatiwe fedha za ujenzi wa hospitali ya Wilaya kwa kuwa ni Halmashauri mpya hivyo, huduma hii ni muhimu kwa wananchi wa Ushetu na kuwa na hospitali za Wilaya itasaidia kupunguza msongamano katika hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu pia, naomba mnapotoa fedha za kutosha katika ujenzi wa hospitali ya Wilaya, nashauri utumike utaratibu wa *force account* ambao unaonekana kuwa na tija kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Shinyanga ipatiwe fedha za kutosha ili iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pia kilio changu katika sekta ya elimu, Halmashauri ya Shinyanga ina shule moja ambayo kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani ya darasa la saba. Shule hii inaitwa Shule ya Msingi Masunula. Shule hii haina nyumba hata moja ya mtumishi, Walimu wanaishi katika nyumba za kupanga huko mtaani. Naomba sana shule hii itazamwe kwa jicho la huruma ili Walimu hawa tuwape nguvu ya kuendelea kufundisha watoto wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza wananchi wa Kata ya Solwa wakiongozwa na Diwani wao, wamekubaliana kwa pamoja, wameanza kampeni na wameweza kujenga vyoo katika shule zote za msingi katika kata yao na wamejenga madarasa matano, Ofisi ya Walimu na wamejenga na kuchimba vyoo matundu sita na Halmashauri imechangia upauaji wa majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uamuzi huu wa wananchi wa Kata ya Solwa, naiomba Serikali iwaunge mkono wananchi hawa ili waweze kukamilisha ujenzi huo wa shule mpya ya msingi inayoitwa Solwa B ambapo ndiyo wamejenga madarasa matano, Ofisi ya Walimu na vyoo matundu sita. Naomba wananchi hawa wapewe fedha ya kutosha ili panapo majaliwa 2019 shule hii iweze kupokea watoto wa darasa la kwanza kwani wameonesha kilio chao kwa kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe ushauri upande wa fedha za wanawake na vijana; naomba vikundi hivi wapewe vitendea kazi na siyo fedha. Hii inaweza kuwa na matokeo mazuri zaidi katika utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuiomba Serikali iweze kuajiri watumishi zaidi hususani sekta ya afya kwa Mkoa wa Shinyanga, kwani kuna upungufu mkubwa sana kuanzia hospitali ya mkoa hadi zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri sana ikiwa ni pamoja na miongozo ambayo imetoa dira katika kuboresha utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Seleman Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Mheshimiwa Joseph

Kakunda na Mheshimiwa Josephat Kandege, Naibu Mawaziri, TAMISEMI pamoja na Watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara za Waziri alipotembelea Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya alishuhudia changamoto za mtandao wa barabara ambazo kwa kiasi kikubwa hazipitiki kipindi chote. Pia alishuhudia daraja la Mto Idiwili katika Kata ya Isuto ambalo lilijengwa chini ya kiwango kupelekea kuvunjika mpaka leo hakuna mawasiliano ya hiyo barabara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Tarafa ya Isangati na Wilaya nzima ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri kupitia TAMISEMI warekebishe hilo daraja la Idiwili, pia barabara nyingi ziko katika hali mbaya sana ikiwemo barabara ya Mjele – Ikukwa, Ilembo – Mwala na Daraja la Izyira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti ya *TARURA*, napendekeza uongezwe mgao kutoka mfuko wa barabara kutoka asilimia 30 na kuwa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ikamilishe ahadi ya Rais ya kumalizia ujenzi wa stendi ya Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu miradi ya maji haikukamilika kutokana na usimamizi usioridhisha ikiwemo ubadhirifu. Napenda kupongeza ziara za Mheshimiwa Kakunda, Naibu Waziri wa TAMISEMI na pia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri wa Maji, ziara zao zimeleta tija kubwa na sasa miradi ya maji imeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ikamilishe kuunganisha Mamlaka ya Maji Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Maji Mji Mdogo wa Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia Wizara iweke mkakati wa kupeleka maji katika vituo vya afya, zahanati na shule zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali na kwa kipekee Wizara ya TAMISEMI kwa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Ikukwa, Sautilya na Ilembo. Pia napenda kushukuru kwa kutenga bajeti ya shilingi bilioni 1.5, kwa ajili ya hospitali ya Wilaya ya Mbeya *DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuomba Serikali kuunga mkono ujenzi wa zahanati zaidi ya 40 na Vituo vya Afya vya Kata ya Ilungu na Isuto ambavyo wananchi wamejenga kwa nguvu zao na vipo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara iweke mkakati wa ujenzi wa mabweni katika shule za kata. Kipekee kuna ujenzi kwa nguvu ya wananchi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Galijembe na Sasyaka (Masoko), ambazo kwa sasa napendekeza Wizara iunge mkono nguvu ya wananchi kumalizia shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara iweke mkakati wa haraka, wa mpango miji kwa Mji wa Mbalizi na Miji Mdogo inayokuwa kwa haraka kama vile, Inyala, Ilembo, Isuto, Igoma na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iridhie/ maombi ya Halmashauri ya Mbeya *DC* ya kubadili matumizi ya shamba ya iliyokuwa *Tanganyika Packers* ili litumike katika kupanga Mji Mdogo wa Mbalizi, ikiwemo maeneo ya ujenzi wa viwanda, hospitali, mashule na makazi ya wananchi na halmashauri imetenga eneo mbadala katika Kijiji cha Mjele kubadilishana na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, inajenga machinjio ya kisasa kwa soko la ndani na nje ya nchi na vifaa vimetolewa na *UNIDO*. Kwa sasa kunahitajika bajeti ya Serikali kumaliza ujenzi wa kiwanda hiki cha nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbeya Vijijini lina ukubwa wa kilomita za mraba 2,432, tarafa tatu na vijiji 152, lakini Tarafa ya Tembela haiungani na tarafa zingine na

kutokana na idadi kubwa ya wananchi, Serikali ya Mkoa *(RCC)* waliomba kugawanywa kwa jimbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali iridhie kugawa Jimbo la Mbeya Vijijini na naunga mkono hoja.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali na Watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo na Naibu Mawaziri wake na Watendaji wote wa Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 10 ya vijana na wanawake; kauli ya Serikali kwamba kuanzia sasa fungu hili la vijana na wanawake halitatozwa riba ni jambo zuri. Ushauri wangu ni vizuri Serikali ijiridhishe suala la kodi ya mapato kwani *TRA* inatoza mapato Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* hivyo ni vyema jambo hili likapewa ufafanuzi ni kwa namna gani pesa hizo zitapitia *SACCOS* bila kutozwa kodi ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo inayosimamia shule za msingi na sekondari. Hali ya uanzishaji wa vyuo vya ufundi VETA hapa nchini si ya kuridhisha na tunatoa elimu ya nadharia zaidi. Nashauri Serikali kufanya maamuzi ya kuagiza kila halmashauri iongeze mchepuo wa ufundi katika shule moja au mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima kuanzisha fani zaidi ya moja katika kila shule ili jambo hili liwezekane kwa urahisi ni vizuri kuanzisha fani zenye gharama nafuu ili vijana wakimaliza kidato cha nne wawe na ujuzi wa kuwawezesha kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa shule ya msingi wenye cheti cha daraja la IIIA, hawana fursa ya kujiendeleza

na daraja la IIIA siyo sifa ya kujiendeza katika chuo chochote hapa nchini. Nashauri Serikali, TAMISEMI wakae na Wizara ya Elimu ili kozi iliyozuiwa na Wizara ya Elimu iliyokuwa ikisimamiwa na *NACTE* na kuendeshwa na vyuo vya kati kwa kuwapa maarifa zaidi Walimu hawa pia kuwawezesha kupata madaraja mapya kwenye kada ya Walimu wa daraja IIIA hii pia itatia morali kwa Walimu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo na Mzee wangu Mkuchika pia bila kuwasahau Naibu Mawaziri Mheshimiwa Kakunda, Kandege pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri zinazofanyika katika Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajitokeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; katika eneo hili kwanza naomba sana hospitali ya Mafinga Mjini iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, ipandishwe hadhi na iwe hospitali ya rufaa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Wilaya nzima ya Mufindi pamoja na wakazi wengine wanaopata huduma kutoka wilaya nyingine na mkoa mwingine kama wakazi wa Madibila, Mapogoro kutoka Wilaya ya Rujewa, Mkoa wa Mbeya pia kumekua na ajali nyingi sana zinazotokea katika maeneo haya na zinakuwa zinahudumiwa na hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mufindi Kaskazini lina Tarafa nne (4) lakini tuna vituo viwili tu vya afya na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi haina hospitali. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliangalie jambo hili kwa macho mawili, kwa kuanzia tu hata tukiwa na kituo kimoja kwenye kila tarafa tutakuwa tumeanza nyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina watumishi asilimia 28 za watumishi. Kwenye Idara ya afya kuna upungufu wa asilimia 72. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alione jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi tuna zahanati nne ambazo zimekamilika, zahanati hizo ni Mwitikila, Mufindi Kaskazini; Kiponda Nyigo na Igoda, Mufindi Kusini; lakini bado hazijafunguliwa sababu wataalam na vifaa, lini zahanati hizo zitafunguliwa ili kutokuvunja au kudhoofisha nguvu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iunge mkono juhudi za wananchi wanaojenga Zahanati kama vile Igomtwa na Wambi Mbelwa na Makongomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara; kuna haja ya kuongeza pesa kwenye Taasisi ya TARURA ili iweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara muhimu sana katika Jimbo la Mufindi Kaskazini lakini wakati wa mvua haipitiki kabisa. Barabara hii ni kutoka Mtili – Ifwagi – Idaburo – Ihanu – Isipii – Mpangatazara - Mrimba. Barabara hii inaunganisha Mikoa miwili, Iringa na Morogoro, Wilaya ya Mufindi na Kilombero ina ukubwa wa zaidi ya kilomita 106.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Jafo anajua tatizo la barabara hii, naomba sana tupewe pesa ya kutosha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii yenye uchumi mkubwa kwani kuna kilimo cha chai, pareto, maharage, misitu mikubwa ya mbao pamoja na eneo la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya bajeti zote mbili ya TAMISEMI pamoja na Utumishi na Utawala Bora.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendeleza suala la kuomba matumizi ya lugha

ya kufundishia katika shule za msingi na shule za upili kuwa Kiswahili. Naelewa kuwa suala hili ni la kisera chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lakini niliomba uamuzi wa Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ndiyo sababu ya kuleta suala hili kupitia Hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake alisemee suala hili la kufundisha shule za msingi na shule za upili kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuleta mkakati wa kuboresha vituo vya afya. Naomba kujua awamu nyingine ya fedha hizi, Mji wa Geita utapewa? Hii inatokana na kutokuwemo katika awamu ya kwanza. Geita Mjini haina hospitali hivi sasa kwa kuwa hospitali yetu ya wilaya kwa miaka minne imebadilishwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kukubali kuwarejesha Watumishi wa darasa la saba kazini. Naomba sana suala hili liwe kwa watumishi wote waliokumbwa na kadhia hili ikiwa ni pamoja na Manesi, Dereva na Idara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kukabiliana na tatizo la upungufu wa Walimu, kwa kuwa hivi sasa tunapunguza Walimu wa sekondari kwenda msingi ni vyema taratibu za kuangalia kwa makini waliokusudiwa zifuatwe kwa kuwa hivi sasa kuna kukomoana. Pia ni muhimu sana wanaohamishwa wawe ni wale wenye *Diploma* kwanza kuepuka kutengeneza tatizo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa elimu, naishauri Serikali hasa kwa elimu ya Sekondari kuacha kuchukua watoto holela wa darasa la saba. Kwa mfano, mwaka 2017 iwapo uwezo wa Serikali nchi nzima ni wanafunzi 200,000 wa mwaka wa kwanza basi mwaka

unaofuata Serikali ichukue kwanza 200,000 na baadaye iongeze idadi iwapo tu inazo taarifa za uwepo wa nafasi zaidi kuliko hivi sasa kuchukua kama kokolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira mpya; bado hakuna uwazi wa kutosha katika mfumo wa kuchuja watahiniwa kwa kuwa hivi sasa ni rahisi sana kwa Watendaji wa Idara ya Utumishi wanaokuja mikoani kuja na watu wao.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nipongeze Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maamuzi yenye busara na haki katika kazi za kuhudumia halmashauri zetu. Pamoja na hayo nilete ombi la kutekelezwa kwa ujenzi wa kilomita tano katika Mji wa Haydom ambapo Rais aliahidi kujengwa kwa kiwango cha lami na Dongobeshi kilomita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fedha za kituo cha Afya cha Dongobeshi. Naomba kupewa tena fedha katika Kituo cha Maretadu, Endamilay, Masieda na Maghangw kwani wananchi wanapata tabu ya kutembea mbali kutafuta huduma ya hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA*; Jimbo la Mbulu Vijijini lina changamoto kubwa ya barabara na madaraja ambayo hayapitiki. Naomba *TARURA* Wilayani ipewe kipaumbele cha kupewa bajeti zaidi ili kutatua au kupunguza changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi; tuna changamoto ya kutokuwa na *Engineer* wa Maji; Idara inakaimiwa na Fundi Mchundo. Walimu wa Sayansi hatuna kwa kiwango kikubwa, hivyo tunaomba tupatiwe pia Maafisa Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa umuhimu wa pekee, napenda sasa kuishukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mawaziri wake wamefanya ziara katika wilaya yetu. Nawashukuru sana Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Joseph Kandege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; wawe na mpango wa kuwaelekeza Watendaji Wakuu mfano, *DC, DED, RC,* wajue sheria za Serikali za Mitaa na kuziheshimu hasa *PPRA, RRA* na *D-by D* ili wafahamu utaondoa mikanganyiko iliyopo huko maana inaleta taswira mbaya na kuchafua picha nzuri ya Serikali bila sababu kwa wananchi. Tusiposhughulikia tunaweza kupoteza ari na kutoungwa mkono kwa Serikali na chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa na kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inakwenda kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo, uchumi, elimu, barabara, afya na kadhalika. Nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kuandaa hotuba ya bajeti nzuri yenye malengo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo na utawala bora Wakuu wa Mikoa yote, mafunzo hayo yametolewa Tanzania Bara. Aidha, Makatibu Tawala wa Mikoa, 26; Wakuu wa Wilaya, 139; Wakurugenzi wa Halmashauri, 185; Maafisa Utumishi,185; Maafisa Mipango, 185; wamepata mafunzo kuhusu majukumu na mipaka ya kazi zao, maadili ya uongozi, utawala bora usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mzuri na uwe endelevu, kwani mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji na kuondoa mwingiliano wa majukumu baina ya viongozi na watendaji. Katika mafunzo hayo, viongozi na watendaji wetu wamekumbushwa wajibu wa kusimamia maendeleo na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika

maeneo yao ya utawala ili kusaidia kumaliza kama si kupunguza malalamiko ya wananchi ya muda mrefu ambayo yanapelekea kusababisha mabango ya kero zao pindi viongozi wetu wa juu wanapofanya ziara mbalimbali nchini. Napendekeza mpango huu uwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi sana katika kuwatetea wananchi wetu kwa kasi ya hali ya juu, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali katika safari hiyo ya maendeleo, changamoto hizo zimenigusa mimi pamoja na wananchi wenzangu wa Kibaha vijijini, kwa muda mrefu sana sasa tunaendelea kupambana na changamoto ya maji, wananchi wangu wanaendelea kukabiliana na changamoto hiyo kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji ambayo ndiyo ingewakwamua wananchi hawa kwa kupata maji safi nayo haikamiliki kwa wakati na ikizingatiwa chanzo cha maji kiko katika eneo lao na wao wamekuwa walinzi wazuri wa chanzo hicho ili kuepuka uharibifu wa aina yoyote unaoweza kutokea na kuleta athari kwa watumiaji wa maji, lakini wamekuwa wakishuhudia maji yakipita na kwenda kutumika katika maeneo mengine na wao kuachwa na changamoto ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yamekuwa sugu kwa changamoto ya maji ni Magindu, Gwata, Kipangenge, Mwanabwito, Kisabi. Naomba katika bajeti hii kupewa kipaumbele katika sekta ya maji hasa katika miradi ya maji ambayo ina changamoto ya kusimama kufanya kazi kutokana na kuharibika vifaa basi nayo ipewe kipaumbele kwa kufanyiwa marekebisho ya haraka, hii itasaidia katika utekelezaji wa miradi ya maji ili wananchi waondokane na kadhia hiyo ya muda mrefu.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazoendelea kuzichukua katika suala zima la kutambua ukuaji wa maji na kuchukua tahadhari ili kuepuka yaliyotokea hapo awali katika miji yetu yasijirudie tena, Serikali inatambua ukuaji wa

miji na fursa ya kimaendeleo kijamii, kiuchumi kimazingira. Kwa kutambua hilo ndio maana mipango ya matumizi bora ya ardhi ikaandaliwa katika vijiji 1,764 ikilinganishwa na vijiji 12,545 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Kibaha Vijijini tumejiwekea utaratibu wa kuandaa maeneo ili kuepuka matatizo ambayo yamejitokeza katika maeneo mbalimbali nchini kwa kutokutenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali, hivyo basi napenda kuleta ombi kwa Serikali yangu sikivu kupitia Wizara walete na kujenga soko kubwa la kushushia mazao Mlandizi ili kuepusha sasa msongamano ambao upo katika masoko yetu ya mijijini kwa mfano Kariakoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlandizi tuna maeneo makubwa yenye nafasi za kutosha na kupangika hivyo kujenga soko hilo kutasaidia kupunguza msongamano kama nilivyosema hapo awali, lakini si msongamano tu bali pia kutoa fursa ya kuendeleza miji yetu kama Serikali inavyoainisha katika mipango yake, kwani machache ya kuweza kutanua mji huo na ukiangalia mifumo ya mipango miji kwa kiasi kikubwa katika Jiji hili haiko sawa, kwa kuwa ilishakosewa tangu hapo awali.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua katika sekta ya afya, hatua hizo ni kama kuratibu na kusimamia hospitali zote za halmashauri, vituo vya afya na zahanati kuhakikisha zinatoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, changamoto hazikosekani. Katika sekta ya afya, katika jimbo langu baadhi ya maeneo bado changamoto zipo, Vituo vya afya Ruvu, Soga, Magindu, Boko, Gwata, Dutumi, Kata ya Kikongo na Kalangalanga vina changamoto mbalimbali ambazo Wizara kama msimamizi na mratibu wa sekta hii hakuna budi kuzitatua changamoto hizo, kuboresha vituo hivyo vya afya ili viweze kutoa huduma bora kwa wananchi na kupungunza idadi ya vifo vinavyotokana na uduni wa vituo hivyo.

Kuongeza ujenzi wa vituo vya afya kutasaidia sana wananchi wangu kupata huduma kwa wakati pale inapohitajika na kuepuka kutembea kwa muda mrefu kufuata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo ipo katika Sekta ya Afya jimboni kwangu ni upungufu wa nyumba za watumishi wa vituo vya afya, zilizojengwa na Serikali bado kasi yake hairidhishi. Nashauri Serikali kuongeza kasi ili zikamilike kwa wakati mnamo 30 Juni, 2018 kama ilivyosema. Mpango huu ukikamilika utasaidia kupunguza adha hiyo. Vilevile usambazaji wa dawa na vifaatiba uongezwe kwa kiwango kikubwa ili kurahisisha upatikanaji wa dawa kwa wananchi na vifaa tiba.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, Serikali inaendelea kupambana na changamoto katika sekta nzima ya elimu; kutoa elimu bure kuanzia darasa la awali hadi sekondari kuwezeshwe kwani shule nyingi kuwa na madarasa ya awali ni hatua nzuri na inahitaji kupongezwa kwani watoto wetu wanapata elimu wakiwa katika vyumba vya madarasa salama kabisa tofauti na hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado changamoto zipo katika sekta ya elimu, baadhi ya maeneo jimboni kwangu tuna changamoto ya matundu ya vyoo, nyumba za Walimu, upungufu wa madarasa, Walimu kulipwa stahiki zao na upungufu wa walimu. Naiomba Serikali kuziangalia changamoto hizi kwa jicho la pekee kwa kuniongezea Walimu, matundu ya vyoo, ujenzi wa nyumba za Walimu na Walimu hawa kulipwa stahiki zao kwa wakati. Mkoa wetu wa Pwani tulikuwa nyuma kielimu ukilinganisha na sasa hivi, changamoto hizi zikiendelea basi zitarudisha juhudi zetu za kuendelea kupandisha kiwango cha elimu jimboni kwangu, matumaini yangu kilio hiki kitapewa kipaumbele kwa maendeleo ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa uendelezaji wa miji ya kimkakati Tanzania ni mpango mzuri kama ulivyoainishwa na Serikali kwa baadhi ya miji, lakini nina ombi;

katika mpango huu pia Halmashauri yetu ya Kibaha Vijijini ingeingizwa katika mpango huu wenye tija kubwa ya kimaendeleo kwa nchi na eneo husika kwani hukuza nyanja nzima ya ukuaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi. Hata hivyo, napenda kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa ya kujenga barabara yenye urefu wa kilometa tano itekelezwe kwani ni muda sasa umepita bila ahadi hiyo kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Nipende kumpongeza sana Waziri wa Utumishi Kapteni George Huruma Mkuchika kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia Utumishi wa Umma. Nakiri kwa kusema nidhamu ya utumishi wa umma imerudi na uwajibikaji umeongezeka kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaulimbiu ya Awamu ya Tano ni uwekezaji katika viwanda unaochochea ukuaji wa nchi. Ili kuwekeza katika viwanda lazima tuwe na rasilimali watu tuliyoiandaa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo inayoratibu na kusimamia utumishi wa umma nchini. Utumishi wa umma unatakiwa kuwa endelevu, unatunza historia na kumbukumbu za Serikali hali kadhalika utumishi wa umma unatakiwa kutekeleza kazi za Serikali iliyoko madarakani bila kujali inatokana na chama gani cha siasa ili kuondoa uwezekano wa mtumishi kutoa huduma kwa upendeleo au ubaguzi kutokana na itikadi za kisiasa. Kuingiza utumishi wa umma katika itikadi za vyama kutayumbisha utumishi wa umma ambao ndiyo injini ya utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii tena kumpongeza Waziri na viongozi wote kwa ujumla kwa maamuzi ya kurudisha kazini watumishi wa darasa la saba,

walioondolewa kazini. Kwanza hii niseme inapunguza gharama kubwa kwa Serikali kuwalipa watumishi hawa. Sambamba na hilo hawa watajifuta wenyewe kwa kuwa baada ya elimu bure Watanzania wengi watatoka hapo na kufikia angalau kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hawa wametumikia Serikali kwa muda mrefu kwenye fani ya udereva na uhudumu wa ofisi nyingi za Serikali yetu. Nimekuwa mtumishi katika Hifadhi za Taifa Tanzania na watumishi wengi walioko kwenye *level* ya darasa la saba ndiyo walinzi wakubwa wa rasilimali zetu, maliasili za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie upungufu wa watumishi, Wataalam kwenye Wizara ya Afya. Hili limekuwa na changamoto kubwa kwenye Idara ya Afya na hivyo kupelekea hospitali zetu za rufaa kubeba mzigo mkubwa. Nashauri eneo hili liangaliwe kwa jicho la pekee sana.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia katika Bunge lako Tukufu angalau kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Napenda kumpongeza Waziri Jafo na Manaibu wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Waziri wa TAMISEMI kwa kazi nzuri wanayofanya. Naishukuru Serikali kwa miradi yote ya maendeleo iliyotolewa kwa Mkoa wetu wa Morogoro, kutokana na Morogoro Vijijini kutokuwa na hospitali ya wilaya naiomba na kuishauri Serikali yangu kupandisha Kituo cha Afya Dutumi na kuwa hospitali ya wilaya, majengo yapo, iko kwenye baadhi ya majengo ambayo yaliachwa na wafadhili bila ya kukamilika, naomba Serikali ione jinsi ya kukamilisha majengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hiki Kituo cha Afya Dutumi kiangaliwe kwa namna ya pekee kwani Wauguzi na Madaktari hawatoshi. Kituo hiki kinachukua takribani kata

saba, lakini kata hizi ziko mbalimbali. Kwa sababu ya kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto, nawaombea wanawake wa Morogoro Vijijini gari la wagonjwa. Wanawake hawa wanapata shida sana kwa kuletwa kwenye kituo cha afya hiki. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI tafadhali awasaidie wanawake wajawazito na watoto na watu wengine (wagonjwa) kwa kuwapatia gari la wagonjwa katika kituo hiki cha Dutumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutupatia hela za baadhi ya vituo vya afya katika Mkoa wetu wa Morogoro. Ombi langu licha ya kutokuwa na hospitali ya wilaya katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, pia hatuna hospitali za wilaya katika Wilaya ya Mvomero na Gairo, pia Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambayo inajengwa kuwa hospitali ya wilaya bado haijakamilika. Tunaomba hospitali za Wilaya katika Wilaya hizo nilizozitaja hapo huu na pia kukamilisha ambazo bado kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Mafiga kinatoa huduma kubwa. Akinamama wajawazito na hasa wanawake wanapenda kujifungulia katika Kituo cha Afya Mafiga. Tatizo wagonjwa wajawazito hasa akinamama wanaishi katika mitaa na kata za mbali, kiasi wakati mwingine hupatwa na matatizo ya uzazi, kwani hakuna gari la wagonjwa la kuwakimbiza kwenye kituo hicho cha afya. Mheshimiwa Waziri nawaombea gari la wagonjwa wanawake hawa wenye matarajio ya kujifungua salama na kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto. Gari lililopo ni la zamani na mara kwa mara ni bovu, pia linatumika kwenye vituo vingine vya afya katika Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro tuna upungufu wa Walimu wa shule za **msingi zaidi ya ……pia** tuna upungufu wa Walimu wa sayansi 641 katika shule za sekondari. Naishauri Serikali izidi kuajiri Walimu wa sayansi mpaka shule za vijijini kadri Walimu wanavyohitimu vyuo. Pia ukosefu wa Walimu, nashauri kuwepo usambazaji wa Walimu hawa wa msingi sawasawa mjini na vijijini kadri nchi yetu inavyosonga mbele kwa miradi ya kisayansi ndivyo

wanasayansi wanavyohitajika. Kwa hiyo, ombi na ushauri wangu, Serikali yangu ya Awamu ya Tano iliangalie suala hili la upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine ni kuhusu *TARURA*. *TARURA* wawezeshwe ili barabara za Manispaa Morogoro zitengenezwe. Barabara nyingine kwa sasa zina mashimo. Je, hao *TARURA* mbona hawaendi *speed* inayotakiwa mpaka barabara za vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu na hasa katika badhi ya mikoa na hasa mikoa inayozalisha sana mazao kuna utapiamlo uliokithiri pamoja za udumavu zaidi ya asilimia 42. Pia kumezuka tatizo la utapiamlo uliopitiliza, viriba tumbo. Nashukuru kwa Serikali kwa mikakati inayoiweka kuhusu masuala ya lishe na uhakika wa chakula Tanzania, tatizo hili bado ni tete kitaifa na hasa kwenye mikoa niliyoitaja inazalisha chakula kwa wingi. Naomba Serikali ilione hili ni tatizo la wananchi wake na izidi kulifanyia kazi na kuweka mikakati ya kutokana na tatizo hili kwa makundi yote ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya lishe ni mtambuka, watu wengine wanawake kwa wanaume, pia mna Wabunge wengi hawajui masuala ya lishe. Ombi langu kwa kuanzia hapa Bungeni na kushirikiana na Serikali masuala ya lishe, uhakika wa chakula yaangaliwe kwa umakini. Namna hii tutakuwa na Taifa la watu wenye afya nzuri na wachapa kazi, pia lishe nzuri, inasaidia kupunguza magonjwa yanayotokana na utapiamlo wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri kuwe na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Lishe na Uhakika wa Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyotekeleza miradi ya maendeleo

inayowagusa wananchi kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora, Wizara imetoa mafunzo kwa watendaji na Wakuu wa Wilaya ili kuboresha utoaji huduma kwa jamii. Ili kuendelea kutoa huduma bora na kutatua kero za wananchi, naiomba Serikali yangu sikivu iwaelekeze watendaji na wakuu hao waliopata mafunzo, kutoa mafunzo kwa walio chini yao na pia katika ngazi za chini ili viongozi hao na wananchi waweze kujua haki na wajibu wao katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo katika Jimbo langu la Singida Kaskazini ambapo vipo Vijiji viwili vya Nduamughanya na Sagara vikishindwa kutoa huduma bora kutokana na jiografia ya maeneo ya vijiji hivi. Kijiji cha Nduamughanya kilichopo Kata ya Mughunge kina vitongoji vitatu ambavyo vipo umbali wa kilometa 23 kutoka Makao Makuu ya Kijiji vilitengwa na Msitu wa Hifadhi wa Mgori una kilometa 26 ukipita Handa katika Wilaya ya Chemba. Aidha, Kijiji cha Sagara pia kina vitongoji vitatu vilivyo kilometa nne kutoka Makao Makuu ya Kijiji na vimetengwa na mlima wa kuteremka bonde la ufa na hakuna miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivyo vitongoji vyake vinaweza kusajiliwa kuwa kamili kwa maana ya Kijiji cha Mukulu kwa vitongoji vitatu vya Kijiji cha Nduamughanya na Kijiji kipya cha Gairo kwa vitongoji vitatu vya Kijiji mama cha Sagara, vijiji tarajiwa vipya viwili tayari vimekwisha jenga shule za msingi ambazo zimekwishasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya afya, tunashukuru Serikali kwa kututengea bajeti ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya. Aidha, Halmashauri ya Singida ina vituo viwili tu vya afya (Ilongero na Mgovi) ambavyo havitoi huduma ya dharura ya upasuaji kutokana na kukosa miundombinu na wataalam.

Niiombe Serikali kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya haina hospitali ya wilaya na kwa sasa inategemea hospitali ya *Mission* ya Mtinko na ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ama Hydom Mkoani Manyara. Serikali itoe kipaumbele kwa vituo hivi viwili vya afya kupatiwa fedha za ukarabati na vifaa ili kunusuru maisha ya wananchi zaidi ya 280,000 wa jimbo hili.

Mheshimiwa, Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi katika suala la elimu ya msingi na sekondari hasa katika miundombinu ya shule. Zipo shule katika jimbo langu mfano Shule ya Mikuyu iliyopo Kata ya Makuro ina madarasa mawili tu tangu watoto wa awali hadi darasa la sita na imesajiliwa na *SG* 02/2/040. Kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 476, hakuna nyumba hata moja wa Walimu, ina choo cha muda, matundu manne kwa Walimu na wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo shule ya Msingi ya Ntundu, Kata ya Kinyeto yenye wanafunzi zaidi ya 1,600 na vyumba sita tu vinavyotumika, wanafunzi wanasomea nje kwenye eneo la wazi na Mwalimu anazunguka na kibao uwanjani kufundisha. Hili hii haiwezi kuleta maendeleo kwa watoto wetu na kuongeza ufaulu. Niombe Serikali iangalie shule hizi kwa jicho la pekee kusaidia juhudi za wananchi na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie juhudi za wananchi katika ujenzi wa maabara nyingi ambazo hazijakamilika, zikamilishwe ili kuanza kutoa huduma kwa kuwa wananchi sasa wana kazi ya kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari kutokana na ongezeko la wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu ya barabara, Jimbo la Singida Kaskazini lenye jumla ya miundombinu ya barabara iliyohakikiwa ya kilometa 772.39 zimekuwa hazipitiki wakati wa mvua kutokana na zaidi ya kilometa 704.28 sawa na asilimia 91.18 kuwa za udongo. Naomba Serikali kwa kweli iweze kuongeza bajeti ili kuongeza urefu wa barabara za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Tatu, tarehe 11 tulimwomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutusaidia kujenga barabara ya kilometa 42 kwa kiwango cha lami inayounganisha Kata za Kinyeto, Kinyagigi, Merya, Maghojoa, Msange na Itaja. Mheshimiwa Rais alikubali kupokea ombi letu na niombe Serikali sasa kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2018/2019 kuanza mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa, Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hoja ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya na kukutana siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu kuhusu Chuo chetu Kikuu cha Dodoma kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kujiunga katika Chuo cha Umma baada ya kuongeza ajira ya Wahadhiri na vifaa ili waweze kujaza chuo chetu na kufikia lengo la kuwa na wanafunzi 45,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kutoa ushauri wangu kwa Serikali kutoa kipaumbele cha kwanza katika udahili wa wanafunzi na kutoa mkopo kwa wanafunzi wa vyuo vyetu vya umma. Kwa sababu hivi vyuo vilijengwa kwa fedha za umma kupitia kodi na mikopo iliyochukuliwa italipwa na umma huu wa Tanzania na kwa maana hiyo ni vizuri kujaza vyuo hivi kwanza ukizingatia tulishafanya uwekezaji mkubwa katika vyuo hivi vya umma na tunafanya mrejesho na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kutoa ushauri wangu katika usimamizi wa ubora wa elimu katika vyuo vikuu vyetu hasa ubora wa mitihani na ufundishaji kwa ujumla. Utakuta Mhadhiri anatakiwa kufundisha *topic* 12 kwa muda wa wiki14, lakini utakuta Mwalimu amefundisha *topic* mbili au tatu tu na kutoa mtihani katika *topic* hizo ili kuficha udhaifu wake wa kutokuwepo chuoni na kutofundisha kwa

muda mrefu. Pia baadhi ya Wahadhiri hawahudhurii madarasani kwa muda mrefu na kuja ama mwisho wa muda wa muhula au mwanzo wa muhula na kufundisha vipindi na mada zilizotakiwa kufundishwa kwa wiki 14, badala yake anafundisha kwa wiki moja au mbili *topic* zote kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tajwa hapo juu zinaathiri kwa kiasi kikubwa ubora wa elimu yetu kwa ngazi ya vyuo vikuu kwa sababu wanafunzi na Wahadhiri wanajali zaidi kupata cheti chenye alama za juu ili kupata ajira kwa urahisi sababu katika soko la ajira mahitaji ya soko yanaelekezwa katika wahitimu waliopata alama za juu badala ya dhamira, uelewa, utaalam, ufahamu na mahitaji. Ili kukabiliana na tatizo la kushuka kwa ubora wa elimu katika vyuo vyetu nina ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuandaa chombo cha udhibiti ubora wa elimu katika ngazi ya Vyuo Vikuu ili kukagua ubora wa elimu katika upande wa Walimu, ufundishaji, mitaala na ubora wa mitihani inayotungwa kama ina tija inakidhi mahitaji katika soko la ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuja na mpango mkakati wa kubadilisha mitaala ya elimu ya juu na chini ili ilingane na mahitaji ya sasa katika soko la ajira hasa kuwaandaa wahitimu kujiajiri wenyewe hasa mkazo kuwekwa katika elimu ya ufundi, ufundi stadi, kilimo, sayansi na elimu ya kiteknolojia na *computer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuunda Tume ya Raisi ya Elimu kama ile ya Makwetta ili kufanya tathmini ya elimu yetu hasa katika ubora wake kuanzia ngazi ya elimu ya awali mpaka Chuo Kikuu ili kubaini upungufu,,fursa na mahitaji na kuja na mapendekezo ya kuboresha ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na sio kama kwa umuhimu nirudi tena kusema changamoto zinazowakabili wananchi wenzangu wa Morogoro Kusini Mashariki

ninaowawakilisha hapa Bungeni na kuiomba Serikali kuyapatia ufumbuzi wake. Naomba Serikali kutupatia magari mawili ya wagonjwa kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais katika Kituo cha Afya Mkuyuni kinachofanyiwa ukarabati na Kituo cha Afya Kinole chenye idadi kubwa ya watu. Kwa kutoa huduma kwenye kata tatu za Kinole, Tegetelo na Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari hayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2010 kwa gari la Mkuyuni na mwaka 2014 kwa gari la Kinole na mbele ya aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na wakati huo ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kutupatia magari haya ili kuokoa vifo vya wagonjwa na hasa watoto na kwa mama. Pia naomba Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ili kufungua mawasiliano ya barabara zifuatazo:-

- Mkuyuni – Ludewa – Mgozo;
- Mkuyuni – Kibuko – Tununguo
- Mkuyuni – Luholole – Kibuko;
- Mwalazi – Kibuko – Luholole;
- Seregefe B - Kuaba;
- Seregefe A – Lubumi – Mafulu;
- Mkulazi – Mvuha;
- Mbarangwe - Kisanga Standi;
- Kwoka – Mfumbwe - Kibwaya;
- Kizinga - Kimbwala – Kwika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Mafia ipo katika hali mbaya sana. Kutokana na jiografia yake Wilaya ya Mafia hadhi yake inatakiwa iwe katika kiwango cha hospitali ya mkoa. Hii ni kwa sababu mazingira ya Kisiwa chenye changamoto kubwa ya usafiri, ukosefu wa huduma ya *x-ray*, vifaa vya maabara, Madaktari na Wauguzi kinapelekea uwepo wa adha kubwa kwa wananchi. Hivyo nikuombe Mheshimiwa Waziri kwa namna ya kipekee atupie jicho hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mafia haina kituo cha afya hata kimoja. Naishukuru Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwaajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kirongwe, kutokana na sisi kuwa na maeneo ya pembezoni nilitarajia Mafia ingekuwa katika awamu ya mwanzo ya kupatiwa fedha hizi za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaomba sana Serikali itekeleze ahadi hii kwani wananchi hususan wakazi wa Tarafa ya Kaskazini wanalazimika kusafiri masafa marefu kufuata huduma ya afya. Wananchi hawa wamefarijika sana na taarifa za ujenzi wa kituo cha hiki cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo hospitali ya Wilaya *ambulance* iliyopo ni kuukuu na inaharibika mara kwa mara. Kwa mazingira ya Mafia tunahitaji kuwa na *ambulance* mpya na ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni pamoja na Mafia kuwa Kisiwa ndani yake kuna visiwa vingine vidogo ambavyo wanaishi watu; Visiwa hivyo ni kama Juani, Jibondo, Chole na Bwejuu ambapo kuna zahanati za Serikali. Kwenye visiwa hivyo, kuna changamoto kubwa ya kuvifikia na kuna wagonjwa wanaopata rufaa ya kuja katika

hospitali ya wilaya, hakuna *ambulance boat* ya kuwaleta na kuwapeleka akinamama wajawazito, kupanda mitumbwi na vyombo vingine ambavyo si salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ametoa *boats* kwenye maeneo mengine ambayo yanaweza kufikika kwa barabara lakini kumepewa *boat*. Hivyo kwa namna ya kipekee, naomba kuwasilisha ombi la wananchi wa Mafia kutoka katika Visiwa vidogo vya Juani, Kibondo, Chole na Bwejuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu pia ni changamoto katika Kisiwa cha Mafia. Tunaishukuru Serikali tumepata shule za kata, lakini uhaba wa Walimu hususani Walimu wa sayansi limekuwa ni tatizo, tunaomba Serikali ituongezee Walimu wa sayansi ili kiwango cha ufaulu kiongezeke. Sambamba na hili ujenzi wa mabweni hususani kwa wanafunzi wasichana, kwa mfano Kata ya Kirongwe yenye shule ya sekondari Kirongwe wanafunzi kutoka Kijiji cha Jiji na Banja wanalazimika kusafiri masafa marefu karibu kilometa 10-15 kila siku jambo ambalo si salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utendaji wa *TARURA* Wilaya ya Mafia linatakiwa kutupiwa macho. Mpaka sasa barabara na madaraja katika Wilaya ya Mafia hakuna kilichofanyika, kwa mfano, barabara ya kunganisha Kijiji cha Banja na Jiji inapitika kwa tabu hasa kipindi hiki cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri Mheshimiwa Jafo kwa kazi nzuri sana ambayo amekuwa akiifanya. Pia niwapongeze Naibu Mawaziri Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege bila kumsahau Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bila malipo, nimpongeze sana kwa sera yake ya elimu bila malipo kwa sababu imesaidia vijana wengi kupata nafasi ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie changamoto katika shule za msingi katika Mkoa wa Iringa. Ukarabati wa majengo na miundombinu, majengo ya shule za msingi yana hali mbaya sana sababu halmashauri nyingi zinaweka vipaumbele katika ujenzi wa sekondari na maabara kutokana na ufinyu wa bajeti zilizopo katika halmashauri.

Changamoto nyingine katika shule hizi ni malipo ya maji, umeme na walinzi na hii inasababisha hata vyoo kutotumika. Naomba Serikali kama ilivyotoa malipo kwa ajili ya elimu iondoe pia gharama za maji na umeme mashuleni, shule zina *bills* kubwa sana wanakatiwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshwaji wa fedha katika miradi ya maendeleo katika halmashauri. Serikali iangalie miradi yenye tija katika halmashauri zetu ili iweze kuleta pesa kwa wakati katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa machinjio ya kisasa Iringa Manispaa. Mradi huu ni wa muda mrefu sana, tulianza toka 2008 unahitaji sasa 1.4 bilioni. Ni chanzo kizuri sana, mapato katika halmashauri yetu na ukimalizika utaweza kutoa ajira kwa wananchi zaidi ya 200. Ni vyema tukae na miradi michache na tuwe na miradi ya vipaumbele kuliko kuwekeza pesa kidogo katika miradi mingi ambayo inachelewa kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* naipongeza Serikali kwa kuamisha huu wakala kwa ajili ya kushughulikia barabara za halmashauri ningeomba Serikali iiwezeshe TARURA kutengewa bajeti ya kutosha ofisi, wataalam na vifaa kama magari kwa sababu pamoja kazi kubwa waliyonayo bado wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Manispaa yetu ya Iringa kuna mradi wa Daraja la Tagamenda lipo Igumbilo. Daraja hili limechukua muda mrefu sana, kuna majanga huwa kila mwaka yanatokea maafa makubwa, vifo, sababu kuna shule ya sekondari na wananchi ambao wanategemea

kutumia daraja hilo. Sasa tumeambiwa daraja hilo limehamishiwa *TARURA,* ningependa kupatiwa majibu, tulipohoji katika manispaa yetu tuliambiwa Serikali imeleta fedha ya kutosha kumaliza daraja, hilo je, ni kweli na je, daraja hilo lini litakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa mgao wa shilingi 4.5 bilioni zilizotengwa wa ajili ya hospitali zetu za Mkoa wa Iringa, Hospitali ya Kilolo, Mufindi na Iringa *DC*. Hospitali yetu Iringa Manispaa haijatengewa pesa yoyote na kuna changamoto kubwa sana ya jengo la vipimo, pia hakuna mashine za *x-ray, T-scan, ultrasound,* hakuna *ward* za kulaza wagonjwa wengine kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya mkoa. Pia tunamshukuru sana Waziri wetu, Mheshimiwa Jafo alipita na aliona hiyo changamoto. Naomba Serikali ilichukue hilo kwa uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri sana inayofanywa na viongozi wa Wizara hii na Rais wetu. Mheshimiwa Rais amekuwa mzalendo na mtu ambaye yuko tayari kufa kwa ajili ya kutekeleza kazi za kizalendo kwa nchi yake. Tumeona hatua mbalimbali alizozichukua kwa kunusuru uchumi wa nchi hata zile ambazo zinahitajika uamuzi mgumu, ni Rais mwenye maamuzi na anasimama kidete kulinda msimamo wake ambapo mara zote ni wa kizalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo ni kijana shupavu mwenye kufanya kazi kwa weledi mkubwa, mara zote anakonga nyoyo za Watanzania. Mheshimiwa Jafo hakika amejaa kwenye nafasi yake hongera sana Mheshimiwa jafo. Nawapongeza pia Manaibu Mawaziri wawili Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Kakunda, wote kwa hakika wanakonga nyoyo za Watanzania kwa uchapakazi wao. Mheshimiwa Rais ni kweli ana macho mengi kubaini wateuzi wake kuwa watendaji wanaoakisi barabara mwelekeo na kasi ya Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwa dhati ya moyo wangu Katibu Mkuu wa Wizara, Mheshimiwa Mussa Iyombe, kiongozi mzoefu wa siku nyingi kwa kazi nzuri sana anayofanya kuongoza Wizara, lakini pia kupata nafasi ya kusikiliza Wabunge katika changamoto mbalimbali, Mungu akuzidishie maisha aendelee kutoa uongozi kwa Watanzania. Mwisho, niwapongeze Manaibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana; ndugu Zainabu Chaula na Tixon Nzunda, Wizara iko vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, elimu, Wilaya ya Nkasi tumejenga vyumba vya madarasa vitatu, kila shule ya msingi kuna madarasa yapatayo 348 yote yamefikia mtambaa panya yaani yamekamilka katika ujenzi wa ukuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walihamasishwa na sisi viongozi tukiongozwa na kamanda wetu *DC* Said Mtonda, watusaidie wananchi watashindwa kutuelewa. Tunaomba watupatie fedha ili juhudi hizi ziwe na manufaa yaliyokusudiwa na nadhani Nkasi inaweza kuwa ni Wilaya ya kwanza nchini, naiomba Wizara ilipe fedha ili pia iwe na maana ya kutupongeza na kuhamasisha maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumekosa watumishi wa kutosha katika sekta ya elimu hasa shule za msingi bado Walimu hawatoshi hasa maeneo ya mwambao mwa ziwa, Kata za Kala, Wampembe, Kizumbi na Ninde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nyumba za Walimu hazitoshi kwenye shule za msingi na sekondari pia tunaomba fedha ili watumishi hawa muhimu wapate mahali pa kuishi ili watulie kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini wamejitahidi kujenga maabara katika sekondari zote na sasa yamebaki magofu, watusaidie kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa maabara ili pia majengo yatumike kupata wataalam wa sayansi kama Walimu wa Waganga na wataalam wa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, fedha za miradi kwenye halmashauri yetu hazijakuja hasa kwa miradi iliyopitishwa mwaka jana. Fedha iletwe haraka kukamilisha miradi iliyopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kilimo, kwa Mikoa wa Nyanda za Juu Kusini msimu wa kilimo huanza Oktoba kumbe pembejeo zifike Agosti kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Mawakala wa mbolea wapewe masharti ya kufikisha pembejeo kwenye mikoa ya uzalishaji siyo kurundika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, Serikali itenge fedha kwa ajili ya *top up* kuwezesha bei za pembejeo zisibadilike badilike katikati ya msimu kutokana na mabadiliko kwenye bei ya dunia ili kutoleta usumbufu kwa wananchi. Hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, wananchi wa Vijiji vya Kaso, Milundikwa, Kisura na Malongwe wameathirika sana na ujio wa jeshi ambapo ardhi yao waliyopewa kihalali na nyaraka zipo wamenyang'anywa. Naishauri Serikali kuliangalia jambo hili vizuri na Mheshimiwa Waziri naomba amwagize Mkuu wa Mkoa akafanye tathmini ili kuona hali iliyojitokeza zaidi ya watu 5,000, hawana pa kulima kabisa na ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, naomba gari ya kusaidia kazi ofisi ya kilimo ambao hawana fedha kabisa za kufanya matengenezo ya mara kwa mara gari yao mbovu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya hali ya huduma za afya kwenye zahanati zetu siyo nzuri kwa tatizo la ukosefu wa watumishi hatuna Waganga, Manesi na watumishi wengine. Tunaomba watusaidie kupata watumishi, zahanati nyingi zinaendeshwa na Wauguzi. Wananchi kujenga zahanati katika Vijiji vya Kautawa, Kipande, Kalundi, Mkomanchimbo, Mlambo, Tundu, Kisambara, Ifundwa, Nchenje, Ntuchi na

zinginevyo, watusaidie kumaliza zahanati hizi. Wananchi pia wanajenga Vituo vya Afya vya Kasu Kala, Kate na Ninde. Tunaomba kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana kuona Serikali imeweka kwenye bajeti yake, ujenzi wa hospitali ya wilaya, nampongeza kwa hatua hiyo, lakini nashauri kutekeleza ujenzi kwa mtindo wa *force account, impact* itaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari ya wagonjwa Wilaya ya Nkasi ina majimbo mawili, gari mbili zimetolewa kwa jimbo moja, mimi sijapata jambo hili halina afya kwa siasa za jimbo. Naomba gari moja Kala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji, jimboni ina kasi ndogo, mwanzo kazi zilikuwa zinaenda vizuri, lakini kwa sasa kazi yake imepungua sana Serikali itoe usimamizi zaidi kwa miradi yote ya maji ikiwepo ya Kisura, Kawa, Mpasa na Isake ili kasi iongezeke na rasilimali zitumike kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* hawana gari ya *supervision*, hawana fedha ya kutosha kwa matengenezo ya dharura, hali siyo nzuri barabara zifuatazo zimefungwa na zingine kupitika kwa tabu kabisa, barabara hizo ni:-

Barabara ya Kitosi- Wampembe kupitika kwa shida na daraja la Kizumbi limekatika na hakuna fedha. Barabara ya Ninde- Kala inapitika kwa shida sana makalvati yamekatika hakuna matengenezo na fedha hakuna. Barabara ya Namanyere- Ninde ijengwe ili kunusuru fedha iliyotumika kujenga madaraja na makalvati, lakini pia kufungua Kata ya Ninde iliyoko kandokando ya mwambao mwa Ziwa Tanganyika.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi sana kwa Waziri Mheshimiwa Jafo pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ujumla.

Nashukuru kwa fedha ya Kituo cha Afya cha Mkoli na kuwekwa kwenye bajeti kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Nyasa kwa kutengewa bilioni 1.5. Naamini zitatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupatiwa Madaktari kwenye Wilaya yangu. Naomba nimpongeze sana Dkt. Aron Hyera, *Ag. DMO* kwa kazi nzuri ambayo mimi binafsi naridhika nayo pamoja na wenzake ambao wapo katika Wilaya ya Nyasa. Naamini kuna siku atapitishwa kuwa kamili, mnyonge mnyongeni haki yake apewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyasa kupitia Kituo cha Afya cha Mbamba *bay* wameweza kuokoa maisha ya mama na mtoto; upasuaji 231 mpaka *last week, operation* nyinginezo 87 kuanza tarehe 19 Mei, 2017. Si kawaida sana lakini imewezekana, ubunifu unaofanyika ni mkubwa tumepoteza mama mmoja tu na sababu ni kuwa alicheleweshwa nyumbani hivyo kwa niaba ya wananchi wa Nyasa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuomba uboreshaji kituo cha Afya cha Lipelambo kipo mbali sana takribani 130 *kilometres (isolated);* Kukamilishwa kwa jengo la utawala Kituo cha Afya cha Kuhagara pamoja na kupata wodi; na Kukamilisha majengo ya Kituo cha Afya cha Chiwanda na Ntipwili ambayo yalijengwa na wananchi angalau yaweze kutumika kama zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumalizika jengo la utawala la mbamba *bay secondary school;* kuweka kwenye mpango ujenzi wa Kituo cha Afya Kingerikiti ili kuendelea kupunguza umbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wangu hauwezi kukamilika kama sitawashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Mbunge, Waziri wetu Mkuu, kwa kazi kubwa na nzuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba pia kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja jimboni kwangu, kama nilivyomnakilisha Naibu Waziri Mheshimiwa Josephat Kakunda aliyeongozana naye na kutoa maagizo kwa Mkuu wa Mkoa kuhusu wodi *Grade A*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa pongezi za dhati kwa Waziri na Manaibu Mawaziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia eneo la huduma za afya, Wilaya ya Wanging'ombe imepata fedha za kukarabati Kituo cha Afya cha Wanging'ombe milioni 300 na Kituo cha Afya cha Palangawanu milioni 100. Naomba Serikali itoe fedha milioni 300 ili kukamilisha kazi ambayo kwa sehemu kubwa imefanywa na nguvu za wananchi. Jengo la kituo cha afya na maabara vimeezekwa, jengo la mtumishi kuta zimekamilika, jengo la upasuaji limefikia usawa wa jamvi, jengo la wodi ya wazazi limefikia usawa wa jamvi na jengo la *mortuary* limefikia usawa wa kuezeka. Ni matumaini yangu Serikali haitaacha kazi hii kubwa bila kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya hii ina tatizo kubwa sana la huduma za afya. Viko vituo viwili tu vya afya vinavyofanya kazi, hatuna hospitali ya Wilaya ya Serikali. Kwa hiyo tukipata msaada wa kukamilisha Kituo cha Palagawanu kitapunguza tatizo hili. Wilaya inayo maboresho ya zahanati na vituo vya afya ambavyo tumeahidiwa fedha za miradi viporo ili kukamilisha Zahanati za Katenge, Ng'anda, Ivigo, Mtapa, Kanomelenge na Kituo cha Afya cha Igagala hakijaletewa fedha za kukamilisha zaidi ya miaka sita. Naomba pia Serikali itoe fedha za kujenga hospitali ya wilaya ambayo kwa miaka minne tumekuwa tumepangiwa fedha lakini fedha haziletwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la elimu, naomba Serikali isaidie kuboresha Shule ya Sekondari ya

Makoga na Wanike ili zisajiliwe kuanza kwa kidato cha V na VI. Wilaya hii imeweza kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kutumia mkandarasi, lakini nyumba mbili zilizokabidhiwa *TBA* toka mwaka 2012 mpaka leo ziko hatua ya msingi na kazi imesimama. Nyumba hizo ni kwa ajili ya makazi ya Mkuu wa Wilaya na Afisa Tawala. Mkuu wa Wilaya anaishi nyumba ya kupanga toka Wilaya hii ilipoanzishwa 2011. Naomba Serikali itoe kibali kwa kutumia utaratibu wa kuajiri wakandarasi ili viongozi hawa waishi kwenye nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na kutegemea maombi yangu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe yatazingatiwa.

**MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha na mimi kutoa mchango wangu kwa maandishi katika Wizara hii nyeti ya TAMISEMI. Nianze kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kujitoa kwake mhanga kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu kwa namna ambavyo amekuwa anafanya kazi usiku na mchana kumsaidia Mheshimiwa Rais. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Seleman Jafo pamoja na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Joseph Kakunda wanafanya kazi kweli bila kuwasahau watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua na kuzithamini kazi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kufika kuwaelekeza na kuwaongoza Watanzania katika uchumi

utokanao na viwanda. Viwanda ni matokeo ya mambo mengi moja ya mambo yatakayowawezesha Watanzania kuumiliki na kuuendesha uchumi wa viwanda ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira bora ya kufundishia na kujifunza ni suala lenye umuhimu wa kipekee kwa wakufunzi na wanafunzi. Nafahamu wakati mwingine rasilimali fedha huwa chache lakini niombe Wizara ya TAMISEMI iangalie kwa jicho la kipekee Shule ya Sekondari ya Kalanga. Shule hii ina uchakavu mkubwa mno wa majengo kiasi ambacho Walimu, wafanyakazi na wanafunzi wakiyaona mawingu yenye dalili ya mvua mawazo yao yote hujielekeza katika kufikaria usalama wao pindi mvua itakaponyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee niiombe Wizara iinusuru shule hii. Pili, naomba niishauri Serikali katika eneo hili la uimarishaji miundombinu ya shule, Serikali iangalie uwezekano wa kutenga na kutumia fedha nyingi katika mambo machache kwa mwaka husika na kisha kuhamia katika masuala mengine. Nionavyo mimi hali hii itaweza kutatua changamoto nyingi za jambo moja kwa kipindi kimoja cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri Jafo apatapo nafasi aje atembelee Shule hii ya Sekondari ya Kalanga iliyopo katika Kijiji cha Kalanga ambayo iko umbali wa kilomita saba tu kutoka Iringa Mjini na itampa fursa pia ya kujifunza mengi ikiwemo utajiri uliolala wa historia ya Wahehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya. Natoa shukrani zangu kwa kazi zifuatazo:-

(1) Kutoa fedha za jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalamo;

(2) Kutoa fedha za uboreshaji wa Kituo cha Afya Kinyambuli (Tshs. 400m);

(3) Ujenzi wa Shule za Msingi (Kitumbili, Senene *(TBA)*, Kibololo *(TBA),* Isanzu Secondary, Iguguno *High School*); na

(4) Kuleta wafanyakazi wa kada ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru kutengwa kwa Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Pamoja na pongezi hizi naishauri Serikali kuona namna ya kutanzua changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; naomba idadi ya watumishi waongezwe. Naomba Wizara isimamie kwa karibu shilingi bilioni 1.5 za Hospitali ya Wilaya, Wizara imekuwa mbali na miradi hii ambayo inagharimu pesa nyingi Serikali. Pia tunaomba *ambulance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; miundombinu ya baadhi ya shule ni hafifu na haitoshelezi, naomba zipatikane pesa kusaidia wilaya mpya ya Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi; tunaomba gari la ukaguzi, kwani ufaulu wa shule za msingi umeshuka kutokana na kutokuwepo ukaguzi *(both)* Waratibu wa Kata pamoja na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara *(TARURA);* baadhi ya maeneo ambayo ni muhimu kwa uchumi wa wilaya na Taifa hayafikiki. Tunaomba fedha za barabara Msingi – Yulansoni – Lyelembo, kilometa 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na tunawaombea mfanye kazi yenu nzuri.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye Wizara tajwa hapo juu. Niishauri Serikali kwamba, iachane na mradi wa Bwawa la Lukuledi

na badala yake iongezee nguvu Idara ya Maji ya *MANAWASA* ili iweze kufikisha maji safi na salama kutoka Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la elimu bure. Suala hili liangaliwe kwa umakini, elimu bure imeshindwa kuangalia suala la *quality* badala yake inaangalia *quantity.* Kuna haja gani kufurahia idadi kubwa ya wanafunzi, lakini Walimu huna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vituo vya afya na zahanati. Bahati mbaya sana kumekuwa na utata mkubwa juu ya ramani, Serikali iseme wazi kabisa juu ya suala hili, wananchi wanahitaji jengo la kupatia huduma. Pale Serikali itakapopeleka pesa basi ndipo ramani hizo zitumike, wananchi hawawezi kukamilisha na kupata huduma, ndiyo mahitaji. Nishauri kwamba, ramani ziendane na mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa sana la madeni ya wazabuni ambao walitoa vyakula na huduma mbalimbali kwenye shule na vyuo. Watu hawa wengine mpaka wamekufa kwa *pressure,* tuwalipe wazabuni hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wilaya ya Masasi. Zimetengwa pesa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya. Nataka kufahamu kazi hii itaanza lini na itafanyika wapi?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzipongeza sana hotuba nzuri sana zilizotolewa na Mawaziri wetu wa Nchi, Mheshimiwa Suleiman Jafo na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika. Mawaziri hawa mahiri wanafanya kazi nzuri sana, wao pamoja na wasaidizi wao wote. Hivyo, naunga mkono hoja zao zilizo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mwanga ina baraka ya kuwa na milima mirefu katikati ya wilaya na tambarare mbili; moja Mashariki ya Milima katika Ziwa Jipe

na moja Magharibi ya Milima ulipo Mji Mkuu wa Mwanga na Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Wilaya iko Usangi juu kabisa milimani. Awali mwaka 1980 tulipopewa hadhi ya Wilaya ya Mwanga, kilichokuwa Kituo cha Afya Usangi kilipandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya, lakini tangu kipandishwe hadhi, hakijafanyiwa ujenzi na ukarabati ili kifikie kiwango cha hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waziri wangu Mheshimiwa Suleiman Jafo; atume timu ya wataalam wafanye mahitaji halisi ya Hospitali ya Wilaya ya Mwanga iliyopo Usangi. Baada ya *assessment* hiyo aiunganishe hospitali hii kwenye vituo vya afya vinavyoboreshwa na *World Bank* ili itengenezwe, ipanuliwe na ipatiwe vifaa stahiki kama hospitali nyingine za wilaya. Tupatiwe Madaktari na wafanyakazi stahiki ili Hospitali ya Wilaya ya Mwanga ifanye kazi kama hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya TAMISEMI ihakikishe kuwa viongozi wote wa Idara ya Afya (15) waliohamisha ofisi zao toka Hospitali ya Wilaya Usangi na sasa wako Ofisini kwa Mkurugenzi wa Wilaya *(DED)* Mjini Mwanga, warudi hospitalini wakatoe huduma ya afya kwa wananchi badala ya kuwa Makarani wa *DED.* Uamuzi huu ulifanywa na *BMW,* lakini uamuzi haujatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na watendaji wenzake kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii. Hata hivyo, napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ugatuaji wa madaraka *D by D* halitekelezwi inavyopaswa kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara hii, ningependa kufahamu ni wapi wanapokutana kuweka masuala ya elimu

sawa? Hizo hati idhini walizonazo zinawakutanisha kwenye masuala gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano suala la Walimu wa Shule za Sekondari kuhamishiwa katika Shule za Msingi ni mambo gani wamejadiliana na Wizara ya Elimu, hususan, suala la mafunzo *(Induction Course)* kwa Walimu hawa? Nani atatoa mafunzo ya *Child Centered Psychology* ambayo ni kipaumbele kwa Walimu hawa kwa kuwa, tunafahamu kwamba, Wizara ya Elimu ndio mtoaji wa mafunzo? Je, Wizara imeshawaandalia fedha zao za uhamisho au posho ya usumbufu? Mheshimiwa Waziri anapohitimisha atuambie ni nini watakachokitekeleza kwa Walimu hawa hasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa Walimu shule za msingi na Walimu wa sayansi kwa shule za sekondari. Tatizo hili ni kubwa, katika Mkoa wa Iringa hadi 2017 kulikuwa na upungufu wa Walimu shule za msingi 785, kwa Walimu wa sekondari sayansi mahitaji yalikuwa 1,290, waliopo 619, upungufu Walimu 671. Tatizo hili ni kubwa, hivyo nashauri Wizara iajiri Walimu wa kutosha na wapelekwe hasa shule zilizopo vijijini na wapewe motisha ya mazingira magumu ya ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya; kuna tatizo ama upungufu wa watumishi katika sekta hii, hasa kwa Mkoa wa Iringa katika zahanati na vituo vya afya, Wilaya ya Kilolo na Iringa Vijijini hasa. Naiomba Serikali iajiri watumishi hawa na kupelekwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara, *TARURA.* Hiki ni chombo muhimu sana, lakini kina changamoto ya uhaba wa fedha. 30% wanayopata ya fedha ni kidogo sana kukamilisha miradi. Naungana na maoni ya Kamati kuongeza hadi angalau 50% ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba barabara inayounganisha Wilaya toka Iringa Manispaa kupitia Jimbo la Kalenga, Kata ya Luhota na Magulilwa kwenda Wilaya ya Kilolo ambazo ni kilometa chache tu zitengewe bajeti na

kujengwa kwa kiwango cha lami kwani kuna wafanyabisahara na wakulima wa mazao mbalimbali kama vile matunda, mahindi, njegere. Miti ambayo inazalisha mbao hupata tabu kupita katika barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na maoni ya Kamati kuhusu suala la kuwasilisha Bungeni Muswada wa kusudio la kutunga sheria itakayosaidia kusimamiwa utengaji, utoaji na urejeshaji wa fedha zinazotokana na 10% ya mapato ili kuwezesha wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la kuondoa kodi au kupunguza kodi kwa taulo za kike ili kuwezesha watoto wa kike hasa kutoka katika familia maskini kumudu gharama hizo na kuweza kuhudhuria masomo kikamilifu na ikiwezekana wapewe bure kama ilivyo katika nchi za Kenya, Shelisheli na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora. Kumekuwa na kawaida katika Awamu hii kutoongeza mishahara kwa wafanyakazi wakati maisha kila siku yanapanda kwa gharama za bidhaa. Wafanyakazi wengi hawana raha kwa kutokuweza kukidhi mahitaji na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi. Serikali iweze kupandisha au kuongeza mishahara kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukiukwaji wa sheria na taratibu. Mfano Mkurugenzi kutotii mamlaka ya Waziri mwenye dhamana mfano Mkurugenzi wa Tunduma Mkoa wa Songwe, Mkuu wa Wilaya na wengineo wateule wa Rais kutofuata taratibu. Hii ni kinyume kabisa na utawala bora tunaotarajia, Serikali ilifanyie kazi suala hili ili wananchi wapate haki yao ya kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya ya kuweza kuhudhuria Bunge letu. Namshukuru Mungu kwa kutupa Rais mwadilifu mwenye mapenzi mema na wananchi wake na

Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na Baraza la Mawaziri wachapa kazi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo na Manaibu wake, Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kandege. Binafsi natoa shukrani za pekee na za unyenyekevu kwa Rais na Baraza zima la Mawaziri kwa jinsi walivyotekeleza miradi ya maendeleo mikubwa Ileje ambayo ilisahauliwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI. Shukrani kwa Mungu. Pongezi kwa Serikali ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Baraza lote la Mawaziri kwa mipango ya maendeleo mikubwa inayotekelezwa kwa ufanisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pongezi kwa ajili ya Ileje. Kwa heshima ya kipekee na kwa niaba ya Wanaileje napenda kuishukuru Serikali kwa mambo makubwa iliyofanya kuleta maendeleo Ileje. Napenda kupiga magoti kutoa shukrani za dhati kwa kuiwezesha Ileje kuinuka, kujulikana na kutambulika. Ileje sasa hivi inaonekana, barabara iliyopigiwa kelele kwa zaidi ya miaka 40 imepata mkandarasi yuko *site* na barabara itajengwa kwa kiwango cha lami kilometa 58, inategemewa kumalizika 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha ya kujenga vituo vya afya viwili, Kituo cha Lubanda ambacho Mheshimiwa Waziri wa Afya mwezi uliopita alitembelea na Kituo cha Ibaba. Hii itatusaidia sana kupunguza athari zilizokuwa zinawapata wananchi kwa sababu ya jiografia na miundombinu na Ileje hizi ni kata ambazo hazifikiki kwa urahisi na ziko mbali sana na hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha ya kujenga hospitali ya wilaya na inajengwa kwa kiwango cha asilimia 75, imesimama kwa miaka mitatu, lakini nashukuru kuwa nina taarifa kuwa, tumetengewa fedha ya kumaliza ujenzi wa hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje ilipokea fedha kwa ajili ya kukarabati shule kongwe na miradi mikubwa ya maji na

masuala ya upimaji viwanja Ngulilo, Ilulu, Izuba. Kupitia Ofisi ya Mbunge nilitafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* kutoka Balozi wa Japan. Chuo kimejengwa na nashukuru kuwa, Serikali imekubali kukichukua chuo hicho na kukimalizia na kukiendesha.

Tunaishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo kwa mwaka mmoja uliopita hadi sasa tumetembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyeweka jiwe la msingi na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri kwa nyakati mbalimbali. Naamini huu ni ugeni mkubwa sana uliowahi kutokea katika historia ya Ileje. Hii, ilitutia moyo sana, lakini iliwawezesha Waheshimiwa viongozi hawa kujionea wenyewe changamoto na fursa za Ileje na kwa hivyo, kujua jinsi gani Ileje isaidiwe. Tunawaomba Mawaziri wengine wote watembelee maeneo yote ya pembezoni ili kujionea changamoto zao na kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote hizo nyingi na shukurani za unyenyekevu kwa miradi mikubwa ya maendeleo, yapo mambo machache ninayotaka kuiomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi. Tutashukuru kama fedha iliyotengwa kwa hospitali ya wilaya itatolewa mara moja ili huduma hii muhimu ya afya wilayani iimarike na tuache kupeleka wagonjwa Malawi maana Mbeya ni mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje ni Wilaya ya mpakani mwa Tanzania na Malawi na kwa sehemu ndogo Mashariki Kusini na Zambia. Mpaka wenye umbali wa kilometa 108. Kwa hiyo, ni mpaka mrefu na wilaya yetu haina kituo cha mpakani madhubuti na mpaka wetu ni Mto Songwe. Kwa hiyo, tunaomba uhitaji mkubwa na wa haraka wa gari la doria kwa ajili ya kudhibiti mpaka wetu. Wahamiaji haramu wengi wanapitia Ileje kuingia Malawi kuelekea Afrika Kusini na imefikia hadi upande wa Malawi kuanzisha Kituo cha Wakimbizi kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2015, *TRA* walionesha haja ya kujenga kituo cha mpakani na tayari

wameshapata eneo la kutosha Isongole, karibu kabisa na mpaka. Umuhimu wa mpaka huu ni mkubwa na hasa ikizingatiwa suala la usalama, lakini pia, kiuchumi na biashara za mipakani. Kwa kuwa, Barabara ya Mpemba – Isongole inajengwa itaunganisha Tanzania na nchi jirani ya Malawi na kituo hiki kitapunguza msongamano wa Kituo cha Tunduma na kuwezesha magari ya mizigo na abiria mengine kupitia upande wa Ileje hasa kwa yale yanayotokea Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizopo ni kuwa barabara ya Chilipa kutokea Ileje ni tambarare zaidi kulinganisha na ya Kasumulo kwa hiyo, madereva wa mizigo wangeweza kuitumia kwa urahisi zaidi. Vilevile Malawi na Tanzania tuna biashara kubwa na kituo cha forodha kitawezesha kukinga mapato mengi na kusimamia ubora wa bidhaa zinazopita hasa za mazao na mifugo kuzuia magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaipongeza Wizara kwa ubunifu wa kuhamisha Walimu wa masomo ya sanaa kutoka shule za sekondari kwenda kujaza nafasi shule za msingi, zoezi hili kama ilivyo kwenye wilaya nyingine chache, kwa Ileje limezua malalamiko kwa Walimu 83 walioguswa nalo na kuleta mgongano kwa kuwa, kuna imani kubwa kuwa zoezi limetumika kukomoa Walimu wanaoonekana kuwa wakorofi na kuhamisha wale ambao wana *degree* hadi *masters* na kuwaacha wenye stashahada kama agizo la Serikali lilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi baada ya kuahidiwa malipo, hii inabadilika, kufuatia Walimu walioitwa mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama na kuhojiwa kwa vitisho. Zoezi la kawaida limegeuka kuwa vita kwa sababu, ya jinsi lilivyotekelezwa na Mkurugenzi wa Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira umesimama kwa miaka zaidi ya nane na pamoja na *STAMICO* kuruhusu hakuna kinachoendelea kwa uhakika. Mwaka huu tulielezwa kuwa, uzalishaji wa majaribio umefanywa, lakini hatujajua kama unaendelea na kwa

utaratibu upi kwa sababu, mpaka sasa hatufahamu mwekezaji ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hatupewi taarifa juu ya taratibu za uhamishaji mgodi toka mwekezaji aliyeshindwa na *STAMICO* kama umekamilika ama vipi na suala la ubora wa makaa na matumizi kusudiwa. Wananchi wa Ileje wangependa kufahamu maana mgodi huu ni tegemeo lao kwa ajira na mapato kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile daraja la mgodini Kiwira kutoka barabara ya Mto Mwalisi linahitajika kujengwa ili kuepuka usumbufu wa kupitia Wilaya ya Kyela kuja Ileje, umbali wa kilometa 36 wakati daraja linalohitajika ni kilometa saba tu kuufikia mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi za ndani ya Ileje zinazounganisha kata zinashindwa kujengwa kwa sababu ya ukomo wa bajeti. Changamoto ipo katika barabara zinazounganisha vijiji na vijiji, mfano, madaraja matatu kutoka Kijiji cha Bwenda kuja Makao Makuu Kata ya Lubanda mpaka uzungukie Kata nyingine ya Luswisi. Daraja toka Kata ya Ibaba kuunganisha Kata ya Ngalilo kupitia daraja la Shilinga lingesaidia kuwaunganisha wananchi na wilaya na mkoa wao lakini hawa wametengwa kwa kukosa daraja hili. Daraja la Kajeshi kuunganisha Sekondari ya Bupogo, daraja la Bupigu kwenda Chongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaliziaji wa zahanati pamoja na Mfuko wa Jimbo haujakamilika. Upungufu wa watumishi ni mkubwa sana Idara ya Afya na ukamilishaji wa vituo vya afya, zahanati na hospitali ya wilaya kutahitaji watumishi wengi zaidi. Vyoo mashuleni pamoja na Mfuko wa Jimbo bado kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu Sekondari na Msingi; kuna upungufu wa Walimu 50 na 482; Uchakavu wa miundombinu ya madarasa na nyumba za Walimu ambayo mengi yalijengwa kwa udongo muda mrefu; Ukosefu wa gari la Idara ya Elimu Msingi; na Upungufu wa matundu ya choo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo kuna kuchelewa kwa pembejeo na Ukosefu wa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji. Upungufu watumishi idara ya maji na vitendea kazi kwa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maji. Kukosekana kwa chujio la maji kwa Mradi wa Maji Humba – Isongole kunafanya tuendelee kupata maji yenye matope na kwa hivyo, siyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotolewa fedha yote ya miradi ya maendeleo na kwa wakati kunaathiri sana miradi ya maendeleo na kuchelewesha maendeleo ya wilaya ambayo tayari imekuwa nyuma kimaendeleo muda mrefu kwa sababu, miradi mingi inawekwa kwenye bajeti kila mwaka bila utekelezwaji. Serikali itoe kipaumbele kwa wilaya za pembezoni na hasa zenye mvua nyingi ili zipatiwe fedha ya kutosha kwa ukarabati wa barabara za vijijini katika wilaya hizi ili ziweze kutumika kwa mwaka mzima kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya wilaya hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inasifika sana kwa utawala bora na tunaishukuru sana Serikali kwa kusimamia utawala bora na amani na utulivu mkubwa. Ziko nchi zinazotuzunguka ambazo hata kwenda kukutana na Waziri utoe rushwa? Pia mishahara inalipwa kwa kubahatisha, nchi zina rutuba lakini uzalishaji hakuna na wanaishia kutegemea nchi jirani. Amani haipo na mifumo yote imevurugwa. Sisi Tanzania tuna kila kitu, tunaomba sana watendaji wachache wanaotuvurugia utawala bora hasa Wakurugenzi na wale wasiozingatia maadili basi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu ili iwe mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje tuna Mkurugenzi ambaye amevuruga sana Madiwani, Walimu, Watendaji chini yake na hata wananchi tumeshatoa malalamiko kwa Waziri Mkuu na kwa Waziri wa TAMISEMI. Tunaomba wamwelekeze aache au kwa kuwa, uwezo wake ni mdogo basi atafutiwe atakapoweza kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwenye Wizara ya TAMISEMI ambayo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu. Maana ndio Wizara inayoratibu utendaji wa Wizara nyingine kwenye ngazi ya halmashauri na tawala za mikoa, lakini tumekuwa tukishuhudia baadhi ya utendaji usioridhisha na hivyo kukwamisha shughuli za maendeleo katika halmashauri zetu na Taifa kwa ujumla. Ni Wizara ambayo inahitaji kupewa kipaumbele na kuhakikisha bajeti tunazoziweka zinatolewa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, halmashauri zetu zina rasilimali watu wenye uwezo na kazi walizopewa au wanawekwa tu kwa itikadi za vyama ili kulinda maslahi ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala. Maana tumeona watendaji wengi wanakaa kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi na sio wananchi wote kwa ujumla bila kujali vyama vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia kuporomoka kwa elimu yetu huku ikichangiwa na mambo mengi. Mojawapo ni uhaba wa madarasa, vyoo, nyumba za Walimu, maabara zisizo na vifaa vya maabara, ofisi za Walimu, kupandishwa madaraja Walimu ili waweze kuwa na motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Waziri ukurasa wa 38 ameonesha kuwa tuna vyumba vya madarasa 123,044 ambapo kwa mwaka wa fedha 2,278, idadi ambayo ni ndogo sana na bado imeonesha changamoto ya upungufu wa madarasa kuwa ni 264,594. Kwa kasi hii tunahitaji miaka 116 ili kujenga hii na ikumbukwe tunavyosonga mbele *population* inaongezeka na idadi ya ya vyumba vilivyojengwa mwaka 2017/2018 havitajengwa kwa miaka ijayo kwa kuwa wananchi wamepunguza kasi ama wameacha kuchanga kufuatia kauli tata za viongozi. Mheshimiwa Rais alisema hamna michango mara Mawaziri wakasema ichangiwe kupitia *DED.* Leo hii tunaendelea

kushuhudia wanafunzi wakisoma hadi 200 kwenye darasa moja, kinyume na sera ya elimu kwa darasa moja kuwa na wanafunzi 45, lakini hata idadi ya Walimu kwa wanafunzi, wanafunzi kwa kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeendelea kushuhudia jitihada za wananchi kama wale wa Jimboni kwangu Tarime Mjini wakijitolea sana kujenga madarasa na shule, lakini wanazuiliwa kuendelea kwa sababu za mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri husika afike Shule ya Msingi Mturu iliyopo Uwanja wa Ndege Tarime Mjini ambao walikuwa wameshajenga madarasa sita na ofisi, lakini wamezuiliwa kwa sababu zisizo za msingi kwa sababu mmiliki wa lile eneo hana shida na ni mtu binafsi ambaye alipata eneo kinyume cha taratibu, lakini pia alishindwa kuendeleza kwa zaidi ya miaka thelathini. Tunaomba sana, tumejitahidi sana na wananchi wangu wana ari kubwa ya kujenga vyumba vya madarasa, vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna upungufu wa Walimu, nyumba za Walimu wanakaa mbali na wanaishi mbali na shule na wanatumia fedha zao kwa nauli na makazi, lakini wakati wa mvua wanashindwa kufika. Kingine ni motisha kwa Walimu hawa haipo kabisa, wanafundisha katika mazingira magumu sana; kutopandishwa madaraja, madeni ya likizo, nyumba za kulala, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa sekta ya afya tuna changamoto juu ya hospitali ya wilaya inayohudumia Wilaya tatu, Serengeti, Rorya na Tarime Halmashauri ya Wilaya, lakini unapofikia muda wa mgawo hii hospitali inakuwa *treated* kama hospitali ya mji inayohudumia wakazi wa Tarime Mjini tu. *Mortuary* yetu ni ndogo sana, *Basket Fund* tumepata shilingi milioni 11, wakati Kituo cha Nyarwana wanapata shilingi milioni 42. Hii si sawa na hata Waziri nilimweleza hili. Tunaomba sana watuongezee fedha pamoja

na vifaa pamoja na Wauguzi. Hili ni tatizo kubwa sana na linasababisha upungufu wa dawa kwa sababu ya kupewa dawa ndogo kwa idadi ya halmashauri ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni vituo vya afya katika mgawo wa shilingi milioni 500 sikupata, kwenye shilingi milioni 400 hatukupata, pamoja na kwamba tuliomba, hii si sawa kabisa. Tunahitaji ku-*upgrade* zahanati ya Magena kuwa Kituo cha Afya, Zahanati ya Gamasara kuwa Kituo cha Afya na kile kituo ambacho Kata ya Kenyamayoni wananchi wameanza kujenga, lakini hatujapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana waangalie jiografia ya utoaji huduma, bado hizo zahanati zinatoa huduma kwa Kata za Jimbo la Rorya na Tarime Vijijini, mfano Gamasara, Nkerege inatoa huduma Kata za Tarime Vijijini.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Pili, nichukue nafasi ya kipekee kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Selemani Jafo kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwatumikia Watanzania wote bila ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza miradi ya Sekta ya Afya hasa katika kufanikisha kunipatia fedha za Vituo vya Afya vya Karema, Mwese na Mishamo; zaidi ya hayo, ni kutenga fedha za Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika. Pia nitoe shukrani kubwa kwa kunipatia gari ya *ambulance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo naomba sana Serikali itusaidie, ni kutupatia magari ya Sekta za Elimu katika Wilaya ya Tanganyika, Ujenzi na Afya. Kuna tatizo kubwa kwani Halmashauri ya Mpanda *DC* haina magari kutokana na halmashauri hii kuwa mama wa halmashauri zote zilizopo Mpanda, hivyo kupelekea kila halmashauri iliyogawanywa kuchukua magari kutoka halmashauri mama na matokeo yake halmashauri hii haina magari ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uhaba wa Walimu; naomba tatizo hili liangaliwe sana hasa katika maeneo ya pembezoni ambako hakuna kabisa walimu hasa wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la barabara za vijijini ambazo zinahudumiwa na *TARURA;* tunaomba eneo la Mishamo lipewe *budget* ya kutosha, kwani eneo hili lina barabara kiasi cha kilometa 1008 ambazo *TARURA* pekee kwa bajeti inayotengwa haiwezi kutekeleza. Hivyo, tunaomba maombi maalum ya kutenga fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji, hasa katika shule na kwenye zahanati tunaomba iangaliwe na kusimamiwa ili iweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Korogwe Mjini; mpango mkakati wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe ulikuwa kujenga hospitali ya wilaya na kwa taarifa tulitengewa bilioni 1.5 lakini zimeondolewa na kupewa Korogwe Vijijini. Nimeridhika na maelezo ya Waziri kwamba imefanyika kwa nia njema baada ya kuona ipo Hospitali ya Wilaya Korogwe Vijijini kwenye Kata ya Magunga iliyopo mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niombe unapohitimisha utamke wazi ndani ya Bunge kauli ya kukabidhi hospitali hiyo ili wananchi wa Korogwe Mjini wapate kusikia mabadiliko haya na kuzipeleka fedha, bilioni 1.5, Korogwe Vijijini ili kuondoa mkanganyiko uliopo. Hata hivyo, niiombe Wizara kunipoza kwa kunisaidia kunipatia fedha kwa ajili ya ujenzi na vituo vya afya; kata zilizo mbali na mji zina shida kubwa ya huduma ya afya nazo ni Kata ya Kwamsisi yenye vijiji sita na Kata ya Mgombezi vijiji vitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru Mheshimiwa Waziri akinisaidia ili wananchi hawa wa vijiji hivyo waweze kupata huduma nzuri.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa hongera kwa kazi nzuri Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, pamoja na Naibu Mawaziri. Pia naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; Ripoti ya *CAG* inaonesha hati safi kwa zaidi ya asilimia 90 ya halmashauri zote nchini. Jambo hili lisitufanye kudhani kwamba hata miradi inakwenda vizuri kwa zaidi ya asilimia 90. Hii ni kwa sababu mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* nimeshuhudia miradi iliyoripotiwa na Ofisi ya *CAG* kwamba imekamilika na inatumika sivyo ilivyo, kwani haitumiki kutokana na kutokamilika ipasavyo. Kimsingi miradi yote miwili ya maji tuliyoikagua Mkoani Tabora ilikuwa haitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Wakurugenzi na watendaji wahimizwe na wawezeshwe kutembelea miradi ya maendeleo vijijini na katika maeneo yao ya utawala ili kusimamia miradi kwa ufanisi. Vilevile, Ofisi ya *CAG* iwezeshwe kwa upande wa rasilimali fedha na rasilimali watu ili waweze kufanya *performance audit* ambayo itaonesha kama mradi kweli ina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo inabidi hata Kamati ya *LAAC* iwezeshwe kufika maeneo mengi zaidi ili kuthibitisha taarifa ya *CAG,* hivyo, ni vyema ipewe muda wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti uliofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2009 kuhusu umuhimu wa *VRTs* katika kuhamasisha maendeleo ndani ya mfumo wa Serikali za Mitaa, ilipendekezwa kwamba *VRTs* wajengewe uwezo waenezwe katika halmashauri zote, wapewe vitendea kazi na usafiri; vilevile uwepo mpango na miongozo sahihi kwa ajili ya kufuatilia utendaji wao. Katika kuhitimisha hoja, ningependa kupata maelezo ni nini kimefanyika kuhusiana na *VRTs* tangu mapendekezo hayo yametolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti suala la lishe katika halmashauri zetu litiliwe mkazo kwa kuajiri Maafisa Lishe na

kusisitiza elimu ya lishe kwa jamii, pia kuhimiza agenda ya lishe katika *RCC, DCC* na Mabaraza ya Madiwani. Hii itapunguza gharama na bajeti katika Sekta ya Afya.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuchangia katika maeneo matatu; eneo la kwanza ni uhaba wa watumishi. Suala hili limekuwa likiathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza ufanisi katika utendaji wa kazi katika halmashauri zetu na limekuwa ni la muda mrefu hata kabla ya uhakiki wa watumishi hewa na wasiokuwa na sifa, malalamiko yalikuwa ni makubwa na baada ya zoezi hilo likaongeza zaidi makali ya changamoto hii ya uhaba wa watumishi. Mfano, katika Mkoa wangu wa Singida, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama pekee ina upungufu wa watumishi 462 katika Sekta ya Afya; Manyoni uhaba wa watumishi 446; Itigi watumishi 269 na Ikungi 822.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi unaweza kuona jinsi gani changamoto hii ilivyo kubwa. Naishukuru Serikali kwa kukubali ushauri na kuwarejesha watumishi kazini kulingana na sifa zao, lakini naishauri ni vyema sasa ikaja na mikakati ya makusudi ya kuajiri watumishi wengi ili kuziba upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulichangia ni ucheleweshwaji wa fedha za shughuli za maendeleo katika halmashauri zetu. Suala hili limesababisha kukwama kwa miradi mingi au kutokukamilika kwa miradi kwa wakati na kuisababishia Serikali hasara na kwa upande wa wananchi imekuwa ni kero kubwa kusubiri mradi kwa muda mrefu na hivyo kuwakosesha huduma muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba bajeti yetu hutegemea makusanyo ya mapato kwa mwezi**,** lakini

uhalisia wa kiasi cha fedha tunachokiidhinisha katika shughuli za maendeleo kinatofautiana kwa kiasi kikubwa cha fedha zinazopelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ni vyema sasa ikajitathmini na kurekebisha hali hii, miongoni mwa mikakati ya kujirekebisha na kujitathmini ni kupeleka fedha zlizobaki za miradi ya maendeleo katika Mkoa wangu wa Singida. Ni vyema Serikali ikaimarisha ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kisasa (kielektroniki) ikiwemo elimu ya mlipakodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo napenda kulichangia ni asilimia 10 ya mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana zitokanazo na mapato ya ndani katika halmashauri zetu. Imekuwa ni kawaida kwa Maafisa Masuuli kutokupeleka kwa makusudi au kutokupeleka kwa wakati asilimia 10 ya mikopo kwa vikundi vya wanawake na vijana. Muda uliopita nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* na tatizo hili tumekuwa tukikutana nalo kila mara tulipokwenda kufanya ukaguzi katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba wanawake na vijana hawa ndio makundi muhimu na nguvu kazi ya Taifa katika kukuza uchumi lakini wengi wao hawana dhamana ya kukopa katika mabenki na taasisi za fedha kwa kutopeleka asilimia 10 ya mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake ni kuwakosesha fursa ya kukua kiuchumi. Naishauri Serikali ije na mikakati mahususi ambayo itawabana Maafisa Masuuli waweze kupeleka asilimia 10 za mikopo kwa vikundi vya vijana na wanawake kwa kiasi kikubwa kinachotakiwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Serikali iimarishe Idara ya Maendeleo ya Jamii ili iweze kufanya kazi yake ipasavyo kwa kukaa na makundi haya na kuwaelimisha juu ya mikopo hiyo hatimaye iweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa

Kakunda kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuwaletea wananchi maendeleo; nawatia moyo waendelee na kasi hiyohiyo ya utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa leo, tumefikia mwisho wa shughuli zetu, hivyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 16 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*